**31 OKTOBA, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 31 Oktoba, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI ZILIIMBWA

## D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## KIAPO CHA UAMINIFU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kiapo cha Uaminifu, Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo.

Mbunge afuataye aliapa kiapo cha uaminifu:-

Mhe. Bahati Keneth Ndingo

**SPIKA:** Katibu.

**31 OKTOBA, 2023**

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilete taarifa yangu kwenu katika Mkutano wa 12 wa Bunge. Bunge lilipitisha Miswada mitatu ya sheria ambayo ni:

Kwanza; Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2023. *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments (No. 2) Bill, 2023],*

Pili; Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2023 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill, 2023]*

Tatu; Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa 2023.

Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa hii napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kuwa tayari Miswada hiyo mitatu imepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kuwa Sheria za Nchi ambazo sasa zitaitwa ama zinaitwa:-

(i) Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2), Sheria (Na. 8) ya Mwaka 2023 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Act, (No. 8) of 2023];*

(ii) Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3), Sheria (Na. 9) ya Mwaka 2023 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3), Act, (No. 9) of 2023];* na

(iii) Sheria ya Ununuzi wa Umma (Na. 10) ya Mwaka 2023.

Waheshimiwa Wabunge, hiyo ndiyo taarifa kuhusu Miswada ambayo Bunge hili lilishapitisha na imeshapata kibali cha

Mheshimiwa Rais na hivyo ni Sheria kwa sasa. Tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**SPIKA:** Hati za kuwasilisha mezani Waziri wa Afya, kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Godwin Mollel.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:**

Maelezo ya Waziri wa Afya kuhusu Azimio la Bunge juu ya Mapendekezo ya Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika la Mwaka 2023 *(Treaty for Establishment of the African Medicines Agency – AMA)*.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, kwa niaba yake Mheshimiwa Kassim.

**MHE. KASSIM HASSAN HAJI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Azimio la Bunge juu ya Mapendekezo ya Kuridhia Mkataba wa Kuanzishwa Taasisi ya Dawa ya Afrika la Mwaka 2023 *(Treaty for Establishment of the African Medicines Agency – AMA)*.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waziri wa Nishati, kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:**

Maelezo ya Waziri wa Nishati kuhusu Azimio la Bunge juu ya Mapendekezo ya Tanzania Kuridhia Kujiunga na Mkataba wa

Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu la mwaka 2009 *(Statute of the International Renewable Energy Agency – IRENA)*.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa niaba yake Mheshimiwa Aleksia Kamguna.

**MHE. ALEKSIA A. KAMUGUNA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Azimio la Bunge juu ya Mapendekezo ya Tanzania Kuridhia Kujiunga na Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu la Mwaka 2009 *(Statute of the International Renewable Energy Agency – IRENA)*.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2023)*.

**SPIKA:** Ahsante sana Waziri wa Katiba na Sheria, kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Pauline Gekul.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Maelezo ya Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria wa Mwaka 2023 (*The Legal Sector Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023)*.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kwa niaba yake Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. OMAR I. KOMBO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya Sekta ya Sheria ya Mwaka 2023 *[The Sector Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023]*.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mbunge sijui kama umepewa zote mbili au kuna mwingine anakuja?

**MHE. OMAR I. KOMBO:** Mheshimiwa Spika, mwingine anakuja.

**SPIKA:** Anhaa! yuko wapi mwingine? Aah! kwa sababu nilishamwita Mwenyekiti kwa hiyo na wewe karibu, Mheshimiwa Shaafi.

**MHE. SALUM MOHAMMED SHAAFI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2023)*.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge hebu tutazame kama kuna mtu kisemeo chake kinawaka.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali, Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Mariam Kisangi.

Na. 1

**Kufanya marekebisho Sheria ya Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y MHE. STELLA I. ALEX** aliuliza:-

Je, upi mkakati wa Serikali kufanya Marekebisho ya Sheria Na. 9 ya mwaka 2010 ya Watu Wenye Ulemavu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobas Katambi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii, lakini uniwie radhi kwamba nataka kutumia fursa hii kukupongeza sana, kwa kuwa Rais wa Mabunge Duniani, hii inadhihirisha uwezo mkubwa lakini weledi mkubwa ulionao katika kuongoza Bunge letu lakini pia kuaminika katika Dunia.

Mheshimiwa Spika, Pia nimpongeze sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukupa fursa hiyo lakini zaidi pia kuweza kuwezesha jambo hili kufanikiwa. Haya ni mafanikio makubwa kwa nchi yetu na kwamba, imekuwa kielelezo wewe pamoja na Dkt. Samia Suluhu Hassan cha kufanya sasa *leadership tourism* katika nchi yetu ya Tanzania, wanaweza kuja kujifunza masuala ya uongozi kupitia Dkt. Samia Suluhu Hassan pia uongozi wako mzuri.

Mheshimiwa Spika, mimi najivunia kuwa wa kwanza kujibu swali leo mbele ya Rais wa Mabunge Duniani. Hili siyo jambo rahisi, najivunia sana hilo lakini pia ni Mbunge wa kipekee kwa sababu hata Waziri Mkuu wa Uingereza anatoka Jimboni kwangu, kwa hiyo ahsante kwa kuniongezea rekodi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba nijibu swali kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu la Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Serikali kwa sasa ni kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2004 ambapo utekelezaji wake umeanza. Baada ya kukamilika kwa mapitio ya Sera ya mwaka 2004, ndipo hatua za Marekebisho ya Sheria ya Watu wenye Ulemavu (Na. 9) ya mwaka 2010 itaanza kwa kuzingatia mapungufu yatakayobainishwa katika tathmini ya utekelezaji wa Sera ya mwaka 2004. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Mheshimiwa Ikupa, napenda kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sheria hiyo Na. 9 ya mwaka 2010 ndiyo sheria pekee ambayo inaonesha haki zote za watu wenye ulemavu; na kwa kuwa marekebisho ya sheria hiyo yanategemea marekebisho ya sera: Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha inaharakisha mchakato huo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa watu wenye ulemavu wana haki nyingi sana za kimsingi na wapo wengi ambao hawaelewi haki zao za kimsingi ikiwepo upatikanaji wa ajira, elimu na mambo mengine: Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kutoa elimu kwa watu wenye ulemavu ili waweze kutambua haki zao na pia kutoa nyongeza katika marekebisho ya sheria hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, tumeshaanza kufanya kazi ya kufanya mapitio ya Sera ya Watu Wenye Ulemavu kwa sababu sera hiyo ni ya mwaka 2004 na sheria ni ya mwaka 2010. Kwa hiyo, katika kufanya hivyo, sera ndiyo inayotangulia ili iweze kutengeneza mazingira mazuri zaidi na kufanya tathmini na kuwashirikisha wadau wote ili kuweza kujua changamoto za sasa zinazowakumba watu wenye ulemavu ili kuweza kuwahudumia vizuri zaidi na kutunga sheria ambayo itakuwa inaendana na mahitaji halisia katika mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tayari tumeanza kwa mwaka huu wa fedha 2023/2024. Matarajio yetu, tutakuwa tumemaliza kwenye hatua ya sera, na 2024/2025 tutakuwa tunaenda sasa kwenye kutunga sheria ambapo tayari hatua ya awali tumeshaanza na *procedure* ya kufanya mabadiliko kwenye sera, kukutanisha wadau, kufanya *situational analysis* kwenye mikoa na maeneo mbalimbali, na pia kukutanisha mashirikisho ikiwemo Shirikisho la Chama cha Watu Wenye Ulemavu na Shirikisho la Wanawake Wenye Ulemavu na taasisi nyingine zote ambazo zinahusika na haki za watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama nilivyoeleza, ndani ya mwaka huu wa fedha tutakuwa tumejitahidi kwenye upande wa sera na mwaka wa fedha unaofuata tutakuwa tumeumaliza katika upande wa kutunga sheria ambapo itakuwa muafaka wa kutibu changamoto ambazo zinawakumba watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ameniuliza kuhusiana na haki za msingi za watu wenye ulemavu kwamba wapo wengi ambao hawazifahamu. Tumeendelea kufanya hivyo, mbali na kuwa na sera na sheria ya watu wenye ulemavu, tumekuwa tunasajili pia taasisi mbalimbali ambazo zinaendelea kutoa elimu na kusimamia haki za watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, upande wa Serikali pia tumeendelea kutoa elimu kupitia vyombo vya habari lakini pia kuyafikia makundi mbalimbali ikiwemo kuunda mabaraza ya kuanzia ngazi ya kata mpaka Taifa ya watu wenye ulemavu ikiwa

ni pamoja na kushirikiana na mashirikisho ya watu wenye ulemavu ili kuendelea kutoa elimu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kufanya hivyo pia, alitoa fedha zaidi ya shilingi bilioni tatu kufufua vyuo zaidi ya saba vya watu wenye ulemavu ambapo tumeshafanya kazi hiyo. Lengo ni kuwapa fursa zaidi watu wenye ulemavu na kuwaingiza waweze kujitegemea. Zaidi tumeboresha hata mwongozo unaotoa haki kwa watu wenye ulemavu kupata mikopo ya asilimia mbili kutoka kundi la watu wenye ulemavu watano na sasa mkopo anaweza kupata mtu mwenye ulemavu mmoja na tunaweza kumpa mkopo wa kuanzia shilingi milioni moja hadi milioni hamsini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jitihada za Serikali zinazofanyika ni kubwa, ahsante.

**SPIKA:** Hakuna maswali mengine. Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ajili ya majibu hayo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ili tuweze kuukomboa wakati, kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, na Waziri Mkuu ndio Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, basi Bunge liwe limepokea pongezi zote kwa mujibu wa kanuni zetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ili tuwapunguzie muda wa kutoa pongezi, nimeshazipokea, ahsanteni sana. Kwa hiyo, wengine wote tuendelee kuuliza maswali. Wote nimezipokea pongezi zenu, ahsanteni sana. Turejee sasa ule utaratibu wetu, maswali mafupi na majibu mafupi.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 2

**Hitaji la zahanati Kata ya Binza – Maswa**

**MHE. MINZA S. MJIKA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Zahanati katika Kata ya Binza – Maswa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mwongozo wa Ujenzi wa Zahanati katika Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) wa mwaka 2007 wananchi wanatakiwa kuanza ujenzi wa boma mpaka hatua ya lenta.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufikia hatua ya lenta Serikali hupeleka fedha kwa ajili ya umaliziaji wa jengo. Hivyo wananchi wa Kata ya Binza wanashauriwa kuanza kwa utaratibu huo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, je, ni lini sasa Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa zahanati katika Kata ya Binza Kijiji cha Iyogero?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, ni lini Serikali itapeleka fedha za kukamilisha kujenga zahanati katika Kijiji cha Ng'hami Wilaya ya Maswa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafuatilia kuona hatua ambazo majengo haya ya zahanati yamefikia ili tuweze kuweka kwenye bajeti kwa ajili ya kukamilisha majengo haya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Dugange ulifika kwenye Zahanati ya Tiling'ati na ukaahidi kuwapelekea shilingi milioni 20…

**SPIKA:** Swali lako?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ni lini atapeleka fedha katika Zahanati ya Tiling'ati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli Zahanati ya Tiling'ati tulifika pale na wanahitaji shilingi milioni kumi kwa ajili ya ukamilishaji na Mheshimiwa Waziri wa Nchi alishaahidi kwamba fedha zitakwenda pale. Namhakikishia kwamba tutafuatilia kuhakikisha kwamba shilingi milioni kumi zinapelekwa pale Zahanati ya Tiling'ati, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, tatizo la maboma ya zahanati nchi nzima imekuwa kero na ya muda mrefu tangu 2010, je, Serikali imefanya utafiti ni yapi yanaweza kutengenezeka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni kweli, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kumekuwa na maboma mengi katika vijiji vyetu kwa ajili ya zahanati lakini kwa kweli katika kipindi cha miaka hii mitatu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amekamilisha maboma zaidi ya 900. Kwa hiyo, kazi ya Serikali ni kuendelea kutambua maboma ambayo tayari yanakidhi vigezo vya kukamilishwa na fedha zinaendelea kutengwa. Mwaka huu wa fedha shilingi bilioni 90 zimetengwa kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma hayo.

Mheshimiwa Spika, tunafanya utafiti na tutaendelea kuyakamilisha kwa awamu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, swali la nyongeza. Mheshimiwa Mwakagenda, swali la nyongeza.

Ulikuwa umeomba Mheshimiwa? Nimeona kama umeshangaa kidogo ndiyo maana nikakuacha. Au ndiyo ulikuwa unaingia Bungeni?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Hapana.

**SPIKA:** Haya sawa. Samahani.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kulingana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri…

**SPIKA:** Ngoja, ngoja. Mheshimiwa, unaweza kutafuta swali lingine kwa sababu niliona umesimama, sasa nilifikiri umesimama kwa ajili ya kuomba swali na sitaki kukuweka mazingira ambayo unauliza kama hukuwa umejiandaa. Unaweza kutafuta lingine nitakupa tu nafasi. *(Kicheko)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Ahsante.

**SPIKA:** Ama ulisimama kwa ajili ya hili? Ndiyo hicho nilichotaka kujua. Tafuta lingine tu nitakupa nafasi ama ulitaka hili? Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nahitaji hili.

**SPIKA:** Naam, ulihitaji hili?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nahitaji kuuliza swali hapo.

**SPIKA:** Haya, karibu. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kulingana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, anaonesha kwamba wananchi wanapaswa kuchangia ujenzi wa zahanati hadi kwenye maboma, lakini wapo watu ambao wamekuwa wakipita kwenye majimbo yetu wakiwaambia wananchi wasichangie ujenzi wa zahanati na maboma mengine ya elimu: Je, nini hatua ya Serikali dhidi ya hao ambao wanapotosha wananchi wasishiriki mendeleo yao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Utaratibu wa ujenzi wa maboma ya zahanati kwa mpango wa maendeleo ya afya msingi upo kwa mujibu wa mwongozo wa 2007. Ni maamuzi ya Serikali kwamba wananchi wanashiriki kwa sehemu na Serikali inahitimisha. Kama wapo watu ambao wanapita katika maeneo yetu na kupingana na maelekezo ya Serikali basi naomba Serikali kwa maana ya Wakurugenzi, Wakuu wa Wilaya na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wawatambue watu hao ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Jimbo la Rungwe, wananchi wameweka nguvu sana katika kujenga maboma ya zahanati, ni lini Serikali itaongeza fedha ili kuweza kumalizia maboma hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma na ninafahamu Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imepata fedha zaidi ya shilingi milioni mia tatu kwa ajili ya maboma sita ya zahanati katika kipindi cha miaka miwili. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma hayo.

Mheshimiwa Spika, pia nawakumbusha Wakurugenzi na Makatibu Tawala wa Mikoa kwamba tulitoa maelekezo lazima tuwe na uratibu wa ujenzi wa maboma badala ya kila mtu kuamua kila siku kujenga boma na mwisho wa siku maboma yanakaa muda mrefu. Wazingatie utaratibu huo kwa maana kuratibu na Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya umaliziaji, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Lini Serikali itaanza mchakato wa ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya Likawage, Jimbo la Kilwa Kusini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Kata ya Likawage katika Wilaya ya Kilwa inahitaji Kituo cha Afya na Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia mara kwa mara. Tulishaelekeza wataalamu kwa maana Mganga Mkuu wa Wilaya na Mganga Mkuu wa Mkoa, wafanye tathmini ya vigezo na

kuwasilisha maombi Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Nasisitiza tupate taarifa hiyo ndani ya wiki mbili ili Mheshimiwa Waziri wa Nchi aweze kuona uwezekano wa kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi huo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni lini Serikali itakamilisha Kituo cha Afya cha Migori kilichopo Kata ya Migori ambacho kimejengwa na nguvu za wananchi karibu takribani shilingi milioni 10.8 ambazo wamechangia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kutumia fursa hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, kumwelekeza Mganga Mkuu wa Mkoa wa Iringa pamoja na Katibu Tawala wa Mkoa wa Iringa waweze kuwasilisha maombi hayo ili tuweze kuona kama inakidhi vigezo tuweze kupeleka fedha kwa ajili ya ukarabati na ukamilishaji wa jengo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salma Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, ni lini Serikali itatupatia fedha ili tuweze kujenga Kituo cha Afya katika Tarafa ya Nangaru?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, hivi sasa tayari Serikali imeanza kufanya tathmini ya pili ya tarafa ambazo hazikupata vituo vya afya vya kutosha kwa awamu ile ya pili ya mwaka wa fedha 2021/2022. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati tunaendelea na tathmini hii, tutatoa kipaumbele katika Kata hii ya Nangaru kuona uwezekano wa kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya uweze kutekelezwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, swali la nyongeza.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi nami niulize swali dogo la nyongeza. Ni lini sasa Serikali itatoa *commitment* ya kuibadilisha Zahanati ya *Town Clinic* Tabora Mjini na kuwa kituo cha afya kwa sababu inazalisha watu wengi kwa mwezi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Munde, inazalisha watu wengi kwa mwezi?

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, inazalisha karibu akina mama 200 kwa mwezi na Mheshimiwa Waziri anajua, lakini bado ni zahanati haijawa kituo cha afya. Tunaomba aipandishe hadhi. Ni lini ataipandisha hadhi?

**SPIKA:** Haya, sawa, ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba *Town Clinic* katika Manispaa ya Tabora ni zahanati ya muda mrefu na inahudumia wananchi wengi sana. Serikali ilishatoa maelekezo kwa Mkurugenzi, walishaelekezwa kuandaa michoro ya ghorofa kwa sababu eneo lile ni dogo ili fedha ziweze kutengwa kwa ajili ya kujenga ile zahanati na kupandisha hadhi kuwa kituo cha afya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, natumia fursa hii kumkumbusha Mkurugenzi na Katibu Tawala wa Mkoa wa Tabora, kutekeleza maelekezo ya Serikali mapema ili tathmini ifanyike, fedha zitafutwe kwa ajili ya kupandisha hadhi zahanati hii kuwa kituo cha afya. Ahsante. *(Makofi)*

Na. 3

**Mahitaji ya watumishi, vifaa tiba na tendanishi – Lupembe**

**MHE. EDWIN E. SWALLE** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kupeleka Watumishi, Vifaa Tiba na Tendanishi kwenye Vituo vya Afya na Zahanati katika Jimbo la Lupembe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Jimbo la Lupembe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imetenga shilingi milioni 700 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba kwa ajili ya hospitali, vituo vya afya na zahanati katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 na 2022/2023, Serikali imepeleka jumla ya watumishi 72 wa Kada mbalimbali za afya kwa ajili ya kutoa huduma katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti ya ununuzi wa vifaa tiba pamoja na kuajiri watumishi wa kada mbalimbali za afya kwa ajili ya kwenda kutoa huduma kwenye vituo kote nchini, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Edwin Swalle, swali la nyongeza.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Jimbo la Lupembe, wananchi wamejenga zahanati nyingi sana. Tunazo zahanati mpya za

Welela, Havanga, Lima, Tagamenda, Ikondo na kila mahali. Pia kuna vituo vya afya kama Ikondo, Mtwango, ni vipya kabisa: Ni nini mpango wa Serikali kupeleka watumishi wa afya kwenye vituo hivi ili vianze kufanya kazi mapema? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa afya ni pamoja na kuwa na magari ya wagonjwa, Serikali ina mpango gani wa kupeleka gari la wagonjwa kwa maana ya *ambulance* katika Jimbo la Lupembe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nawapongeza wananchi wa Jimbo la Lupembe kwa kujitolea nguvu zao na kujenga zahanati na kuanza ujenzi wa vituo vya afya. Nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji mzuri. Kwa hakika Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuleta fedha katika Wilaya ya Njombe na katika Jimbo la Lupembe.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunaongelea Kituo cha Afya cha Ikuna kinaendelea kujengwa, lakini pia zahanati zimepata fedha shilingi milioni 50 kwa ajili ya ukamilishaji. Vile vile watumishi wataendelea kuletwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kwa maana ya watumishi wa kada za afya kama ambavyo zilishapelekwa 72, lakini ajira nyingine zinazofuata watatoa kipaumbele katika Halmashauri hii.

Mheshimiwa Spika, siku tatu zilizopita Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amegawa magari ya wagonjwa 199 katika halmashauri zetu zote na magari ya usimamizi wa huduma za afya na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe Jimbo la Lupembe limepata gari hilo. Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba gari lipo njiani linafika wakati wowote kwa ajili ya kuhudumia wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, je, upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba watumishi wanapelekwa katika Kituo cha Afya cha Songwe katika Kata ya Nanyara ambacho kina upungufu mkubwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali, kwanza tumeainisha maeneo yenye upungufu mkubwa wa watumishi na ajira zinazofuata tutahakikisha kituo hiki kinapatiwa watumishi wa sekta ya afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deus Sangu, swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Serikali imejenga vituo vya afya vitatu katika Kata ya Kaegesa, Kipeta na Kaoze: Je, ni upi mkakati wa kupeleka vifaatiba na watumishi katika vituo hivyo vya afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka wa fedha huu imetenga jumla ya shilingi bilioni 69.9 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba kwa ajili ya kupeleka kwenye vituo vya afya. Mwaka wa fedha uliopita, halmashauri zote zilipata vifaatiba. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba zoezi hili ni endelevu na tutapeleka vifaa tiba kwa ajili ya vituo hivi vya afya lakini na pia tutapeleka watumishi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba vituo hivi vinaanza kutoa huduma, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali itapeleka vifaatiba katiba Halmashauri ya Itigi ambapo tumejenga zahanati na vituo vya afya lakini vifaa tiba na watumishi ni haba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Katika mwaka wa fedha uliopita, Halmashauri ya Itigi pia imepata vifaatiba, pia mwaka huu wa fedha, bajeti hii ambayo inatekelezwa, tutapeleka vifaatiba na fursa za ajira zitakapojitokeza, tutahakikisha tunatoa kipaumbele kwa watumishi ili Halmashauri ya Itigi iweze kupata huduma bora za afya. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anastazia Wambura, swali la nyongeza.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mkoa wa Mtwara una zahanati sita ambazo hazijaanza kutoa huduma kutokana na kutokupata mgao wa watumishi katika ajira mpya: Je, ni lini Serikali itapeleka watumishi ili kusudi zahanati hizi ziweze kuanza kufanya kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, tulishatoa maelekezo kwa Wakurugenzi na Makatibu Tawala wa Mikoa kwamba pale zahanati zinapokamilika, hatuna sababu ya kuziacha zisianze kutoa huduma za awali. Natumia fursa hii kwanza kumkumbusha Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo na Katibu Tawala wa Mkoa wa Mtwara kwamba watumie utaratibu wa kuwa-*reallocate* watumishi ndani ya halmashauri ili angalau huduma za *OPD* zianze kwenye zahanati hizi.

Mheshimiwa Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatoa kipaumbele kwenye ajira zinazofuata ili watumishi wafike katika zahanati hizi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH KASHEKU MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri; Zahanati ya Kijiji cha Nkome inazalisha watoto 400 kwa mwezi, na Mheshimiwa Naibu Waziri Silinde tulienda naye akaona…

**SPIKA:** Mheshimiwa swali lako.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa kituo cha afya Nkome?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Zahanati ya Nkome inazalisha wakina mama wengi sana kwa mwezi na inahudumia wananchi wengi kwa ujumla wake. Pia, nimhakikishie kwamba tayari imekwishaingizwa kwenye orodha ya vituo vya afya ambavyo vinatafutiwa fedha kwa ajili ya kujengwa ili iweze kutoa huduma kwa ngazi ya kituo cha afya. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Pamoja na kwamba Serikali imekuwa ikipeleka vifaa tiba kwenye baadhi ya zahanati zetu na vituo vya afya lakini bado kuna tatizo la vifaa tiba hivyo kukosa watumiaji (wataalamu). Nini kauli ya Serikali kupeleka watumishi kwenye hizi zahanati na vituo vya afya ambavyo vina vifaa tiba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumekuwa na upungufu wa wataalamu wa kutumia baadhi ya vifaa tiba ambavyo vimepelekwa katika vituo vyetu. Kwa kulitambua hilo, Serikali imeandaa utaratibu wa mafunzo ya muda mfupi wa miezi mitatu mpaka miezi sita kwa wataalamu wa mionzi na wataalamu wengine ili tuweze kuziba hili *gap* la wataalamu wa kutumia vifaa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, wataalamu hao tayari wamekwishaingia katika ngazi ya masomo na tunahakikisha mapema iwezekanavyo wakihitimu wanapelekwa kwenye vituo vyetu ili waweze kutumia vifaa hivyo ipasavyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ali Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kituo cha Afya cha Chikolopola kina mtumishi mmoja tu. Lakini pia Zahanati ya Mputeni na zahanati ya Makanyama haina watumishi kabisa. Ni lini Serikali itapeleka watumishi katika maeneo haya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchungahela, ni swali la nyongeza kwa hiyo unaruhusiwa kuuliza moja. Sasa, wewe umeuliza matatu katika moja wakati ni swali la nyongeza. Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri atachagua ajibu lipi. Wewe usiwe na wasi wasi. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama ambavyo katika mwaka wa fedha uliopita halmashauri hii ya Masasi vijijini walipata watumishi. Nafahamu kwamba bado wanaupungufu mkubwa katika Kituo cha Afya cha Chikolopola. Nimhakikishie kwamba tutatoa kipaumbele kwenye ajira zitakazofuata ili waweze kupata watumishi wa kutosha katika eneo hilo. ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abbas Tarimba, swali la nyongeza.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pale Jimbo la Kinondoni, kwa kupitia fedha za mfuko wa Jimbo tumejenga jengo la mionzi kwa maana ya *(Radiology)*.

Je, Serikali iko tayari sasa kutupatia vifaa tiba kama vile *x-ray, ultrasound* pamoja na wafanyakazi ili kituo kile kiweze kuanza kazi? Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kutenga fedha kupitia Mfuko wa Jimbo na kujenga Jengo la mionzi na nafahamu amekuwa akifuatilia mara kwa mara. Nimhakikishie kwamba Serikali itashirikiana na halmashauri ya Kinondoni kupitia mapato ya ndani ili waweze kununua baadhi vifaa tiba ambavyo viko ndani ya uwezo wao kama *ultrasound*, wakati Serikali kuu inaangalia uwezekano wa kupata fedha kwa ajili ya *x-ray* ili wananchi wapate huduma bora, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa mujibu wa taarifa ya *CAG* iliyotoka mwezi Machi, 2023. Halmashauri 106 zilikuwa na idara na vitengo ambavyo vinaongozwa na watumishi 747 wasiokuwa na sifa. Matokeo yake ufanisi ni duni. Ni lini Serikali itaenda kuziba nafasi hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna baadhi ya halmshauri ambazo zina wakuu wa idara na vitengo ambao hawajathibitishwa. Kwa sababu hizo Serikali inafanya utaratibu ikiwemo upekuzi lakini pia kuwatafuta wenye sifa za kuweza kujaza nafasi hizo ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko kazini. Tunafanya *vetting* ya wataalamu wenye sifa hizo ili waende kujaza nafasi za wakuu wa idara na waweze kutoa huduma ipasavyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, sasa aulize swali lake.

Na. 4

**Kukamilisha ujenzi wa Zahanati ya *Masagalu Mission* – Kilindi**

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatoa fedha kukamilisha ujenzi wa majengo ya zahanati Kijiji cha *Masagalu Mission,* Kilindi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Jimbo la Kilindi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Serikali ilipeleka shilingi milioni 100 katika Halmashauri ya Kilindi kwa ajili ya kukamilisha boma la Zahanati ya Masagalu. Kwa kuwa boma hilo lilijengwa kwa ramani ya zamani ambayo ni kubwa zaidi, ujenzi haukuweza kukamilika.

Mheshimiwa Spika, Zahanati ya Masagalu imeanza kutoa huduma kwenye baadhi ya vyumba ambavyo vimekamilika. Aidha, Serikali kupitia Mapato ya ndani ya Halmashauri ya Kilindi itatenga shilingi millioni 100 katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 ili kukamilisha ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 inatarajia kutenga au itatenga shilingi

milioni 100 kwa ajili ya kumalizia Kitua cha Afya cha Kilindi asilia na shilingi milioni 40 kwa ajili ya hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Spika, sasa, nataka tu nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri, hizi taarifa za kwamba tumetenga shilingi milioni 100 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa Zahanati ya Masagalu amezipata wapi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali imekuwa na utaratibu wa kuhamasisha wananchi kujenga majengo na wao kutenga milioni 50. Je, Serikali haioni iko sababu ya kutenga milioni 50 na kuwapelekea wananchi wa Masagalu na kumalizia majengo haya? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo ameendelea kuweka kipaumbele katika Baraza la Madiwani ili kuhakikisha kwamba wanatenga fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo ya Zahanati na Vituo vya Afya.

Mheshimiwa Spika, Serikali ni moja. Mkurugenzi wa halmashauri, Katibu tawala wa mkoa wana wajibu wa kupokea maelekezo kutoka katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI, hasa tunapoona vigezo vya ukamilishaji wa majengo hayo vinakidhi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa mujibu wa jengo hili ambalo lina zaidi ya miaka mitano halijakamilika, tumemwelekeza Mkurugenzi na amechukua hiyo *commitment* kwamba, atenge milioni 100 kama kipaumbele katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 kukamilisha boma hili ambalo lina muda mrefu na baadaye tutaendelea na maboma mengine.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ina utaratibu wa kutenga milioni 50 kwa ajili ya kukamilisha maboma na Halmashauri hii ya Kilindi imekuwa ikipata fedha hizo. Pia, nimhakikishie tu kwamba

tutaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuhakikisha tunachangia ukamilishaji wa zahanati hiyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu zodo, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, toka Desemba, 2022 Mheshimiwa Rais amepeleka milioni hamsini hamsini kwenye maboma ya zahanati. Mpaka leo hayajakamilika ikiwepo Zahanati ya Mpasilasi kwenye Jimbo la Korogwe vijijini. Je, ni upi mkakati wa Serikali sasa kuhakikisha wanakwenda kusimamia ili maboma yale yakamilike?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Serikali inapeleka milioni 50 kwa ajili ya kukamilisha maboma kwenye maeneo ya halmashauri zetu ambako kuna viongozi. Kuna wakuu wa idara, Wakurugenzi, wakuu wa wilaya na wakuu wa mikoa. Sasa, ni wajibu wao kuhakikisha kwamba, fedha hizi ambazo Mheshimiwa Rais anazipeleka zinafanya kazi kwa wakati na kukamilisha ujenzi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, nittumie fursa hii kuwakumbusha Wahesjhimiwa wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, Makatibu tawala wa mikoa pamoja na wakurugenzi kwamba, ni wajibu wao na sisi tutafuatilia kuona maboma haya yanakamilika kwa wakati na kuanza kutoa huduma kwa wananchi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vedastu Msthayo, swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya swali dogo la nyongeza. Kila mwaka Serikali imekuwa ikiahidi kutoa fedha kwa ajili ya kumalizia kituo cha afya cha Bweri. Sasa ni lini tutapata hizo fedha ili kile kituo kiweze kukamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Bweri tayari kimeingizwa kwenye orodha ya vituo vya kimkakati ambavyo vinatafutiwa fedha kwa ajili ya ukamilishaji. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge awe mvumilivu, aamini kwamba Serikali ipo kazini na mara fedha itakapopatikana tutahakikisha kwamba tunaipeleka kwa ajili ya kukamilisha Kituo cha Afya cha Bweri. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba ya Mganga katika Zahanati ya Kijiji cha Mchalambuko Wilayani Kilwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutafanya tathmini ya mahitaji ya gharama zinazohitajika kwa ajili ya ukamilishaji wa nyumba ya mtumishi. Lakini tutatafuta fedha kwa kupitia mapato ya ndani, lakini pia na Serikali Kuu ili nyumba hiyo ikamilike na watumishi wetu waweze kuishi pale. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wakati wa Bunge la Bajeti niliahidiwa shilingi milioni 500 kwa ajili ya uboreshaji wa vituo vya Kalenge na Nyubusozi wilayani Biharamulo. Ni lini pesa hiyo itatumwa ili huduma hiyo iweze kufanyika kwa ajili ya wananchi wa Biharamulo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika,

ahsante sana. Vituo hivi vya afya ambavyo viliahidiwa katika Bunge la Bajeti, ni sehemu ya kipaumble cha Serikali katika kuhakikisha kwamba tunatafuta fedha na kuzipeleka ili ujenzi uweze kufanyika. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Mbunge uwe na Subira kidogo wakati Serikali inatafuta fedha na mara fedha zikipatikana kwa awamu tutahakikisha kwamba tunaanza ujenzi wa vituo vya afya katika maeneo hayo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni lini Serikali itapeleka fedha za kumalizia Zahanati ya Kidanda katika Kata ya Itwangi – Shinyanga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nielekeze halmashauri husika iweze kuleta taarifa ya hatua ya ujenzi wa boma hilo la zahanati ulipofikia, ili liweze kuingizwa kwenye mpango wa kutafutiwa fedha kwa ajili ukamilishaji wa jengo hilo. ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Mageni, swali la nyongeza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za kutosha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Zahanati katika Kijiji cha Chamva ili hali fedha iliyokuwa imetumwa awali haikutosha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, maeneo yote ambayo Serikali ilipeleka milioni 50 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma, kwanza maelekezo ilikuwa ni kwamba boma liwe limefikia hatua ya *linter*. Pia, kwa tathimini zetu kwa kiasi kikubwa milioni 50 ilikuwa inatakiwa kukamilisha boma. Sasa kama eneo hili la Chamva fedha ilipelekwa lakini boma halikukamilika,

kwanza tunataka Mkurugenzi wa Halmashauri atupatie taarifa rasmi kwa nini milioni 50 hazikutosha kukamilisha boma, tujiridhishe na matumizi sahihi ya fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, pili, wanatakiwa kutenga fedha kwenye mapato ya ndani ili kuhakikisha kwamba wanakamilisha jengo la Zahanati ya Chamva. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Mimi katika Jimbo langu la Sikonge, wananchi pamoja na Mfuko wa Jimbo tumeshirikiana. Tuna maboma 14 ambayo yanahitaji milioni hamsini hamsini, jumla milioni 700 na halmashauri haina uwezo. Je, Serikali kuu haiwezi kutusaidia tuweze kumaliza maboma hayo 14.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Safari ni hatua, Serikali imeendelea kupeleka fedha katika Jimbo la Sikonge kwa ajili ya umalizaji wa maboma. Nimhakikishie kwamba tutaendelea kwa awamu kutafuta fedha ili kuendelea kukamilisha maboma haya. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtemvu swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Kwa muda mrefu Jimbo la Kibamba halijapata fedha hizi za mambo na ninayo maboma ya zahanati ya Saranga King'azi na Msakuzi. Je, ni lini Serikali inaweza kuweka *commitment* hasa kwa mwaka huu 2023/2024 ili waweze kuleta fedha tumalizie maboma haya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika,

ahsante sana. Maboma ya zahanati katika Jimbo la Kibamba Halmashauri ya Ubungo yatatafutiwa fedha kwa ajili ya ukamilishaji. Hata hivyo, nitumie fursa hii kuwakumbusha wakurugenzi wa Manispaa zenye mapato makubwa kama Ubungo na Manispaa nyingine, kuweka kipaumbele cha fedha za miradi ile asilimia 40,60 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma hayo wakati Serikali ikiendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma hayo. Ahsante.

**SPIKA:** Haya, Mbunge wa Dar es salaam mwingine naye kasimama. Mheshimiwa Dorothy Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, ni lini sasa Serikali itatuletea fedha za kujenga chumba cha maiti na jengo la *emergence* katika Kituo cha Malawi katika Kata ya Vituka ukizingia sasa Temeke hospitali ni ya kimkoa na si kituo tena.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba huduma zote za msingi zinapatikana katika maeneo ya vituo vya huduma ikiwemo majengo haya ya *mortuary* na majengo ya dharura. Ndiyo maana mwaka 2022 majengo ya dharura zaidi ya 80 yamejengwa, majengo ya *ICU* yamejengwa.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo, naomba nitumie fursa hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutafanya tathimini ya majengo hayo tujue gharama zake lakini pia tuone mapato ya ndani yatachangia kiasi gani na Serikali kuu itachangia kiasi gani. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawaona lakini Mheshimiwa Naibu Waziri amekwishaulizwa maswali mengi sana. Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 5

**Ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto Kituo cha Afya Loliondo**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Jengo la Mama na Mtoto kwenye Kituo cha Afya – Loliondo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Loliondo ni moja ya Vituo vya Afya chakavu 199 vilivyoainishwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa ajili ya upanuzi. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati pamoja na kuongeza miundombinu mbalimbali ikiwemo majengo ya Mama na Mtoto yenye uwezo wa kutoa huduma ya upasuaji wa dharura. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa kituo hiki kinahudumia zaidi ya Kata tatu na wananchi wanalazimika kutembea zaidi ya kilometa kumi kutafuta huduma hizi za Mama na Mtoto.

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwenye Kituo cha Afya Loliondo ili basi ujenzi wa jengo la Mama na Mtoto liweze kujengwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, wananchi wa Kata ya Songoro katika Wilaya ya Meru wamejitolea kwa nguvu zao binafsi kujenga jengo la Kituo cha Afya hadi kufikia kwenye ngazi ya lenta.

Je, ni lini Serikali itawasaidia wananchi hawa kumalizia kituo hiki cha afya ambacho kitakwenda kuhudumia zaidi ya wananchi 10000? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Loliondo kinahudumia wananchi wengi wa ndani ya Kata tatu. Pia ni kweli kwamba wananchi wanalazimika kutembea umbali mrefu.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan ni kupunguza umbali wa wananchi kufuata huduma za afya. Ndiyo maana tayari kituo hiki cha Afya cha Loliondo kimeingizwa kwenye orodha ya vituo 199 vinavyotafutiwa fedha. Vile vile, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatoa kipaumbele kwenye kituo hiki cha afya ili kiweze majengo hayo.

Mheshimiwa Spika, pili, niwapongeze wananchi wa Kata ya Songoro Halmashauri ya Meru kwa kuanza kwa nguvu zao kujenga majengo ya Kituo cha afya. Tutakwenda kufanya tathmini kuona ni kiasi gani cha fedha kinahitajika ili tuweze kutafuta fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa kituo cha afya cha Songoro. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana.

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Ali Juma Mohamed Mbunge wa Shaurimoyo, sasa aulize swali lake.

Na. 6

**Nchi zilizofungua Ofisi Ndogo za Ubalozi Zanzibar**

**MHE. ALI JUMA MOHAMED** aliuliza: -

Je, kuna nchi ngapi zimefungua Ofisi Ndogo za Ubalozi Zanzibar?

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Balozi Mbarouk.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. BALOZI MBAROUK NASSOR MBAROUK)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri…*(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa ngoja ngoja. Hebu zima hata hii nafikiri haisikiki. Hebu rejea pale Ukajaribu kuwasha pale. Hata hii nafikiri haisikiki. Jaribu kuwasha.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. BALOZI MBAROUK NASSOR MBAROUK)**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya…

**SPIKA:** Haisikiki hata ya kwako?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. BALOZI MBAROUK NASSOR MBAROUK):** Haifanyi kazi. kwa niaba ya Waziri wa…

**MBUNGE FULANI:** *Hello, hello, hello.* Kwangu inafanya.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa endelea.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. BALOZI MBAROUK NASSOR MBAROUK):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, Mbunge wa Shaurimoyo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Agosti, 2023 jumla ya nchi tano zimefungua Ofisi Ndogo za Ubalozi (Konseli Kuu) Zanzibar. Nchi hizo ni; China, India, Msumbiji, Oman na Umoja wa Falme za Kiarabu *(UAE),* ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, swali la nyongeza.

**MHE. ALI JUMA MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina masuala mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2025 iliielekeza Serikali kuhakikisha inaongeza Ofisi ndogo za ubalozi kule Zanzibar lakini pia mashirika pamoja na taasisi za kimataifa.

Mheshimiwa Spika, suala la mwanzo nililokuwa nataka kujua. Je, kuna ofisi ngapi na mashirika mangapi ya kimataifa ambayo yamefunguliwa kule Zanzibar?

Mheshimiwa Spika, suala la pili, nilikuwa nataka kufahamu ni sababu zipi ambazo zimesababisha kufungwa kwa Ofisi ndogo ya Ubalozi wa Egypt kule Zanzibar? Ukizingatia, Egypt ni nchi ya mwanzo baada ya mapinduzi ya mwaka 1964 kutambua Mapinduzi ya Zanzibar. Pia, kipindi chote imekuwa ikiisaidia sana Zanzibar katika sekta ya elimu na kilimo. Je, ni sababu zipi zimesababisha Ofisi hii kufungwa ambayo iko takribani miaka 40 sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. BALOZI MBAROUK NASSOR MBAROUK):** Mheshimiwa Spika, mbali na Konseli kuu ambazo ziko Zanzibar lakini pia kuna ofisi za mashirika ya kimataifa hususani ya *UN* kama vile *UNDP, UNESCO, UN AIDS, UN WOMEN, FAO, ILO* na nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nchi ya Misri kufunga ubalozi wake mdogo Zanzibar. Katika ulimwengu wa kidplomasia, kufungua na

kufunga ubalozi ni suala la kawaida. Mara nyingi sababu zinazopelekea nchi kufunga ubalozi au ubalozi mdogo inakuwa kwanza ni kutetereka au kuharibika kwa mahusiano baina ya nchi na nchi. Pia, kubadilika kwa muelekeo wa nchi kistratejia na kimaslahi, pia kuna suala la usalama na mwisho kuna suala la uchumi katika kubana matumizi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Misri hawakueleza bayana sababu zilizosababisha kufunga ubalozi wao mdogo Zanzibar mwaka 2012. Vilevile naomba kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, mbali na Nchi ya Misri kufunga ubalozi wake hapo Zanzibar lakini uhusiano kati ya Misri na Zanzibar umeendelea kuimarika siku hadi siku. Pia, wanashirikiana katika katika masuala mbalimbali ya kimkakati kama vile kilimo na elimu. Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa…

*(Saa 4.05 Asubuhi na Bunge Lilisitishwa kwa muda kutokana na hitilafu katika vipaza sauti)*

*(Saa 4.35 Asubuhi Bunge Lilirejea)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMIO

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa kutokana na dharura tuliyoipata na muda wa maswali umekwisha, isipokuwa nimewaambia Waheshimiwa Wabunge maswali yote ya leo ambayo hayajajibiwa yatajibiwa kuanzia kesho mpaka Ijumaa yote tutayamaliza. Waziri wa Afya; Waziri wa Nishati. *(Makofi)*

## Azimio la Bunge kuhusu Wakala wa Kimataifa wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu *(International Renewable Energy Agency - IRENA)*

**NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI (MHE. DKT. DOTO M. BITEKO):** Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Kimataifa wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu *(International Renewable Energy Agency - IRENA)* ni taasisi iliyoanzishwa tarehe 26 Januari, 2009 na ilianza kazi rasmi mwaka 2011.

Kwa mujibu wa Mkataba wa *IRENA* ulioanzwa kutekelezwa Julai 2010 lengo la taasisi hiyo ni kuendeleza na kuhamasisha matumizi endelevu ya aina zote za nishati jadidifu kwa kuzingatia manufaa yanayotokana na nishati hiyo na mchango wake katika kuhifadhi mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kuimarisha upatikanaji wa nishati safi na salama na kuhakikisha kuwa upatikanaji wa nishati unakuwa wa gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu mwaka 2011 *IRENA* ilipoanza kutekeleza majukumu yake idadi ya nchi zilizoridhia mkataba huo zimeendelea kuongezeka kutoka nchi 85 hadi nchi 168 mwaka 2022 ambapo katika Ukanda wa Afrika Mashariki, nchi ya Kenya, Uganda, Rwanda zimejiunga na Ukanda wa *SADC* nchi ya Angola, Botswana, Comoro, Eswatini, Lesotho, Mauritius, Msumbiji, Namibia, Shelisheli, Afrika ya Kusini, Zambia na Zimbabwe na zenyewe zimejiunga. Tanzania ilisaini mkataba huo tarehe 15 Juni mwaka 2009, na kwa mujibu wa Ibara ya 19 ya mkataba huo Tanzania inatambuliwa kuwa mwanachama wa taasisi hiyo baada ya siku 30 toka kusainiwa kwa mkataba huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vya usimamizi wa utendaji wa *IRENA* vinahusisha mkutano mkuu *(assembly)* ambacho ndicho chombo cha juu cha maamuzi. Baraza la *IRENA* linaloundwa na wawakilishi kuanzia 11 hadi 21 kutoka wanachama waliochaguliwa na mkutano mkuu na sekretarieti inayoongozwa na Mkurugenzi Mkuu na watumishi wengine wa *IRENA*. Bajeti ya uendeshaji wa taasisi hiyo inatokana na michango ya lazima na michango ya hiari inayotoka kwa wanachama pamoja na vyanzo vingine. Aidha, bajeti hiyo huandaliwa na sekretarieti kwa

kuwasilishwa kwenye Baraza la *IRENA* na uchambuzi hufanyika kwenye mkutano mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba wa *IRENA* unabainisha majukumu mbalimbali ya taasisi hiyo yanayolenga kuleta manufaa kwa wanachama wake kupitia nishati jadidifu ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri wa kisera kwa kujenga uwezo kupitia mafunzo, teknolojia, elimu na kubadilishana ujuzi pamoja na utafiti. Kuwezesha vilevile upatikanaji wa rasilimali fedha zitakazoendeleza miradi ya nishati jadidifu pamoja na kuwezesha upatikanaji wa taarifa muhimu za uendelezaji wa nishati hiyo jadidifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba wa Taasisi ya Kimataifa ya Nishati Jadidifu *(IRENA)* kwa mwaka 2009 una jumla ya Ibara 20 kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Kwanza inahusisha kuanzishwa kwa taasisi hiyo. Ibara ya Pili ina malengo ya taasisi hiyo, Ibara ya Tatu ni tafsiri ambapo Ibara hii inahusu tafsiri ya vyanzo mbalimbali vya nishati jadidifu ikiwemo nishati ya tungamo taka, jotoardhi, maporomoko ya maji, jua, upepo na mawimbi ya bahari. Ibara ya Nne ni majukumu ya *IRENA*, Ibara hii inafafanua kuhusu majukumu ya *IRENA*, majukumu hayo ni pamoja na kufanya uchambuzi wa masuala ya kisera, uwekezaji, uzoefu na teknolojia kwa lengo la kutoa ushauri mahsusi kwa wanachama katika kuendeleza nishati jadidifu katika nchi zao. Kuwajengea uwezo wanachama katika kusimamia na kuendeleza nishati jadidifu kupitia elimu na mafunzo, teknolojia, masuala ya ubora, ubadilishanaji wa taarifa za utafiti na ujuzi; kusaidia upatikanaji wa fedha za kuendeleza miradi ya nishati jadidifu na kuwezesha upatikanaji wa taarifa za nishati kwa viwango vya Kimataifa. Ibara hii inaielekeza *IRENA* kuwasilisha taarifa za mwaka za utekelezaji kwa majukumu yake kwa wanachama wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Tano ni mpango kazi na Ibara ya Sita ni Ibara inayoonyesha uanachama wa *IRENA*. Ibara hii inaelekeza utaratibu na kanuni za wanachama wa *IRENA* ambapo ili nchi iweze kuwa mwanachama inapaswa kuwa mwanachama wa Umoja wa Mataifa au Taasisi ya Ushirikiano wa

Kiuchumi wa Kikanda. Nchi au taasisi hizo zinazokuwa mwanachama wa *IRENA* kwa kusaini mkataba wa kuanzishwa kwake na kuwasilishwa kwa muhifadhi wa hati na kuridhiwa na mkataba huo au wanachama wapya kwa kuwasilisha hati ya kuridhia mkataba baada ya maombi ya kujiunga uanachama kukubaliwa. Jumuiya ya Ushirikiano wa Kikanda kama vile *SADC*, Afrika Mashariki, *ECOWAS*, *EU* zinaweza kupatiwa uanachama wa kutambua kazi zao kwa kuhusiana na malengo ya *IRENA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Saba ni wanachama wasiokuwa na turufu *(observers)*. Ibara hii inaelezea nchi na taasisi ambazo siyo wanachama wanaoweza kushiriki katika masuala ya *IRENA*. Aidha, taasisi zinazopaswa kuwa na asasi za kiraia zinazojishughulisha na masuala ya nishati jadidifu, nchi iliyosainiwa na mkataba na kuanzishwa kwa *IRENA* lakini bado haijaridhia mkataba huo na nchi hiyo inayosubiri kupatiwa uanachama baada ya kukamilisha taratibu zote za kujiunga na *IRENA*. Aina hii ya wanachama wanaweza kushiriki katika vikao vya *IRENA* ikiwemo mkutano mkuu bila kuwa na haki ya kupiga kura

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 8 ni muundo wa *IRENA,* ambayo inaeleza vyombo au *organs* muhimu za *IRENA*, ambavyo ni mkutano mkuu, baraza la sekretarieti; mkutano mkuu wa baraza vinaweza kuunda chombo mahsusi cha kutekeleza kazi zao kulingana na mkataba kwa ridhaa ya mkutano mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Tisa ni mkutano mkuu na Ibara 10 inaeleza juu ya baraza; na Ibara ya 11 inaeleza juu ya sekretarieti ambapo inaeleza muundo na majukumu ya Sekretarieti ya *IRENA* ambapo Mkurugenzi Mkuu ndio Msimamizi Mkuu wa masuala ya utawala, rasilimali na shughuli za kila siku za taasisi. Sekretarieti pamoja na mambo mengine ina jukumu la kuandaa la kuwasilisha kwenye baraza rasimu ya mpango kazi wa bajeti ya taasisi, kutekeleza mpango kazi na maamuzi, kuandaa na kuwasilisha kwenye baraza rasimu ya taarifa ya shughuli za taasisi na kuratibu mawasiliano kati ya taasisi pamoja na wanachama wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 12 inahusiana na bajeti. Ibara hii inaeleza vyanzo vya fedha vya kugharamia utekelezaji wa majukumu ya *IRENA*. Vyanzo hivyo vinajumuisha michango ya wanachama kulingana na kikokotoo cha Umoja wa Mataifa, michango ya hiari na vyanzo vingine. Rasimu ya bajeti itaandaliwa na sekretarieti na kuwasilishwa kwenye Baraza la *IRENA* kwa uchambuzi kabla ya kuwasilishwa na baraza katika mkutano mkuu kwa ajili ya kujadili na kuidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 13 utu kisheria na haki na kinga. Ibara hii inaelezea utu wa kisheria, haki na kinga kwa taasisi kwa kutumia sheria za ndani za nchi wanachama wakati wa utekelezaji wa shughuli zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 14 ni uhusiano na taasisi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 15 marekebisho, kujitoa na mapitio. Ibara hii inaelezea taratibu za kufanya marekebisho, mapitio na kujitoa katika Mkataba wa *IRENA*. Marekebisho ya mkataba yanaweza kupendekezwa na nchi wanachama au mwanachama yeyote na Mkurugenzi Mkuu atawasilisha mapendekezo ya marekebisho yaliowasilishwa kwa angalau siku 90 kabla ya kujadiliwa kwenye mkutano mkuu. Mwanachama yeyote anaweza kujitoa uanachama kwa kutoa *notice* ya maandishi kwa muhifadhi wa hati ya mkataba ambaye ataliarifu Baraza la *IRENA* na wanachama wote kuhusu kusudio hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 16 inahusu usuluishi wa migogoro. Ibara hii inaelezea namna ambavyo wanachama watakavyosuluhisha migogoro inayoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa Mikataba ya *IRENA*. Ibara hii inaweza kuwa mgogoro wowote unaohusu tafsiri ya mkataba, kusuluhishwa kwa njia ya amani kulingana na kanuni na taratibu za mkataba wa mataifa. Aidha, Baraza la *IRENA* linaweza kuhusishwa katika utatuzi wa mgogoro baina ya wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 17 inaongelea juu ya kusitisha haki ya kusitisha kwa muda. Ibara hii inaelezea masuala

ambayo yanaweza kusababisha kusitishwa kwa haki ya mwanachama kupiga kura katika maamuzi ya IRENA. Mwanachama atakayekuwa na malimbikizo ya mchango ya wanachama hatakuwa na haki ya kupiga kura endapo malimbikizo hayo yatakuwa yanafikia au kuzidi kiasi kilichopaswa kuchangiwa kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita. Aidha, Ibara hii inaeleza kuwa mkutano mkuu unaweza kumruhusu mwanachama kuwa na haki ya kupiga kura baada ya kujiridhisha kuwa malimbikizo hayo yote yako nje ya uwezo wa mwanachama husika. Pia mwachama yeyote atakayeendelea kukiuka matakwa ya mkataba au makubaliano yoyote anaweza kusitishiwa haki ya uanachama wa mkutano mkuu kwa kupigiwa kura na theluthi mbili ya wajumbe wa mkutano kulingana na mapendekezo ya baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 18 ni makao makuu ya taasisi ambapo Ibara hii inaeleza mahali ambapo patakuwa makao makuu ya *IRENA* ambapo mkutano mkuu wa kwanza utaamua mahali makao makuu yatakapokuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 19, kujiunga na kuridhia Mkataba wa *IRENA*. Ibara hii inaelezea utiaji saini, kuridhiwa na kuanza kutumika kwa mkataba. Mkataba huu uko wazi kwa nchi wanachama ambapo ni wanachama wa Umoja wa Mataifa na taasisi za ushirikiano wa kiuchumi wa kikanda. Nchi nyingine za taasisi za ushirikiano wa kiuchumi kikanda ambazo hazijajiunga na taasisi hiyo zitaridhia mkataba huu baada ya maombi ya uanachama kuidhinishwa na mkutano mkuu. Utekelezaji wa mkataba huu utaanza siku 30 baada ya nchi mwanachama wa 25 kuwasilisha mkataba ulioridhiwa. Kwa nchi au taasisi za ushirikiano wa kikanda zitakazoridhia mkataba huu baada ya kuanza utekelezaji wa mkataba. Mkataba utaanza kutumika baada ya siku 30 ya kuwasilisha hati ya kuridhia mkataba kwa muhifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 20 ni muhifadhi, usajili na uhalali wa nyaraka. Ibara hii inaelezea pamoja na mambo mengine kuhusu nchi itakayokuwa muhifadhi wa mkataba, taratibu za kusajili masuala mengine yanayohusiana na mkataba. Ibara hii inaeleza kuwa Nchi ya Ujerumani ndio itakayokuwa muhifadhi wa mkataba utasajiliwa na Serikali ya nchi muhifadhi

kulingana na kifungu cha 102 cha mkataba wa kimataifa. Lugha ya mkataba itakuwa Kiingereza na nyaraka zitahifadhiwa katika ofisi za mtunzaji nyaraka za kumbukumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wajibu wa nchi baada ya kujiunga; endapo mkataba huu utaridhiwa, wajibu wa nchi utakuwa ni pamoja na kulipa michango ya ada ya uanachama kila mwaka ambao ni ndogo na inayozingatiwa na uwezo wa nchi kiuchumi kulingana na nchi moja kwenda nchi nyingine pamoja na kushiriki katika utekelezaji wa shughuli za kitaasisi ikiwemo mikutano mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera, mipango na sheria mbalimbali kuhusu uendelezaji wa nishati jadidifu nchini. Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2015 inatambua kuwa rasilimali kubwa ya nishati jadidifu iliyopo nchini ni pamoja na upepo, jua, tungamo taka, maporomoko madogo ya maji, jotoardhi na mawimbi ya bahari. Sera inafafanua kuhusu changamoto zinazokabili utekelezaji wa rasilimali hizo ikiwa ni pamoja na ukosefu wa mitaji kwa kuzingatia gharama kubwa zinazohitajika katika uwekezaji. Uhaba wa takwimu, teknolojia pamoja na gharama kubwa za uwekezaji zinazohitaji fedha nyingi katika kuwekeza. Sera imeweka lengo linalojikita katika kuimarisha mchango wa nishati jadidifu katika uzalishaji wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Umeme ya mwaka 2008 inatoa mwongozo wa kisheria wa uwekezaji katika nishati jadidifu na kwa upande wa mpango kabambe wa uendelezaji wa sekta ndogo ya umeme ya mwaka 2012 iliyorekebishwa mwaka 2020. Mpango huu umelenga kuzalisha megawati 800 sawa na asilimia 3.96 kutokana na upepo. Megawati *715* sawa na asilimia 3.54 kutokana na umeme wa jua na *megawatt 995* sawa na asilimia 4.93 kutokana na jotoardhi ifikapo mwaka 2044. Vilevile kwa sasa unaandaliwa Mkakati wa Taifa wa Nishati Jadidifu *(The National Renewable Energy Strategy)* unaolenga kuimarisha uendelezaji wa nishati jadidifu nchini ili zichangie ipasavyo katika uendelezaji wa sekta ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kutokana na mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea hapa duniani pamoja na uharibifu mkubwa wa mazingira. mwelekeo wa dunia kwa sasa ni kuimarisha matumizi ya nishati jadidifu kama chanzo cha nishati. Kuridhiwa kwa Mkataba wa *IRENA* kutachangia katika kufikiwa kwa malengo ya kisera, mikakati na mipango mbalimbali wa kitaifa na ya kimataifa kwa kuzingatia malengo na majukumu ya Taasisi ya *IRENA*. Mkataba huu hauzuii nchi kuendeleza vyanzo vyake vingine vya nishati ikiwemo mafuta, gesi asilia, makaa ya mawe; bali inahimiza kuwepo kwa vyanzo vingi mchanganyiko *(energy mix)* kwa lengo la kuwezesha kuhakikisha uendelevu na upatikanaji wa nishati kwa maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendeleza nishati jadidifu zilizopo hapa nchini hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwemo kuanzishwa kwa Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Nchini *(Tanzania Geothermal Development Company Limited),* kufanya tathmini ya gharama za uzalishaji kutokana na maporomoko madogo ya maji *(small hydro)* ili kuhakikisha bei ya wazalishaji wa umeme inavutia wawekezaji. Kuhakikisha viwanda vinavyozalisha taka kama vile vya sukari kuwekeza kwenye uzalishaji wa umeme, kufanya upembuzi yakinifu na tahmini kwa ajili ya kuzalisha umeme wa upepo na jua; kuweka mfumo na utaratibu wa kuwashindanisha waendelezaji wa miradi, kuchanganya miradi ya nishati jadidifu kwa kuwezesha kupitia majukwaa mbalimbali ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kuna wazalishaji mbalimbali wa umeme wa nishati jadidifu wenye leseni za kuzalisha umeme huo ikiwemo Kiwanda cha *TPC* Moshi, *NextGen Solarwazi* Kigoma pamoja na miradi mingine tuliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuridhiwa kwa mkataba huu kutakuwa na manufaa yafuatayo: -

(i) Kwanza kuimarisha mchango wa nishati jadidifu katika uzalishaji wa nishati ya umeme hapa nchini.

(ii) Nchi kupata taarifa na takwimu sahihi kuhusu masuala ya nishati jadidifu na pia fursa za uwekezaji katika nishati jadidifu zilizopo Nchini.

(iii) Kuimarisha utaalam, teknolojia, utafiti, uelewa kuhusu nishati jadidifu kwa watoa maamuzi na wadau mbalimbali wa nishati.

(iv) Pia kuimarisha uwekezaji wa mitaji, upatikanaji na ushauri wa kiufundi katika kuendeleza kwa nishati jadidifu.

(v) Kupungua kwa uharibifu wa mazingira unaotokana na uzalishaji wa nishati jadidifu na nishati isiyokuwa rafiki kwa mazingira na pia kukabiliana na mabiliko ya tabianchi.

(vi) Kuimarisha upatikanaji wa nishati ya gharama nafuu na rafiki kwa mazingira ambayo ni kichocheo cha ukuaji wa uchumi hapa nchini.

(vii) Kuchochea kasi ya kufikiwa kwa malengo na shabaha ya Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2015, Malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020, Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Umeme ya Mwaka 2020 na Shabaha ya Lengo Namba Saba la Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ya Mwaka 2030 inazozitaka nchi kuhakikisha kuwa upatikanaji wa nishati ya uhakika, endelevu na ya kisasa yenye gharama nafuu kwa watu wake;

(viii) Kuimarisha kasi ya utekelezaji wa mwelekeo wa dunia kwa sasa kuhusu matumizi ya vyanzo vya nishati vinavyoathiri mazingira na kusababisha mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya awali, naomba kwa sasa niwasilishe Azimio hili la kuridhia Tanzania kujiunga na Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu *(Statute of the International Renewable Energy Agency - IRENA)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 60(6)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Azimio la Bunge kuhusu Mapendekezo ya Tanzania Kuridhia Kujiunga na Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu wa mwaka 2009 *(IRENA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitia masharti ya Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu wa Mwaka 2009, Kamati imejiridhisha kuwa masharti yake yanahitaji Mkataba huu kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge. Lengo la Mkataba huu ni kuanzisha Wakala au Taasisi ambayo itahusika na kuendeleza na kuhamasisha matumizi ya aina zote za nishati jadidifu katika Nchi Wanachama kwa kuzingatia vipaumbele vya Taifa husika. Kupitia malengo haya kutakuwa na faida mbalimbali ikiwemo kukabiliana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonyesha kuwa tangu Mkataba huu ulipoanza kutumika rasmi mwezi Julai, 2010, kumekuwa na ongezeko la nchi zinazosaini na kuridhia kutoka nchi 85 mwaka 2011 hadi kufikia nchi 168 mwezi Oktoba, 2023 na Umoja wa Ulaya kama inavyoonekana katika kielelezo namba moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wa Mkataba, Kamati ilipenda kujiridhisha kuhusu baadhi ya masuala kwa lengo la kupata uelewa ili kuepuka au kukabiliana na changamoto zozote zinazoweza kutokea baada ya kuridhia Mkataba huu. Maelezo au masuala hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Sababu zilizopelekea kuchelewa kuwasilishwa kwa Mkataba wa Wakala wa *IRENA* ili uridhiwe na Bunge. Tanzania ilisaini Mkataba huu mwaka 2009 na sasa ni takribani miaka 14 imepita. Kamati ilipata wasiwasi kuhusu suala hili na hivyo kutaka kujiridhisha kuhusu sababu zilicholewesha ama hasara au faida ya kuchelewa. Serikali ilieleza sababu mbalimbali ikiwemo ya kujipa muda wa kutosha kabla ya kuamua kuridhia Mkataba huu.

Kamati ilielezwa kuwa kwa muda huo wote Serikali imekuwa ikishiriki kazi za *IRENA* ikiwemo kuhudhuria mikutano ya *IRENA* kama mwangalizi *(observer)* kwa mujibu wa Ibara ya 7 ya Mkataba huu na kupitia hili, Kamati imejiridhisha vya kutosha kuwa kuridhia Mkataba huu kuna faida nyingi kiasi kwamba ni vigumu kuona kama kuna hasara yoyote; kwa sababu hiyo, Kamati ilikubaliana na majibu ya Serikali;

(b) Nafasi ya matumizi ya vyanzo vya nishati zisizokuwa jadidifu ikiwemo makaa ya mawe, gesi na mafuta ikiwa nchi itaridhia Mkataba huu. Nchi yetu ina rasilimali nyingi za makaa ya mawe, gesi asilia na fursa za mafuta. Kamati kwa kutambua hili ilipata wasiwasi kuhusu kuridhia Mkataba huu ambao unaunda taasisi ambayo inahamasisha na kuendeleza matumizi ya nishati jadidifu peke yake. Hata hivyo, Serikali ilieleza kuwa kuridhia Mkataba huu hakupelekei kuacha kutumika kwa nishati zingine au nyingine kwa kuwa hakuna ibara yoyote ya Mkataba inayopinga au kuelezea matumizi ya nishati zisizo jadidifu hivyo kuridhia kwa Mkataba huu hakuathiri mipango na miradi ya makaa ya mawe, miradi ya gesi na miradi ya mafuta iliyopo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilielezea Kamati kuwa Mkataba huu unaanzisha taasisi pekee ambayo itatekeleza kazi zake kwa kuzingatia vipaumbele vya Taifa husika. Hivyo basi, hakuna adhabu zaidi ya zile zilizoainishwa kwenye Mkataba huu. Pia Serikali ilieleza kuwa Mkataba huu ni wa hiari na nchi ina uwezo wa kujitoa pale ambapo itaona kuna haja ya kufanya hivyo bila

hata kutoa sababu ya kujitoa. Kwa sababu hiyo, Kamati ilikubaliana na majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa maudhui ya Mkataba kwa kuwianisha na mwelekeo wa nchi katika suala la nishati jadidifu. Kamati ilipata fursa ya kupitia mambo mbalimbali yanayoweka mtazamo wa nchi katika Sekta Ndogo ya Nishati Jadidifu kwa lengo la kupima ikiwa maudhui ya Mkataba yanaendana na mtazamo wa nchi kwa ujumla. Katika maelezo hayo yote, Kamati imebaini kwamba yanaendana na Mkataba huu na baadhi ya mambo hayo ni haya yafuatayo:-

(i) Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025 kipengele namba 63(a) na (m) cha Ilani hii ya Chama cha Mapinduzi vimeeleza lengo la kuongeza uzalishaji na uwezo wa uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya nishati jadidifu *(renewable energy)* ikiwemo miradi ya umeme jua, jotoardhi na upepo hadi kufikia *megawatt* 1100. Hata hivyo kufikia mwezi Agosti, 2023 umeme umezalishwa kwa nchi kupitia nishati jadidifu takribani *megawatt* 585.1, sawa na 53.2% ya lengo. Kwa sababu hii, kunahitajika juhudi za makusudi ili kufikia lengo la kuwa na *megawatt* 1100;

(ii) Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2015. Kipengele cha 3.1(iii) cha Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015 kinahamasisha matumizi ya nishati jadidifu ili kuchangia uzalishaji wa umeme hapa nchini;

(iii) Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Kipengele cha 5.4.6 cha Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (2021/2022 – 2025/2026) kinasisitiza uimarishaji wa mifumo ya utunzaji wa mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali asilia ikiwemo pamoja na kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu. Aidha, kipengele cha 5.4.11 kinaelezea kuboresha mazingira wezeshi ya uwezeshaji wa Sekta Binafsi kwa kuhamasisha na kuendeleza teknolojia ya miradi ya nishati jadidifu;

(iv) Malengo ya Wizara ya Nishati; uchambuzi wa Kamati umeenda mbali zaidi na kuangalia malengo ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara ya Nishati imejiwekea malengo nane ambapo lengo la pili ni la kuongeza mchango wa nishati jadidifu na mbadala katika matumizi mbalimbali ya nishati ambapo zaidi ya kiasi cha shilingi trilioni 1.5 kimeidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kama inavyoonekana katika taarifa ya Kamati ukurasa wa 24 hadi 25;

(v) Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa. Katika Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa, lengo namba 7 linasisitiza Nchi Wanachama kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa nishati ya kisasa na gharama nafuu inayotegemewa na endelevu kwa watu wote. Ili kufikia lengo hili, *United Nations* inayo mikakati mbalimbali ikiwemo kukuza ushirikiano wa Kimataifa katika utafiti na teknolojia ya nishati safi ikiwemo nishati mbadala ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kuwa *IRENA* ni mojawapo ya taasisi za Umoja wa Mataifa, ni dhahiri kuwa kuna uwezekano mkubwa wa Umoja wa Mataifa kuitumia taasisi hii katika kufanikisha malengo yake. Hivyo basi ikiwa Tanzania imejiunga na taasisi hii, inajiweka katika nafasi nzuri ya kunufaika na malengo ya Umoja wa Mataifa katika Sekta ya Nishati Jadidifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kamati. Kutokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati kwa kuzingatia matakwa ya Ibara ya 63(3)(e)…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa umebakiwa na dakika mbili.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**…ya Katiba ya mwaka 1977, Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

(a) Uendelezaji wa matumizi ya nishati zisizo jadidifu nchini; Kamati inasisitiza Serikali ihakikishe kuwa, kuridhiwa kwa

Mkataba huu siyo kifungo ambacho kitazuia matumizi ya nishati nyingine; *(Makofi)*

(b) Kuzalisha wataalam wa kutosha. Wataalamu tuliowaona ni wachache kwa hiyo Serikali tumeishauri kwamba iweze kuunganisha baadhi ya vyuo vingine kama kile cha kiteknolojia kile cha Mbeya ili tuweze kuongeza wataalam wa kutosha kuhusiana na suala la nishati jadidifu;

(c) Serikali iweze kutumia Sekta Binafsi ili iweze kusaidia katika kuendeleza nishati jadidifu;

(d) Serikali vile vile iweze kuongeza bajeti ili iweze kukidhi au kuhudumia miradi ile ambayo inaendeleza nishati jadidifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta Binafsi imeshiriki na wadau mbalimbali na tumepokea maoni. Kwa hiyo tunapenda kusema kwamba Kamati hii imetambua juhudi za Serikali katika kuendeleza nishati jadidifu ikiwa ni pamoja na kuwa katika mchakato wa kuandaa mkakati wa kuendeleza nishati jadidifu na Kamati inashauri Wizara kuhakikisha inakamilisha mkakati huu kama ilivyopangwa na kuhakikisha inasimamia *program* za nishati safi ya kupikia na matumizi sahihi ya nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; kwa mara nyingine napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii, lakini naomba majina yao yote yaingie kwenye ripoti, napenda kuishukuru Sekretarieti yetu kwa kutusaidia katika kufanya kazi pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii vilevile kuwashukuru wadau wote ambao wamewezesha kutuandalia na kushirikiana pamoja kuandaa maoni haya. Nawashukuru pia Watumishi wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa hoja; kwa mamlaka ambayo Bunge limepewa kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, naomba sasa lijadili na kuridhia Azimio la Bunge kuhusu

mapendekezo ya Tanzania kuridhia kujiunga na Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu wa mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KUHUSU AZIMIO LA BUNGE KUHUSU MAPENDEKEZO YA TANZANIA KURIDHIA KUJIUNGA NA MKATABA WA WAKALA WA KIMATAIFA WA NISHATI JADIDIFU WA MWAKA 2009 *(STATUTE OF THE INTERNATIONAL RENEWABLE ENERGY AGENCY – IRENA)* KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

**----------------**

*[Yanawasilishwa kwa Mujibu wa Kanuni ya 60(6)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]*

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1 Maelezo ya Awali**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 60 (6) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Azimio la Bunge kuhusu Mapendekezo ya Tanzania kuridhia kujiunga na Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu wa Mwaka 2009 (Statute of the International Renewable Energy Agency -IRENA).

**Mheshimiwa Spika**, uwasilishaji wa maoni haya umezingatia masuala mbalimbali kwanza; majukumu ya msingi ya Kamati kama ilivyoainishwa kwenye Kifungu cha 7(1)(c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.[1] Pili, uwasilishaji wa maoni haya ni utekelezaji wa jukumu la Kikatiba ambalo Bunge limepewa kama chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano kwa niaba ya wananchi katika kuisimamia na kuishauri

[1] 7.-(1) Majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta yatakuwa yafuatayo: (b) kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake. Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, imelipatia Bunge mamlaka ya kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa. Baada ya kupitia masharti ya Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu wa Mwaka 2009 (IRENA), Kamati imejiridhisha kuwa masharti yake yanahitaji Mkataba huu kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge hili.

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 107(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, imeorodhesha mambo nane (8) muhimu yanayohitaji kuelezwa na Wizara inayohusika katika hoja ya Kuridhia Mkataba wa Kimataifa. Mambo hayo ni:

(i) Jina la Mkataba na Mwaka;

(ii) Maudhui ya Mkataba;

(iii) Wajibu wa nchi baada ya kujiunga na mkataba unaohusika;

(iv) Uzingatiaji wa Katiba;

(v) Uzingatiaji wa Sera za Nchi;

(vi) Manufaa na Athari kama zipo ambazo nchi itapata kwa kujiunga;

(vii) Mapendekezo ya kutokuridhia baadhi ya masharti kama itaonekana hivyo; na

(viii) Jambo lingine lolote lenye tija kuhusiana na mkataba huo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kusoma na kujadili kwa kina Azimio lililowasilishwa na Wizara ya Nishati ya kuliomba Bunge kuridhia Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu wa Mwaka 2009 (IRENA) ili kuona kama mambo yote nane (8) yamezingatiwa ipasavyo. Baada ya kupitia Azimio lililobeba hoja iliyowasilishwa, Kamati ilibaini kuwa mambo yote nane (8)

yalikuwepo kwenye Azimio linalojadiliwa na ndiyo yalikuwa miongoni mwa vigezo vya uchambuzi katika mchakato wa kuridhia Mkataba huu.

**1.2 Kamati ilivyotekeleza kazi ya Uchambuzi wa Mkataba**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia mamlaka yako yaliyoainishwa kwenye Kanuni ya 108(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, uliileta hoja ya kuridhia Mkataba huu kwenye Kamati ya Nishati na Madini ili iweze kufanyiwa kazi. Katika kushughulikia Mkataba huu, na kwa kuzingatia Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitekeleza kazi ya kuchambua hoja pamoja na mkataba husika kama ifuatavyo:

(a) Tarehe 17 Oktoba 2023, Kamati ilipokea na kujadili Uchambuzi wa Sekretarieti kuhusu Dhana ya Nishati Jadidifu pamoja na Uchambuzi wa kisheria kuhusu maudhui ya kila Ibara ya Mkataba huu.

(b) Tarehe 18 Oktoba, 2023, Kamati ilikutana na Wizara ya Nishati kwa ajili ya kupokea maelezo ya Serikali kuhusu Mkataba huu. Aidha, Kamati ilichambua na kujadili kwa lengo la kupata ufafanuzi wa hoja mbalimbali zinazohusu Mkataba huu.

(c) Baada ya kupokea dhana, uchambuzi wa kisheria na maelezo ya Serikali, Kamati ilipokea na kujadili maoni ya wadau katika Mkutano wa maoni *(Public Hearing)* uliofanyika tarehe 19 Oktoba, 2023 ili kutimiza masharti ya Kanuni ya 108 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika Mkutano huo, Kamati ilipokea maoni kutoka Jumuiya ya Nishati Jadidifu Tanzania (TAREA) na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inawashukuru kwa dhati wadau hao kwa maoni yao ambayo kwa sehemu kubwa yameisaidia Kamati katika uchambuzi wa Mkataba huu. Baada ya maoni ya wadau, uchambuzi wa Sekretarieti na wasilisho la Serikali kuhusu Mkataba huu, Kamati ilikuwa na hoja mbalimbali kuhusu mkataba huu ambazo zilihitaji majibu ya Serikali. Kufuatia hoja hizo, tarehe 20

Oktoba 2023, Kamati ilikutana na Serikali kwa ajili ya kufanya majumuisho ya hoja zilizoibuliwa na Kamati kuhusu Mkataba huu.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa Mkataba huu kwa kuangalia masuala yafuatayo:-

(a) Chimbuko kuhusu Nishati jadidifu;

(b) Chimbuko la Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu (IRENA);

(c) Uchambuzi wa vifungu vya Mikataba;

(d) Hoja za Kamati kuhusu Mkataba huu; na

(e) Upembuzi wa Maudhui ya Mkataba kwa kuwianisha na mwelekeo wan chi katika suala la Nishati Jadidifu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa masuala yote haya kwa kuyahusianisha na nishati na hususan sekta ndogo ya nishati jadidifu nchini kisha kuyazingatia katika uchambuzi wa Mkataba kama ifuatavyo:-

### 2.1 Chimbuko la Nishati Jadidifu

**Mheshimiwa Spika,** Nishati Jadidifu ilianza takribani miaka 2000 iliyopita. Maandiko mengi likiwemo Jarida la Nishati Jadidifu (Renewable Energy Journal) yanaonesha kuwa matumizi ya nishati jadidifu yalianzia barani Ulaya.

**Mheshimiwa Spika**, Jarida hili na maandiko mengine yanaeleza kuwa nishati jadidifu ilianza kutumika Ulaya zaidi ya miaka 2,000 iliyopita kwa kuzungusha magurudumu ya maji ili kupata umeme. Aidha, kadri miaka ilivyozidi kusogea, aina mbalimbali za nishati nyingine jadidifu ikiwemo nishati itokanayo na nguvu ya upepo inasemekana ilivumbuliwa nchini uholanzi mwaka 1590.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa zinaeleza kuwa, kufikia Mwaka 2016, iligundulika kwamba kuna takriban mitambo ya upepo na jua 341,320 inayofanya kazi duniani kote na kwamba, sekta hiyo duniani ilichangia ajira 1,555,000 mwishoni mwa 2016.

**Mheshimiwa Spika**, Jarida Maarufu la nchini Amerika lijulikanalo ***The Wall Street Journal*** kwenye andiko lake linaloitwa ***Going Green: A brief History of Renewable Energy*** la tarehe 25 April 2022, inaelezwa kuwa, wakati upepo umekuwa ukitumika karne nyingi katika kuendesha meli, hata hivyo ni mpaka Mwaka 1800 ndipo upepo, maji na mwanga wa jua vilianza kutumika kuzalisha umeme.

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania ikiwa ni nchi ambayo inaunga mkono na kuendeleza jitihada za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi inazalisha umeme kutokana na nishati jadidifu na hususan kutokana na maji kwa **asilimia 31.54 (574.60 MW)** na Tungamotoka kwa **asilimia 0.58 (10.50MW).** Aidha, Tanzania imebarikiwa vyanzo vingi vya nishati jadidifu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla matumizi ya nishati jadidifu duniani yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka na yalianza zamani kama ilivyoelezwa kwenye majarida mbalimbali. Kwa sasa nchi nyingi zinatumia nishati jadidifu kutokana na faida zake za kiuchumi na kimazingira.


### 2.1 Chimbuko la Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu (IRENA) wa Mwaka 2009

**Mheshimiwa Spika,** Mkataba wa kuanzisha Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu (IRENA) ulianzishwa tarehe 26 Januari 2009. Mkataba huu unazihusu nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa na Mashirika ya ushirikiano wa kiuchumi wa kikanda. Tanzania ni miongoni mwa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa tangu tarehe 14 Desemba, 1961, na hivyo kama nchi mwanachama, ilisaini pia Mkataba huu mwaka 2009 na sasa umewasilishwa hapa Bungeni ili uweze kuridhiwa.

**Mheshimiwa Spika,** lengo la Mkataba huu ni kuanzisha Wakala au taasisi ambayo itahusika na kuendeleza na kuhamasisha matumizi ya aina zote za nishati jadidifu katika nchi wanachama kwa kuzingatia vipaumbele vya taifa husika. Kupitia malengo haya, kutakuwa na faida mbalimbali ikiwemo kukabiliana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabia ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Taasisi ya IRENA pamoja na taarifa ya Serikali zinaeleza kuwa, mkataba huu ulianza kutekelezwa Mwezi Julai, 2010 baada ya idadi ya nchi zinazotakiwa kuridhia kuanza kutumika kwa mkataba huu kufikia idadi inayotakiwa kisheria. Aidha, kufuatia kukidhi matakwa hayo, Taasisi ya IRENA ilianza kutekeleza rasmi majukumu yake mwezi Aprili, 2011. Takwimu zinaonesha kuwa, tangu Mkataba huu ulipoanza kutumika rasmi mwezi Julai, 2010, kumekuwa na ongezeko la nchi zinazosaini na kuridhia kutoka nchi 85 mwaka 2011 hadi kufikia nchi 168 Mwezi Oktoba, 2023 na Umoja wa Ulaya (EU) kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na.1**.

**KIELELEZO NA. 1: WANACHAMA WA IRENA**




*Chanzo: Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu (IRENA)*

**Mheshimiwa Spika**, Baadhi ya nchi za Afrika Mashariki ambazo zimesaini na kuridhia Mkataba huu ni pamoja na Kenya, Uganda na Rwanda.  Kwa upande wa Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara ni Angola, Botswana, Msumbiji na Zambia.

## 2.2 Uchambuzi wa Vifungu vya Mkataba

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua Ibara zote ishirini (20) za Mkataba wa IRENA kwa lengo la kujiridhisha na maudhui yake. Maudhui ya Ibara hizo zinaeleza yafuatayo:-

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya I inaanzisha Taasisi ya Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu ambayo kwa kifupi inajulikana kwa jina la IRENA. Ibara hii inaeleza kuwa, taasisi hii itazingatia kanuni za usawa, haki za uhuru wa nchi na uwezo wa wanachama katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya II ina masharti yanayohusu malengo ya kuundwa kwa Wakala (IRENA). Kwa ujumla lengo lake kuu ni kuhamasisha na kuongeza matumizi endelevu ya vyanzo vyote vya nishati jadidifu pamoja na mchango wake katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya III inaeleza maana ya nishati jadidifu kuwa ni aina zote za nishati zinazozalishwa kutokana na vyanzo vya nishati ya kibaiolojia, jotoardhi, maji, Bahari ikijumuisha mawimbi na jotoardhi, jua na upepo. Kamati ilibaini kuwa, katika vyanzo vya nishati jadidifu, nishati itokanayo na makaa ya mawe, gesi na mafuta sio sehemu ya nishati jadidifu.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya IV inaeleza majukumu na wajibu mbalimbali wa Wakala. Majukumu hayo ni pamoja na kuchambua, kufuatilia na kuweka mfumo wa matumizi ya nishati jadidifu kwa kujumuisha vyombo vya sera, motisha, mbinu za uwekezaji, mazoea bora, teknolojia iliyopo, vifaa na changamoto zake. Kazi nyingine ni kutoa ushauri na usaidizi wa sera kwa wanachama wake, kuwajengea uwezo wanachama wake kwa njia ya mafunzo na kuwashauri wanachama kuhusu ufadhili wa nishati jadidifu.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya V inaeleza kuwa IRENA itatekeleza kazi zake kwa kuzingatia mpango kazi wa mwaka uliopitishwa na Mkutano wa Wanachama wote (Mkutano Mkuu). Aidha, IRENA pia inaweza kutekeleza miradi iliyoanzishwa na kufadhiliwa na

wanachama kwa kuzingatia upatikanaji wa rasilimali zake zisizo za kifedha.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya VI inaeleza kuwa uanachama wa IRENA upo wazi kwa nchi ambazo ni wanachama wa Umoja wa Mataifa. Pia mashirika ya ushirikiano wa kiuchumi wa kikanda yanayoundwa na mataifa huru yanaweza kuwa wanachama baada ya kukidhi vigezo.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya VII inaweka masharti yanayohusu wanachama wenye haki ya kushiriki mambo ya IRENA ikiwemo kuhudhuria mikutano lakini bila ya kuwa na haki ya kupiga kura (observers). Uanachama wa aina hii unazihusu asasi za kiraia zinazojishughulisha na masuala ya nishati jadidifu, nchi ambazo bado hazijaridhia au kusaini mkataba wa IRENA.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya VIII, IX, X na XI zinaeleza muundo wa IRENA pamoja na majukumu ya vyombo hivyo. Ibara zinaeleza kwa mtiririko kuwa IRENA itaundwa na vyombo vikuu vitatu ambavyo ni Mkutano Mkuu ambacho ni chombo cha juu na kitaundwa na wanachama wote wa IRENA. Chombo cha pili ni Baraza linaloundwa na wajumbe wasiopungua 11 na wasiozidi 21 wanaochaguliwa na Mkutano Mkuu kwa utaratibu wa mzunguko. Chombo cha tatu ni Sekretarieti ya IRENA ambayo inahusika na utekelezaji wa majukumu ya kila siku na itakuwa chini ya Mkurugenzi Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya XII inaeleza bajeti ya IRENA ambayo itatokana na michango ya wanachama kulingana na kikokotoo cha Umoja wa Mataifa, michango ya hiyari na vyanzo vingine.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya XIII inaeleza kuwa IRENA itakuwa na hadhi ya kisheria ya Kimataifa na wanachama wake wanaweza kuamua juu ya haki na kinga inayopaswa kupewa.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya XIV inaeleza mahusiano ya IRENA na mashirika mengine yenye majukumu yanayoshabihiana nayo. Ushirikiano huo utaanzishwa kupitia Baraza baada ya kupata ridhaa ya Mkutano Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya XV inatoa haki mbalimbali kwa wanachama ikiwa ni pamoja na haki ya kupendekeza marekebisho ya Mkataba huu, haki ya kujitoa na haki ya kufanya mapitio.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya XVI inaweka masharti yanayohusu utatuzi wa migogoro baina ya wanachama ambapo njia mbadala ikiwemo maelewano na usuluhishi zimepewa kipaumbele.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya XVII inaweka masharti yanayohusu adhabu kwa mwanachama wa IRENA. Mwanachama ambaye atashindwa kutoa mchango aliopangiwa kwa muda wa miaka miwili mfululizo bila ya kuwa na sababu za msingi atanyimwa haki ya kupiga kura. Pia, mwanachama ambaye ataendelea kukiuka masharti ya Mkataba huu au makubaliano yaliyoingiwa kwa mujibu wa Mkataba huu anaweza kunyimwa haki na manufaa yatokanayo na Mkataba huu.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya XVIII inaeleza kuwa Makao Makuu ya Wakala yataamuliwa na Mkutano Mkuu katika kikao chake cha kwanza. Aidha, kwa kuwa taasisi hii ya IRENA ilishaanza tangu mwezi Aprili mwaka 2011, Kamati ilielezwa na Serikali kuwa Makao makuu ya IRENA yapo katika mji wa Abu Dhabi uliopo Falme za Kiarabu.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya XIX inaeleza taratibu za uwekaji Saini katika Mkataba huu, uridhiaji, kuanza kutumika na kuijunga na Mkataba huu.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya XX inaweka masharti kuhusu mhifadhi wa Mkataba huu, Usajili wake na uhalali wa Nyaraka. Kwa ujumla, nchi ya Ujerumani ndio mhifadhi wa Mkataba huu na ndiyo inayohusika na usajili wa Mkataba kwa mujibu wa Kifungu cha 102 cha Mkataba wa Umoja wa Mataifa.

**2.3 Majumuisho ya Serikali kutokana na hoja za Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa Mkataba, Kamati ilipenda kujiridhisha kuhusu baadhi ya masuala kwa lengo la kupata uelewa ili kuepuka au kukabiliana na changamoto zozote zinazoweza kutokea baada ya kuuridhia. Maelezo ya masuala hayo ni kama ifuatavyo:-

**(a) Sababu zilizopelekea kuchelewa kuwasilishwa kwa Mkataba wa Wakala-IRENA ili uridhiwe na Bunge**

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ilisaini Mkataba huu Mwaka 2009 na sasa ni takribani miaka 14 imepita. Kamati ilipata wasiwasi kuhusu suala hili na hivyo kutaka kujiridhisha kuhusu sababu zilizochelewesha, hasara na faida za kuchelewa. Serikali ilieleza sababu mbalimbali ikiwemo kujipa muda wa kutosha kabla ya kuamua kuridhia Mkataba huu. Kamati ilielezwa kuwa, **kwa muda huo wote Serikali imekuwa ikishiriki kazi za IRENA ikiwemo kuhudhuria vikao vya IRENA kama mwangalizi (observer) kwa mujibu wa Ibara ya VII ya Mkataba. Na kupitia hili, imejiridhisha vya kutosha kuwa kuridhia Mkataba huu kuna faida nyingi kiasi kwamba ni vigumu kuona kama kuna hasara yoyote. Kwa sababu hiyo, Kamati ilikubaliana majibu ya Serikali.**

**(b) Nafasi ya Matumizi ya vyanzo vya Nishati zisizokuwa jadidifu ikiwemo Makaa ya Mawe, gesi na Mafuta ikiwa nchi itaridhia Mkataba huu**.

**Mheshimiwa Spika**, nchi yetu ina rasilimali nyingi ya makaa ya mawe, gesi asilia na fursa ya mafuta kwa kuzingatia kuwa nchi ipo katika ubia wa ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta kutokea Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani nchini Tanzania. Aidha, kwa sasa gesi asilia kutokea katika ghuba ya Mnazi Mkoani Mtwara na Songosongo mkoani Lindi inachangia kwa kiasi kikubwa uzalishaji wa nishati ya umeme nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati kwa kutambua hili, ilipata wasiwasi kuhusu kuridhia Mkataba huu ambao unaunda taasisi ambayo inahamasisha na kuendeleza matumizi ya nishati jadidifu pekee. **Hata hivyo, Serikali ilieleza kuwa kuridhia kwa Mkataba huu hakupelekei kuacha kutumika kwa nishati nyingine kwa kuwa**

**hakuna Ibara yoyote ya Mkataba inayopinga au kuelezea matumizi ya nishati zisizo jadidifu.**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali pia ilieleza Kamati kuwa, hata katika nchi ambazo ni vinara wa Mkataba huu ikiwemo India na Ujerumani ambayo ndio mhifadhi, bado inatumia nishati zisizo mbadala ikiwemo nishati ya Makaa ya Mawe. **Hivyo kuridhia kwa Mkataba huu hakutaathiri mipango na miradi ya makaa ya mawe, gesi na mafuta iliyopo nchini. Kwa sababu hiyo, Kamati ilikubaliana na majibu ya Serikali.**

**(c) Adhabu au hatua zinazoweza kuchukuliwa dhidi ya Nchi ikiwemo Tanzania kwa kutokutekeleza matakwa ya Mkataba huu**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia kuwa Ibara ya XIII ya Mkataba inaeleza kuwa IRENA ina nguvu ya kisheria na Ibara ya XVII inaeleza adhabu kwa nchi ambazo zitashindwa kulipia ada, na kwa kuzingatia kuwa nchi yetu bado inategemea nishati ya umeme ambayo kwa kiasi kikubwa inachangiwa na nishati isiyokuwa jadidifu, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu adhabu nchi inazoweza kupata ikiwemo kuwekewa vikwazo vya kiuchumi ikiwa haitatekeleza masharti ya Mkataba huu.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali iliieleza Kamati kuwa, **Mkataba huu unaanzisha taasisi pekee ambayo itatekeleza kazi zake kwa kuzingatia vipaumbele vya Taifa. Hivyo basi, hakuna dhabu zaidi ya zile zilizoainishwa kwenye Mkataba huu. Pia Serikali ilieleza kuwa, Mkataba huu ni wa hiari na nchi ina uwezo wa kujitoa pale ambapo itaona kuna haja ya kufanya hivyo bila hata ya kutoa sababu za kujitoa. Kwa sababu hiyo, Kamati ilikubaliana na majibu ya Serikali.**

**2.4 Upembuzi wa Maudhui ya Mkataba kwa kuwianisha na mwelekeo wa Nchi katika suala la Nishati Jadidifu**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kuchambua vifungu na maudhui ya Mkataba na kupata majibu ya Serikali kwenye hoja mbalimbali, Kamati ililazimika kupitia mambo mbalimbali yanayoweka mtazamo wa nchi katika sekta ndogo ya nishati jadidifu kwa lengo

la kupima ikiwa maudhui ya Mkataba yanaendana na mtazamo wa nchi. Mambo hayo ni:-

**(i) Ilani ya Chama Tawala Chama cha Mapinduzi (CCM)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipitia Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2020-2025 ya Chama Tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa lengo la kuchambua mlengo wake kuhusu nishati jadidifu. Kipengele **Namba 63 (a)** cha Ilani hiyo kimeeleza malengo mojawapo ya Serikali ya Chama Tawala kuwa ni **kukamilisha ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere (Julius Nyerere Hydro Power Project-JNHPP) unaotarajia kuzalisha MW 2,115.**

**Mheshimiwa Spika**, **Kipengele Namba 63(m)** kimeeleza lengo mojawapo la Chama Tawala cha CCM ni **kuongeza uwezo wa uzalishaji umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya nishati jadidifu (renewable energy) ikiwemo miradi ya umemejua, jotoardhi na upepo hadi kufikia MW 1,100.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa takwimu za Wizara kupita TANESCO, hadi kufikia Mwezi Agosti 2023, umeme unaozalishwa nchini kupitia nishati jadidifu ni takribani **MW 585.10** sawa na **asilimia 53.2** ya lengo. Hii inadhihirisha kuwa mchango wa nishati jadidifu katika umeme nchini upo chini ya malengo ya Chama Tawala. **Kwa sababu hii, kunahitajika juhudi za makusudi ili kufikia lengo la kuwa na MW 1,100 itokanayo na nishati jadidifu itokanayo na umemejua, jotoardhi na upepo ifikapo mwaka 2025.**

**Mheshimiwa Spika**, Ilani pia ya Chama Tawala CCM haikuwa mbali kuitaka Serikali yake kuwa na ushirikiano wa Kimataifa katika suala la nishati jadidifu. **Kipengele Namba 63(n)** cha Ilani kinaeleza kuwa **chama cha CCM kitaendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika kuendeleza shughuli mbalimbali za umeme na nishati Jadidifu**.

**Mheshimiwa Spika**, Itakumbukwa kuwa, kwa mujibu wa Ibara ya III ya Mkataba wa IRENA, umeme wa maji, upepo na jua ni aina mojawapo ya nishati jadidifu. Aidha, kwa mujibu wa Ibara ya II ya Mkataba, IRENA inalengo la kuhamasisha aina ya nishati za maji, upepo, jua na jotoardhi. Kwa sababu hii, Kamati imejiridhisha kuwa malengo ya kuanzishwa kwa IRENA yanashabihiana na ilani ya Chama Tawala cha CCM.

**(ii) Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015**

**Mheshimiwa Spika,** Kipengele 3.1(iii) cha Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015 kinahamasisha matumizi ya nishati jadidifu ili kuchangia uzalishaji wa umeme nchini. Pamoja na mambo mengine, Sera inasisitiza umuhimu wa kutumia vyanzo vyote vya nishati jadidifu kwa kuanzisha mifumo ya ujumuishaji wa nishati mbadala katika gridi ya taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya II ya Mkataba wa IRENA imeeleza lengo mojawapo la kuanzishwa kwa IRENA kuwa ni kuhamasisha na kuongeza matumizi endelevu ya vyanzo vyote vya nishati jadidifu katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi. **Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Ibara hii ya Mkataba inashabihiana kwa kiasi kikubwa na Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015.**

**(iii) Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano**

**Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22- 2025/26) umeeleza kuhusu nishati jadidifu. **Kipengele 5.4.6 cha Mpango** pamoja na mambo mengine kinasisitiza uimarishaji wa mifumo ya utunzaji wa mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali asilia ikiwa ni pamoja na kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu. Aidha, **Kipengele 5.4.11** kinaeleza mambo mbalimbali ikiwemo kuboresha mazingira wezeshi ya uwekezaji wa sekta binafsi kwa kuhamasisha na kuendeleza teknolojia na miradi ya nishati jadidifu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kurejea malengo ya Mkataba wa IRENA na majukumu yake kama nilivyoyaeleza katika Ibara ya II na III ya Mkataba, ni wazi kuwa **Mkataba huo unashabihiana kwa kiasi kikubwa na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22- 2025/26).**

**(iv) Malengo ya Wizara ya Nishati**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umeenda mbali zaidi na kuangalia Malengo ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Katika Mwaka huu wa fedha, Wizara ya Nishati imejiwekea malengo 8 ambapo lengo Na. 2 ni "**Kuongeza mchango wa nishati jadidifu na mbadala katika matumizi mbalimbali ya nishati**".

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa lengo hili, Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu bajeti ya **takribani Shilingi Trilioni 1.5** kwa lengo la kuendelea kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya umeme unaotokana na nishati jadidifu. Miradi hiyo ni pamoja na Bwawa laJulius Nyerere (MW 2115), Ruhudji (MW 358), Rusumo (MW 80), Rumakali (MW 222), Kakono (MW 80), Malagarasi (MW 49.5); Kikonge (MW 300) na miradi mingine ya nishati jadidifu ya jotoardhi, upepo na jua.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya IV ya Mkataba wa IRENA inaeleza majukumu na wajibu mbalimbali wa IRENA ikiwa ni pamoja na kuchambua, kufuatilia na kuweka mfumo wa matumizi ya nishati jadidifu. Kazi hii itatekelezwa kwa kujumuisha mambo mbalimbali ikiwemo motisha, mbinu za uwekezaji, vifaa na utatuzi wa changamoto zake. Wakala pia itakuwa na jukumu la kushauri na kusaidia wanachama wake kuhusu sera husika, kuwajengea uwezo na kuwashauri kuhusu ufadhili wa nishati jadidifu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kutazama malengo ya Wizara ya Mwaka 2023/204 licha ya kwamba yanashabihiana kwa kiasi kikubwa na Mkataba wa IRENA, lakini pia **ikiwa nchi itakuwa mwanachama wake, itafaidika kupitia majukumu ya IRENA katika utekelezaji wa miradi yake inayohusu nishati jadidifu hususani katika suala la kujengewa uwezo, ushauri wa kisera, mbinu za uwekezaji na ufadhili unaohusu nishati jadidifu.**

**Mheshimiwa Spika,** Katika kujiridhisha na hili, Kamati iliihoji Serikali kuhusu faida ambazo nchi Jirani zimenufaika kwa kuridhia Mkataba huu wa IRENA. **Kamati ilielezwa kuwa baadhi ya nchi jirani zimenufaika na misaada ya kifedha na kiushauri katika sekta ndogo ya nishati jadidifu na hivyo Tanzania ikijiunga pia itakuwa katika nafasi ya kunufaika na fursa za aina hiyo.**

**(v) Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDG's)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ililazimika kufanya rejea kwenye Malengo ya Maendeleo endelevu ya Umoja wa Mataifa (UN) - SDGs ili kujiridhisha ikiwa malengo hayo yanahusu pia masuala ya nishati jadidifu. Kamati ilifanya haya kwa kutambua kuwa Tanzania ni mojawapo ya nchi ambayo ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa na mnufaika pia wa malengo ya Umoja huu.

**Mheshimiwa Spika**, Katika malengo endelevu ya Umoja wa Mataifa, lengo namba 7 linasisitiza nchi wanachama **kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa nishati ya kisasa kwa gharama nafuu, inayotegemewa na endelevu kwa watu wote.** Ili kufikia lengo hili, UN inayo mikakati mbalimbali ikiwemo kukuza ushirikiano wa Kimataifa katika utafiti na teknolojia wa nishati safi ikiwemo nishati mbadala ifikapo mwaka 2030.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kupima mikakati hii, mojawapo ya vigezo ambavyo vitatumika na UN ni pamoja na uwepo wa misaada ya kifedha kwa nchi zinazoendelea inayolenga kuunga mkono masuala ya utafiti na mandeleo ya nishati jadidifu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia kuwa IRENA ni mojawapo ya taasisi ya Umoja wa Mataifa, ni dhahiri kuwa kuna uwezekano mkubwa wa Umoja wa Mataifa kuitumia taasisi hii katika kufanikisha malengo yake. **Hivyo basi, ikiwa Tanzania itajiunga na Taasisi hii, inajiweka katika nafasi nzuri ya kunufaika na malengo ya Umoja wa Mataifa katika sekta ya nishati jadidifu.**

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati na kwa kuzingatia matakwa ya Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Mwaka 1977, Kamati inaona ipo haja kwa Serikali kuzingatia maoni na ushauri ufuatao kwa lengo la kuweka mazingira mazuri ya utekelezaji wa Mkataba huu:

### 3.1 Uendelezaji wa Matumizi ya Nishati zisizojadidifu Nchini

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kuwa kama nchi bado tunaendelea kuvumbua lakini pia kutumia nishati nyingine kama Makaa ya mawe na Gesi Asilia. **Kamati inasisitiza Serikali ihakikishe kuwa, kuridhiwa kwa Mkataba huu siyo kifungo cha nchi kwenye matumizi ya nishati nyingine kama Makaa ya mawe, gesi asilia na mafuta ambayo nchini yetu inaendelea kunufaika kwa kiasi kikubwa katika mchango wake kwenye sekta ya nishati ya umeme nchini**. Aidha, kwa kuwa dunia imeendelea kujiwekea malengo ya kupunguza matumizi ya nishati zisizo mbadala ambapo itafika wakati matumizi yake yatapungua kwa kiasi kikubwa, **ni vyema nchi ikatekeleza kikamilifu mikakati yake ili kuvuna nishati isiyo mbadala na kuitumia kikamilifu wakati bado mahitaji yake ni makubwa duniani.**

### 3.2 Kuzalisha Wataalam wa kutosha

**Mheshimiwa Spika,** moja ya changamoto ambayo Kamati inaiona ni uhaba wa wataalam wa sekta hii ndogo ya Nishati jadidifu. Kamati inatambua kuwa Wizara imejipanga kuimarisha Taasisi za Teknolojia za Dar es Salaam (DIT) na Chuo cha Ufundi cha Arusha (ATC) ili kuzalisha wataalam wa kutosha. **Ni Rai ya Kamati kuwa, Wizara ishirikiane na vyuo vingi zaidi kama Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya ili kuweza kuzalisha Wataalam wa kutosha wenye ujuzi wa kutengeneza vifaa vya nishati jadidifu kama *solar panel,* kufanya matengenezo ya vifaa vinavyotumika katika miradi ya nishati jadidifu na weledi wa kusimamia ipasavyo utekelezaji wa miradi hiyo.**

### 3.3 Kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Nishati Jadidifu

**Mheshimiwa Spika**, moja kati ya aina za nishati jadidifu ambazo Tanzania tumebarikiwa kuwa nazo ni Joto ardhi. Hata hivyo, matumizi ya nishati hii siyo ya kuridhisha sana kama zilivyo nchi nyingine ikiwemo baadhi ya nchi Jirani za Afrika Mashariki. Moja ya sababu inayofanya kutotumika ipasavyo kwa nishati hii ni ukosefu wa sheria na hivyo kuwa kikwazo katika kuvutia wawekezaji.

Kamati imekuwa ikisisitizia mara kwa mara kuletwa kwa Muswada huu Bungeni na Serikali imekuwa ikieleza kuwa inakamilisha mchakato wake. **Kamati inasisitiza tena Muswada huu uletwe Bungeni ili kukamilisha mchakato wa utungwaji wa Sheria hii ili kuvutia wawekezaji na pia kuchochea uzalishaji wa umeme nchini na manufaa mengine ya kiuchumi.**

### 3.4 Kuhamasisha Ushiriki wa Sekta Binafsi katika Sekta ya Nishati

**Mheshimiwa Spika**, nchi nyingi zinazotumia kwa wingi nishati jadidifu hazifanyi zenyewe kama Serikali bali kupitia au kwa kushirikiana na sekta binafsi. **Kamati inashauri Serikali kuishirikisha kikamilifu Sekta binafsi kwa kuhakikisha inawekewa mazingira rafiki yatakayovutia wawekezaji na hivyo kuongeza uzalishaji wa nishati kama ilivyoelezwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.**[2]

### 3.5 Kuongezwa kwa Bajeti

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na umuhimu wa nishati jadidifu katika uzalishaji wa umeme na utunzaji wa mazingira, **Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inaendela kuongeza Bajeti ya utekelezaji wa miradi ya nishati jadidifu ili utekelezaji wa miradi hiyo uweze kukamilika mapema.**

### 3.6 Ushiriki wa Sekta Mtambuka

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa suala la nishati jadidifu ni mtambuka kwa maana linahusisha Wizara mbalimbali, **Kamati inasisitiza Wizara zote zinazohusika zishirikiane na Wizara ya Nishati iwe Mratibu ili nchi iweze kunufaika na fursa hii.**

[2] 63(k) Kuendeleza juhudi za kupunguza matumizi ya kuni na mkaa kama chanzo cha nishati kwa kuimarisha na kuhamasisha matumizi ya vyanzo mbadala kwa kushirikisha sekta binafsi wakiwemo wabunifu wadogo katika kubuni na kutekeleza miradi ya nishati

### 3.7 Mkakati wa kuendeleza Nishati Jadidifu (Renewable Energy Development Strategy)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kuendeleza nishati jadidifu ikiwa ni pamoja na kuwa katika Mchakato wa kuandaa Mkakati wa kuendeleza nishati jadidifu (Renewable Energy Development Strategy).

**Kamati inashauri Wizara kuhakikisha inakamilisha Mkakati huu kama ilivyopangwa na kuhakikisha inasimamia programu za nishati safi ya kupikia na matumizi sahihi ya nishati (*cleaning cooking and energy efficiency*) kikamilifu.**

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine na kwa dhati kabisa naomba nikushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuliongoza vema Bunge letu wakati wote. Maelekezo, ushauri na busara zako vimekuwa ni nyenzo muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa kujitoa na kuchambua Azimio hili kwa uweledi mkubwa. Kwa kutambua mchango wao katika kujadili Hoja hii, naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ifuatavyo: -

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Dkt. David Mathayo David, Mb | - | **Mwenyekiti** |
| 2. | Mhe. Kilumbe Shaaban Nge'nda, Mb | - | **M/Mwenyekiti** |
| 3. | Mhe. Aleksia Asia Kamguna, Mb | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Tabasamu Hamisi Mwagao, Mb | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Iddi Kassim Iddi, Mb | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Jesca David Kishoa, Mb | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. John Marco Sallu, Mb | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Juliana Didas Masaburi, Mb | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Maimuna Ahmad Pathan, Mb | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Masache Njelu Kasaka, Mb | - | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Ndaisaba George Ruhoro, Mb | - | Mjumbe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 12. | Mhe. Nicodemas Henry Maganga, Mb | - | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb | - | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Saada Mansour Hussein, Mb | - | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb | - | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Martha Festo Mariki, Mb | - | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Constantine John Kanyasu, Mb | - | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb | - | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Eng. Samweli Xaday Hhayuma, Mb | - | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Tumaini Bryceson Magessa, Mb | - | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Angeline Sylvester Mabula, Mb | - | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Joseph Kasheku Musukuma, Mb | - | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inamshukuru Mtoa Hoja, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto M. Biteko (Mb), Naibu Waziri Mhe. Judith Salvio Kapinga (Mb) kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati wakati wa uchambuzi wa Azimio la Kuridhia Mtakaba huu. Aidha, nawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Nishati wakiongozwa na Katibu Mkuu Mhandisi Felchesmi Mramba kwa ushirikiano walioipatia Kamati wakati wote wa uchambuzi wa Mkataba huu na kutoa ufafanuzi pale walipohitajika kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa, napenda kuwashukuru wadau wote walioweza kutoa maoni yao kuhusu Mkataba huu ambayo umeiwezesha Kamati katika uchambuzi wake.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru sana Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge, Bi. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc*, kwa ushirikiano anaoipa Kamati wakati wote. Aidha, naishukuru Sekretarieti ya Kamati kwa ushauri wa kitaalam wakati wa uchambuzi wa Mkataba na kuwezesha kukamilika kwa taarifa hii.

### 4.2 Uamuzi wa Hoja

**Mheshimiwa Spika**, kwa mamlaka ambayo Bunge limepewa kwa mujibu wa **Ibara ya 63(3)(e)** ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya Mwaka 1977, naomba sasa lijadili na kuridhia **Azimio la Bunge kuhusu Mapendekezo ya Tanzania kuridhia kujiunga na Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu**

**wa Mwaka 2009 (Statute of the International Renewable Energy Agency -IRENA)**, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono Hoja.

Dkt. David Mathayo David, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**

31 Oktoba, 2023

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Waziri wa Afya kuna wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Wageni waliokaa Jukwaa la Spika, wageni wa Mheshimiwa Spika na Rais wa *IPU* ambaye ni Mjumbe kutoka Bunge la Ukraine *Honorable Oleksander Sanchenko, Head of the Friendship Group with Tanzania and Ukraine, Head of Youth Wing of Zelensky Party. Honorable Oleksii Zhmerenetskyi, Head of EU Integration Sub Committee of Anti-Corruption Committee. Honorable Zhan Beleniuk, First Deputy Chairman Committee on the Youth and Sports Olympic. (Makofi)*

Ujumbe huu umeambatana na Mwenyeji wao Mwenyekiti wa Chama cha Kirafiki kati ya Bunge la Tanzania na Bunge la Ukraine, Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama. Karibuni sana; *Welcome to the Parliament of Tanzania. (Makofi)*

Tuna mabalozi, Mheshimiwa Balozi Suleiman Suleiman, Naibu Mwakilishi wa Kudumu, Uwakilishi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania *New York;* endelea kusimama Balozi. Tuna Mheshimiwa Balozi Hoyce Temu, Naibu Mwakilishi wa Kudumu Uwakilishi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Geneva. Mheshimiwa Balozi Robert Kahendaguza, Mwakilishi Maalum wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hii ndiyo timu ya Mabalozi walioambatana na Rais mpya wa *IPU,* Angola kwenye mikakati ya

*engagement* ya *bilateral* na diplomasia ambao Mabalozi hawa watatu wakishirikiana na Waziri wa Mambo ya Nje chini ya usimamizi na maagizo ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha mgombea kutoka Tanzania anashinda kwa kishindo. Kwa niaba ya Mheshimiwa Spika na Rais wa *IPU* tunawashukuru sana kwa utiifu wenu, uzalendo wenu na kazi kubwa mliyoifanya kuiheshimisha Tanzania, kumheshimisha Rais wetu wa Tanzania, kuliheshimisha Bunge na kuipa heshima Afrika na dunia kwa ujumla. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tuna Bi. Prisca Mwanjesa, Afisa Mambo ya Nje na yeye alikuwa pamoja na wenzake hawa. *(Makofi)*

Viongozi kutoka Wilaya ya Mbeya Mjini, Ndugu Afrey Nsomba, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mbeya Mjini; Mheshimiwa Dormohamed Issa, Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Jiji la Mbeya; Ndugu Mohamed Mavalla, Katibu wa CCM Wilaya ya Mbeya Mjini; Ndugu Philimon Mngongo, Mwenezi wa CCM Wilaya ya Mbeya Mjini; Mheshimiwa Juma Simbeyanje, Diwani Kata ya Nsoho; na Ndugu Pascal Mwaiseje, dereva wao. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Mgeni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, jamaa yake kutoka Dar es Salaam Ndugu Wesley Majura Ettutu, karibu. *(Makofi)*

Wageni 32 wa Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Watumishi wa Halmashauri ya Mlimba, Mkoani Morogoro, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Mheshimiwa Aloyce Kwezi, walimu kutoka Kaliua, Mkoani Tabora, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 12 wa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Chama cha Wafugaji kutoka Bunda, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 45 wa Mheshimiwa Anna Lupembe, Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, familia yake kutoka Mbeya, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Francis Ndulane, Wadau wa Maendeleo kutoka Kilwa Mkoani Lindi; karibuni. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Neema Mwandabila, ndugu zake kutoka Tunduma, Mkoa wa Songwe, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu, Viongozi wa CCM kutoka Geita, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Mwantumu Zodo, wadogo zake kutoka Morogoro, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunao wanafunzi na walimu 70 kutoka Tanzania *Assembles of God Central Bible College Dodoma,* karibuni. *(Makofi)*

Wapo pia vijana 24 wa UVCCM kutoka Jijini Dodoma, karibuni, Ndugu Fredy Lwilla kutoka Kata ya Makulu Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *NHIF* watatoa huduma ya upimaji wa afya kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na watumishi wa Bunge katika kituo chetu cha afya kilichopo katika Jengo la Utawala *Annex*. Zoezi hili linaanza leo tarehe 31 Oktoba na litaendelea hadi Tarehe 10 Novemba, upimaji huo utahusu magonjwa yafuatayo:-

Magonjwa ya moyo, magonjwa ya homoni na sukari, magonjwa ya mkojo na magonjwa ya mifupa. Zoezi hili linashirikisha Madaktari Bingwa kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Ugonjwa wa Moyo - *JKCI* na Mloganzila.

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Bunge

Bonanza la mwezi Januari linatarajia kufanyika Tarehe 27 Januari, 2024 kwa mashindano ya timu za Wabunge na watumishi mashabiki wa Simba dhidi ya Wabunge na watumishi mashabiki wa *club* ya Yanga katika michezo yote. Hivyo, Wabunge na watumishi wote wanaombwa kujisajili mapema kwa viongozi hao kwa malengo ya timu wanazozishabikia na aina ya michezo ili kurahisisha uratibu na ugawaji wa mavazi yanayoendana na rangi za timu watakazozishabikia.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namuita Waziri wa Afya.

**Azimio la Bunge kuhusu mapendekezo ya kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika wa Mwaka 2019 *(Treaty for the Establishment of the African Medicine Agency - AMA)***

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha maelezo ya Azimio la Bunge kuhusu mapendekezo ya kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika wa mwaka 2019 *(Treaty for the Establishment of the African Medicine Agency - AMA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu nisitoe pongezi kwa sababu ya muda, lakini niseme kwamba Sera ya Afya ya mwaka 2007 inasisitiza kuhusu umuhimu wa upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaatiba na vitendanishi vyenye ubora unaotakiwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya hapa nchini. Hii ni kutokana na umuhimu wa bidhaa tiba katika kupambana na kuthibiti magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa bidhaa tiba zenye ubora, usalama na ufanisi unaotakiwa zinapatikana wakati wote katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Katika kutekeleza Sera ya Afya ya mwaka 2007 Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba, *TMDA* imepewa jukumu la kudhibiti bidhaa tiba chini ya Sheria ya Dawa na Vifaatiba Sura ya 219. Sheria hii imeweka mifumo thabiti ya udhibiti wa bidhaa tiba kwa kuhakikisha kuwa bidhaa tiba zinazoingizwa au kutengenezwa

nchini ni bora, salama na zenye ufanisi. Hivyo ili bidhaa tiba ziweze kuruhusiwa kuingizwa au kutengenezwa na kutumika nchini ni lazima ziwe zimekidhi masharti ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TMDA* imefanikiwa kuwa miongoni mwa taasisi bora zenye uwezo wa kudhibiti bidhaa tiba na hivyo kutambuliwa na Shirika la Afya Duniani *(WHO)* kuwa imefikia kiwango cha ngazi ya tatu *(maturity level three)* kati ya ngazi nne za umahiri katika udhibiti wa bidhaa za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ina maana kwamba mifumo ya udhibiti wa bidhaa tiba inayotumika nchini inakidhi viwango vinavyokubalika Kimataifa. *TMDA* ilifikia hatua hiyo Mwaka 2018 na ilikuwa taasisi ya kwanza Barani Afrika. Taasisi ambazo baadhi zimefikia hatua hiyo baada ya *TMDA* ni *Food and Drug Authority* ya Ghana, *National Agency for Food and Drug Administration and Control* ya Nigeria na *Egyptian Drug Authority* ya Misri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mfanikio hayo *TMDA* inakabiliwa na changamoto mbalimbali katika udhibiti wa bidhaa tiba. Changamoto hizo ni pamoja na upungufu wa wataalam, uwepo wa njia zisizo rasmi katika maeneo ya mipaka na vituo vya forodha visivyoruhusiwa kuingiza bidhaa tiba. Changamoto nyingine ni mabadiliko ya mara kwa mara ya teknolojia yanayohitaji mbinu mpya na weledi maalum katika kudhibiti bidhaa tiba hali ambayo inahatarisha afya ya jamii kwa kuwa bidhaa tiba duni na bandia zisizofaa kwa matumizi ya binadamu zinaendelea kuwepo katika soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza jitihada za pamoja za kutatua changamoto hizo wakuu wa nchi na Serikali za Jumuiya ya Umoja wa Afrika *(AU)* katika mkutano wa kawaida wa 32 uliofanyika Addis Ababa – Ethiopia, Tarehe 11 Februari, 2019 walikubaliana kuanzishwa kwa Taasisi ya Dawa ya Afrika *(Africa Medicine Agency – AMA)*. Lengo la taasisi hii ni kuratibu na kusaidia nchi wanachama wa Umoja wa Afrika katika kuboresha uwezo wa kudhibiti ubora wa bidhaa tiba hususan katika maeneo ambayo ni changamoto kwa nchi nyingi Barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha ili taasisi hiyo iweze kufanya kazi nchi wanachama zinatakiwa kusaini na kuridhia mkataba huo. Hadi kufikia Tarehe 31 Julai, 2023 jumla ya nchi 30 zimesaini na kati ya hizo nchi 23 zimeridhia mkataba wa *AMA* zikiwemo Rwanda na Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, masharti ya kuanzisha *AMA* ni nchi 15 kuridhia mkataba, *AMA* ilianzishwa Tarehe 05 Novemba, 2021. Tanzania ilisaini mkataba huo Tarehe 10 Agosti, 2021 na hatua inayofuata ni kuridhia ili kujiunga na taasisi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa *AMA* umegawanyika katika sehemu kuu Sita na Ibara 41 kama ilivyoainishwa hapa chini. Sehemu ya Kwanza inazungumzia ufupisho, tafsiri, kuundwa kwa *AMA* na madhumuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Kwanza inafafanua vifupisho vya maneno yaliyotumika katika mkataba; Ibara ya Pili, inatoa tafsiri ya misamiati inayotumika tatika mkataba; Ibara ya Tatu, inaelezea uanzishwaji wa *AMA* kama taasisi maalum chini ya Umoja wa Afrika; Ibara ya Nne, inaelezea madhumuni ya *AMA* kuwa ni kuimarisha uwezo wa nchi wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda, kudhibiti bidhaa tiba ili kuhakikisha zinapatikana kwa haraka zikiwa zenye ubora, ufanisi na salama; Ibara ya Tano inaaisha kanuni elekezi *(guiding principles)* Saba za *AMA* ikiwemo uongozi, kuaminika, umiliki, uwazi, uwajibikaji, kuongeza thamani, usiri na usimamizi bora; Ibara ya nane inaeleza majukumu ya *AMA* ambayo ni:-

(a) Kuratibu na kuimarisha jitihada ya kuwianisha mifumo ya udhibiti wa bidhaa tiba na kuboreshga umahiri wa wakaguzi wa viwanda kulingana na miongozo ya utengenezaji bora wa bidhaa tiba.

(b) Kuratibu ukusanyaji, usimamizi, utunzaji na kubadilishana bidhaa tiba zikiwemo zile duni na bandia kwa nchi wanachama na dunia kwa ujumla.

(c) Kuratibu tathmini za pamoja za maombi ya majaribio ya bidhaa tiba na kutoa msaada wa kitaaluma katika uchunguzi wa kimaabara kwa nchi wanachama ambazo hazina huduma hizo.

(d) Kuhamasisha kuridhiwa na kuainishwa kwa sera, miongozo, masharti na mifumo ya udhibiti iliyopo kupitia Jumuiya za Kikanda na Taasisi za huduma za afya.

(e) Kuteua, kuhamasisha, kuimarisha, kuratibu na kufuatilia vituo vya kikanda vya umahiri wa udhibiti kwa lengo la kujenga uwezo wa wataalam wa udhibiti wa bidhaa tiba.

(f) Kuratibu na kushirikisha pale inapobidi masuala ya ukaguzi wa viwanda vya bidhaa tiba ikiwemo kusimamia udhibiti na ufuatiliaji wa usalama kama itakakavyoelekezwa na kuhakikisha kwamba ripoti zinawasilishwa kwa nchi wanachama wa *AMA*.

(g) Kuhamasisha ushirikiano na ubia na kuhakikisha kuwa mamlaka za udhibiti zinatambua maamuzi yaliyoofikiwa katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niruke majukumu ni mengi lakini tumeainisha katika taarifa yangu naomba iingie kwenye *Hansard* kama nilivyoiwasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili ni hadhi ya *AMA* na watumishi wake, hadhi ya kisheria. Ibara ya Saba inaainisha kuwa *AMA* itakuwa na hadhi ya kisheria inayoweza kuingia mikataba, uwezo wa kumiliki mali na kuuza au kushtaki na kujitetea pale inaposhtakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Nane ni Kinga na Upendeleo. Ibara hii inaeleza masharti yatakayotumika kuhusu kinga na upendeleo kwa *AMA* na watumishi wake ambapo inabainisha kuwa yatafanana na msharti ya kiitifaki za masuala ya kinga na upendeleo kwa Umoja wa Afrika. Ibara ya Tisa inafafanua kuwa Makao Makuu ya *AMA* yatatokana na uamuzi wa Wakuu wa

nchi za *AU* na nchi itakayochaguliwa itaingia mkataba wa uwenyeji *(Host Agreement)* na *AU.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu inazungumzia muundo na Utawala. Sehemu hii inajumuisha Ibara ya 10 hadi Ibara ya 25 zinazoeleza muundo wa kiutendaji wa *AMA* na inajumuisha masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 10 ninafafanua muundo wa *AMA* kuwa, utajumuisha mkutano mkuu wa nchi wanachama zilizoridhia mkataba, bodi tendaji, sekretarieti na kamati za kitaaluma. Ibara ya 11 inaeleza kuwa chombo cha juu cha maamuzi ya *AMA* ni mkutano mkuu wa nchi wanachama zilizoridhia mkataba. Ibara ya 12 inaeleza wajumbe wa mkutano wa nchi wananchama ambao watakuwa Mawaziri wenye dhamana ya Afya au wawakilishi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkutano huo utachagua Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na mchukua taarifa kwa mfumo wa mzunguko wa mazingira kijiografia ya nchi wanachama wa *AU.* Viongozi waliochaguliwa watakuwa madarakani kwa muda wa miaka miwili na watakutana mara moja kwa kila mwaka. Ibara hii inaendelea kufafanua zaidi kwamba endapo Mwenyekiti hatakuwepo, Makamu Mwenyekiti au mchukua taarifa atakuwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 13 inaeleza kuhusu masharti ya kipindi cha mkutano wa kawaida wa nchi wanachama ambao utafanyika angalau mara moja kila baada ya miaka miwili na ule wa dharura utategemea maombi ya Spika au viongozi wenzake au kuombwa na theluthi mbili ya nchi wanachama. Ibara ya 14 inaeleza majukumu ya mkutano mkuu wa nchi wanachama ambayo yanajumuisha kupanga viwango vya michango ya fedha za bajeti ya kuendesha *AMA*, kuteua na kuwaondoa Wajumbe wa Bodi ya *AMA*, kuweka kanuni na majukumu ya Mkurugenzi Mkuu wa *AMA* na miiongozo ya utendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 15 inaeleza kuwa Bodi ya *AMA* itateuliwa na kuwajibika kwa Mkutano Mkuu wa nchi

wanachama. Ibara ya 16 inaeleza bayana kuwa bodi itakuwa na Wajumbe Tisa, kati ya hao Wajumbe Watano ni Watendaji Wakuu wa Taasisi za Udhibiti kutoka kila Jumuiya za Kikanda inayotambuliwa na *African Union,* Mjumbe mmoja mwakilishi wa Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda kwa mzunguko, mwakilishi mmoja kutoka taasisi za afya kwa mzunguko, mwakilishi mmoja wa Kamati za Kitaifa za masuala ya *bioethics* na Kamishna wa Huduma za Jamii wa *African Union.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 17 inazungumza vikao vya Bodi Tendaji ya *AMA,* Ibara ya 18 inazungumza majukumu ya Bodi Tendaji, Ibara ya 19 inazungumzia muda wa Wajumbe kutumikia Bodi Tendaji ambapo ni miaka mitatu na Ibara ya 20 inafafanua uanzishwaji wa Kamati za kitaaluma za muda na za kudumu ambazo zitaundwa na bodi ya *AMA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 21 inaweka masharti ya kazi za Kamati za kitaaluma yanayojumuisha kufanya tahmini ya kisayansi kwa maombi yote ya usajili, ukaguzi wa viwanda vya dawa, maoni ya kisayansi ya kitaaluma kuhusu utekelezaji wa majukumu ya *AMA*. Ibara ya 22 inazungumzia muundo wa Kamati za Kitaaluma, Ibara ya 23 inafafanua majukumu ya Sekretarieti ya *AMA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 24 inaeleza kwamba atakuwepo Mkurugenzi Mkuu wa *AMA* ambae ndiye atakuwa Kiongozi wa Sekretarieti na atakuwa msimamizi wa shughuli za kila siku za *AMA*. Mkurugenzi Mkuu atateuliwa na mkutano wa nchi wanachama baada ya kupendekezwa na Bodi Tendaji na atakuwa Afisa Mtendaji Mkuu anayewakilisha *AMA* katika masuala yote. Ibara ya 25 inazungumzia mapingamizi kuhusu maoni ya kisayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nne ni Masharti ya Fedha. Ibara ya 26 inazungumzia rasilimali fedha za *AMA* ambapo kila Mkutano Mkuu wa wanachama utapanga viwango vya michango kwa kila mwanachama na kupitisha bajeti ya mwaka ya *AMA*. Ibara ya 27 inafafanua gharama za uendeshwaji wa Sekretarieti ya *AMA* kwa mujibu wa mpango kazi ulioidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tano inazungumzia Uhusiano na Nchi wanachama na wabia wengine. Ibara ya 28 inaeleza kuwa *AMA* itafanya kazi kwa kushiirikiana na *African Union* na itawasilisha taarifa ya utendaji kazi ya kila mwaka kwa *AU.* Ibara ya 29 inazungumzia uhusiano wa *AMA* na nchi wanachama na wasiowanachama wa Umoja wa Afrika na kuweka utaratibu wa kuteua waratibu wa kazi za *AMA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 30 inaweka masharti ya ushirikiano na *WHO,* Kituo cha Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Afrika, Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda, Wakala za Umoja wa Mataifa na Mashirika ya Kiserikali na yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Sita ni Masharti Mengineyo, ambapo yapo katika Ibara ya 31 hadi ibara ya 41. 31 lugha zitakazotumika ni lugha za *AU* ambazo ni Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa na Kireno.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 32 Usuluhishi wa Migogoro ambapo mkataba umeweka tafsiri, matumizi na utekelezaji wa kutatua migogoro kwa njia ya mazungumzo na mapatano kwa amani. Ibara ya 33 masharti ya kuridhia kwa mkataba. Ibara hii inaeleza kuwa nchi wanachama wakati wa kuridhia ina haki ya kuridhia kwa mashaka baadhi ya masharti ya mkataba huu. Masharti hayo hayapaswi kuwa kinyume na madhumuni ya mkataba. Ibara ya 34 inaainisha masharti ya nchi mwanachama kujitoa kwenye uwanachama, Ibara ya 35 inaeleza kuwa ama inaweza kufutwa baada ya theluthi mbili ya nchi wanachama kukubaliana kwenye mkutano mkuu wa nchi wanachama na baada ya kupitishwa na mkutano mkuu wa *African Union*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 36 inaeleza kuwa nchi wanachama inaweza kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho au mapitio na mapendekezo hayo yatajadiliwa katika Mkutano Mkuu wa nchi wanachama. Ibara ya 37 inaeleza kuwa nchi mwanachama inaweza kusaini na kisha kuridhia na kuwasilisha hati ya kuridhia kwa Mwenyekiti wa Umoja wa nchi za Afrika. Ibara ya 38 inaainisha kuanza kutumika kwa mkataba kuwa ni siku 30 baada ya wanachama 15 kuwasilisha hati za kuridhia mkataba kwa

Mwenyekiti wa Umoja wa Nchi za Afrika. Ibara ya 39 inaelezea kuwa hati ya kuridhia mkataba iwasilishwe kwa Mwenyekiti wa *AU,* Ibara ya 40 usajili wa mkataba, Ibara ya 41 nakala halali za mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza Ibara 41 za mktaba wa *AMA* tunapendekeza kama Serikali kuridhiwa kwa Ibara zote isipokuwa Ibara ya 6 Kifungu Kidogo (i), (m) na (o). Ibara ya 6(i) inapendekezwa kutoridhiwa kwa kuwa inaipa *AMA* jukumu la kutoa maelekezo na maoni ya kisayansi wakati wa milipuko ya magonjwa, dharura na majaribio ya dawa. Hivyo kuridhiwa kwa bara hiyo, kunaweza kuhatarisha usalama wa nchi kwa kuruhusu dawa kutumika bila nchi kujiridhisha kuhusu ufanisi na usalama wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 6(m) inapendekezwa kutoridhiwa kwa kuwa jukumu la kusimamia na kuchukua sampuli na kuzichunguza ubora wake ni jukumu la Kitaifa ambapo Tanzania ina mfumo wa kutekeleza jukumu hilo. Ibara ya 6(o) inapendekezwa kutoridhiwa kutokana na *AMA* kuwa mamlaka ya kuamua bidhaa tiba ambazo zitafanyiwa tathmini kama ilivyoamuliwa na *African Union au WHO.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni ibara ya 26(1) (a), 26(4) na 31. Ibara ya 26(1)(a) inapendekeza kuridhiwa kwa matarajio ya kufanyiwa marekebisho ili iendane na taratibu zinazotumika na taasisi zilizo za *AMA*. Ibara ya 31 na 41 zimebainisha lugha zitakazotumika ni lugha za *AU* ambazo ni Kiarabu, Kingereza, Kifaransa na Kireno. Aidha, kwa kuwa lugha ya Kiswahili imepitishwa kama lugha rasmi katika shughuli za *AU,* Serikali itatumia fursa ya Ibara ya 36(1) kuwasilisha mapendekezo ya kurekebisha Ibara hizo ili isomeke kuwa lugha rasmi za *AU* ndizo zitakazotumika ikiwemo lugha ya Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo Tanzania itaridhia utekelezaji wa *AMA,* tunategemea tutaimarisha mfumo wetu wa udhibiti wa bidhaa tiba, kudhibiti bidhaa tiba bandia na zenye ubora hafifu, kuwezesha viwanda vya bidhaa tiba vya hapa nchini

kuwasilisha taarifa kwa nchi wanachama na kudhibiti mifumo ya udhibiti wa bidhaa tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo naomba niwasilishe Azimio la Bunge kuhusu mapendekezo ya kuridhia mkataba wa kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika ya Mwaka 2023.

Kwa kuwa, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika kupitia hati iliyosainiwa na Serikali na kuwasilishwa Sekretarieti ya Umoja huo mnamo tarehe 25 Mei, 1963;

Na kwa kuwa, Wakuu wa Nchi na Serikali za Jumuiya ya Umoja wa Afrika katika Mkutano wa Kawaida wa 32 uliofanyika Adiss Ababa, tarehe 11 Februari, 2019 walikubaliana kuanzishwa kwa Taasisi ya Dawa ya Afrika;

Na kwa kuwa, mkataba huu unalenga kuratibu na kusaidia nchi wanachama wa Umoja wa Afrika katika kuboresha uwezo wa kudhibiti ubora wa bidhaa tiba suala ambalo ni changamoto kwa nchi nyingi barani Afrika;

Na kwa kuwa, hadi kufikia tarehe 31 Julai, 2023 nchi 30 ikiwemo Tanzania zimesaini mkataba huo;

Na kwa kuwa, Ibara ya 33 ya Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa Afrika inaruhusu kuridhia kwa mashaka masharti yoyote ya mkataba huo wakati wa kuridhiwa na Bunge;

Na kwa kuwa, Ibara ya 6(i), 6(*m)* na 6(*o)* hazina maslahi kwa nchi yetu, kwa kuwa, yanaweza kuhatarisha usalama wa nchi, yanaweza kusababisha mgongano wa kimajukumu na yanaweza kuinyima nchi uhuru wa kuamua;

Na kwa kuwa, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni miongoni mwa nchi zilizosaini mkataba huo inapaswa kuridhia mkataba huo ili iweze kunufaika na kuwezesha utekelezaji wa Mkataba wa Kuanzishwa Taasisi ya Dawa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona kwa kuwa ziko nyingi, niendelee nazo?

**WABUNGE FULANI:** Endelea…*(Kicheko)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshiwa Naibu Spika, na kwa kuwa kuridhiwa…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri muda wako unakaribia kwisha, zungumza yale mambo ambayo ni muhimu kwa Bunge.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tumesambaza pia kwa Waheshimiwa Wabunge Azimio hili la mapendekezo ya kuridhia kwa Mkataba wa *AMA*, naomba Bunge lako Tukufu likubali kuridhia Mkataba wa Taasisi ya Dawa ya Afrika kwa kuwa litaweza kuimarisha uwezo wa nchi wanachama na nchi yetu katika kudhibiti bidhaa tiba ili kuhakikisha zinapatikana kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ambalo tunaamini tutanufaika nalo kama nchi ni pale ambapo dawa imeshasajiliwa Tanzania na *AMA* wakaisajili, basi dawa hiyo inaweza kuuzwa katika nchi yoyote barani Afrika bila kufuata mifumo ya kuisajili katika nchi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari chanya ni kwamba dawa kama imeshasajiliwa katika nchi ya *AMA* pia inaweza kuingizwa moja kwa moja katika nchi yetu bila kupitia mifumo ya urasimu. Sisi kama Serikali tumejipanga kuimarisha viwanda vya dawa vya ndani ili tuweze kunufaika na mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia manufaa hayo ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itapata kutokana na kuridhia mkataba wa kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika wa Mwaka 2019; kwa kuzingatia kuridhiwa kwa mashaka mkataba huu isipokuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano katika Mkutano wake wa Kumi na Tatu; na kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977; tunaomba Bunge lako Tukufu liazimie kuridhia mkataba wa kuanzisha Taasisi

ya Dawa ya Afrika wa Mwaka 2019 isipokuwa Ibara ya 6(i) 6(m) na 6(o) ambazo zinaridhiwa kwa mashaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**MAELEZO YA UMMY ALLY MWALIMU (MB), WAZIRI WA AFYA AKIWASILISHA MAPENDEKEZO YA KURIDHIA MKATABA WA KUANZISHA TAASISI YA DAWA YA AFRIKA YA MWAKA 2019 AGENCY - AMA) KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA TAREHE 31 OKTOBA, 2023 (TREATY FOR THE ESTABLISHMENT OF THE AFRICAN MEDICINES – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha maelezo ya Azimio la Bunge kuhusu Mapendekezo ya kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika wa Mwaka 2019 (Treaty for the Establishment of The African Medicines Agency – AMA).

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee naomba uniruhusu nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mhe. **Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb**), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aidha natoa pongezi na kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika jitihada zao zinaonekana katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Tunawapongeza sana kwa kuendelea kufanya uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya kutolea huduma za afya, ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa vya uchunguzi wa magonjwa, kuongeza bajeti kwa ajili ya ununuzi wa dawa na bidhaa nyingine za afya na kuimarisha upatikanaji wa wataalam wa afya.

**Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kumpongeza **Mhe. Dkt. Dotto Mashaka Biteko** kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Naibu

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, kwa kuongoza vyema Bunge letu na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. **Aidha, nakupongeza kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (Inter-Parlimenatary Union). Uchaguzi wako umeleta heshima kubwa kwa Tanzania na watanzani**a. Vile vile nawapongeza Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia vyema katika kuliendesha Bunge letu. Pia ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga Sheria pamoja na kuisimamia Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI inayoongozwa na Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo - Mwenyekiti wa Kamati, na Mhe. Faustine Ndungulile - Makamu Mwenyekiti, kwa ushirikiano na ushauri mzuri waliotupatia wakati wa kupitia Mkataba huu mbele ya Kamati. Kamati hii ilifanya kazi kubwa ya kuchambua Mkataba huu kwa makini, weledi na umahiri mkubwa na kuishauri Serikali ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, Sera ya Afya ya Mwaka 2007 inasisitiza kuhusu umuhimu wa upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vyenye ubora unaotakiwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya hapa nchini. Hii ni kutokana na umuhimu wa bidhaa tiba katika kupambana na kudhibiti magonjwa. Hivyo, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa bidhaa tiba zenye ubora, usalama na ufanisi unaotakiwa zinapatikana wakati wote katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza Sera ya Afya ya Mwaka 2007, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imepewa jukumu la kudhibiti bidhaa tiba chini ya Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219. Sheria hii imeweka mifumo thabiti ya udhibiti wa bidhaa tiba kwa kuhakikisha kuwa bidhaa tiba zinazoingizwa au

kutengenezwa nchini ni bora, salama na zenye ufanisi. Hivyo, ili bidhaa tiba ziweze kuruhusiwa kuingizwa au kutengenezwa na kutumika nchini, ni lazima ziwe zimekidhi masharti ya Sheria hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** TMDA imefanikiwa kuwa miongoni mwa Taasisi bora zenye uwezo wa kudhibiti bidhaa tiba, na hivyo kutambuliwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kuwa imefikia kiwango cha ngazi ya tatu (Maturity level three) kati ya ngazi nne za umahiri. Hii ina maana kwamba, mifumo ya udhibiti wa bidhaa tiba inayotumika nchini inakidhi viwango vinavyokubalika kimataifa. TMDA ilifikia hatua hiyo mwaka 2018 na ilikuwa Taasisi ya Kwanza barani Afrika. Taasisi ambazo zimefikia hatua hiyo baada ya TMDA ni Food and Drugs Authority (FDA) - Ghana, National Agency for Food and Drug Administration and Control (NAFDAC) - Nigeria na Egyptian Drug Authority (EDA) - Misri.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio hayo, TMDA inakabiliwa na changamoto mbalimbali katika udhibiti wa bidhaa tiba. Changamoto hizo ni pamoja na upungufu wa wataalamu, uwepo wa njia zisizo rasmi katika maeneo ya mipaka na vituo vya forodha visivyoruhusiwa kuingiza bidhaa tiba. Changamoto nyingine ni mabadiliko ya mara kwa mara ya teknolojia yanayohitaji mbinu mpya na weledi maalumu katika kudhibiti bidhaa tiba, hali ambayo inahatarisha afya ya jamii kwa kuwa bidhaa tiba duni na bandia zisizofaa kwa matumizi ya binadamu zinaendelea kuwepo katika soko.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza jitihada za pamoja za kutatua changamoto hizo, Wakuu wa Nchi na Serikali za Jumuiya ya Umoja wa Afrika (AU) katika mkutano wa kawaida wa 32 (Assembly/AU/Dec. 735(XXXII)) uliofanyika Addis Ababa Ethiopia tarehe 11 Februari, 2019, walikubaliana kuanzishwa kwa Taasisi ya Dawa ya Afrika (African Medicines Agency – AMA).

**Mheshimiwa Spika,** Lengo la Taasisi hii ni kuratibu na kusaidia nchi wanachama wa AU katika kuboresha uwezo wa kudhibiti ubora wa bidhaa tiba hususan katika maeneo ambayo ni changamoto kwa nchi nyingi barani Afrika**.** Aidha, ili taasisi hiyo ianze kufanya kazi, nchi wanachama zinatakiwa kusaini na kuridhia Mkataba

huo. Hadi kufikia tarehe 31 Julai, 2023 jumla ya nchi 30 zimesaini na kati ya hizo 23 zimeridhia Mkataba wa AMA zikiwemo Rwanda na Uganda. Kwa kuwa masharti ya kuanzisha AMA ilikuwa ni nchi 15 kuridhia Mkataba, AMA ilianzishwa tarehe 5 Novemba 2021. Tanzania ilisaini Mkataba huo tarehe 10 Agosti, 2021 na hatua inayofuata ni kuridhia ili kujiunga na Taasisi hiyo.

**VIPENGELE VYA MKATABA WA AMA**

**Mheshimiwa Spika,** Mkataba huu umegawanyika katika sehemu Kuu sita na Ibara 41 kama ilivyoainishwa hapa chini.

**SEHEMU YA KWANZA: VIFUPISHO, TAFSIRI, KUUNDWA KWA AMA NA MADHUMUNI**

Sehemu hii inaainisha Ibara 6 zinazohusu AMA na madhumuni yake kama ifuatavyo:

**Ibara ya 1: Vifupisho vya maneno**

Ibara hii inafafanua vifupisho vya maneno yaliyotumika katika Mkataba.

**Ibara ya 2: Tafsiri ya maneno**

Ibara hii inatoa tafsiri ya misamiati iliyotumika katika Mkataba.

**Ibara ya 3: Uanzishwaji wa AMA**

Ibara hii inaelezea uanzishwaji wa AMA kama taasisi maalum chini ya AU.

Ibara ya 4: Madhumuni ya AMA

Ibara hii inaelezea madhumuni ya AMA kuwa ni kuimarisha uwezo wa nchi wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda kudhibiti bidhaa tiba ili kuhakikisha zinapatikana kwa haraka zikiwa zenye ubora, ufanisi na salama.

Ibara ya 5: Kanuni Elekezi

Ibara hii inaainisha kanuni elekezi (guiding principles) saba (7) za AMA ikiwemo uongozi, kuaminika, umiliki, uwazi na uwajibikaji, kuongeza thamani, usiri na usimamizi bora.

Ibara ya 6: Majukumu ya AMA
Ibara hii inaelezea majukumu ya AMA ambayo ni: -

a. Kuratibu na kuimarisha jitihada za kuwianisha mifumo ya udhibiti wa bidhaa tiba na kuboresha umahiri wa wakaguzi wa viwanda kulingana na miongozo ya utengenezaji bora wa bidhaa tiba;

b. Kuratibu ukusanyaji, usimamizi, utunzaji na kubadilishana taarifa za bidhaa tiba zikiwemo zile duni na bandia kwa nchi wanachama na dunia kwa ujumla;

c. Kuratibu tathmini za pamoja za maombi ya majaribio ya bidhaa tiba na kutoa msaada wa kitaalamu katika uchunguzi wa kimaabara kwa nchi wanachama ambazo hazina huduma hizo;

d. Kuhamasisha kuridhiwa na kuwianishwa kwa sera, miongozo, masharti na mifumo ya udhibiti iliyopo kupitia Jumuiya za Kikanda na taasisi za huduma za afya;

e. Kuteua, kuhamasisha, kuimarisha, kuratibu na kufuatilia vituo vya kikanda vya umahiri wa udhibiti kwa lengo la kujenga uwezo wa wataalamu wa udhibiti wa bidhaa tiba;

f. Kuratibu na kushirikisha, pale inapobidi masuala ya ukaguzi wa viwanda vya bidhaa tiba ikiwemo kusimamia udhibiti na ufuatiliaji wa usalama kama itakavyoelekezwa na kuhakikisha kwamba ripoti zinawasilishwa kwa nchi wanachama wa AMA;

g. Kuhamasisha ushirikiano na ubia, na kuhakikisha kuwa mamlaka za udhibiti zinatambua maamuzi yanayofikiwa katika ngazi mbalimbali na kuziunga mkono mamlaka hizo katika kupata rasilimali fedha na watu ili AMA iweze kuwa endelevu;

h. Kufanya mikutano kwa kushirikiana na WHO, taasisi za udhibiti na mashirika mengine yanayohusiana na udhibiti wa bidhaa tiba Afrika;

i. Kutoa miongozo na maoni ya kisayansi na kiudhibiti kuhusu miundo ya udhibiti wa bidhaa tiba wakati wa dharura na milipuko inayoathiri afya ya jamii katika bara la Afrika, hususan wakati wa uchunguzi na majaribio ya bidhaa tiba mpya;

j. Kutathmini, kujadili na kutoa mwongozo kwenye masuala ya kiudhibiti yaliyopo ndani ya mamlaka ya AMA au pale inapoombwa na AU, Jumuiya za kiuchumi za kikanda au nchi wanachama;

k. Kutoa Mwongozo wa udhibiti wa bidhaa za tiba asili;

l. Kutoa ushauri juu ya usajili wa bidhaa tiba za kipaumbele au kemikali zinazopendekezwa na maabara za uchunguzi wa ubora;

m. Kusimamia soko la bidhaa tiba kupitia ukusanyaji wa sampuli za kimaabara kutoka kwa nchi wanachama ili kuhakikisha ubora wa bidhaa husika na kuzifanyia tathmini na kutoa majibu kwa nchi hizo na pande zingine zenye maslahi ili kuwawezesha kuwa na taarifa za kuaminika kuhusiana na ubora wa dawa zinazopatikana katika nchi hizo na ikiwezekana wachukue hatua stahiki;

n. Kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya uimara wa mifumo ya udhibiti wa dawa kwa kila nchi kwa lengo la kupendekeza namna ya kuboresha na kuongeza ufanisi;

o. Kufanya tathmini na maamuzi juu ya bidhaa tiba zitakazochaguliwa au kemikali za matibabu zikiwemo zile zinazohitaji utaalamu maalumu kwa ajili ya matibabu ya magonjwa ya kipaumbele kama itakavyoamuliwa na AU au WHO;

p. Kutoa msaada wa kitaalamu na rasilimali, pale inapowezekana katika masuala ya udhibiti kwa nchi wanachama zinazoomba msaada na wataalamu wabobezi na kuimarisha uwezo katika matumizi bora ya rasilimali zilizopo;

q. Kuratibu upatikanaji wa huduma za kimaabara za uchunguzi wa ubora zilizopo kwenye nchi wanachama na Jumuiya za Kikanda; na

r. Kuhamasisha kuhusu nchi wanachama na Jumuiya za kikanda kutumia muundo wa Sheria ya mfano ya AU inayohusu udhibiti wa bidhaa za dawa katika kuwianisha sheria za kiudhibiti barani Afrika.

**SEHEMU YA PILI: HADHI YA AMA NA WATUMISHI WAKE**

Sehemu hii inajumuisha Ibara ya 7 hadi 9 kama ifuatavyo: -

Ibara ya 7: Hadhi ya kisheria

Ibara hii inaainisha kuwa AMA itakuwa na hadhi ya kisheria inayoweza kuingia mikataba, uwezo wa kumiliki mali na kuuza au kushitaki na kujiteteta pale inaposhitakiwa.

Ibara ya 8: Kinga na Upendeleo

Ibara hii inaeleza masharti yatakayotumika kuhusu kinga na upendeleo kwa AMA na watumishi wake ambapo inabainisha kuwa yatafanana na masharti ya itifaki za masuala ya kinga na upendeleo kwa Umoja wa Afrika.

Ibara ya 9: Makao Makuu ya AMA

Ibara hii inafafanua kuwa Makao Makuu ya AMA yatatokana na uamuzi wa wakuu wa nchi za AU na nchi itakayochaguliwa itaingia Mkataba wa uenyeji (Host Agreement) na AU.

SEHEMUYA TATU: MUUNDO WA UTAWALA

Sehemu hii inajumuisha Ibara ya 10 - 25 zinazoeleza muundo wa kiutendaji wa AMA na inajumuisha masharti yafuatayo:-

Ibara ya 10: Muundo wa AMA
Ibara hii inafafanua muundo wa AMA kuwa utajumuisha Mkutano Mkuu wa nchi wanachama zilizoridhia Mkataba, Bodi Tendaji, Sekretarieti na Kamati za Kitaalamu.

Ibara ya 11: Mkutano Mkuu wa nchi Wanachama
Ibara hii inaeleza kuwa chombo cha juu cha maamuzi ya AMA ni mkutano mkuu wa nchi wanachama zilizoridhia Mkataba.

**Ibara ya 12: Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Nchi Wanachama**
Ibara hii inaeleza wajumbe wa mkutano wa nchi wanachama ambao watakuwa Mawaziri wenye dhamana ya afya au wawakilishi wao. Mkutano huo utachagua Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na mchukua taarifa (rapporteur) kwa mfumo wa mzunguko wa mazingira ya kijiografia ya nchi wanachama. Viongozi waliochaguliwa watakuwa madarakani kwa muda wa miaka miwili na watakutana mara moja kwa kila mwaka. Ibara inaendelea kufafanua zaidi kwamba endapo Mwenyekiti hatakuwepo, Makamu Mwenyekiti au mchukua taarifa atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano. Vilevile, imeelezwa kuwa waangalizi wa mkutano wanaweza kualikwa isipokuwa hawatakuwa na haki ya kupiga kura.

Ibara ya 13: Mikutano Mikuu ya nchi wanachama
Ibara hii inaeleza kuhusu masharti ya kipindi cha mkutano wa kawaida wa nchi wanachama ambao utafanyika angalau mara moja kwa kila miaka miwili na ule wa dharura utategemea maombi ya Spika au viongozi wenzake ama kuombwa na theluthi mbili ya nchi wanachama. Aidha, akidi ya mkutano itakuwa ni uwepo wa wanachama wengi waliohudhuria. Maamuzi yatafanyika kwa maridhiano na iwapo maridhiano hayatafikiwa, uamuzi utapitishwa na theluthi mbili ya wanachama kuafiki maamuzi.

Ibara ya 14: Majukumu ya Mkutano Mkuu wa Nchi Wanachama
Ibara hii inaeleza majukumu ya Mkutano Mkuu wa nchi wanachama ambayo yanajumuisha kupanga viwango vya michango ya fedha za bajeti ya kuendesha AMA, kuteua na kuwaondoa wajumbe wa Bodi ya AMA, kuweka kanuni na

majukumu ya Mkurugenzi Mkuu wa AMA na miongozo ya utendaji wa Sekretarieti. Majukumu mengine yanayofafanuliwa ni mwongozo wa kisera wa AMA, kupendekeza makao makuu ya AMA kwa mujibu wa vigezo vya AU vya mwaka 2005, Kuidhinisha Vituo vya Umahiri wa Udhibiti (centres of excellence), Kupitisha masharti ya utendaji wa wajumbe wa Bodi, taratibu na Kanuni za uendeshaji na kupendekeza marekebisho yoyote ya Mkataba wa AMA.

Ibara ya 15: Uanzishwaji wa Bodi Tendaji
Ibara hii inaeleza kuwa Bodi ya AMA itateuliwa na kuwajibika kwa Mkutano Mkuu wa Nchi wanachama.

Ibara ya 16: Wajumbe wa Bodi Tendaji
Ibara hii inaeleza bayana kuwa Bodi itakuwa na wajumbe tisa (9). Kati ya hao, wajumbe watano (5) ni Watendaji Wakuu wa Taasisi za Udhibiti kutoka kila Jumuiya za Kikanda inayotambuliwa na AU, mjumbe mmoja (1) mwakilishi wa Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda kwa mzunguko, mwakilishi mmoja (1) kutoka Taasisi za Afya kwa mzunguko, mwakilishi mmoja (1) wa kamati za kitaifa za masuala ya bioethics na Kamishna wa huduma za Jamii wa AU.

Ibara ya 17: Vikao vya Bodi Tendaji
Ibara hii inaeleza kuwa Bodi itaitisha mkutano wa kawaida angalau mara moja kwa mwaka na kama kuna dharura utaitishwa na Mwenyekiti wa Bodi, Viongozi wa Mkutano wa nchi wanachama au wajumbe walio wengi wa Bodi. Akidi ya wajumbe itakuwa ni theluthi mbili ya wajumbe na maamuzi yake yatakuwa ni yale yaliyoungwa mkono au kupigiwa kura na wajumbe wengi waliopo kwenye kikao.

Ibara ya 18: Majukumu ya Bodi Tendaji
Ibara hii inafafanua majukumu ya Bodi ya AMA ambayo ni pamoja na kuidhinisha mpango mkakati, mpango kazi na bajeti itakayoandaliwa na Mkurugenzi Mkuu, kupendekeza jina la Mkurugenzi Mkuu kwenye Mkutano Mkuu wa nchi wanachama, Kuteua au kumtengua Mkurugenzi Mkuu na Mkaguzi huru wa AMA, kuweka masharti ya utumishi wa Sekretarieti, kusaidia Sekretarieti kutafuta rasilimali, kuunda kamati za kitaalamu,

kuweka kanuni za kutoa maoni ya kisayansi ya kuruhusu dawa wakati wa mlipuko wa magonjwa na kutekeleza majukumu yatakayoelekezwa na Mkutano Mkuu wa nchi wanachama.

Ibara ya 19: Muda wa wajumbe kutumikia Bodi Tendaji
Ibara hii inaweka muda ambao wajumbe wa Bodi watahudumu ambapo ni miaka mitatu kutoka kuteuliwa kwao na hawatateuliwa kwa kipindi kingine. Wajumbe wawakilishi watahudumu kwa miaka miwili (2) isipokuwa Kamishna wa Huduma za Kijamii ambaye atakuwa mjumbe wa kudumu. Spika wa Bodi atatumikia kwa muda wa miaka mitatu (3) na hataweza kuteuliwa tena. Spika na wajumbe watateuliwa kutoka miongoni mwa wakuu wa taasisi za udhibiti za nchi wanachama kwa mzunguko.

**Ibara ya 20: Uanzishwaji wa kamati za Kitaalamu za AMA** Ibara hii inafafanua uanzishwaji wa kamati za kitaalamu za muda na za kudumu ambazo zitaundwa na Bodi ya AMA. Vilevile, inaainisha huduma maalum za kitaalamu zitakazotolewa na kamati hizo kama vile tathmini ya bidhaa tiba zitokanazo na jeni (gene), seli, tishu(tissue) kwa ajili ya magonjwa ya saratani na misuli ; bidhaa tiba zinazotumika wakati wa dharura, bidhaa tiba zisizopewa kipaumbele, ukaguzi wa viwanda vinavyozalisha viambata hai, bidhaa tiba zinazohitaji utaalamu wa hali ya juu, uchunguzi wa kimaabara wa bidhaa tiba, ulinganifu hai, ufuatiliaji wa madhara yatokanayo na matumizi ya bidhaa tiba na tiba asili.

Ibara ya 21: Majukumu ya Kamati za Kitaalamu
Ibara hii inaweka masharti ya kazi za kamati za kitaalamu yanayo jumuisha kufanya tathmini ya kisayansi kwa maombi yote ya usajili, ukaguzi wa viwanda, maoni ya kisayansi ya kitaalamu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya AMA. Kamati hizo pia zinaweza kufanya kazi yoyote itakayo elekezwa na Bodi ya AMA.

Ibara ya 22: Muundo wa Kamati za Kitaalamu
Kamati za kitaalamu zitakuwa na wajumbe wasiozidi tisa (9) wenye ubobezi na uzoefu katika udhibiti wa bidhaa tiba. Wajumbe watateuliwa na Bodi ya AMA kutoka katika Taasisi za udhibiti wa bidhaa tiba za nchi wanachama kwa uwakilishi wa maeneo ya

kijiografia. Wataalamu kwenye maeneo mengine wanaweza kutoka nje ya Afrika kadri itakavyohitajika.

Ibara ya 23: Sekretarieti ya AMA
Ibara hii inafafanua majukumu ya Sekretarieti ya AMA itakayokuwa katika makao makuu ya AMA na itawajibika kuratibu na kutekeleza maamuzi ya Mkutano Mkuu wa Nchi wanachama, Chombo cha kisera cha AU na Bodi ya AMA. Aidha, Sekretarieti itaratibu mipango na kazi ya kamati za Kitaalamu na Bodi, kuanzisha na kujenga uwezo wa mifumo ya udhibiti kwa manufaa ya nchi wanachama.

Ibara ya 24: Mkurugenzi Mkuu wa AMA
Mkurugenzi Mkuu atakuwa kiongozi wa Sekretarieti na atakuwa msimamizi wa shughuli za kila siku za AMA. Mkurugenzi Mkuu atateuliwa na Mkutano wa nchi wanachama baada ya kupendekezwa na Bodi tendaji na atakuwa afisa mtendaji mkuu anayewakilisha AMA katika masuala yote. Aidha, atawajibika kwenye Bodi, Mkutano Mkuu wa nchi wanachama na AU. Mkurugenzi Mkuu atatumikia ofisi kwa kipindi cha miaka minne (4) na anaweza kutumikia tena kwa kipindi kingine kimoja kwa kuzingatia mzunguko wa kikanda.

Ibara ya 25: Mapingamizi kuhusu maoni ya kisayansi
Ibara hii inaeleza kuwa, endapo mtu yeyote au taasisi itakuwa na pingamizi kuhusu maoni, ushauri au uamuzi uliotolewa na AMA, anaweza kuwasilisha pingamizi lake kwenye Bodi. Baada ya kupokea pingamizi hilo, Bodi itaunda kamati huru kwa ajili ya kushughulikia pingamizi hilo kwa mujibu wa taratibu zilizokubaliwa.

SEHEMU YA NNE: MASHARTI YA FEDHA Ibara ya 26: Rasilimali fedha
Ibara hii inaainisha masharti ya upatikanaji wa fedha ambapo Mkutano Mkuu wa Wanachama utapanga viwango vya michango kwa kila nchi mwanachama, utapitisha bajeti ya mwaka ya AMA itakayosimamiwa kwa mujibu wa kanuni zitakazoandaliwa na AMA, na kwamba Mkutano Mkuu utaamua hatua za kuchukua kwa nchi ambayo haitachangia kwenye bajeti ya AMA kwa mujibu wa utaratibu utakaowekwa. Aidha, AMA itapanga namna ya kupata fedha za uendeshaji ikiwemo

kupokea misaada, mikopo, michango na fedha zinazotokana na shughuli zao za huduma kwa mashirika ya kimataifa, serikali, sekta binafsi au vyombo vingine kadri itakavyopangwa na Mkutano Mkuu wa nchi wanachama.

Ibara ya 27: Gharama
Ibara hii inafafanua gharama za uendeshwaji wa Sekretarieti kwa mujibu wa mpango kazi ulioidhinishwa. Akaunti za fedha za AMA zitakaguliwa na mkaguzi huru atakayeteuliwa na Bodi.

SEHEMU YA TANO: UHUSIANO NA NCHI WANACHAMA NA WABIA WENGINE Ibara ya 28: Uhusiano na AU
Ibara hii inaeleza kuwa AMA itafanya kazi kwa kushirikiana na AU na itawasilisha taarifa ya utendaji kazi ya kila mwaka kwa AU.

Ibara ya 29: Uhusiano na Mataifa
Ibara hii inaainisha mahusiano ya AMA na nchi wanachama na wasio wanachama wa AU na kuweka utaratibu wa kuteua waratibu wa kazi za AMA katika kila nchi.

Ibara ya 30: Uhusiano na mashirika na Taasisi nyingine
Ibara hii inaweka masharti ya ushirikiano na WHO, Kituo cha kuzuia na kudhibiti magonjwa Afrika, Jumuiya za Uchumi za kikanda, Wakala za Umoja wa Mataifa (UN) na mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali katika kutekeleza malengo ya Mkataba huu.

SEHEMU YA SITA: Masharti mengineyo (IBARA YA 31 – 41) Ibara ya 31: Lugha
Lugha zitakazotumika ni lugha za AU ambazo ni Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa na Kireno.

Ibara ya 32: Usuluhishi wa Migogoro
Ibara hii inaeleza kuwa endapo mgogoro utaibuka kuhusiana na tafsiri, matumizi na utekelezaji wa Mkataba huu utasuluhishwa kwa njia ya mazungumzo na mapatano kwa amani. Aidha, ikitokea kuwa ufumbuzi haujapatikana kwa njia ya usuluhishi, mgogoro huo unaweza kuwasilishwa kwa waamuzi watatu (3) ambao kila upande utateua muamuzi mmoja na muamuzi wa tatu atakuwa Mwenyekiti wa Baraza la Uamuzi atakaeteuliwa na pande zote.

Uamuzi wa waamuzi utazifunga pande zote. Pia mgogoro unaweza kuwasilishwa katika Mahakama ya Haki za Binadamu ya Afrika.

Ibara ya 33: Masharti ya kuridhia kwa mashaka
Ibara hii inaeleza kuwa nchi mwanachama wakati wa kuridhia ina haki ya kuridhia kwa mashaka baadhi ya masharti ya Mkataba huu. Masharti hayo hayapaswi kuwa kinyume na madhumuni ya Mkataba huu. Hata hivyo, masharti ya kuridhia kwa mashaka yanaweza kuondolewa wakati wowote kwa kumjulisha kwa maandishi Mwenyekiti wa Tume ya AU.

Ibara ya 34: Kujitoa
Ibara hii inaainisha masharti ya nchi mwanachama kujitoa kwenye uanachama ambapo itatakiwa kuwasilisha taarifa ya maandishi. Kujitoa huko kutaanza kuhesabika baada ya mwaka mmoja tangu tarehe ya notisi au kadri itavyoainishwa kwenye notisi ya kujitoa.

Ibara ya 35: Kufutwa
Ibara hii inaeleza kuwa AMA inaweza kufutwa baada ya theluthi mbili ya nchi wanachama kukubaliana kwenye Mkutano Mkuu wa nchi wanachama na baada ya kupitishwa na Mkutano wa AU. Aidha, pale ambapo kufutwa kwa AMA kutajadiliwa, itatakiwa kutolewa notisi ya angalau miezi sita (6) kabla ya Mkutano mkuu wa nchi wanachama. Makubaliano ya kufutwa kwa AMA yatakapofikiwa, Mkutano mkuu wa nchi wanachama wataanzisha namna ya mgawanyo wa mali za AMA.

Ibara ya 36: Marekebisho na Mapitio
Ibara hii inaeleza kuwa nchi mwanachama inaweza kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho au mapitio na mapendekezo hayo yatajadiliwa katika Mkutano mkuu wa nchi wanachama. Mapendekezo yatawasilishwa kwa Mwenyekiti wa AU ambaye atayawasilisha kwa Mwenyekiti wa Bodi tendaji. Pale ambapo mapendekezo yatakubaliwa na Mkutano wa nchi wanachama yataanza kutumika kwa mujibu wa Ibara ya 38 ya Mkataba.

Ibara ya 37: Utaratibu wa kusaini na kuridhia
Ibara hii inaeleza kuwa nchi mwanachama inaweza kusaini na kisha kuridhia na kuwasilisha hati ya kuridhia kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Nchi za Afrika

Ibara ya 38: Kuanza kutumika
Ibara hii inaainisha kuanza kutumika kwa Mkataba kuwa ni siku 30 baada ya nchi wanachama 15 kuwasilisha hati za kuridhia Mkataba kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Nchi za Afrika. Kwa nchi itakayoridhia baada ya kuanza kutumika Mkataba huu, tarehe ya kuwasilisha hati ndiyo itakuwa siku ya kuanza kutumika kwa Mkataba kwa nchi husika.

Ibara ya 39: Uwasilishaji wa Hati
Ibara hii inaeleza kuwa hati ya kuridhia Mkataba iwasilishwe kwa Mwenyekiti wa AU ambaye atasambaza kwa nchi wanachama zilizoridhia.

Ibara ya 40: Usajili wa Mkataba
Ibara hii inaeleza kuwa baada ya kuanza kutumika kwa Mkataba huu, Mwenyekiti wa Tume atasajili Mkataba huu kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kwa mujibu wa Ibara ya 102 ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa.

Ibara ya 41: Nakala halali za Mkataba
Ibara hii inaeleza kuwa Mkataba huu umeandaliwa katika nakala halisi nne (4) katika lugha ya Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa na Kireno ambapo zote ni nyaraka halali.

IBARA ZINAZOPENDEKEZWA KURIDHIWA NA KUTORIDHIWA

**Mheshimwa Spika,** Kwa kuzingatia maslahi ya nchi, wasilisho hili linapendekeza kuwa Mkataba wa kuanzishwa AMA uridhiwe isipokuwa ibara 6 (i), (m) na (o).

Ibara ya 6(i) inapendekezwa kutoridhiwa kwa kuwa inaipa AMA jukumu la kutoa maelekezo na maoni ya kisayansi wakati wa milipuko ya magonjwa, dharura na majaribio ya dawa. Hivyo, kuridhiwa kwa ibara hiyo kunaweza kuhatarisha usalama wa nchi

kwa kuruhusu dawa kutumika bila nchi kujiridhisha kuhusu ufanisi na usalama wake.

Vilevile, ibara ya 6(m) inapendekezwa kutoridhiwa kwa kuwa jukumu la kusimamia na kuchukua sampuli na kuzichunguza ubora wake ni jukumu la kitaifa ambapo Tanzania ina mfumo wa kutekeleza jukumu hilo ikiwa ni pamoja na kuwa na maabara inayotambuliwa na Shirika la Afya Duniani. Hivyo, kuridhia ibara hiyo kutasababisha mgongano wa kimajukumu kati ya AMA na TMDA.

Aidha, Ibara ya 6(o) inapendekezwa kutoridhiwa kutokana na AMA kuwa mamlaka ya kuamua bidhaa tiba ambazo zitafanyiwa tathmini kama itakavyoamuliwa na AU au WHO. Hivyo, nchi itakosa uhuru wa kuamua aina ya bidhaa tiba zitakazofanyiwa tathmini na kusajiliwa kwa kuzingatia vipaumbele vya nchi. Ibara hii pia, itaathiri maslahi ya Taifa ikiwa ni pamoja na kupoteza mapato yatokanayo na tathmini na usajili wa bidhaa hizo nchini.

IBARA ZINAZOPENDEKEZWA KUFANYIWA MAREKEBISHO

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia maslahi ya nchi katika kuridhia Mkataba wa AMA, baadhi ya Ibara zinapendekezwa kufanyiwa marekebisho baada ya kuridhiwa kwa kutumia fursa ya ibara ya 36(1) kuwasilisha mapendekezo ya kurekebisha ibara ya 26(1)(a), 26(4) na 31.

Ibara ya 26(1)(a) inapendekezwa kuridhiwa kwa matarajio ya kufanyiwa marekebisho ili iendane na taratibu zinazotumika na Taasisi nyingine zilizo chini ya AU kuhusu chanzo cha bajeti ya uendeshaji wa Taasisi hizo. Aidha, Ibara ya 26(4) inapendekezwa kuwa fedha za uendeshaji wa AMA zisimamiwe na kanuni za Jumuiya ya Umoja wa Afrika badala ya kusimamiwa kwa kutumia kanuni zitakazoanzishwa na AMA.

Vilevile, Ibara 31 na 41 zimebainisha kuwa lugha zitakazotumika ni lugha za AU ambazo ni Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa na Kireno. Aidha, kwa kuwa lugha ya Kiswahili imepitishwa kama lugha rasmi katika shughuli za AU, Serikali itatumia fursa ya ibara ya 36(1)

kuwasilisha mapendekezo ya kurekebisha ibara hizo ili isomeke kuwa "Lugha rasmi za AU ndizo zitakazotumika katika uendeshaji wa shughuli za AMA". Lengo la mapendekezo hayo ni kutoa fursa kwa lugha zinazotambuliwa na AU ikiwa ni pamoja na Kiswahili kutumika katika uendeshaji wa shughuli za AMA.

**Mheshimiwa Spika**, Endapo Tanzania itaridhia utekelezaji wa AMA, upo uwezekano kwa nchi kupata manufaa zaidi ikiwa ni pamoja na;

a. Kuimarika kwa mfumo wa udhibiti wa bidhaatiba na hivyo kuweza kudhibiti bidhaa ambazo kwa sasa hazijaanza kudhibitiwa kama vile viambata hai, damu na bidhaa zake, tiba za kijenetiki na chembe msingi (stem cells);

b. Kuwezesha viwanda vya bidhaa tiba vya hapa nchini kuwasilisha taarifa kwa nchi wanachama wa AMA za kuomba usajili zenye vigezo vinavyofanana na hivyo kupunguza usumbufu na muda wa kusajili bidhaa zao katika nchi hizo;

c. Kuimarika kwa mifumo ya udhibiti wa bidhaa tiba duni na bandia na hivyo kuwezesha kukabiliana na bidhaa tiba zinazopitishwa kwa kutumia njia zisizo rasmi katika mipaka ya nchi jirani;

d. Kukua kwa soko la bidhaa tiba za viwanda vya ndani kutokana na kuwianishwa kwa masharti ya usajili wa bidhaa tiba kwa nchi wanachama kama ilivyo ainishwa katika Mkataba wa AMA;

e. Kuwezesha usajili na upatikanaji wa bidhaa tiba kwa haraka pamoja na kupunguza gharama zinazotokana na taratibu za usajili wa bidhaa hizo, kwa kuwianisha mifumo ya usajili na kuondoa utaratibu wa sasa ambapo kila nchi huhitaji kukagua viwanda vinavyozalisha bidhaa tiba miongoni mwa nchi wanachama wa AMA;

f. Kuimarika kwa mifumo ya udhibiti wa bidhaa tiba duni na bandia miongoni mwa nchi wanachama wa AMA kutokana na kurekebishwa kwa mfumo wa kisheria wa nchi hizo kwa kuzingatia Sheria ya Mfano ya AU iliyopitishwa mwaka 2016;

g. Kuharakisha upatikanaji wa bidhaa tiba hususan wakati wa dharura na majanga kutokana na kuwa na mifumo ya usajili iliyowianishwa; na

h. Kupata taarifa kwa urahisi kutoka kwa nchi mbalimbali zilizoridhia na zinazotekeleza Mkataba.

Kwa mantiki hiyo, na kwa kutambua umuhimu wa kufikia malengo ya kitaifa na kimataifa kwa ufanisi katika kuimarisha uwezo wa nchi kudhibiti bidhaa tiba na kuhakikisha zinapatikana kwa haraka na zikiwa zenye ubora, ufanisi na salama, Serikali inaiomba Bunge lako lijadili na kuridhia pendekezo hili kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

Ummy A. Mwalimu (Mb)
**WAZIRI WA AFYA**

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Afya. *(Makofi)*

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA Bunge YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023, Nyongeza ya Nane, Kanuni ya Saba (1) (b) inazipa Kamati za Bunge za Kisekta ikiwemo Kamati ya Afya na Masuala ya

Ukimwi jukumu la kushughulikia Miswada ya Sheria na mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge ambayo ipo chini ya Wizara inayosimamia. Jukumu hili pia ni la Kikatiba chini ya Ibara ya 63 (3) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 60 (6) (b) na Kanuni za Kudumu za Bunge na kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya Ukimwi, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika ya Mwaka 2019 *(Treaty for the Establishment of Africa Medicine Agency of 2019)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupokea maelekezo ya kushughulikia jambo hili kwa mujibu wa Kanuni ya 108 (1) na (2) Kamati ilianza kutekeleza jukumu lake kwa kufanya yafuatayo: -

(a) Kufanya uchambuzi wa awali ikiwa ni pamoja na kupokea maelezo ya Sekretarieti kuhusu dhana na uchambuzi wa kisheria.

(b) Kupokea maelezo ya Serikali kuhusu mapendekezo ya Azimio la Kuridhia Mkataba husika siku ya Jumanne tarehe 17 Oktoba, 2023.

(c) Kupokea na kuchambua maoni ya wadau siku ya tarehe 18 hadi 26 Oktoba, 2023. Kamati inasikitika kutoa taarifa kuwa hakuna mdau aliyefika mbele ya Kamati au kutuma maoni na ushauri kwa njia ya maandishi kuhusu mkataba huu japokuwa Kamati ilitoa mwaliko mahsusi kwa barua zilizotumwa kuanzia tarehe 29/09/2023. Licha ya barua za mwaliko, Kamati iliomba kibali tena kwa ajili ya kutoa tangazo la mwaliko wa wadau kupitia tovuti ya Bunge, ukurasa wa *Instagram*, *Twitter* na *Facebook.* Hata hivyo, hakuna mdau yeyote aliyejitokeza kutoa maoni na ushauri kwa Kamati yetu.

(d) Kufanya uchambuzi wa Mkataba husika kwa kuzingatia uchambuzi wa awali, maelezo ya Serikali pamoja na maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilipata nafasi ya kufanya tathmini ili kupima iwapo kuna manufaa au athari ambazo Tanzania inaweza kupata ikiwa Bunge litaridhia Mkataba huu kwa kuzingatia Kanuni ya 107 (2) (f) na (g).

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 11 Februari, 2019 nchi 55 zinazounda Umoja wa Nchi za Afrika *(African Union)*, zilikutana kufanya Mkutano Jijini *Addis Ababa, Ethiopia.* Katika Mkutano huo, nchi wanachama walikubaliana kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika *(African Medicines Agency)* kwa kifupi tunaita *AMA,* kwa madhumuni ya kuimarisha uwezo wa nchi wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda kudhibiti bidhaa tiba. Nia ni kuhakikisha kuwa dawa zinapatikana kwa haraka zikiwa na ubora, ufanisi na usalama na kupunguza athari zinazoweza kuipata jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba huo ulianza kutekelezwa tarehe 5 Novemba, 2021 siku 30 baada ya nchi ya 15 kati ya nchi wanachama wa Umoja wa Afrika kuwasilisha Hati za Kuridhia Mkataba huo kwa Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika *(Chairman of the Commission)* kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 38 ya Mkataba. Miongoni mwa nchi hizo 15 ni Zimbabwe, Lesotho, Morisi, Namibia na Shelisheli ambazo ni wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(Southern African Development Community – SADC),* Rwanda na Uganda ambazo ni wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(East African Community)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu za mwenendo wa idadi ya nchi zilizosaini na kuridhia Mkataba wa Uanzishaji wa Taasisi ya Dawa ya Afrika zinaonesha kwamba nchi 37 kati ya nchi 55 zinazounda Umoja wa Afrika, sawa na asilimia 67.3 zimesaini Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika. Hadi kufikia mwezi Agosti, 2023, kati ya nchi zilizosaini, nchi 26 sawa na asilimia 70.3 zimeridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jedwali la vielelezo limeonyesha nchi zilizoridhia na zile ambazo hazijaridhia. Vilevile, Tanzania ni nchi mwanachama wa mtangamano wa Kikanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(East African Community)* yenye nchi wanachama saba. Kati ya nchi hizo, Tanzania na Burundi ni miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki ambazo zimesaini na hazijaridhia Mkataba huu. Aidha, nchi moja tu kati ya nchi saba za Afrika Mashariki haijasaini Mkataba huu. Kwa ujumla, nchi nne za Jumuiya ya Afrika Mashariki sawa na asilimia 57 zimesaini Mkataba huu na Kuridhia lakini Tanzania haimo katika nchi hizo hadi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonesha hatua zilizofikiwa na nchi wanachama wa Afrika Mashariki katika mchakato wa kuridhia Mkataba huu ambapo nchi mbili zimesaini Mkataba lakini bado hazijaridhia, nchi moja haijasaini, nchi mbili zimeridhia na kuwasilisha hati na nchi mbili zimeridhia lakini bado hazijawasilisha hati. Tumeonesha katika kielelezo katika jedwali Na. 2.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *(SADC)* yenye nchi wanachama 16, takwimu zinaonesha kwamba nchi sita kati ya nchi 16 wanachama wa *SADC*, sawa na asilimia 37.5 hazijasaini Mkataba huu, lakini nchi sita zilizosaini Mkataba huu ambazo ni sawa na asilimia 37 zimesharidhia na hivyo, Tanzania ni miongoni mwa nchi za *SADC* zilizoridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonesha hatua zilizofikiwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika katika mchakato wa kuridhia Mkataba huu ambapo nchi nne zimesaini Mkataba bado kuridhia, nchi sita hazijasaini, nchi tano zimeridhia na kuwasilisha hati na nchi moja imeridhia lakini bado haijawasilisha hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 107 na Kanuni ya Kudumu ya Bunge imeweka utaratibu wa Bunge kujadili hoja ya kuridhia Mikataba ya Kimataifa ambapo utaratibu huo unaitaka Serikali kuwasilisha hoja yake Bungeni pamoja na Mikataba iliyokusudiwa kuridhiwa kwa lengo la kutimiza masharti ya Ibara ya

63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mawanda ya Uchambuzi. Katika kufanya uchambuzi wa Mkataba huu, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 107 na Kanuni za Bunge inayotaka uchambuzi kuzingatia yafuatayo: -

(i) Jina la Mkataba na Mwaka wake;

(ii) Maudhui ya Mkataba;

(iii) Wajibu wa nchi baada ya kujiunga na mkataba unaohusika;

(iv) Uzingatiaji wa Katiba;

(v) Uzingatiaji wa Sera za Nchi;

(vi) Manufaa na athari kama zipo ambazo nchi itapata kwa kujiunga;

(vii) Mapendekezo ya kutokuridhia baadhi ya masharti kama itaonekana hivyo; na

(viii) Jambo lingine lolote lenye tija kuhusiana na mkataba huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kwa Bunge lako tukufu kuwa Kamati imepitia kwa kina sana sehemu zote sita za Mkataba zenye jumla ya Ibara 41, na kuyazingatia masharti ya Kanuni ya 107 ya Kanuni za Bunge ikiwa ni pamoja na miongoni mwa vigezo vya uchambuzi katika mchakato wa kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika wa mwaka 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wake, Kamati ilizingatia kutaka kujua maudhui ya Mkataba huu ambayo Taifa letu linataka kuridhia. Kamati imebaini kuwa msingi wa uanzishwaji wa Taasisi ya Dawa ya Afrika ni kuimarisha uwezo wa nchi

wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda katika kudhibiti bidhaa tiba ili kuhakikisha zinapatikana kwa haraka zikiwa na ubora, ufanisi na usalama na kupunguza athari zinazoweza kuipata jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, manufaa yatokanayo na kuridhia Mkataba huu, kwa mujibu wa mapendekezo yaliyowasilishwa na Serikali, kuridhia Mkataba huu kutatoa fursa na manufaa yafuatayo kwa Taifa: -

(i) Kuimarika kwa mfumo wa udhibiti na kuweza kudhibiti bidhaa ambazo kwa sasa hazijaanza kudhibitiwa kama vile viambata hai, damu na bidhaa zake, tiba za kijenetiki na chembe msingi;

(ii) Kuimarika kwa mifumo ya udhibiti wa bidhaa tiba duni na bandia;

(iii) Kuwezesha viwanda vya bidhaa tiba nchini kuwasilisha taarifa kwa nchi wanachama za kuomba usajili na kupunguza usumbufu, muda na gharama za usajili wa bidhaa zao kwa nchi hizo;

(iv) Kukua kwa soko la bidhaa tiba na viwanda vya ndani; na

(v) Kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa tiba hususan wakati wa dharura na majanga kutokana na kuwa na mifumo ya usajili iliyowianishwa;

(vi) Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa kwa kuridhia Mkataba huu, Tanzania itakuwa kwenye nafasi nzuri ya kunufaika na fursa hizo zilizotajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefanya uchambuzi wake na kuukamilisha na hivyo Kanuni za Bunge zinaeleza uwezekano wa uamuzi wa hoja kwa namna tatu ambazo ni kama ifuatavyo: -

(a) Kuridhia masharti yote ya Mkataba;

(b) Kuridhia baadhi ya masharti ya Mkataba iwapo Mkataba unaruhusu kufanya hivyo; au

(c) Kukataa kuridhia Mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ni *option* tatu ambazo tunaweza tukazichukua. Kwa kuzingatia Kanuni hii; na kwa kuwa Mkataba huu unaruhusu nchi husika kutokuridhia baadhi ya Ibara, Kamati inashauri Bunge lisiridhie kama ilivyopendekeza Serikali kwamba Ibara ya 6 (i) kuhusu kutoa miongozo na maoni ya kisayansi na kudhibiti kuruhusu miundo ya udhibiti wa bidhaa tiba wakati wa dharura na milipuko inayoathiri afya ya jamii katika Bara la Afrika, hususan wakati wa uchunguzi na majaribio ya bidhaa tiba mpya; Kamati inashauri Ibara hii isiridhiwe kwa kuwa Taasisi ya Dawa ya Afrika imepewa jukumu ambalo linaweza kuhatarisha usalama wa nchi kwa kuruhusu dawa kutumika bila nchi kujiridhisha kuhusu ufanisi na usalama wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 6 (m) kuhusu kusimamia soko la bidhaa tiba kupitia ukusanyaji wa sampuli za kimaabara kutoka kwa nchi wanachama ili kuhakikisha ubora wa bidhaa husika na kuzifanyia tathmini na kutoa majibu kwa nchi hizo na pande nyingine zenye maslahi ili kuwezesha kuwa na taarifa ya kuaminika kuhusiana na ubora wa dawa zinazopatikana katika nchi hizo na ikiwezekana kuchukua hatua stahiki; Kamati inashauri Ibara hii isiridhiwe kwa kuwa inatoa jukumu ambalo litaweza kusababisha mgongano wa Taasisi ya Dawa ya Afrika, yaani Mamlaka ya Dawa *(TMDA)*, kwani jukumu tajwa limekuwa likifanywa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania kupitia maabara ya ndani inayotambuliwa na Shirika la Afya Duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 6 (o), kuhusu kufanya tathmini na maamuzi juu ya bidhaa tiba zitakazochaguliwa au kemikali za matibabu zikiwemo zile zinazohitaji utaalamu maalumu kwa ajili ya matibabu ya magonjwa ya kipaumbele kama itakavyoamuliwa na Umoja wa Afrika au Shirika la Afya Duniani, Kamati inashauri Ibara hii isiridhiwe, kwani inakusudia kuhamisha jukumu la kufanya tathmini na kusajili bidhaa tiba kwenda Taasisi ya Dawa ya Afrika *(AMA)*. Jukumu hilo limekuwa likifanywa na

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba *(TMDA)* ambayo ni Mamlaka ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia maslahi ya nchi, katika kuridhia Mkataba huu wa *AMA*, baadhi ya Ibara zinapendekezwa kufanyiwa marekebisho baada ya Mkataba kuridhiwa kwa Ibara ya 36.

Mheshimiwa Naibu Spika, rekebisho la kwanza ni:-

(i) Ibara ya 26(1) (a) inapendekezwa kuridhiwa kwa matarajio ya kufanyiwa marekebisho ili iendane na taratibu zinazotumika na Taasisi nyingine zilizo chini ya Umoja wa Afrika kuhusu chanzo cha bajeti ya uendeshaji wa taasisi hizo;

(ii) Ibara ya 26(4) inapendekezwa kuwa fedha za uendeshaji wa *AMA* zisimamiwe na kanuni za Jumuiya ya Umoja wa Afrika badala ya kusimamiwa kwa kutumia kanuni zitakazoanzishwa na *AMA*; na

(iii) Ibara 31 imebainisha kuwa lugha zitakazotumika ni lugha za Umoja wa Afrika ambazo ni Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa na Kireno. Kamati inaona umuhimu mkubwa wa kupeleka mapendekezo ili Kiswahili kiweze kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa jumla. Pamoja na maoni na ushauri kuhusu baadhi ya Ibara za Mkataba huu. Vilevile, Kamati inatoa maoni na ushauri wa jumla kuwa Serikali izingatie mikataba ambayo ni mizuri kama huu yenye faida kwa nchi yetu na kuiwasilisha Bungeni mapema ili kuridhiwa kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mkataba huu wa kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika, nchi yetu imechelewa kuridhia tangu nchi wanachama wa Umoja wa Afrika zilipofanya Mkutano na kukubaliana mnamo Mwezi Februari, 2019 na kufikia vigezo vya kuanza kutekelezwa rasmi tarehe 5 Novemba, 2021. Kuchelewa huku kunaweza kuwa moja ya sababu zilizosababisha Makao Makuu ya Umoja huu kupelekwa Rwanda badala ya Tanzania

ambayo ina Mamlaka bora ya Dawa na Vifaa Tiba inayotambuliwa na Shirika la Afya Duniani *(WHO)* kwa kiwango cha ngazi ya tatu kati ya ngazi nne za umahiri.

Mheshimiwa Naibu Spika,

Kwa kuwa, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa nchi 55 zinazounda Umoja wa Nchi za Afrika;

Na kwa kuwa, kati ya nchi hizo 55, Tanzania ni miongoni mwa nchi 11 ambazo zimesaini Mkataba huu, lakini bado hazijaridhia *(Kama inavyoonekana katika jedwali namba 1)*.

Na kwa kuwa, kwa Tanzania kuridhia mkataba huu kutapatikana faida mbalimbali zikiwemo kuimarika kwa mfumo wa udhibiti wa bidhaa tiba duni na bandia, kukua kwa soko la bidhaa tiba za viwanda vya ndani na kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa tiba hususan wakati wa dharura na majanga.

Hivyo basi, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuridhia Mkataba wa kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika wa mwaka 2019 *(Treaty for the Establishment of the African Medicines Agency, 2019)* ili kuungana na nchi wanachama wenzetu kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa namna mnavyotimiza majukumu yenu na kwa weledi na umakini mkubwa na hivyo kuwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu Mbunge ambaye ni Waziri wa Afya pamoja na Mheshimiwa Daktari Godwin Oloyce Mollel, Mbunge na Naibu Waziri, kwa ushirikiano wanaotupa katika Kamati muda wote. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Daktari John Jingu, Naibu Katibu Mkuu, Daktari Grace Maghembe na Mganga Mkuu wa Serikali Profesa Tumaini Nagu pamoja na watendaji wote

wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakitupatia katika Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Wajumbe wa Kamati yetu, Wajumbe wote bila kuwataja majina yao. Mwisho nipende kusema kwamba ninamshukuru sana Katibu wa Bunge na watumushi wote wa Bunge na hivyo basi ninaunga mkono Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI KUHUSU AZIMIO LA BUNGE KURIDHIA MKATABA WA KUANZISHA TAASISI YA DAWA YA AFRIKA WA MWAKA 2019 *(TREATY FOR THE ESTABLISHMENT OF THE AFRICAN MEDICINES AGENCY, 2019)* – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1 Maelezo ya Awali**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, Nyongeza ya Nane, Kanuni ya 7(1) (b) inazipa Kamati za Bunge za kisekta ikiwemo kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI jukumu la kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge ambayo ipo chini ya Wizara inazozisimamia. Jukumu hili pia ni la Kikatiba chini ya Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 60(6) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, na kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika wa Mwaka 2019 *(Treaty for the Establishment of the African Medicines Agency, 2019)*.

## 1.2 Namna Kamati ilivyofanya Kazi

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kupokea maelekezo ya kulishughulikia jambo hili kwa mujibu wa Kanuni ya 108 (1) na (2), Kamati ilianza kutekeleza jukumu lake kwa kufanya yafuatayo: -

(a) Kufanya uchambuzi wa awali ikiwa ni pamoja na kupokea maelezo ya Sekretarieti kuhusu dhana na uchambuzi wa kisheria;

(b) Kupokea maelezo ya Serikali kuhusu mapendekezo ya Azimio la Kuridhia Mkataba husika siku ya Jumanne tarehe 17 Oktoba, 2023;

(c) Kupokea na kuchambua maoni ya wadau siku ya tarehe 18 hadi 26 Oktoba, 2023; Kamati inasikitika kutoa taarifa kuwa hakuna mdau aliyefika mbele ya Kamati au kutuma maoni na ushauri kwa njia ya maandishi kuhusu Mkataba huu japokuwa Kamati ilitoa mwaliko mahsusi wa barua zilizotumwa kuanzia tarehe 29/9/2023. Licha ya barua za mwaliko, Kamati iliomba kibali kwa ajili ya kutoa tangazo la mwaliko wa wadau kupitia tovuti ya bunge, ukurasa wa *Instagram, twitter* na *facebook*. Hata hivyo, hakuna mdau yeyote aliyejitokeza kutoa maoni na ushauri kwa Kamati.

(d) Kufanya uchambuzi wa Mkataba husika kwa kuzingatia uchambuzi wa awali, maelezo ya Serikali pamoja na maoni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilipata nafasi ya kufanya tathmini ili kupima iwapo kuna manufaa au athari ambazo Tanzania inaweza kupata ikiwa Bunge litaridhia Mkataba huu kwa kuzingatia Kanuni ya 107 (2) (f) na (g).

## 1.3 Chimbuko la Mkataba

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 11 Februari, 2019 nchi 55 zinazounda Umoja wa Nchi za Afrika (African Union- AU), zilikutana kufanya Mkutano Jijini Addis Ababa, Ethiopia. Katika Mkutano huo,

nchi wanachama walikubaliana kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika *(African Medicines Agency – AMA)* kwa madhumuni ya kuimarisha uwezo wa nchi wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda kudhibiti bidhaa tiba. Nia ni kuhakikisha kuwa dawa zinapatikana kwa haraka zikiwa na ubora, ufanisi na usalama na kupunguza athari zinazoweza kuipata jamii.

**Mheshimiwa Spika,** Mkataba huo ulianza kutekelezwa tarehe 5 Novemba, 2021 siku thelathini baada ya nchi ya kumi na tano kati ya nchi wanachama wa Umoja wa Afrika kuwasilisha hati ya kuridhia Mkataba huo kwa Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika *(The Chairperson of the Commission)* kama ilivyoelekezwa katika Ibara ya 38 ya Mkataba. Miongoni mwa nchi hizo 15 ni Zimbabwe, Lesotho, Morisi, Namibia na Shelisheli ambazo ni wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(Southern African Development Community- SADC)* na Rwanda na Uganda ambazo ni wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(East African Community-EAC)*.

### 1.4 Mwenendo wa Kusaini na Kuridhia Mkataba

**Mheshimiwa Spika,** takwimu za mwenendo wa idadi ya nchi zilizosaini na kuridhia Mkataba wa uanzishaji wa Taasisi ya Dawa ya Afrika zinaonesha kwamba, nchi 37 kati ya nchi 55 zinazounda Umoja wa Afrika sawa na asilimia 67.3 zimesaini Mkataba wa kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika hadi kufikia mwezi Agosti, 2023. Kati ya nchi zilizosaini, nchi 26, sawa na asilimia 70.3 zimeridhia Mkataba.

**Mheshimiwa Spika,** Jedwali Na. 1, linaonesha hatua zilizofikiwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika katika mchakato wa kuridhia Mkataba huu ambapo nchi (11) zimesaini Mkataba bado kuridhia, nchi (18) hazijasaini, nchi (21) zimeridhia na kuwasilisha hati na nchi (5) zimeridhia lakini bado hazijawasilisha hati.

**Jedwali Na. 1; Mchanganuo wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika na Hatua Zilizofikiwa katika Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika**

| Na. | Nchi zilizosaini bado kuridhia (11) | Nchi ambazo hazijasaini (18) | Nchi zilizoridhia na kuwasilisha hati (21) | Nchi zilizoridhia bado kuwasilisha hati (05) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Burundi | Angola | Algeria | Cape Verde |
| 2. | Komoro | Botswana | Benin | Kenya |
| 3. | Cote d'Ivoire | Jamhuri ya Afrika ya Kati | Burkina Faso | Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (JDK) |
| 4. | Guinea ya Ikweta | Djibouti | Kamerun | Jamhuri ya Sahara ya Kidemokrasia ya Kiarabu |
| 5. | Ethiopia | Eritrea | Chad | Senegal |
| 6. | Madagaska | Eswatini | Misri | |
| 7. | Msumbiji | Gambia | Gabon | |
| 8. | Jamhuri ya Kongo | Guinea-Bissau | Ghana | |
| 9. | Sao Tome and Principe | Liberia | Guinea | |
| 10. | Tanzania | Libya | Lesotho | |
| 11. | Togo | Malawi | Mali | |
| 12. | | Mauritania | Morisi | |
| 13. | | Nigeria | Moroko | |
| 14. | | Sudani Kusini | Namibia | |
| 15. | | Somalia | Niger | |
| 16. | | Afrika Kusini | Rwanda | |
| 17. | | Sudan | Shelisheli | |
| 18. | | Zambia | Sierra Leone | |
| 19. | | | Tunisia | |
| 20. | | | Uganda | |
| 21. | | | Zimbabwe | |

**Chanzo:** *Health Policy Watch: https://healthpolicy-watch.news/African-medicines-agency multimedia/*

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni nchi mwanachama wa mtangamano wa Kikanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) yenye nchi wanachama 7. Kati ya nchi hizo, Tanzania na Burundi ni miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki ambazo zimesaini na hazijaridhia Mkataba huu. Aidha, nchi moja tu kati ya nchi saba za Afrika Mashariki haijasaini Mkataba huu. Kwa ujumla nchi nne za Jumuiya ya Afrika Mashariki sawa na asilimia 57 zimesaini Mkataba huu na Kuridhia lakini Tanzania haimo katika nchi hizo hadi sasa.

**Mheshimiwa Spika,** Jedwali Na. 2, linaonesha hatua zilizofikiwa na nchi wanachama wa Afrika Mashariki katika mchakato wa kuridhia Mkataba huu ambapo nchi (2) zimesaini Mkataba lakini bado hazijaridhia, nchi (1) haijasaini, nchi (2) zimeridhia na kuwasilisha hati na nchi (2) zimeridhia lakini bado hazijawasilisha hati.

**Jedwali Na. 2; Hatua zilizofikiwa na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) katika Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika**

| Na | Nchi zilizosaini bado kuridhia (02) | Nchi ambazo hazijasaini (01) | Nchi zilizoridhia na kuwasilisha hati (02) | Nchi zilizoridhia bado kuwasilisha hati (02) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Burundi | Sudani Kusini | Uganda | Kenya |
| 2. | Tanzania | | Rwanda | Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (JDK) |

**Chanzo**: *Health Policy Watch: https://healthpolicy-watch.news/African-medicines-agency-multimedia/*

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) yenye nchi wanachama 16, takwimu zinaonesha kwamba, nchi 6 kati ya nchi 16 wanachama wa SADC, sawa na asilimia 37.5 hazijasaini Mkataba huu; nchi 6 zilizosaini Mkataba huu ambazo ni sawa na asilimia 37.5 zimekwisha ridhia. Hata hivyo, Tanzania si miongoni mwa nchi za SADC zilizokwisha ridhia.

**Mheshimiwa Spika,** Jedwali Na. 3, linaonesha hatua zilizofikiwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika – SADC katika mchakato wa kuridhia Mkataba huu ambapo nchi (4) zimesaini Mkataba bado kuridhia, nchi (6) hazijasaini, nchi (5) zimeridhia na kuwasilisha hati na nchi (1) imeridhia lakini bado haijawasilisha hati.

**Jedwali Na. 3; Hatua zilizofikiwa na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) katika Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika**

| Na. | Nchi zilizosaini bado kuridhia (04) | Nchi ambazo hazijasaini (06) | Nchi zilizoridhia na kuwasilisha hati (05) | Nchi zilizoridhia bado kuwasilisha hati (01) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Madagaska | Angola | Zimbabwe | Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo |
| 2. | Komoro | Botswana | Lesotho | |
| 3. | Msumbiji | Eswatini | Shelisheli | |
| 4. | Tanzania | Malawi | Mauritius | |
| 5. | | Zambia | Namibia | |
| 6. | | Afrika Kusini | | |

**Chanzo:** *Health Policy Watch: https://healthpolicy-watch.news/African-medicines-agency-multimedia/*

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 UCHAMBUZI WA KAMATI

### 2.1 Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 107 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka utaratibu wa Bunge kujadili hoja ya kuridhia Mikataba ya Kimataifa ambapo utaratibu huo unaitaka Serikali kuwasilisha hoja yake Bungeni pamoja na Mkataba inayokusudiwa kuridhiwa kwa lengo la kutimiza masharti ya Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

## 2.2 Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** katika kufanya uchambuzi wa Mkataba huu, Kamati ilizingatia masharti ya **Kanuni ya 107 (2**) ya Kanuni za Bunge inayotaka uchambuzi kuzingatia yafuatayo; -

(i) Jina la Mkataba na Mwaka;
(ii) Maudhui ya Mkataba;
(iii) Wajibu wa nchi baada ya kujiunga na mkataba unaohusika;
(iv) Uzingatiaji wa Katiba;
(v) Uzingatiaji wa Sera za Nchi;
(vi) Manufaa na Athari kama zipo ambazo nchi itapata kwa kujiunga;
(vii) Mapendekezo ya kutokuridhia baadhi ya masharti kama itaonekana hivyo; na
(viii) Jambo lingine lolote lenye tija kuhusiana na mkataba huo.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa taarifa kwa Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati imepitia kwa kina sehemu zote sita (6) za Mkataba zenye jumla ya Ibara 41, na kuyazingatia masharti ya Kanuni ya 107 (2) ya Kanuni za Bunge ikiwa kama miongoni mwa vigezo vya uchambuzi katika mchakato wa kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika wa Mwaka 2019.

## 2.3 Maudhui ya Mkataba

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati ilizingatia kutaka kujua maudhui ya Mkataba huu ambayo Taifa letu linataka kuridhia. Kamati imebaini kuwa msingi wa uanzishwaji wa Taasisi ya Dawa ya Afrika ni kuimarisha uwezo wa nchi wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda katika kudhibiti bidhaa tiba ili kuhakikisha zinapatikana kwa haraka zikiwa na ubora, ufanisi na usalama na kupunguza athari zinazoweza kuipata jamii.

## 2.4 Manufaa yatokanayo na kuridhia Mkataba huu

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa mapendekezo yaliyowasilishwa na Serikali, kuridhia Mkataba huu kutatoa fursa na manufaa yafuatayo kwa Taifa: -

i. Kuimarika kwa mfumo wa udhibiti na kuweza kudhibiti bidhaa ambazo kwa sasa hazijaanza kudhibitiwa kama vile viambata hai, damu na bidhaa zake, tiba za kijenetiki na chembe msingi;

ii. Kuimarika kwa mifumo ya udhibiti wa bidhaa tiba duni na bandia;

iii. Kuwezesha viwanda vya bidhaa tiba nchini kuwasilisha taarifa kwa nchi wanachama za kuomba usajili na kupunguza usumbufu, muda na gharama za usajili wa bidhaa zao kwa nchi hizo;

iv. Kukua kwa soko la bidhaa tiba za viwanda vya ndani; na

v. Kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa tiba hususani wakati wa dharura na majanga kutokana na kuwa na mifumo ya usajili iliyowianishwa;

**Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kuwa kwa kuridhia Mkataba huu, Tanzania itakuwa kwenye nafasi nzuri ya kunufaika na fursa hizo zilizotajwa.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wake na kuukamilisha na hivyo kuwasilisha Bungeni ili kuliwezesha Bunge kutekeleza Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba na pia kuiwezesha Serikali kuendelea na taratibu nyingine za uridhiwaji wa Mkataba huu. Hivyo, Kamati imepitia na kuchambua Mkataba huu ibara kwa ibara na kwa kuzingatia Kanuni ya 111(3) ya Kanuni za Bunge inayoelekeza uwezekano wa uamuzi wa hoja kwa namna tatu ambazo ni: -

a) Kuridhia masharti yote ya Mkataba;

b) Kuridhia baadhi ya masharti ya Mkataba iwapo Mkataba unaruhusu kufanya hivyo; au

c) Kukataa kuridhia Mkataba.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni hii, na kwa kuwa Mkataba huu unaruhusu nchi husika kutokuridhia baadhi ya Ibara, Kamati inashauri Bunge lisiridhie Ibara ya 6 (i), (m) na (o)

(i) Ibara ya 6(i), Kutoa miongozo na maoni ya kisayansi na kiudhibiti kuhusu miundo ya udhibiti wa bidhaa tiba wakati wa dharura na milipuko inayoathiri afya ya jamii katika bara la Afrika, hususan wakati wa uchunguzi na majaribio ya bidhaa tiba mpya.
Kamati inashauri ibara hii isiridhiwe kwa kuwa Taasisi ya Dawa ya Afrika imepewa jukumu ambalo linaweza kuhatarisha usalama wa Nchi kwa kuruhusu dawa kutumika bila nchi kujiridhisha kuhusu ufanisi na usalama wake.

(ii) Ibara ya 6(m), kusimamia soko la bidhaa tiba kupitia ukusanyaji wa sampuli za kimaabara kutoka kwa nchi wanachama ili kuhakikisha ubora wa bidhaa husika na kuzifanyia tathmini na kutoa majibu kwa nchi hizo na pande zingine zenye maslahi ili kuwawezesha kuwa na taarifa za kuaminika kuhusiana na ubora wa dawa zinazopatikana katika nchi hizo na ikiwezekana wachukue hatua stahiki.

Kamati inashauri ibara hii isiridhiwe kwa kuwa inatoa jukumu ambalo litaweza kusababisha mgongano kati ya Taasisi ya Dawa ya Afrika na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba- TMDA, kwani jukumu tajwa limekuwa likifanywa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania-TMDA kupitia maabara ya ndani inayotambuliwa na Shirika la Afya Duniani.

(iii) Ibara ya 6(o), kufanya tathmini na maamuzi juu ya bidhaa tiba zitakazochaguliwa au kemikali za matibabu

zikiwemo zile zinazohitaji utaalamu maalumu kwa ajili ya matibabu ya magonjwa ya kipaumbele kama itakavyoamuliwa na Umoja wa Afrika au Shirika la Afya Duniani.

Kamati inashauri ibara hii isiridhiwe kwani inakusudia kuhamisha jukumu la kufanya tathmini na kusajili bidhaa tiba kwenda Taasisi ya Dawa ya Afrika- AMA. Jukumu hilo limekuwa likifanywa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba-TMDA ambayo ni Mamlaka ya ndani.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia maslahi ya nchi katika kuridhia Mkataba wa AMA, baadhi ya ibara zinapendekezwa kufanyiwa marekebisho baada ya Mkataba kuridhiwa, kwa kuwa ibara ya 36(1) ya Mkataba inatoa fursa ya kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho. Kamati inapendekeza marekebisho ya Ibara ya 26(1)(a), 26(4) na 31.

(i) Ibara ya 26(1) (a) inapendekezwa kuridhiwa kwa matarajio ya kufanyiwa marekebisho ili iendane na taratibu zinazotumika na Taasisi nyingine zilizo chini ya Umoja wa Afrika kuhusu chanzo cha bajeti ya uendeshaji wa Taasisi hizo.

(ii) Ibara ya 26(4) inapendekezwa kuwa fedha za uendeshaji wa AMA zisimamiwe na kanuni za Jumuiya ya Umoja wa Afrika badala ya kusimamiwa kwa kutumia kanuni zitakazoanzishwa na AMA.

(iii) Ibara 31 na 41 zimebainisha kuwa lugha zitakazotumika ni lugha za Umoja wa Afrika ambazo ni Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa na Kireno. Kamati inaona umuhimu mkubwa wa kupeleka mapendekezo ya kuongeza lugha ya Kiswahili katika uendeshaji wa shughuli za AMA, kwa kuwa lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha rasmi zinazotumika katika shughuli za AU.

### 3.1 Maoni na Ushauri ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na maoni na ushauri kuhusu baadhi ya Ibara za Mkataba huu. Vilevile, Kamati inatoa maoni na ushauri wa jumla kuwa Serikali izingatie mikataba ambayo ni mizuri na yenye faida kwa nchi yetu na kuiwasilisha Bungeni mapema ili kuridhiwa kwa manufaa ya Taifa. Kwa Mkataba huu wa kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika, nchi yetu imechelewa kuridhia tangu nchi wanachama wa Umoja wa Afrika zilipofanya Mkutano na kukubaliana mnamo mwezi Februari, 2019 na kufikia vigezo vya kuanza kutekelezwa rasmi tarehe 5 Novemba 2021. Kuchelewa huku kunaweza kuwa moja ya sababu zilizosababisha Makao Makuu ya Umoja huu kupelekwa nchini Rwanda badala ya Tanzania ambayo ina Mamlaka bora ya Dawa na Vifaa Tiba inayotambuliwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa kiwango cha ngazi ya tatu kati ya ngazi nne za umahiri.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa nchi hamsini na tano (55) zinazounda Umoja wa Nchi za Afrika. Na kwa kuwa kati ya nchi hizo hamsini na tano (55), Tanzania ni miongoni mwa nchi kumi na moja ambazo zimesaini Mkataba huu lakini bado hazijaridhia (*Kama inavyoonekana katika kielelezo namba 1)*. Na kwa kuwa kwa Tanzania kuridhia mkataba huu kutapatikana faida mbalimbali zikiwemo kuimarika kwa mfumo wa udhibiti wa bidhaa tiba duni na bandia, kukua kwa soko la bidhaa tiba za viwanda vya ndani na kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa tiba hususani wakati wa dharura na majanga.

**Hivyo basi**, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuridhia Mkataba wa kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika wa Mwaka 2019 *(Treaty for the Establishment of the African Medicines Agency, 2019)* ili kuungana na nchi wanachama wenzetu kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na Mkataba huu.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa namna mnavyotimiza majukumu yenu kwa weledi na umakini

mkubwa na hivyo kuliwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Mheshimiwa Ummy Mwalimu (Mb) – Waziri wa Afya pamoja na Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel (Mb) Naibu Waziri kwa ushirikiano wanaoipa Kamati wakati wote. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. John Jingu, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Grace Maghembe na Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu pamoja na watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI pamoja na Mheshimiwa Dkt. Faustin Engelbert Ndugulile, (Mb), Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa ushirikiano mzuri ambao wananipa. Naomba kuwatambua majina yao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Dkt. Faustin Engelbert Ndugulile, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Aysharose Ndagholi Mattembe, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Bernadeta Kasabango Mushashu, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb- ‘’
6. Mhe. Christopher Olenyokie Ole Sendeka, Mb - ‘’
7. Mhe. Dkt. Christine Christopher Mnzava, Mb - ‘’
8. Mhe. Dkt. Hamis Andrea Kigwangala, Mb - ‘’
9. Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu, Mb - ‘’
10. Mhe. George Ranwell Mwenisongole, Mb - ‘’
11. Mhe. Hassan Haji Kassim, Mb - ‘’
12. Mhe. Hassan Seleman Mtenga, Mb - ‘’
13. Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb - ‘’
14. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb - ‘’
15. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb - ‘’
16. Mhe. Mohamed Lujuo Monni, Mb - ‘’
17. Mhe. Mrisho Mashaka Gambo, Mb - ‘’
18. Mhe. Seif Salum Seif, Mb - ‘’
19. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb - ‘’
20. Mhe. Zubeida Khamis Shaib, Mb - ‘’
21. Mhe. Agness Mathew Marwa, Mb ‘’

22. Mhe. Jacquline Andrew Kainja, Mb ‘’

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wetu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema. Pamoja nae namshukuru Mkurugenzi Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, *ndc* na Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Gerald Magili kwa ushirikiano wanaoipa Kamati yetu wakati wote. Aidha, tunawashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndg. Hosiana John Mvunta na Ndg. Jairo Joseph Odero pamoja na msaidizi wa Kamati Ndg. Grace Gwivaha kwa kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu ikiwemo Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** ninaunga mkono Azimio, naomba kuwasilisha.

Stanslaus Haroon Nyongo, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA**
**AFYA NA MASUALA YA UKIMWI**

31 OKTOBA 2023

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti Ahsante. Sasa tunaanza mjadala namwita Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, ajiandae Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro, ajiandae Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kuwa mchangiaji wa kwanza siku ya leo kwenye kuazimia Azimio hili la Tanzania kuweza kujiunga na *IRENA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala huu wa Kimataifa wa Nishati Jadididifu- *IRENA* ilianzishwa toka mwaka 2009 na sisi toka kipindi hicho 2009 tuliweza kusaini mkataba lakini hatukuweza kuridhia hili Azimio. Hatukuweza kuridhia hili Azimio kwa sababu tulitaka pia tuweze kujiridhisha tufanye utafiti wa kutosha, tuone kwamba manufaa ambayo tunaweza tukayapata kuridhia Azimio hili na changamoto ambazo pia tunaweza tukazipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ambavyo utafiti umeweza kufanyika kwa kipindi chote hiki toka 2009 tulivyosaini mkataba huu na tumeona baadhi ya nchi jirani ambazo zimeweza kuingia na kusaini mkataba huu wakiwepo nchi jirani za Afrika Mashariki, Kenya, Uganda, Rwanda na baadhi ya nchi za *SADC*. Mwaka 2011 waliweza kuridhia mkataba huu na wameweza kuendelea kufanya kazi kwenye utekelezaji wake na manufaa wameweza kuyapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo na sisi kupitia Serikali ya Awamu ya Sita baada ya kuwa muda mrefu kuweza kuhakikisha kwamba majadiliano yamefanyika na kujiridhisha vya kutosha. Sasa umefika muda muafaka wa kuona namna iliyokuwa nzuri Bunge letu tukufu kwa maana ya Tanzania turidhie mkataba huu na sisi tuweze kunufaika na Wakala wa Nishati Jadidifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Watanzania huko nje wanaweza wakawa wanajiuliza hizi nishati jadidifu ni nini? Manake inaweza ikawa ni neno geni kwao lakini nishati jadidifu hizi ni pamoja na uwepo wa umeme wa jua, umeme wa upepo, umeme wa maporomoko, joto ardhi na mengineo. Kwa hiyo, mtu asije akaona nishati jadidifu akaona ni jina geni, hapana ni hizi nishati ambazo sisi tumekuwa tunazitumia lakini tumeendelea kuzitumia kuhakikisha kwamba umeme wetu umeweza kuwa wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba huu ambao sisi tulisaini lakini bado tulikuwa hatujauridhia, tukishauridhia hautufungi kwa namna yoyote ile ambayo tutaona kuweza kwenda kujitoa. Tukiona mambo hayapo sawasawa pia tuna nafasi ya kuweza kujitoa na baadaye kuweza kujipanga upya ili tuweze kurudi tena. Kwa hiyo, hakuna masharti yoyote ambayo yatatufunga kuhakikisha kwamba Mkataba huu au Azimio hili linaweza likaja likatufunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza nishati jadidifu hizi sisi Tanzania tayari tulishakuwa wanufaika na tunatekeleza vya kutosha nishati ya umeme jadidifu. Tayari kwenye umeme wa upepo tunatekeleza Mradi wa Zuzu wa takribani *megawatt* 50,

tunaanza hapa hapa Dodoma, hapa Zuzu. Pale Manyoni tunatekeleza Mradi wa *megawatt* 100 kwa maana ya pale Mkoa wa Singida. Same vilevile megawati 50 pia Kishapu kule megawati 150. Kwa hiyo, tayari kwenye utekelezaji huu tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hivi vyanzo vya umeme jadidifu ambavyo sisi tunavyo vina uwezo wa kuzalisha takribani *megawatt* zaidi ya 5000 kutokana na joto ardhi na upepo tunaweza tukazalisha takribani *megawatt* 5000 baada ya utafiti ambao umeweza kuwa umefanyika. Kwa hiyo sisi wala tusiwe na shaka utekelezaji tumeshauanza, kwa hiyo turidhie kwa pamoja kuhakikisha kwamba Azimio hili liweze kupita ili tuweze kwenda kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo baadhi pia tuna manufaa ambayo tunaweza kunufaika ya moja kwa moja kupitia kuridhia Mkataba huu, ikiwemo kuliwezesha Taifa kuwa na vyanzo mchanganyiko vya uzalishaji wa umeme. Sasa hivi chanzo kikubwa tulichokuwa nacho ni cha uzalishaji wa maji, lakini sasa hivi kupitia Azimio hili na vyanzo tulivyokuwa navyo ambavyo tunakwenda kuvitekeleza kwa maana ya upepo, kwa maana ya joto ardhi, vinaweza kutusaidia sana kuweza kwenda mbele vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kuweza kuimarisha utaalamu. Kupitia wanachama wenzetu wa *IRENA* wao kule kuna nchi ambazo tayari zimeshapiga hatua kwa kiasi kikubwa sana. Hivyo ushirikiano ambao tutakuwa nao sisi tutapata utaalamu pale wa kutosha kuhakikisha kwamba Tanzania tunapata wataalamu wa kutosha. Pia kupitia vyuo vyetu vya ndani tayari imeshasemwa hapa tunao *DIT* pamoja na Arusha *Technical College*. Sisi kama kamati pia tuliweza kuiambia Serikali, tuweze kuongoza na Chuo cha *MUST* pale Mbeya na wao pia waweze kuongeza kutoa hizi *course* ili tuweze kupata wataalam hawa wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu itatuwezesha pia kupata wawekezaji wa kutosha kupata mitaji pia kuweza kupata ushauri kutoka kwenye nchi ambazo zinakuwa zimeendelea. Kwa hiyo, kupitia Bunge hili niombe sana turidhie mkataba huu ili na sisi

kama watanzania tuweze kunufaika kwenye umeme jadididfu kupitia *IRENA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ndaisaba, jiandae Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia Azimio la Bunge la kuunga mkono Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea na mchango wangu naomba nitumie angalau sekunde chache kuweza kumshukuru Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati ambaye mara baada ya kuteuliwa alifika Ngara na kuzindua miradi ya umeme kwenye vijiji vya Ntanga na Kaburanzwili na kwa kweli ziara ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kule Ngara imekuwa na matunda makubwa. Mbali na kuzindua umeme Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, aliwasiliana na Waziri wa Maji Aweso, ili aweze kufika Ngara kutatua changamoto ya maji kule Murusagamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli naomba Waziri Aweso na Naibu Waziri Mkuu wachukue maua yao, kwa sababu kazi nzuri waliyoifanya kule Ngara imeleta matunda makubwa na wananchi wa Murusagamba sasa wanapata maji ambayo walikuwa hawana kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli huyu ndugu yangu Aweso ni mzee wa kutolaza zege alivyopokea simu ya Naibu Waziri Mkuu alifika Ngara ndani ya sku mbili, Mheshimiwa Aweso pokea maua yako. Sisi Wabunge tunajua namna unavyotuhudumia na namna unavyohudumia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nielekeze mchango wangu kwenye eneo hili la Mkataba wa *IRENA*. Nishati Jadidifu imeanza kutumika miaka 2000 iliyopita. Wenzetu huko Ulaya walianza

kuzungusha magurudumu kwenye mito na yale magurudumu yakawa yanazalisha umeme wakagundua kwamba kumbe maji yanaweza yakazalisha umeme. Wakati huo sisi Afrika tulikuwa tunayatumia maji kwa ajili ya shughuli za kawaida, kuoga, kuogelea humo humo kwenye maji, kuyanywa, kufua nguo na kipindi kingine kuendesha mitubwi kwenye maji. Lakini wenzetu Ulaya miaka 2000 iliyopita walikuwa wameshaendelea na wameshaanza kuyatumia maji kwa ajili ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na kuanza kwao kutumia maji kuzalisha umeme wenzetu mwaka 1590 waligundua kwamba upepo unaweza ukatumika kuzalishia umeme na wakaanza kuzalisha umeme kwa kutumia upepo. Hawakuishia hapo mpaka mwaka 1800 wenzetu huko Ulaya waligundua kwamba jua na lenyewe linaweza likatumika kuzalisha umeme na wakaanza kupata umeme kutokana na nguvu ya jua. Mpaka wanakaa kwenye mkutano wa kugawana Bara la Afrika mwaka 1885 wenzetu walikuwa walishapiga hatua na walipokuja Afrika kuanza kugawana wenzetu walikuwa tayari wana hiyo teknolojia ya kuweza kuzalisha umeme kutokana na upepo maji pamoja na jua.

Mheshimiwa Naibu Spika, na sisi wakoloni walivyofika hapa tulibahatika kuridhi teknolojia hizo za kuzalisha umeme jadidifu mathalani kwa upande wa maji. Wote ni mashuhuda kwamba wakoloni ndio ambao wamefika Tanzania na kuanza kujenga mabwawa ya maji ambayo mengine tunayatumia mpaka sasa na kwa minadili hiyo Tanzania imepiga hatua kwenye eneo hilo la nishati jadidifu na mpaka sasa Tanzania inazalisha asilimia 31.5 ya umeme unaotokana na nishati jadidifu kwa maana ya *renewable energy. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni sawa uzalishaji wa megawati 5704.60. Mataifa ambayo ni wanachama wa Umoja wa Mataifa, baada ya kuona kwamba matumizi ya nishati jadidifu ndio mwelekeo na njia sahihi ya kuepukana na mabadiliko ya tabia ya nchi, ambayo mabadiliko ya tabia ya nchi yanasababishwa na matumizi ya nishati zisizo jadidifu wenzetu wakaamua kutengeneza Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu kwa maana ya *IRENA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009 wenzetu waliunda hiki chombo na Tanzania ikabahatika kusaini mkataba huu mwaka 2009 lakini kwa bahati mbaya watanzania tumeendelea kujivuta kwa miaka 14. Tumekuwa tukishiriki kwenye vikao vya *IRENA* kama watazamaji tu kama *Observer* na matokeo yake wenzetu wamekuwa wakikutana wana-*share* ujuzi, wanafundishaji mambo ya nishati jadidifu, wanapeana fursa mbalimbali za uwekezaji kwenye nishati jadidifu, sisi Tanzania tukiwa tunashuhudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni sawasawa na kule vijijini unakwenda kwa majirani unakuta wanachinja ng'ombe wewe unatazama watu wanachinja ng'ombe wanagawana minofu, wewe unaondoka bila kuwa hata na unyoya. Ndicho ambacho Tanzania kwa miaka 14 imekuwa ikikifanya. Tunakwenda kwenye mikutano ya *IRENA* sisi tunabaki kuwa *Observer,* wenzetu wanagawana minofu tunaondoka tunarudi kama tulivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna kipindi watanzania tumejichelewesha ni sasa na kama kuna kipindi kama Taifa tunatakiwa haraka sana iwezekanavyo turidhie na tujiunge na *IRENA* ni sasa. Huu ndio mwelekeo sahihi wa kuepukana na athari za mabadiliko ya tabia nchi zinazotokana na matumizi ya nishati chafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania ni mashuhuda kwamba maeneo ambayo mvua zilikuwa zinanyesha mwezi wa nane, mwezi wa tisa, sasa hivi zinachelewa kunyesha. Watanzania ni mashuhuda kwamba kuna kipindi unaweza ukapanda mbegu, baada ya kupanda mbegu mvua ikanyesha mara moja na baada ya hapo ikapotea, yote hayo yanatokana na mabadiliko ya tabia ya nchi yanayoletwa na kutumia nishati zisizo jadidifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania ni mashahidi kwamba kipindi hiki jua limeongezeka, kuna kipindi jua linawaka utadhania limetumwa au utafikiria linawaka kwenye kichwa chako peke yako. Unajiuliza hivi hili jua limekuwa namna gani? Lakini yote haya ni kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi yanayotokana na matumizi ya nishati zisizo jadidifu. Muda sasa umewadia watanzania kuweza kuridhia na kujiunga moja kwa moja tuwe

wanachama tuanze kushiriki na tufanye maamuzi na tunufaike na fursa kedekede zilizopo kwenye *IRENA*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba kengele ya pili ilishalia ahsante kwa mchango mzuri.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu, jiandae Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono Azimio. Kama ambavyo Mwenyekiti wetu amewasilisha sisi kama Kamati tumepata muda wa kutosha kupitia wasilisho la Serikali lakini kuwasikiliza wadau mbalimbali ambao walikuja kuwasilisha maoni yao na ninaomba kutumia fursa hii kuunga mkono hoja na kuomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuridhia ili nchi yetu iweze kuwa mwanachama wa *IRENA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ilikubali kuwa mwanachama mwaka 2009 lakini imetuchukua miaka takribani 13 leo kuja kupitisha Azimio. Zilikuwepo sababu za msingi, tuliuliza kwa nini tumechukua miaka yote hiyo wakati tumeendelea kushiriki? Serikali ilisema, ilikuwa inajipa nafasi ya kuona wale walioingia wamefaidika kiasi gani na baada ya kujiridhisha kwamba walioingia wamefaidika sasa nimegundua ni muda muafaka wa kuingia. Jambo hili ni jema ingawa kuchelewa kwetu kumetuchelewesha kwenye kufaidika na faida ambazo wanachama wengine wamepata.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ndilo eneo ambalo lina umeme wa bure au lina nishati ya bure. Amezungumza hapa Mheshimiwa Masache aina za umeme unaopatikana kwenye eneo hili pamoja na *solar energy.* Afrika jua lipo la bure, ziko nchi duniani wanavizia jua litoke, siku jua likitoka wanashangilia. Yaani jua linatoka kwa mwezi mmoja kwa mwaka mzima, sisi tuna umeme wa bure kutoka kwenye jua lakini tuna upepo wa kutosha *(wind energy)*. Tuna joto

ardhi *(geothermal),* yako maeneo yamepimwa na umethibitika kwamba yanaweza kutoa umeme wa kutosha lakini tuna maeneo mengi yanaweza ku-*generate hydroelectric power.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza Serikali kwa sababu sehemu kubwa ambayo tunataka kutumia ni *hydroelectric power* lakini bado hatujatumia kiasi cha kutosha fursa hii tuliyonayo. Bado tuna umeme mwingine wa *bioenergy* sehemu kubwa ya uharibifu wa misitu inatokana na utafutaji wa nishati na watafutaji wengi wa nishati ni wafugaji. Wafugaji wana uzalishaji mkubwa wa kinyesi cha ng'ombe ambacho kinaweza kutumia kutengeneza *biogas.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa uzembe ambao tunao ni kwenye ku-*transform* hizi fursa tulizonazo kupelekea hao wanaotumia zaidi ukataji wa kuni waache kutumia watumie *biogas*. Kwa hiyo, nadhani huu ni muda muafaka ambao Serikali kwa kuridhia Azimio hili, sio twende kama *ceremonial,* tuweke mkakati wa kutosha kuhakikisha kwamba sasa tunakwenda kupambana kuvuna hizi fursa ambazo tunazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi jirani wanazalisha zaidi ya *megawatt* 1000 kutoka kwenye *geothermal*. Mtu anaweza kufikiri kwamba Serikali itapata wapi pesa kwa ajili ya kufanya jambo hili. Tumeshauri Wizara tutumie zaidi *PPP* au tuhamasishe watu binafsi kuingia kwenye eneo hili na kazi ya *TANESCO* iwe kuhamasisha wawekezaji lakini kutengeneza mazingira ambapo wao wanaweza kuwa *recipient* wa umeme na kuhakikisha watanzania wanapata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tuna upungufu wa umeme kwenye nchi yetu na kwenye Kamati tuliambiwa kwamba hata baada ya Mwalimu Nyerere kuingia mahitaji ya umeme wa majirani zetu ni makubwa sana wataendelea kuhitaji umeme. Ni muda muafaka sasa kwa sababu kujiunga kwa Azimio hili kunafungua milango ya teknolojia, kunafungua milango ya mitaji, lakini kunafungua milango ya uzoefu ambao majirani zetu tayari wanao na tayari wateja tunao ambao tunapaka nao kwenye maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ambayo tayari yamekwishathibitika, Singida kuna upepo, Kishapu kuna joto lakini Same kuna upepo na maeneo mengine ya *geothermal* ambayo utafiti unaonesha tayari Wizara ilikwishafanya kazi kubwa lakini shida imekuwa ni kuvutia teknolojia, kuvutia mitaji na kutengeneza sera ambayo inakaribisha watu waje.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, sera tunayo ya ujumla lakini tunapungukiwa sheria mahususi kwenye eneo hili. Tumemweleza Mheshimiwa Waziri na tutaitaka Serikali kutengeneza sheria ambayo wawekezaji ambao wana historia ya kuona kwamba tuna sera zinabadilikabadilika, tuwe na sheria ambayo mtu anaweza kuwa na uhakika nayo. Anapokuja kuwekeza asitarajie kesho au kesho kutwa kujikuta anakosa soko la kuuza umeme au anajikuta anaamuriwa kufunga biashara yake. Tuwe na sheria na sera ambayo Wizara tunaiomba iitengeneze na tuitangaze kuvutia maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana naunga mkono Azimio. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sasa tunakwenda kwa Mheshimiwa Sophia ajiandae Mheshimiwa Gwajima.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia eneo hili. Wenzangu wamekwishakueleza kwamba kitu hiki kilianzishwa tangu 2009 mpaka 2011 ndipo ilipoanza kazi. Lengo kuu kabisa na malengo manne kutokana na Wizara walivyoweza kutueleza lakini mimi tataja malengo makubwa mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhamasisha teknolojia mbalimbali za kusaidia kuweza kupata nishati salama; la pili ni kuwezesha upatikanaji wa nishati safi na salama yenye gharama nafuu, tunajua kabisa fika kama Taifa kutegemea umeme huo mwingine ambao tunaotegemea sasa tunapitia kwenye madhira makubwa sana kutokana na tabianchi pia. Hivyo tutakapoamua kupitisha itatusaidia sana kuweza kupata umeme huu mwingine ambao tunafikiri utakuwa mzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu kubwa sana sana la hii *IRENA* ni kujengea uwezo nchi mwanachama. Tunajua watalamu wetu watajengewa uwezo, lakini pamoja na hayo kwa jinsi ambavyo tumeelezwa na tumesoma tumeelewa tutakapojiunga kuwa wanachama ni rahisi kupata fedha kwa ajili ya kusaidia Taifa letu na kuweza kusaidia teknoloji hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, itatusaidia sana pia kupata umeme kwa urahisi zaidi ikiwemo gesi joto ambazo tayari utafiti umekwishafanywa. Na ili uweze kufanikiwa Serikali imeamua kuanza kufanya utafiti na kuweza kuelewa ni maeneo gani ambayo tunaweza tukapata nishati hii. Hilo peke yake hata wawekezaji itakuwa ni rahisi kufika kwa sababu tayari tumekwisha warahisishia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niseme kama Mjumbe wa Kamati lakini kama Mbunge mwenzenu kwamba kuna haja ya kupitisha sheria hii. Mimi siilaumu sana kwa kuchelewa kwa sababu wasi wasi ni akili. Mimi naamini muda mrefu uliyochukuliwa imetusaidia sisi kujua kwa kina, watalamu wetu kusimamia kwa kina. Kwa hiyo tusikimbie kusema tungefanya haraka hivyo walivyochelewa wamefanya vizuri na sasa ndiyo wakati sahihi wa kutoa maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Wizara mnaendelea; na kuna maeneo mengine tufanye taratibu kama nchi tukubaliane mwisho wa siku tupitishe kwa umoja. Ninaipongeza Wizara, ninampongeza Waziri husika kwa kuwa amefanya vizuri, pia hata Katibu wa Wizara amefanya kitu kizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaamini baada ya kupitisha *IRENA* tutaenda kufanikiwa kama Taifa. Wameishasema wenzangu kuna nchi ambazo zimetutangulia katika *East Africa,* tunafahamu Uganda na Kenya pamoja na Rwanda walishajiunga. Kwa hiyo na sisi tutakapojiunga Taifa letu linaenda kupata faida na kwa hivyo ninaunga mkono kwa mara ya kwanza mia kwa mia tuunge ajenda hii, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Gwajima, wajiandae Dkt. Mnzava na baadaye jiandae Dkt. Ndugulile.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi kuchangia katika hoja hii. Kwa makusudi ya kuokoa wakati nitaenda moja kwa moja kwenye Azimio la Bunge kuhusu kuanzisha kwa Taasisi ya Dawa ya Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa maana kwamba tarehe 11 Februari, 2019 ni mahala ambapo Umoja wa Nchi za Kiafrika na wakuu wa nchi walikubaliana kwa pamoja kuanzishwa kwa Taasisi hii ya Dawa ya Afrika. Kwa hiyo nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa sehemu ya viongozi hawa na kukubaliana kwenye Mkataba huu wa muhumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, dawa ni matibabu katika ulimwengu wa leo lakini pia dawa ni silaha katika ulimwengu wa leo. Tunapozungumza kuhusu dawa inatoka mahala ambapo si nchini kwetu na inakuja nchini kwetu kwa lengo la kutibu watu ni maeneo muhimu sana kwenye *component* ya nchi ili tuwalinde watu wetu wawe salama leo, kesho na siku zijazo. Na kwa sababu hiyo nimeona moja ya sababu ya manufaa yanayotokana kuridhia kwa mkataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, manufaa ya kwanza ni kuhimarika kwa mfumo wa udhibiti na kuweza kudhibiti bidhaa ambazo haziwezi kudhibitiwa kwa naamna ya kawaida. Wametoa mfano kama bidhaa zinazotokana na *genetic* au *genetic connections*. Ninaomba nitoe mfano kwa jambo ambalo nalifahamu vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna aina ya matibabu yanaitwa *genome editing by Crispr technology*. *Genome editing by crispr technology* ni aina ya matibabu ambayo unamtibu mtu mwenye selimundu *(sickle cell)* kwa kutumia utalamu wa ku-*edit gene* yake. Ndugu yangu Daktari Mollel anafaahamu vizuri sana. Matibabu haya ni kwamba una-*edit gene* ya mtu na unaondoa ule uwepo wa selimundu kwenye *genetic inheritance* yake ili

umtibu. Haya ni matibabu yanayotokana na *genetic* lakini pia ni matibabu yanaweza kuwa na madhara makubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kwenye *genetic editing by crispr technology* ni kwamba utu wa mtu upo kwenye *gene* ya mtu. Ukifanikiwa ku-*edit gene* ya mtu unaweza ku-*edit* utu wa mtu, unaweza ku-*edit* urefu wake, saizi ya kichwa chake, uwezo wake wa kuelewa, *IQ* yake, *intellectualism y*ake, rangi ya ngozi na utu wake kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Waafrika haatuna maabara za kutosha za kuweza kuchuja kila kitu kinachotoka kwa wenzetu kule magharibi. Sasa kwa Mataifa ya Kiafrika kuja pamoja na kuwa na azimio ya kuanzisha Umoja wa Dawa za Kiafrika inasaidia sana mataifa ya Kiafrika kuwa na maabara ya pamoja kwa ajili ya kudhibiti mambo yenye lengo ya kuiangamiza Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hata kabla sijaenda mbali ninaunga mkono azimio kwa asilimia mia moja pamoja na hayo machache nitakayoyaelezea. Ninaomba ni-*highlight* jambo moja; katika kila dawa inayotoka nje ya Afrika inaingia kwenye nchi kila nchi inakuwa na jukumu ya ku-*analyze* hiyo dawa, kujua usalama wake, kujua madhara yake kwa siku za karibuni, siku za kati na siku za mbele. Lakini kama unavyojua kwa mapato ya nchi ya Kiafrika ni nchi za Kiafrika chache sana zenye uwezo wa kufanya jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakumbuka tulipokaribiwa na chanjo ya *COVID*-19 tulivyoanza kurukaruka hapa; hakuna Mzungu aliyekuwa tayari kutupa *intellectual property* ya hiyo chanzo. Lakini tungekuwa tumeishatengeneza tayari Jumuiya ya Kiafrika ya kuziangalia hizi dawa kwa pamoja tungekuwa na maabara za pamoja za Kiafrika zinazochuja dawa zetu zitumikeje na kwamba zina madhara gani kwa siku za karibuni, siku za kati, na siku za usoni. Kwa hiyo azimio hili lazima tuliliridhie kwa haraka na kwa usahihi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema dawa inatibu lakini pia dawa ni silaha. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa

Jumuhuri ya Muungano ya Tanzania kwa maana hii yeye na wakuu wa nchi wenzake tarehe 11 Februari, 2019 walipoamua kusaini mkataba huu na sisi sasa kama Bunge tunatakiwa kuazimia na kuridhia. Mimi ninalishawishi Bunge lako tuazimie kwa haraka, tuwe na Jumuiya hii ya pamoja, tuwe na maabara za pamoja ili dawa zote zinazotoka nje ya nchi ya Afrika tuwe na uwezo wa kuzichuja na kujua zinawasaidiaje watu wetu; na kama zina madhara iwe ni rahisi kuwa na jukumu la pamoja kama Waafrika kudhibiti na kwenda kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba azimio hili lipite, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Gwajima kwa mchango mzuri. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, jiandae Mheshimiwa Ndugulile.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kutoa mchango wangu katika mkataba huu wa kuanzishwa kwa Taasisi ya Dawa ya Afrika ya mwaka 2019. Ni ukweli usiopingika kwamba sisi kama nchi tumechelewa. Kati ya nchi hamsini na tano zilizokaa mwaka 2019 kupitisha azimio hili la kuwa na Taasisi hii sisi tumechelewa sana. Leo ndiyo Serikali yetu imeleta Bungeni ili tuweze kujadili na kuridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi naomba niunge mkono hoja, na niwashauri na kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba turidhie mkataba huu kwa sababu una manufaa kwa Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona kwamba Rwanda imepata nafasi au fursa ya kuweza kujenga Makao Makuu ya Taasisi hii. Labda na sisi Tanzania tungeridhia miaka sita iliyopita tangu mkataba huu wamekaa mezani na kusaini na kuridhia kwamba waanzishe Taasisi hii inawezekana kabisa sisi nchi yetu ingekuwa miongoni mwa nchi ambayo kungekuwa na hii Taasisi. Kwa sababu tuna Mamlaka ya Dawa na Tiba ambayo ni bora sana

katika Bara la Afrika kwa sababu inakidhi iko katika kiwango cha tatu cha umahiri, na *WHO* imepitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi sitakuwa na mambo mengi ya kuzungumza katika mkataba huu; ni mkataba ambao unatija ni mkataba ambao utahimarisha na utadhibiti na kufuatilia masuala yote ya umahiri ya ufanisi wa dawa zote ambazo zitakuwa zinatumika katika bara letu la Afrika hususani Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na dawa nyingi ambazo zinatengenezwa. Nyingine zinatengenezwa na sisi Watanzania kienyeji na zinaingia Tanzania, zinatumika kwa wananchi wetu. Lakini tukishakuwa na taasisi ambayo inadhibiti na kusimamia popote zitakapotoka na popote zitakapokwenda zitakuwa zimehakikiwa, kudhibitiwa, kuwa na ubora halisi na hazitaleta madhara kwa wananchi wetu. Hata kama kutakuwa na madhara basi taasisi hii itakuwa na uwezo wa kudhibiti yale madhara ambayo yatatokana na hizo dawa ambazo wananchi watakuwa wanazitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi niombe kwa mara nyingine, kwa mikataba mingine ambayo ina manufaa kwa Taifa letu. Serikali ijitahidi kuwezesha, kusukuma hili suala ili mikataba kama hii ambayo inajenga na yenye manufaa kwa Watanzania na kwa nchi, inapokuwa imetolewa wailete mapema, waishughulikie, waichakate na ije kwa wakati. Miaka sita toka 2019 mpaka leo ndipo Mkataba unaingia Bungeni binafsi naona kwamba tumechelewa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Rais ambaye ndiye Amir Jeshi Mkuu anaendesha nchi hii kwa sasa hivi. Tangu mwaka 2021 mpaka leo ni kama mwaka mmoja au miaka miwili mkataba umeweza kufika Bungeni; lakini tangu 2019 mkataba uko kwenye mchakato hatujaridhia. Hivyo basi niwashawishi Wabunge wenzangu kwamba mkataba huu kuundwa wa taasisi hii tuweze kuridhia ili na sisi tuwe miongoni mwa nchi hamsini na tano za Afrika ambazo tumeridhia na tutanufaika na mkataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Dkt. Ndugulile, jiandae Mheshimiwa Nusrat. Dkt Ndugulile hayupo? Mheshimiwa Nusrat, dakika tano.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia. Kwa sababu ya muda na kwa sababu nilikuwa nimejiandaa sana na upande huu nitachangia eneo moja tu upande wa Mkataba wa Kuridhia Uanzishwaji wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme kwamba mimi ni mdau wa masuala ya mabadiliko ya tabianchi; kwa hiyo kitendo cha Serikali yangu japokuwa ni baada ya miaka ya kumi na nne na wameishajiridhisha kwamba imetosha sasa wametuletea Bungeni ili kujadili na kuridhia. Jambo ambalo niko *proud* sana na nchi yangu kwa sababu ni kitu ambacho kina faida nyingi na mkataba huu watu wote wenye mkataba wameuona, una ibara ishirini. Kimsingi Ibara zote zimejielezea vizuri sana mambo yetu ya msingi, muundo uendeshaji na kila kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni *concern* yangu iko kwenye miongoni mwa Ibara ambazo ziko humu ambazo kimsingi ni nzuri pia. Kwa sababu tunajua kuna mashaka, na nikubaliane na Wajumbe wa Kamati pia na wao pia wameeleza kwamba inawezekana tukawa tunaingia mkataba huu lakini pengine ikatuzuia kufanya shughuli zetu nyingine. Kwa hiyo kitu kizuri ni kwamba tunaweza kujitoa wakati wowote tutakapoona mambo hayaendi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa sababu nilisema nini ni mdau wa masuala ya mabadiliko ya tabianchi, nilisoma andiko moja la Tume ya Muhamo wa Nishati ya Ulimwengu *energy transition commission (ETC)* ambayo ilizungumzia kuhusiana na *clean electrification* kama *primary route to* decarbonization, hicho ni kinyaturu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume hii imezungumzia namna ambavyo kuna umuhimu wa kuelekea kwenye nishati jadidifu au nishati safi ili kupunguza ongezeko kubwa la mabadiliko ya tabianchi ambalo lina athari kubwa kwa jamii yetu; kwa hiyo ni kitu cha msingi sana. Na wote tunafahamu kwamba mpaka sasa hivi nishati jadidifu tunayozungumza ambayo tunaenda kupata mitaji baada ya kuridhia mkataba huu inaenda kuongeza nguvu kwenye nishati jadidifu ambazo sasa hivi zinachangia kwenye gridi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba mpaka sasa hivi gesi asilia ni asilimia 62.12, maji ni asilimia 32.33, mafuta ni asilimia 4.96 na tungamotoka asilimia 0.59. Kwa hiyo bado tunaona tunahitaji kuongeza nguvu kwenye nishati jadidifu, huu ndio uwezo wetu kwenye gridi ya Taifa. Kwa hiyo ninafurahi kwa sababu hata sisi watu wa Singida sasa kwa kupitia kuridhia mkataba huu tunavutia wawekezaji ili tupate mitaji ili twende tukaanzishe Miradi ya Umeme wa Upepo Singida na kwingineko, kama vile Tabora pamoja na nishati ya jua ambayo ni sehemu ya nishati jadidifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia pale Songwe kuna joto ardhi, nilienda pale kutembea kwa ajili ya kukagua wakati ule nikiwa kwenye Kamati ya Nishati. Ukweli ni kwamba tuna-*resource* kubwa sana pale lakini hatuna mitaji ya kwenda kufanya uzalishaji kwa ajili ya kupata umeme unaotokana na nishati ya joto ardhi. Kwa hiyo mimi kwangu ni furaha kubwa na ni mafakio kwa sababu tunakwenda kuvutia uwekezaji ili tupate fedha kwa ajili ya kwenda kuanzisha *project* hizi za kuongeza nguvu kwenye gridi ya Taifa, kwenye nishati jadidifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niko kwenye Kamati ya Elimu sasa hivi; tumeenda kukagua pale Kituo cha Utafiti wa Masuala ya Nishati Jadidifu na *training, training center* cha ku-*train* pale Arusha *ETC*. Pale kuna uwekezaji mkubwa lakini bado hakuna *infrastructure*. Kwa hiyo kuridhia mkataba huu kutakuwa ni sehemu moja wapo katika kuelekea katika kutafuta mitaji kwa ajili ya kwenda kuwekeza miongoni mwa miradi ambayo inahitaji fedha ikiwemo mradi ule wa pale Arusha ambao ni kituo ambacho

tunategemea kiwe *center of excellence* kwenye masuala ya nishati jadidifu, kwa hiyo kwangu mimi ni kitu kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niseme pamoja na kwamba tulikuwa hatujaridhia mkataba huu bado niko *proud* na nchi yangu kwa sababu tuliweza ku-*establish* mradi mkubwa kama Mwalimu Nyerere. Na hizi takwimu zitabarika muda si mrefu kwa sababu ujenzi kwenye Mwalimu Nyerere unaendelea na *soon* unafika asilimia mia, kwa hiyo *story* itabadilika sana, na ni lazima tukubali kwamba hatujachelewa; kama tuliweza kuanzisha *project* kubwa ile ambayo ni ya kwanza katika Afrika Mashariki na ya tatu kwa Afrika. Wakati tunatumia *resources* za ndani maana yake ni kwamba sisi tunatakiwa tujipige kifua mbele, kwamba tuliweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ndiyo maana tunasema ni sehemu tunaenda kuongezea katika kuendelea kufanya *investment* ili tuendelee kuwa na upatikanaji wa umeme wa uhakika kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado ipo Mikataba ya Kimataifa ambayo nchi yetu ilikubali kiasi kuridhia, bado hatuja-*ratify*. Niwaombe sana Serikali muendelee kujiridhisha, pelekeni watalamu wapitie mikataba ile ambayo mingine ina faida kwenye nchi ili muilete tuijadili na kuipitisha katika Bunge hili Serikali yetu ipate manufaa na wananchi wapate manufaa kwenye mikataba hiyo ya Kimataifa, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika mada ambazo zimewasilishwa siku ya leo. Na mimi nitajielekeza katika kuchangia wasilisho linalohusu Taasisi hii ya Dawa Afrika *(African Medicene Agency)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba naunga mkono azimio hili lipitishwe na Bunge lako tukufu. Dawa ni

kitu muhimu sana katika tiba za binadamu lakini dawa vile vile ni siasa, dawa ni biashara. Na katika matumizi ya dawa kuna watu wana nia njema na wengine na nia isiyokuwa njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu ambao wanatengeneza dawa bandia na watu ambao wanatengeneza dawa ambazo hazina ubora unaotakiwa. Kwa hiyo, Azimio hili linakwenda kuwezesha Nchi Wanachama kuweka mfumo mzuri wa kuweza kudhibiti bidhaa za tiba, kwa kuhakikisha kwamba dawa zinakuwa zina ubora, zenye ufanisi na usalama unaojitosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza sana Serikali ya Tanzania katika masuala ya udhibiti wa dawa tuko vizuri na Taasisi yetu ya *TMDA* inafanya vizuri sana. Hongera sana Mheshimiwa Waziri na timu yako, kwa usimamizi mzuri ambao unaufanya katika Wizara hii, ambao umepelekea Tanzania tunasifika katika masuala ya udhibiti wa dawa na vifaa tiba katika Bara la Afrika na dunia nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nini manufaa ya Mkataba huu? Kwanza, unakwenda kuboresha masuala ya mifumo ya udhibiti katika Bara letu la Afrika. Sambamba na hilo, litasaidia sana kuweka mfumo wa kuweza kubadilishana taarifa na kuweza kujengeana uwezo katika nchi zetu za Bara la Afrika. Pia sambamba na hilo, kila nchi ya Afrika ina mifumo yake ya udhibiti na usajili wa dawa. Azimio hilo litakwenda sasa kuweka mfumo mzuri wa kuweka viwango na vigezo ambavyo vitatumika katika Bara zima la Afrika. Hii itapelekea kuweka sasa mifumo ambayo inafanana na kuwavuta wale ambao wako chini na sisi ambao tuko katika viwango vya juu kwenda viwango vya juu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetoka kusema hapa katika viwango vile vya kimataifa vina hatua nne. Sisi Tanzania tuko katika hatua ya tatu, ni jambo la kujivunia sana kama Watanzania. Naamini kwa kupitisha Azimio hili, litatusaidia hata sisi katika viwanda vyetu vya ndani, kupunguza mlolongo wa usajili na pale ambapo tutahitaji sasa bidhaa zetu kuzipeleka nje ya nchi, sasa hivi Tanzania tuna Viwanda vya Dawa takribani 18. Mfumo huu

utasaidia sana bidhaa zetu kuweza kuuzwa nje ya nchi na kupunguza mlolongo wa usajili. Utaratibu uliopo sasa hivi ndani ya nchi yetu kila dawa tiba ni lazima isajiliwe na mlolongo wake haupungui miezi sita. Utaratibu huu utasaidia kuweka *benchmarks* nzuri ambazo naamini nazo zitasaidia sana katika udhibiti, vile vile katika suala la usajili wa dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nataka niweke angalizo moja. Sisi kama nchi tumefanya vizuri sana. Mifumo yetu iko vizuri sana katika suala zima la usajili na udhibiti wa dawa katika nchi yetu. Sasa ni muhimu sana wakati tunapitisha azimio hili, kuhakikisha kwamba taasisi yetu ya *TMDA* inaendelea kufanya majukumu yake ya kimsingi bila kuathirika na vipengele ambavyo vinaweza vikasababisha taasisi yetu na sisi kushuka chini, kwa sababu wote hatuko katika viwango vya pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kwamba, kwa kupitisha azimio hili Taasisi yetu ya *TMDA* ndiyo itakuwa kinara cha kusaidia nchi nyingine za Afrika na wao waweze kufikia katika viwango vya juu vya udhibiti wa ubora wa dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuomba jambo moja. Hili nitaendelea kulisema, lipo nje hapa kidogo, lakini tunaongelea masuala ya udhibiti wa vyakula. Katika nchi nyingi duniani suala la udhibiti wa dawa linakwenda sambamba na udhibiti wa usalama wa chakula. Suala la usalama wa chakula ni suala la afya, siyo suala la viwanda wala la biashara. Usalama wa chakula linapotokea changamoto katika suala la usalama wa chakula, uwe ni mlipuko wa magonjwa ambao umesababishwa na chakula, Wizara inayoshughulika ni Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tulihamishe hili jukumu kutoka Wizara ya Afya kwenda Wizara ya Viwanda na Biashara. Niwaombe sana, katika nchi nyingi mamlaka zinaitwa *FDA (Food Drug Authorities),* siyo *Medical Authority*. Kwa hiyo, niendelee kuiomba Serikali iende ikaliangalie suala hili, ikiwezekana suala la usalama wa chakula lirejeshwe chini ya *TMDA* ili sasa jukumu hili liweze kufanyika. Hili nalisema kwa sababu gani? Sasa hivi kuna

uingizaji mwingi wa chakula na vyakula vingine havina ule ubora ambao unatakiwa. Najua kwamba *TMDA*…

**MHE. ASKF. JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa taarifa tu anayezungumza. Ni kweli kabisa kwa sababu, *genetic modified food* au chakula ambacho kimetengenezwa ku-*genetic,* ni hiyo hiyo sayansi ya dawa. Kwa hiyo, ikiwa pamoja itarahisisha sana kulinda watu wetu. *(Makofi)*

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mbunge wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima kwa kuunga mkono hoja yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kwamba, pamoja na kukubali Bunge lako liweze kuliridhia Azimio hili, basi naliomba Bunge lako vile vile litafakari kurejesha majukumu ya usalama wa chakula chini ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Wachangiaji wetu wote wamekwisha sasa mtoa hoja. Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru wachangiaji wote ambao wamechangia hoja yangu ya kuomba Bunge lako lipitishe Azimio kuhusu Mapendekezo ya Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli maoni yote ambayo yametolewa yanaunga mkono Azimio. Niseme kubwa, sisi kama Serikali tunaamini kwamba kuridhiwa kwa mkataba huu wa *AMA*, itakuwa ni moja ya nyenzo muhimu katika kupambana na bidhaa

tiba duni na bandia, kukuza soko la bidhaa tiba ambazo zinaweza kuzalishwa na nchi nyingine. Kwa hiyo, kubwa tunaamini tutanufaika zaidi na Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeunga mkono jambo kubwa ambalo Kamati imesema na Mheshimiwa Christina Mnzava, ni kwa nini tumechelewa? Ndiyo taratibu zetu za Serikali, lakini naamini maazimio mengine ambayo yana maslahi makubwa kwa nchi tutajitahidi kuyaleta kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askofu Josephat Gwajima kwa kweli ameongea jambo kubwa sana zuri na inaonekana amefanya *research* kwenye masuala ya teknolojia ya *genetics*. Ni kweli ndiyo tiba sasa hivi, hata kwenye masuala ya *stem cell therapy,* masuala sasa hivi ndiyo yanajitokeza. Kwa hiyo, Azimio hili pia linakwenda kudhibiti, maana sasa hivi hatuna sheria ya kudhibiti masuala kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwa kusema kama walivyosema Dkt. Ndugulile, Askofu Gwajima na Mheshimiwa Christina Mnzava na Kamati ya Mheshimiwa Nyongo. Kweli dawa ni maisha, biashara na siasa. kwenye biashara ukiangalia baada ya biashara haramu ya silaha, dawa za kulevya, dawa ni moja pia ya biashara tatu kubwa ambazo zina-*generate* mapato makubwa sana. Kwa hiyo ni lazima pia tuimarishe mifumo na uwezo wa nchi katika kudhibiti dawa, vifaa tiba vitendanishi pamoja na bidhaa nyingine za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalizo ambalo limetolewa na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile tumelipokea, kuhusu masuala ya udhibiti wa chakula tutaendelea kujadiliana ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalizo lingine ambalo tunaenda nalo ni kuimarisha uzalishaji wa ndani wa dawa. Sasa hivi kwa mfano katika maji tiba *(drip)* tunavyo viwanda viwili ambayo vinazalisha Maji tiba na kukidhi soko la nchi. Tunayo Kairuki *Pharmaceuticals* na *Alfa Pharmaceuticals,* wana uwezo wa kuzalisha chupa 98,000,000 za maji tiba wakati mahitaji ya nchi ni chupa 24,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunaamini kabisa tukipitisha Azimio hili pia *as long as* nchi nyingine zimeridhia Mkataba wa *AMA* tuna uwezo wa kwenda kuuza ziada katika chi nyingine za Afrika. Pia kubwa tumepata maoni kuna wawekezaji wako tayari kuja nchini, lakini wananiambia *Minister, when we come to Tanzania, we can't sell for Tanzanian market. We have also to sell for SADC and EAC. What are the requirements?* Kwamba, *do we need also to register our products in Kenya, Rwanda, Burundi?*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tukipitisha mkataba huu na kama Kenya ameridhia, Zambia, Rwanda, Burundi, Zimbabwe, maana yake wawekezaji pia watavutika kuja kuwekeza Tanzania na hivyo bidhaa zao kuuzwa katika nchi nyingine za Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, kama Serikali tutaendelea kutoa kipaumbele kwa bidhaa za afya, bidhaa tiba zinazozalishwa ndani ya nchi. Mwaka jana tulinunua bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi zenye thamani ya shilingi 14,000,000,000. Mwaka 2023 tumenunua bidhaa za afya zinazozalishwa ndani ya nchi zenye thamani ya shilingi 36,000,000,000. Kutoka shilingi 14,000,000,000 mpaka shilingi 36,000,000,000. Kwa hiyo naiona *commitment* ya Serikali katika kuimarisha uzalishaji wa ndani wa bidhaa tiba. Tunaamini kabisa mkataba huu pia utatuwezesha kufikia lengo la Serikali la kupunguza uagizaji bidhaa tiba kutoka nje ya nchi angalau kwa 50% ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Bunge lako lipitishe Azimio kuhusu Mapendekezo ya Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika *(Treaty for the Establishment of the African Medicines Agency - AMA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Sasa Waheshimiwa nitawahoji, kuwa, Bunge sasa likubali Mapendekezo ya Mkataba

wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika ya Mwaka 2023 *(Treaty for the Establishment of the African Medicines Agency - AMA)*, pamoja na marekebisho yaliyoletwa na Kamati na Serikali yenyewe.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekezo ya Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika ya Mwaka 2023 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Nikupongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wako na timu yako kwa kazi nzuri, lakini michango ya Wabunge imekuwa ni mizuri sana, imeonesha *maturity*, uelewa na namna Wabunge na wao walivyotafuta taarifa mbalimbali ambazo za kuweza kuisaidia Serikali, hongereni sana. *(Makofi)*

Sasa namuita Waziri wa Nishati. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI (MHE. DKT. DOTO M. BITEKO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja hii.

Pili, naomba niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, chini ya Mwenyekiti wetu Dkt. David Mathayo kwa umakini wao na uchambuzi mzuri sana walioufanya wakati tumewasilisha mapendekezo ya kuridhiwa kwa mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya kazi kubwa sana na kwa kweli imeturahisishia sana hata sisi Wizara wakati wa kupitia mambo mbalimbali. Kamati ilifanya kazi kubwa ya kuwatafuta na kuwasikiliza wadau, kuona maoni yao, mashaka na wasiwasi walio nao kwenye Azimio hili. Kwa kweli, niwashukuru sana ubunifu wao umetusaidia. Wadau waliofika kwama *TPSF* na Jumuiya ya Nishati Jadidifu walitoa maoni ambayo kwa kweli yalikuwa yamewekwa kwa umakini mkubwa. Yaliandikwa kabisa na wengine walisema kwa michango yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi, michango ya Waheshimiwa Wabunge wengi waliozungumza kuhusiana na Azimio hili, ni michango iliyounga mkono sisi turidhie na hoja kwamba, tulichelewa ni hayo waliyoyasema kwamba, wasiwasi ni akili na kwamba kawia ufike, bora tumechelewa tuwe na uhakika wa kile tunachoingia. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote waliotoa michango yao tunawashukuru sana, sana kwa sababu wamefanya kazi hii iwe rahisi na tutakapokuwa tunapitia sera zetu hasa za nishati jadidifu, tutazingatia kwa umakini mkubwa maoni waliyoyatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wengi wameunga mkono, niseme wote wametuunga mkono kwenye jambo hili. Hivyo, nisingependa kuchukua muda wako kutoa maelezo marefu. Naomba tena nikushukuru wewe na niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao. Nataka niwahakikishie kwamba, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliposema anaifungua nchi ni pamoja na sisi kuingia kwenye Majukwaa ya Kimataifa kama haya, ambapo tunaweza kupata fursa mbalimbali za kujua taarifa mbalimbali hasa kwa sababu dunia ipo kwenye *stress* ya nishati na nishati jadidifu ndiyo kimbilio la kila mmoja hapa duniani, kwa sababu ya masuala ya kimazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwatoe wasiwasi kwamba Mkataba huu hautufungi kwa namna yoyote. Mkataba huu hata gharama ya kulipa ni ndogo, lakini muhimu zaidi tukiona kuna jambo haliendi sawa tuna uwezo wa ku-*call off* na kuweza kuendelea na maisha mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niwasilishe Azimio kwa kusema yafuatayo:-

Kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa;

Na kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa Nchi Mwanachama wa Taasisi za Ushirikiano wa Kiuchumi Kikanda wa Jumuiya mbalimbali hapa Afrika;

Na kwa kutambua kuwa malengo yaliyomo katika mkataba wa *IRENA* iliyoanzishwa tangu tarehe 26 Januari, 2009 yana lengo ambalo sisi kama Taifa tunahitaji pia kujiunga;

Na kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inazo rasilimali za nishati jadidifu katika maeneo mbalimbali hapa nchini na yaliyotajwa katika Sera yetu ya Mwaka 2015 na madhumuni yaliyoko kwenye Mkataba huu nimeyaeleza kwa kina kwenye maelezo yangu ya awali pamoja na manufaa tutakayoyapata,

Hivyo basi kwa kuzingatia manufaa ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakayoyapata, naliomba Bunge lako lipitishe Azimio hili kuhusu Mapendekezo ya Tanzania kuridhia Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu wa Mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, hoja imeungwa mkono.

Sasa nitawahoji, kuwa Bunge sasa likubali Mapendekezo ya Tanzania Kuridhia Kujiunga na Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu wa Mwaka 2009. *(Statute of the International Renewable Energy Agency - IRENA)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekezo ya Tanzania Kuridhia Kujiunga na Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu wa Mwaka 2009 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsanteni sana, Azimio limepita na sasa huo ndiyo Msimamo wa Bunge. *(Makofi)*

Nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri wewe na timu yako, lakini na michango mizuri ya Wabunge ambao mmeonesha umahiri na uelewa wa suala hili.

Vilevile tunavyosema wasiwasi ni akili, tujiulize tunachelewa mambo mangapi na tunapoteza mambo mangapi? Ni bora kufanya kosa lakini ukaja kujirekebisha, lakini siyo kukaa miaka 10 au 15 kutokwenda na dunia inavyokwenda. *(Makofi)*

Niwapongeze Serikali, mazingira ya umeme yameanza kurekebika, polepole tutafika tunapotaka kufika. Kwa Mkataba huu vile vile tuko na fursa ya kuingia kwenye mikataba na mataifa mengine na taasisi za *private*. Madhara ya umeme kwenye uchumi ni makubwa sana. Kwa hiyo, yapo mambo itabidi Watanzania tujifunge mkanda kwa kutegemea huko tunapokwenda gharama zipo, pia umeme utapatikana.

Wale wenye matumizi makubwa, wenye uwezo wanaweza wakawachangia wale ambao uwezo wao upo chini lakini umeme upatikane. Hongereni sana Mheshimiwa Waziri, tunaona sasa hivi umeme unaanza kupatikana na tunategemea kwa siku chache zijazo, mambo yatakamilika na kila kitu kitakuwa vizuri na Watanzania watafaidi matunda ya Serikali hii ya Awamu ya Sita.

Baada ya kusema hayo, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 Jioni.

*(Saa 6.55 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2023)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria wa Mwaka 2023 *(The Legal Sector Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya maelezo yake kwa Muswada ulio mbele yetu.

Mheshimiwa Dkt. Feleshi.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2023)*.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuingoza nchi kwa malengo, ujasiri na uzalendo wa hali ya juu. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu kuendelea kumuombea na kumuomba Mwenyezi Mungu amjalie Rais wetu kila la heri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani, *(IPU)*. Pia, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo kwa kuchaguliwa na kuapishwa leo hii kuwa Mbunge wa Mbarali. Aidha, nakupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza pia, Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali. Naishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge, Bi Nenelwa Joyce Mwihambi, *(ndc)* na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Balozi Prof. Kennedy Godffrey Gaston, kwa kuendelea kutekeleza vema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, kwa ushirikiano na ushauri

waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu katika Kamati. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri ya kuuchambua Muswada huu kwa umakini wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2023 unapendekeza marekebisho katika sheria zifuatazo:-

i. Sheria ya Utoaji Leseni za Biashara (Na. 25) ya Mwaka 1972.

ii. Sheria ya Chuo cha Teknolojia Dar-es-Salaam, Sura ya 144.

iii. Sheria ya Stahili na Mafao ya Majaji, Sura ya 424.

iv. Sheria ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Sura ya 93.

v. Sheria ya Mafao ya Kustaafu katika Utumishi wa Kisiasa, Sura ya 225.

vi. Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298.

vii. Sheria ya Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo, Sura ya 112.

viii. Sheria ya Mamlaka ya Uendelezaji wa Biashara Tanzania, Sura ya 155.

ix. Sheria ya Usajili wa Maafisa Mipango Miji, Sura ya 426.

x. Sheria ya Vipimo, Sura ya 440.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu 11. Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi yanayojumuisha jina la Muswada na namna ambavyo sheria mbalimbali zinapendekezwa kurekebishwa na Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Utoaji Leseni za Biashara (Na. 25) ya mwaka 1972, ambapo kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongezwa tafsiri ya baadhi ya misamiati ambayo imetumika katika sheria na ambayo haikuwa imetafsiriwa kwa lengo la kutoa ufafanuzi wa misamiati hiyo kama inavyotumika katika sheria.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 8 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuoanisha masharti ya kifungu hicho na masharti ya kifungu cha 7 cha Sheria ambacho kimeainisha ukomo wa Leseni ya Biashara kuwa miezi 12 tangu tarehe ya kutolewa kwa leseni husika.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa hitaji la kuambatanisha Hati ya Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi *(TIN)* wakati wa kuhuisha Leseni ya Biashara kwa kuwa hati hiyo huwasilishwa wakati wa maombi ya leseni ya biashara kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, kifungu kipya cha 14 (B), kinapendekezwa kuongezwa ili kuiwezesha Mamlaka ya Utoaji Leseni kufuta au kusitisha Leseni ya Biashara pamoja na kuweka utaratibu wa kufuatwa na Mamlaka ya Utoaji Leseni kabla ya kufuta au kusitisha leseni husika. Pia, inapendekezwa kufuta na kuandika upya, kifungu cha 17 kwa lengo la kuboresha majukumu ya Mamlaka ya Utoaji Leseni wakati wa kufanya ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, vilevile inapendekezwa kuongeza kifungu kipya cha 18(A) ili kubainisha wajibu wa mmiliki wa leseni ya biashara kuitaarifu mamlaka ya utoaji leseni ikiwa ataacha au kusitisha kufanya biashara, kufilisika, kubadili aina ya biashara au kubadili mahali pa kufanyia biashara. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha Mamlaka ya Utoaji Leseni inakuwa na taarifa sahihi na zenye uhalisia wakati wote.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 19 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho, ili kuongeza adhabu kwa makosa

yaliyoainishwa katika kifungu hicho kwa lengo la kuzuwia makosa kuendelea kutendeka.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 24 kimependekezwa kurekebishwa ili kutoa fursa kwa mmiliki wa leseni kupinga uamuzi uliotolewa na Mamlaka ya Utoaji Leseni. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa haki ya rufaa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Chuo cha Teknolojia Dar-es-Salaam, Sura ya 144 ambapo sheria inafanyiwa marekebisho ya jumla ili kukidhi matakwa ya Baraza la Mitihani, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(NACVET)* na muundo mpya wa chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha pili kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha tafsiri ya misamiati mbalimbali na kuongeza tafsiri ya misamiati ambayo imetumika kwenye sheria lakini haijatafsiriwa kwa lengo la kutoa ufafanuzi wa misamiati hiyo kama ilivyotumika katika sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha nne kinapendekezwa kurekebishwa ili kukipa Chuo mamlaka ya kutoa huduma za ushauri elekezi na kurahisisha uratibu wa kuchagua programu zitakazotolewa kulingana na mabadiliko ya kiteknolojia na mahitaji ya soko. Aidha, kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa ili kukiwezesha Chuo kuanzisha vitengo mbalimbali vya utawala na kufanya teuzi za viongozi wa vitengo hivyo. Lengo la marekebisho hayo ni kuboresha utaratibu wa uanzishwaji wa vitengo hivyo ili kuendana na muundo mpya wa Chuo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 7 kinapendekezwa kurekebishwa ili kupunguza idadi ya Wajumbe wa Baraza, lengo la marekebisho haya ni kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza ufanisi wa Baraza hilo.

Mheshimiwa Spika, vifungu vya 9(A) na 9(B) vinapendekezwa kuongezwa ili kuunda Kamati ya Taaluma itakayoshughulikia udhibiti na uhakiki wa ubora wa taaluma.

Mheshimiwa Spika, vifungu vya 10, 11, 12 na 15 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuainisha muda wa kushika uongozi wa Mkuu wa Chuo na Wasaidizi wake. Lengo la marekebisho haya ni kuzingatia miongozo ya *NACVET* ili kuendana na muundo mpya wa chuo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 16 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa ukomo wa kubadili matumizi ya fedha kwa lengo la kuoanisha na kuzingatia sheria za fedha. Vilevile kifungu cha 20 kinapendekeza kurebishwa kwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuboresha utaratibu unaohusu ada na posho za Baraza. Aidha, Jedwali linapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta aya ya kwanza na kuiandika upya kwa lengo la kuboresha muundo wa Baraza.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Stahili na Mafao ya Majaji Sura ya 424, ambapo inapendekezwa kuongezwa kifungu kipya cha 10(A) ili kuweka masharti ya kufanyika kwa gwaride la heshima kila mwaka kwa ajili ya kuwaaga Majaji wanaostaafu. Lengo la marekebisho haya ni kutambua na kuthamini mchango wa Majaji katika utoaji haki nchini.

Mheshimiwa Spika, Jedwali la Sheria linapendekezwa kurekebishwa ili kumuwezesha Jaji Mkuu Mstaafu kubadilishiwa gari kila baada ya miaka saba. Lengo la marekebisho haya ni kulinda hadhi ya Jaji Mkuu Mstaafu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Sura ya 93, ambapo sheria inafanyiwa marekebisho ya jumla kwa kubadili majina ya vyeo vya Mkuu wa Chuo na Wasaidizi wake ili kuendana na miongozo ya *NACVET*.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha tafsiri ya misamiati mbalimbali na kuongeza tafsiri ya misamiati ambayo imetumika kwenye sheria,

lakini haijatafsiriwa. Marekebisho haya yanakusudia kutoa ufafanuzi wa miasamiti hiyo kama ilivyotumika kwenye sheria.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa ili kutumia neno Mamlaka badala ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kama ilivyo sasa, ili kuondoa ulazima wa kurekebisha sheria hii kila yanapotokea mabadiliko ya jina la Mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kukipa chuo mamlaka ya kuanzisha matawi na vitengo vya utawala ili kuimarisha uongozi na utawala bora katika pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 6 kinapendekezwa kurekebishwa ili kupunguza idadi ya Wajumbe wa Bodi ya Uongozi. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza ufanisi wa Bodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 7 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuipa Bodi mamlaka ya kutoa maelekezo kwa uongozi wa Chuo au kupendekeza kwa Wizara hatua za kuchukuliwa kwa ajili ya uongozi na usimamizi bora wa chuo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 8 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuiwezesha Kamati ya Uteuzi kutoa mapendekezo kwa ajili ya uteuzi wa Makamu Mkuu wa Chuo na viongozi wengine wa chuo. Marekebisho haya yanalenga kuondoa upungufu katika sheria na hivyo kuweka bayana suala la teuzi za viongozi wa chuo.

Mheshimiwa Spika, vilevile kifungu cha 9 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha muundo wa Kamati ya Taaluma kuendana na miongozo ya *NACVET*. Aidha, kifungu hicho kinapendekezwa kurekebishwa ili kuiwezesha Kamati ya Taaluma kualika Mjumbe yeyote kutoka katika vikao vyake kadri itakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, vifungu vya 12 na 13 vinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuainisha uteuzi na majukumu ya

Makamu Mkuu wa Chuo. Lengo ni kuweka mgawanyo wa majukumu ya kitaaluma, utafiti na ushauri, pia majukumu yanayohusiana na mipango, fedha na utawala kwa ajili ya utendaji kazi wa chuo. Vilevile marekebisho haya yanalenga kuweka utaratibu wa kukaimu majukumu ya Mkuu wa Chuo endapo hayupo kwa kuzingatia miongozo ya *NACVET*. Aidha, marekebisho haya yanapendekezwa ili kuipa Bodi ya Uongozi mamlaka ya kutengeneza miongozo ya miundo na taratibu za Kamati ya uteuzi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 20 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuboresha utaratibu kuhusu ada na posho za Bodi ya Uongozi. Aidha, Jedwali linapendekezwa kurekebishwa ili kutoa nafasi ya kuteuliwa kwa awamu nyingine kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi na kuboresha utaratibu wa vikao vya Bodi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mafao ya Kustaafu katika Utumishi wa Kisiasa, Sura ya 225 ambapo vifungu vipya vya 9A, 12A na 14A vinapendekezwa kuongezwa ili kuwawezesha wenza wa Rais Mstaafu, Makamu wa Rais Mstaafu na Waziri Mkuu Mstaafu kulipwa kiinua mgongo kwa kipindi cha uongozi wa wenza wao. Sambamba na marekebisho hayo vifungu vya 11, 13 na 15 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka utaratibu wa malipo ya fadhila kwa wenza wa Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu endapo watafariki wakiwa madarakani au baada ya kumaliza muda wao na kufariki kabla ya kulipwa mafao au stahiki zao.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwawezesha Mawaziri Wakuu Wastaafu waliostaafu kabla ya kuanza kutumika kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria ya Mafao ya Kustaafu katika Utumishi wa Kisiasa ya mwaka 1999 kuwa na wasaidizi, yaani Makatibu, kwa ajili ya kuwasaidia katika kazi zao.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 18 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka utaratibu wa mwenza wa Spika Mstaafu, aliyefariki, kupokea mafao ya pensheni ya kila mwezi. Vilevile

Jedwali linapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuboresha stahiki za Viongozi Wakuu wa kisiasa pamoja na wenza wao.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 ambapo kifungu cha 25A kinapendekezwa kurekebishwa ili kumtaka mwenza wa Rais anayeingia madarakani, Makamu wa Rais anayeingia madarakani au Waziri Mkuu aliyeteuliwa ambaye ni mtumishi wa umma kustaafu katika utumishi wa umma kwa sababu za kiusalama pale mwenza wake anaposhika wadhifa husika. Vilevile kifungu cha 26 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumuwezesha mjane au mgane wa Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu aliyefariki kulipwa mafao ya pensheni kila mwezi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo, Sura ya 112 ambapo kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha tafsiri ya misamiati mbalimbali iliyotumika lakini haijatafsiriwa na kuongeza misamiati mipya kwenye sheria. Marekebisho haya yanalenga kutoa ufafanuzi wa misamiati hiyo kama ilivyotumika kwenye sheria na kuongeza misamiati mingine mipya iliyotumika kwenye sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kujumuisha viwanda vidogo sana na viwanda vya kati katika mawanda ya kifungu hicho ili kuhakikisha viwanda hivyo vinasimamiwa na kuhudumiwa na shirika.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 6 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuboresha mamlaka ya bodi. Lengo la marekebisho haya ni kuyaainisha kwa usahihi mamlaka ya bodi katika kusimamia shirika. Aidha, kifungu cha 7 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumtambua Mkurugenzi Mkuu wa shirika kama Katibu wa Bodi. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji wa maelekezo ya bodi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa ukomo wa kubadili matumizi ya fedha

kwa lengo la kuainisha masharti ya sheria hii na Sheria ya Fedha. Vile vile, Kifungu kipya cha 20 kinapendekezwa kuongezwa ili kumwezesha Waziri mwenye dhamana na masuala ya viwanda, kutengeneza kanuni zitakazowezesha utekelezaji bora wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tisa ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mamlaka ya Uendelezaji Biashara Tanzania, Sura ya 155 ambapo Kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya msamiati "shughuli za ukuzaji biashara." Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa msamiati huo ambao umetumika katika sheria lakini haukutafsiriwa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuzifanya shughuli za ukuzaji biashara kuwa miongoni mwa shughuli zinazoidhinishwa na mamlaka. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha maonesho ya ndani kudhibitiwa na mamlaka. Kifungu cha 20 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka chini ya usimamizi wa mamlaka mali na madeni yaliyokuwa yanamilikiwa na Bodi ya Biashara ya Ndani. Baada ya kufutwa kwa Sheria ya Bodi ya Biashara ya Ndani ya mwaka 1973 ambayo nafasi yake imechukuliwa na mamlaka.

Mheshimiwa Spika, kifungu kipya cha 23A kinapendekezwa kuongezwa kwa kuweka masharti ya vibali vya kufanya maonesho ya kibiashara na kuweka adhabu kwa mtu atakayefanya maonesho ya kibiashara bila kibali. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha waandaaji wa shughuli za maonesho wanazingatia masilahi ya washiriki. Kifungu kipya cha 24A kinapendekezwa kuongezwa ili kutoa mamlaka ya kufifisha makosa kwa wakosaji wanaotenda na kukiri makosa yako kwa hiari, chini ya sheria. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza muda na gharama za kuendesha mashauri mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 10 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Usajili wa Maafisa Mipango Miji, Sura ya 426 ambapo kifungu kipya cha 10A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti yanayohusu madaraja ya Wataalamu wa Mipango Miji. Kifungu cha 11 kinapendekezwa

kurekebishwa na vifungu vipya vya 11A, 11B, 11C na 11D, vinapendekezwa kuongezwa kwa lengo la kuboresha Masharti ya Usajili wa Wataalamu wa Mipango Miji na kuainisha madaraja na sifa za usajili wa wataalamu hao. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha bodi kudhibiti wataalamu hao na kusimamia mienendo yao.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 12 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumtaka mtu anayeomba usajili wa muda kuwa na sifa sawa na Mtaalamu wa Mpango Mji, mwenye usajili kamili nchini Tanzania. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha raia wa kigeni anayejihusisha na shughuli za mipango miji nchini, anakuwa na ujuzi stahiki. Kifungu cha 13 kinapendekezwa kufutwa kwa sababu maudhui yake yamejumuishwa katika Kifungu kipya cha 10A kinachopendekezwa kuongezwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile kifungu cha 24A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka Masharti ya Usajili wa Miradi ya Mipango Miji. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha unakuwepo udhibiti…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, kengele ya pili imegonga. Nakupa dakika tatu, malizia.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, udhibiti wa usimamizi wa ubora wa miradi ya Mipango Miji. Kifungu cha 31 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumwezesha Waziri mwenye dhamana na masuala ya mipango miji, kutengeneza kanuni.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 11 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Vipimo, Sura ya 340 ambapo sheria inapendekezwa kufanyiwa marekebisho ya ujumla ili kufuta maneno *"for use for trade"* na badala yake kuweka maneno *"for trade in use.'*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya na kama yanavyosomeka yote kwa ujumla kwenye *Hansard*, kwa mujibu wa

Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2023, naomba kutoa hoja kwamba Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) ya mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 4) Bill of 2023),* ujadiliwe na kupitishwa na kupitishwa katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa, yawe sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA JAJI DKT. ELIEZER MBUKI FELESHI, MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (Na. 4) WA MWAKA 2023 (THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (No. 4) BILL, 2023) KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2023 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2023).

**Mheshimiwa Spika,** napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza Nchi kwa malengo, ujasiri na uzalendo wa hali ya juu. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wenzangu kuendelea kumwomba Mwenyezi Mungu amjaalie Rais wetu kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** ninawapongeza Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu waJamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Dotö Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Mawaziri wote kwa kazi

kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kuchukua nafasi hii ukupongeza kwa kuchaguliwa kuwa rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU). Pia, nichukue nafasi kumpongeza Mhe. Bahati Keneth Ndingo kwa kuchaguliwa na kuapishwa leo hii kuwa mbunge wa Mbarali. Aidha, nawapongeza wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali. Ninaishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Joyce Mwihambi, (ndc.) na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mnaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** ninawapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Balozi Profesa Kennedy Godfrey Gastorn kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mbunge wa Madaba) na Makamu Mwenyekiti Mhe. Florent Laurent Kyombo (Mbunge wa Nkenge) kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu katika Kamati. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Muswada huu kwa makini.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2023, unapendekeza marekebisho katika Sheria zifuatazo:

1. Sheria ya Utoaji Leseni za Biashara, Na. 25 ya Mwaka 1972 *(The Business Licensing Act, No. 25 of 1972);*

2. Sheria ya Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam, Sura ya 144 *(The Dar es Salaam Institute of Technology Act, Cap. 144)*

3. Sheria ya Stahili na Mafao ya Majäji, Sura ya 424 *(The Judges (Remuneration and Terminal Benefits) Act, Cap.424);*

4. Sheria ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Sura ya 93 *(The Mwalimu Nyerere Memorial Academy Act, Cap. 93);*

5. Sheria ya Mafao ya Kustaafu katika Utumishi wa Kisiasa, Sura ya 225 *(The Political Service Retirement Benefits Act, Cap. 225);*

6. Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 *(The Public Service Act, Cap. 298);*

7. Sheria ya Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo, Sura ya 112 *(The Small Industries Development Organisation Act, Cap. 112);*

8. Sheria ya Mamlaka ya Uendelezaji wa Biashara Tanzania, Sura ya 155 *(The Tanzania Trade Development Authority Act, Cap. 155);*

9. Sheria ya Usajili wa Maafisa Mipango Miji, Sura ya 426 *(The Town Planners (Registration) Act, Cap. 426); na*

10. Sheria ya Vipimo, Sura ya 340 *(The Weights and Measures Act, Cap. 340)*.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kumi na Moja. Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi yanayojumuisha Jina la Muswada na namna ambavyo Sheria mbalimbali zinapendekezwa kurekebishwa na Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Utoaji Leseni za Biashara, Na. 25 ya Mwaka 1972 ambapo kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya baadhi ya misamiati ambayo imetumika katika Sheria na ambayo haikuwa imetafsiriwa

kwa lengo la kutoa ufafanuzi wa misamiati hiyo kama ilivyotumika katika Sheria.

Kifungu cha 8 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuoanisha masharti ya kifungu hicho na masharti ya kifungu cha 7 cha Sheria ambacho kimeainisha ukomo wa leseni ya biashara kuwa miezi kumi na mbili tangu tarehe ya kutolewa kwa leseni husika. Kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa hitaji la kuambatisha hati ya Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) wakati wa kuhuisha leseni ya biashara kwa kuwa hati hiyo huwasilishwa wakati wa maombi ya leseni ya biashara kwa mara ya kwanza.

Kifungu kipya cha 14B kinapendekezwa kuongezwa ili kuiwezesha mamlaka ya utoaji leseni kufuta au kusitisha leseni ya biashara, pamoja na kuweka utaratibu wa kufuatwa na mamlaka ya utoaji leseni kabla ya kufuta au kusitisha leseni husika. Pia, inapendekezwa kufuta na kuandika upya kifungu cha 17 kwa lengo la kuboresha majukumu ya mamlaka ya utoaji leseni wakati wa kufanya ukaguzi.

Vilevile, inapendekezwa kuongeza kifungu kipya cha 18A ili kubainisha wajibu wa mmiliki wa leseni ya biashara kuitaarifu mamlaka ya utoaji leseni ikiwa ataacha au kusitisha kufanya biashara, kufilisika, kubadili aina ya biashara au kubadili mahali pa kufanyia biashara. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha mamlaka ya utoaji leseni inakuwa na taarifa sahihi na zenye uhalisia wakati wote. Kifungu cha 19 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kuongeza adhabu kwa makosa yaliyoainishwa katika kifungu hicho kwa lengo la kuzuia makosa kuendelea kutendeka.

Kifungu cha 24 kinapendekezwa kurekebishwa ili kutoa fursa kwa mmiliki wa leseni kupinga uamuzi uliotolewa na mamlaka ya utoaji leseni. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa haki ya rufaa.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam,

Sura ya 144 ambapo Sheria inafanyiwa marekebisho ya jumla ili kukidhi matakwa ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) na muundo mpya wa Chuo hicho. Kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha tafsiri Ya misamiati mbalimbali na kuongeza tafsiri ya misamiati ambayo imetumika kwenye Sheria lakini haijatafsiriwa kwa lengo la kutoa ufafanuzi wa misamiati hiyo kama ilivyotumika katika Sheria.

Kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa ili kukipa Chuo mamlaka ya kutoa huduma za ushauri elekezi na kurahisisha utaratibu wa kuchagua programu zitakazotolewa kulingana na mabadiliko ya kiteknolojia na mahitaji ya soko. Aidha, kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa ili kukiwezesha Chuo kuanzisha vitengo mbalimbali vya utawala na kufanya teuzi za viongozi wa vitengo hivyo. Lengo la marekebisho hayo ni kuboresha utaratibu wa uanzishwaji wa vitengo hivyo ili kuendana na muundo mpya wa Chuo.

Kifungu cha 7 kinapendekezwa kurekebishwa ili kupunguza idadi ya wajumbe wa Baraza. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza ufanisi wa Baraza hilo.

Vifungu vya 9A na 9B vinapendekezwa kuongezwa ili kuunda Kamati ya Taaluma itakayoshughulikia udhibiti na uhakiki wa ubora wa taaluma. Vifungu vya IO, 11, 12 na 15 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuainisha muda wa kushika uongozi wa Mkuu wa Chuo na wasaidizi wake- Lengo la marekebisho haya ni kuzingatia miongozo ya NACTVET ili kuendana na muundo mpya wa Chuo.

Kifungu cha 16 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa ukomo wa kubadili matumizi ya fedha kwa lengo la kuoanisha na kuzingatia sheria za fedha. Vilevile, kifungu cha 20 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuboresha utaratibu unaohusu ada na posho za Baraza. Aidha, Jedwali linapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta aya ya 1 na kuiandika upya kwa lengo la kuboresha muundo wa Baraza-

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Stahili na Mafao ya Majaji, Sura ya

424 ambapo inapendekezwa kuongeza kifungu kipya cha IOA ili kuweka masharti ya kufanyika kwa gwaride la heshima kila mwaka kwa ajili ya kuwaaga majaji wanaostaafu. Lengo la marekebisho haya ni kutambua na kuthamini mchango wa Majaji katika utoaji haki nchini. Jedwali la Sheria linapendekezwa kurekebishwa ili kumwezesha Jaji Mkuu mstaafu kubadilishiwa gari kila baada ya miaka saba. Lengo la marekebisho haya ni kulinda hadhi ya Jaji Mkuu mstaafu.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Sura ya 93 ambapo Sheria inafanyiwa marekebisho ya jumla kwa kubadili majina ya vyeo vya Mkuu wa Chuo na wasaidizi wake ili kuendana na miongozo ya NACTVET. Kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha tafsiri ya misamiati mbalimbali na kuongeza tafsiri ya misamiati ambayo imetumika kwenye Sheria lakini haijatafsiriwa. Marekebisho haya yanakusudia kutoa ufafanuzi wa misamiati hiyo kama ilivyotumika kwenye Sheria.

Kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa ili kutumia neno "mamlaka" badala ya "Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi" kama lilivyo sasa ili kuondoa ulazima wa kurekebisha Sheria kila yanapotokea mabadiliko ya jina la mamlaka hiyo. Kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kukipa Chuo mamlaka ya kuanzisha matawi na vitengo vya utawala ili kuimarisha uongozi na utawala bora katika pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano. Kifungu cha 6 kinapendekezwa kurekebishwa ili kupunguza idadi ya wajumbe wa Bodi ya Uongozi. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza ufanisi wa Bodi hiyo.

Kifungu cha 7 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuipa Bodi mamlaka ya kutoa maelekezo kwa uongozi wa Chuo au kupendekeza kwa Wizara hatua za kuchukuliwa kwa ajili ya uongozi na usimamizi bora wa Chuo. Kifungu cha 8 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuiwezesha Kamati ya Uteuzi kutoa mapendekezo kwa ajili ya uteuzi wa Makamu Mkuu wa Chuo na viongozi wengine wa Chuo. Marekebisho haya

yanalenga kuondoa upungufu katika Sheria na hivyo kuweka bayana suala la teuzi za viongozi wa Chuo. Vilevile, kifungu cha 9 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha muundo wa Kamati ya Taaluma kuendana na miongozo ya NACTVET. Aidha, kifungu hicho kinapendekezwa kurekebishwa ili kuiwezesha Kamati ya Taaluma kualika mjumbe yeyote katika vikao vyake kadiri itakavyoona inafaa.

Vifungu vya 12 na 13 vinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuainisha uteuzi na majukumu ya Makamu Mkuu wa Chuo. Lengo ni kuweka mgawanyo wa majukumu ya kitaaluma, utafiti na ushauri, Pia, majukumu yanayohusiana na mipangoy fedha na utawala kwa ajili ya utendaji kazi wa Chuo. Vilevile, marekebisho hayo yanalenga kuweka utaratibu wa kukaimu majukumu ya Mkuu wa Chuo endapo hayupo kwa kuzingatia miongozo ya NACTVET. Aidha, marekebisho haya yanapendekezwa ili kuipa Bodi ya Uongozi mamlaka ya kutengeneza miongozo ya muundo na taratibu za Kamati ya Uteuzi.

Kifungu cha 20 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuboresha utaratibu kuhusu ada na posho za Bodi ya Uongozi. Aidha, Jedwali linapendekezwa kurekebishwa ili kutoa nafasi ya kuteuliwa kwa awamu nyingine kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi na kuboresha utaratibu wa vikao vya Bodi.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mafao ya Kustaafu katika Utumishi wa Kisiasa, Sura ya 225 ambapo vifungu vipya vya 9A, 12A na 14A vinapendekezwa kuongezwa ili kuwawezesha wenza wa Rais Mstaafu, Makamu wa Rais Mstaafu na Waziri Mkuu Mstaafu kulipwa kiinua mgongo kwa kipindi cha uongozi wa wenza wao. Sambamba na marekebisho hayo, vifungu vya 11, 13 na 15 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka utaratibu wa malipo ya fadhila kwa wenza wa Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu endapo watafariki wakiwa madarakani au baada ya kumaliza muda wao na kufariki kabla ya kulipwa mafao au stahiki zao.

Kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwawezesha Mawaziri Wakuu wastaafu waliostaafu kabla ya kuanza kutumika

kwa Sheria ya Mafao ya Kustaafu katika Utumishi wa Kisiasa ya Mwaka 1999 kuwa na wasaidizi (makatibu) kwa ajili ya kuwasaidia katika kazi zao. Kifungu cha 18 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka utaratibu wa mwenza wa Spika Mstaafu aliyefariki kupokea mafao ya pensheni ya kila mwezi. Vilevile, Jedwali linapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuboresha stahiki za Viongozi Wakuu wa kisiasa pamoja na wenza wao.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 ambapo kifungu cha 25A kinapendekezwa kurekebishwa ili kumtaka mwenza wa Rais anayeingia madarakani, Makamu wa Rais anayeingia madarakani au Waziri Mkuu aliyeteuliwa ambaye ni mtumishi wa Umma kustaafu katika utumishi wa Umma kwa sababu za kiusalama pale mwenza wake anaposhika wadhifa husika. Vilevile, kifungu cha 26 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumwezesha mjane au mgane wa Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu aliyefariki kulipwa mafao ya pensheni ya kila mwezi.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo, Sura ya 112 ambapo kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha tafsiri ya misamiati mbalimbali inayotumika lakini haijatafsiriwa na kuongeza misamiati mipya kwenye Sheria. Marekebisho haya yanalenga kutoa ufafanuzi wa misamiati hiyo kama ilivyotumika kwenye Sheria na kuongeza misamiati mingine mipya itakayotumika kwenye Sheria hiyo.

Kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kujumuisha viwanda vidogo sana na viwanda vya kati katika mawanda ya kifungu hicho ili kuhakikisha viwanda hivyo vinasimamiwa na kuhudumiwa na Shirika. Kifungu cha 6 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuboresha mamlaka ya Bodi. Lengo la marekebisho haya ni kuainisha kwa usahihi mamlaka ya Bodi katika kusimamia Shirika. Aidha, kifungu cha 7 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumtambua Mkurugenzi Mkuu wa Shirika kama Katibu wa Bodi. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji wa maelekezo ya Bodi kwa ufanisi.

Kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa ukomo wa kubadili matumizi ya fedha kwa lengo la kuoanisha masharti ya Sheria hii na sheria za fedha. Vilevile, kifungu kipya cha 20 kinapendekezwa kuongezwa ili kumwezesha Waziri mwenye dhamana na masuala ya viwanda kutengeneza kanuni zitakazowezesha utekelezaji bora wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tisa ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mamlaka ya Uendelezaji wa Biashara Tanzania, Sura ya 155 ambapo kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya msamiati "shughuli za ukuzaji biashara". Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa msamiati huo ambao umetumika katika Sheria lakini haujatafsiriwa.

Kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuzifanya shughuli za ukuzaji biashara kuwa miongonj mwa shughuli zinazoidhinishwa na Mamlaka. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha maonesho ya ndani kudhibitiwa na Mamlaka. Kifungu cha 20 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka chini ya usimamizi wa Mamlaka mali na madeni yaliyokuwa yanamilikiwa na Bodi ya Biashara ya Ndani baada ya kufutwa kwa Sheria ya Bodi ya Biashara ya Ndani ya mwaka 1973 ambayo nafasi yake ilichukuliwa na Mamlaka.

Kifungu kipya cha 23A kinapendekezwa kuongezwa kwa kuweka masharti ya vibali vya kufanya maonesho ya kibiashara na kuweka adhabu kwa mtu atakayefanya maonesho ya kibiashara bila kibali. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha waandaaji wa shughuli za maonesho wanazingatia maslahi ya washiriki. Kifungu kipya cha 24A kinapendekezwa kuongezwa ili kutoa mamlaka ya kufifilisha makosa kwa wakosaji wanaotenda na kukiri makosa yao kwa hiari Chini ya Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza muda na gharama za kuendesha mashauri Mahakamani.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Kumi ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Usajili wa Maafisa Mipango Miji, Sura ya 426 ambapo kifungu kipya cha IOA kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti yanayohusu madaraja ya watalaamu wa mipango miji.

Kifungu cha 1 1 kinapendekezwa kurekebishwa na vifungu vipya vya 1 IA, IIB, 1IC na 1 ID vinapendekezwa kuongezwa kwa lengo la kuboresha masharti ya usajili wa wataalamu wa mipango miji na kuainisha madaraja na sifa za usajili wa wataalamu hao. Lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha Bodi kudhibiti wataalamu hao na kusimamia mienendo yao.

Kifungu cha 12 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumtaka mtu anayeomba usajili wa muda kuwa na sifa sawa na mtaalamu wa mipango miji mwenye usajili kamili nchini Tanzania. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha raia wa kigeni anayejihusisha na shughuli za mipango miji nchini anakuwa na ujuzi stahiki. Kifungu cha 13 kinapendekezwa kufutwa kwa sababu maudhui yake yamejumuishwa katika kifungu kipya cha 10A kinachopendekezwa kuongezwa. Vilevile, kifungu cha 24A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti ya usajili wa miradi ya mipango miji. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha unakuwepo udhibiti na usimamizi bora wa miradi ya mipango miji.

Kifungu cha 31 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumwezesha Waziri mwenye dhamana na masuala ya mipango miji kutengeneza kanuni zitakazoainisha majukumu yatakayotekelezwa na kila daraja la mtalaamu wa mipango miji aliyesajiliwa. Marekebisho yanalenga kubainisha wigo wa majukumu yatakayotekelezwa na kila daraja la mtalaamu wa mipango miji kulingana na daraja lake. Aidha, Jedwali la Kwanza linapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha muundo wa Bodi kwa lengo la kuiongezea Bodi ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Kumi na Moja ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Vipimo, Sura ya 340 ambapo Sheria inapendekezwa kufanyiwa marekebisho ya jumla

ili kufuta maneno "for üşe for trade" na badala yake kuweka maneno 'Tor trade üşe". Lengo la marekebisho haya ni kurekebisha makosa ya kiuandishi. Kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha, kufuta na kuongeza baadhi ya misamiati katika kifungu hicho. Lengo la marekebisho haya ni kutoa tafsiri sahihi ya maneno yaliyotumika katika Sheria.

Vifungu vya 5, 6, 7 8, 9, 10, 14 na 18 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuhamisha majukumu ya kiutendaji kutoka kwa Waziri kwenda kwa Kamishna wa Vipimo. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wakala wa Vipimo ili kuendana na mabadiliko ya kiutendaji yaliyotokana na kuanzishwa kwa Wakala wa Vipimo, Kifungu cha 16 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwapa wakaguzi wajibu wa kuzingatia Sheria katika utekelezaji wa majukumu yao kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria.

Vifungu vya 19, 21, 23, 24, 39, 42, 48 na 49 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha masharti yanayohusu utekelezaji wa majukumu ya mamlaka ya wakaguzi. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa upungufu uliobainika wakati wa utekelezaji wa Sheria na kuongeza ufanisj katika utekelezaji wa Sheria husika.

Vifungu vya 26 na 50 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuipa Mahakama mamlaka ya kutoa amri ya kutaifisha au kuelekeza namna ya uondoshaji wa bidhaa zisizokidhi masharti ya Sheria ili kuzuia makosa kuendelea kutendeka. Aidhaı kifungu cha 54 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha masharti kuhusu mamlaka ya Waziri kutengeneza kanuni ili kuendana na marekebisho mengine yanayopendekezwa katika masharti mbalimbali ya Sheria hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2023 ,ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2023 (the Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2023) ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya Kusomwa kwa mara ya Pili

na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

**Mheshimiwa Spika,** NAOMBA KUTOA HOJA.

Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi (Mb.),
**MMWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**
31 Oktoba, 2023

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Hoja imeungwa mkono. Tunaendelea na utaratibu wetu. Namwita sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria. Wasomaji inabidi mkae upande wangu wa huku kulia, ikiwa mmechaguliwa kusoma na wale wengine upande wa kushoto ili tuwe tunakomboa wakati. *(Makofi)*

Kwa niaba ya Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO – MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) ya mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 4) Bill, 2023)*.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) ya mwaka 2023. Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93(2) ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza katika Mkutano wa Kumi

na Mbili, Kikao cha Tisa kwenye Bunge la Kumi na Mbili, tarehe 8 Septemba, 2023.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136(14) na kifungu cha 7(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ulielekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muwada huu kwa kuzingatia Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, namna Kamati ilivyotekeleza jukumu la uchambuzi wa Muswada. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 18 Oktoba, 2023 ili kupokea maelezo ya Mheshimiwa Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Mbunge na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kuhusu maudhui ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo ya ufafanuzi katika Ibara mbalimbali za Muswada.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge, Kamati ilifanya Mkutano wa Kusikiliza Maoni ya Wadau *(Public Hearing)*. Tarehe 19 Oktoba 2023 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao, kutoka kwa watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuboresha Muswada huu. Nachukua fursa hii kuwatambua kama ifuatavyo: -

(i) Chama cha Wanasheria Tanganyika;

(ii) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu; pamoja na

(iii) Watu binafsi kutoka maeneo mbalimbali nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwa kuzingatia maoni ya wadau. Mnamo tarehe 23 Oktoba, 2023, Kamati ilikutana tena na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye alijibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu Ibara mbalimbali za Muswada.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni ya Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) ya mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 4) Bill, 2023)*, ukiwa umegawanyika katika sehemu 11 na unapendekezwa kufanya marekebisho katika sheria 10, kwa madhumuni ya kuondoa upungufu na kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika kutekeleza sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni kama zifuatavyo: -

(a) Sheria ya Leseni ya Biashara (Na. 25) ya Mwaka 1972 *(The Business Licensing Act (No. 25) 1972)*.

(b) Sheria ya Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Sura ya 144 *(The Dar es Salaam Institute of Technology Act, CAP. 144)*

(c) Sheria ya Stahili na Mafao ya Majaji, Sura ya 424 *(The Judges Remuneration and Terminal Benefits Act, CAP. 424)*

(d) Sheria ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Sura ya 93 *(The Mwalimu Nyerere Memorial Academy Act, CAP. 93)*

(e) Sheria ya Mafao ya Kustaafu katika Utumishi wa Kisiasa, Sura ya 225 *(The Political Service Retirement Benefits Act, CAP. 225)*

(f) Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 *(The Public Service Act, CAP. 298)*

(g) Sheria ya Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo, Sura ya 112 *(The Small Industries Development Organization Act, CAP. 112)*

(h) Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara, Sura ya 155 *(The Tanzania Trade Development Authority Act, CAP. 155)*

(i) Sheria ya Usajili wa Wataalamu wa Mipango Miji, Sura 426, *(The Towns Planners Registration Act, CAP 426);* na

(j) Sheria ya Vipimo Sura ya 340 *(The Weight and Measures Act, CAP. 340)*

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inayohusu Masharti ya Utangulizi, inajumuisha Ibara ya 1 inayohusu jina fupi na Ibara ya 2 inayoelezea marekebisho yanayofanyika katika sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, wakati wakufanya uchambuzi wa Muswada huu pamoja na maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati ilibaini changamoto au upungufu katika sheria nne kati ya sheria 10 zilizopendekezwa kufanyiwa marekebisho, kama zilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Leseni za Biashara (Na. 25) ya 1972, marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 3 hadi Ibara ya 11 ya Muswada. Marekebisho katika sehemu hii kwa ujumla yanalenga kuongeza tafsiri ya misamiati ambayo awali haikuwa imefafanuliwa, kuhariri masharti ya ukomo wa leseni na kuweka utaratibu wa kufuta au kusitisha leseni ya biashara. Pia, marekebisho haya yanahusisha kuongeza majukumu ya Mamlaka

ya Utoaji Leseni wakati wa ukaguzi na kuongeza adhabu kwa makosa yaliyoainishwa katika sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya pia yanaweka masharti kwa mmiliki wa leseni ya biashara, kuwasilisha taarifa kwa mamlaka husika ikiwa atapanga kusitisha au kuacha kufanya biashara, kubadili aina ya biashara au kubadili mahali pa biashara.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Chuo cha kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Sura ya 93 *(The Mwalimu Nyerere Memorial Academy Act, CAP 93)*. Sehemu hii inahusu Ibara ya 29 hadi 41 ambapo marekebisho yanayopendekezwa katika sheria hii ni kuboresha na kurekebisha sheria ili kuendana na miongozo ya *NACTVET* (Baraza na Taifa la Mafunzo ya Ufundi na Ufundi Stadi) ambayo ni Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi nchini.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 32 ya Muswada inapendekeza kuweka jina la jumla la mamlaka ya usimaimzi badala ya jina kamili la *NACTVET*. Hii inalenga kuondoa ulazima wa kurekebisha sheria kila yanapotokea mabadiliko ya jina la mamlaka hiyo. Marekebisho mengine katika sehemu hii yanalenga kuboresha uongozi na utawala katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Baadhi ya marekebisho yanahusisha kubadili majina ya vyeo vya Mkuu wa Chuo na Wasaidizi wake ili kuendana na miongozo ya *NACTVET*. Pia, marekebisho haya yanahusu kuongeza na kuboresha tafsiri ya misamiati mbalimbali ili kutoa ufafanuzi wa misamiati inayotomika kwenye sheria lakini haijatafsiriwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Mafao ya Kustaafu katika Utumishi wa Kisiasa, Sura ya 225 *(The Political Service Retirement Benefits Act, CAP. 225)*. Kamati ilielezwa kuwa marekebisho kwa ujumla yanalenga mambo yafuatayo: -

(a) Kuongezwa kwa Vifungu vipya vya 9 (a), 12 (a) na 14 (a) ili kuwawezesha wenza wa Rais Mstaafu, Makamu wa Rais

Mstaafu na Waziri Mkuu Mstaafu, kulipwa kiinua mgongo wakati wa kipindi cha uongozi wa wenza wao.

(b) Kufanya marekebisho katika Vifungu vya 11, 13 na 15 ili kuweka utaratibu wa malipo ya *pension* kwa wategemezi wa Rais Mstaafu, Makamu wa Rais Mstaafu na Waziri Mkuu Mstaafu, endapo watafariki wakiwa madarakani au baada ya kumaliza muda wao na kufariki kabla ya kulipwa mafao na stahiki zao.

(c) Kurekebisha Kifungu cha 14 ili kuwawezesha Mawaziri Wakuu Wastaafu ambao walistaafu kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria ya Mafao ya Kustaafu katika Utumishi wa Kisiasa mwaka 1999, kuwa na wasaidizi yaani Makatibu kwa ajili ya kuwasaidia katika kazi zao.

(d) Kurekebisha Kifungu cha 18 ili kuweka utaratibu wa mwenza wa Spika Mstaafu aliyefariki, kupokea mafao ya *pension* ya kila mwezi.

(e) Kufanya marekebisho katika Jedwali la Sheria ili kuboresha stahiki za viongozi wakuu wa kisiasa pamoja na wenza wao ama familia za karibu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 11 ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Vipimo, Sura ya 340 *(The Weight and Measures Act, CAP. 340)*. Marekebisho haya yanafafanuliwa katika Ibara ya 77 hadi Ibara ya 98 ya Muswada. Kamati ilielezwa kuwa, marekebisho kwa ujumla yanalenga kurekebisha makosa ya kiuandishi pamoja na kutoa tafsiri sahihi ya maneno yaliyotumika katika kuleta maana iliyokusudiwa kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wakala wa Vipimo, kwa kuhamishia majukumu ya kiutendaji kwa Kamishna wa Vipimo badala ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho haya yanatarajiwa kuongeza ufanisi na kuboresha utekelezaji wa majukumu ya wakala. Muswada huu unapendekeza kuwaongezea uwezo Mamlaka ya Vipimo ya kukamata bidhaa ambazo hazijakidhi

vigezo vya kisheria, ikiwa ni pamoja na kufunga eneo ambalo mkaguzi au Afisa Vipimo anaamini limetumika kutenda kosa chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, Ibara ya 97 inafuta Kifungu cha 49 na kukiandika upya ili kutambua uthibitisho wa mkaguzi au Afisa Vipimo wa Maandishi kuhusu uzito wa bidhaa au bidhaa yenyewe na kuwa utapokelewa Mahakamani kama ushahidi bila uthibitisho *(Judicial Notes)*. Vile vile Ibara hiyo inafuta na kukiandika upya Kifungu cha 50 ili kutoa nafasi ya mmiliki wa vifaa vya kupimia au bidhaa zilizozuiliwa kujieleza na akishindwa kufanya hivyo ndipo vitaifishwe na hatimaye kuondolewa kadiri ya amri ya Mahakama. Lengo ni kuondoa upungufu uliobainika wakati wa utekelezaji na kuongeza ufanisi katika utendaji.

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni na mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zifuatazo: -

Mheshimiwa spika, marekebisho ya Sheria ya Leseni ya Biashara; katika Ibara ya 8, Kamati ilipendekeza kuwaondoa Askari Polisi kwenye jukumu la moja kwa moja la kuingia kwenye biashara na kufanaya ukaguzi wa leseni, bila kutokuwa na sharti la kuandamana na Afisa Biashara. Aidha, Kamati ilishauri kuwa, sheria isiwekewe ulazima kwa Maafisa Biashara kuambatana na Polisi kwenye ukaguzi, isipokuwa kama wataona kuwa kuna umuhimu wa kuambatana nao.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati nayo imefanya mabadiliko kwa kuzingatia ushauri wa Kamati. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufuata ushauri wa Kamati na kuwaondoa Askari Polisi kwenye jukumu la moja kwa moja la ukaguzi wa Leseni za Biashara na kuambatana na Maafisa Biashara, pale watakapoona wanahitajika.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere; Ibara ya 37 inaunda Kamati ya Taaluma inayoshugulikia udhibiti na uhakiki wa ubora wa taaluma kwenye chuo hiki. Aidha, Ibara hiyo imeainisha Wajumbe walioko kwenye Kamati hiyo. Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Serikali kuhusu umuhimu wa kuwepo kwa uwakilishi wa Mwamini wa Mwanafunzi *(Deans of Students)*, pamoja na Wakuu wote wa Vitivo na Idara za chuo kwenye Kamati hiyo. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho na kuongeza Wajumbe kama ilivyoshauriwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Mafao ya Kustaafu ya Utumishi wa Kisiasa; katika Ibara ya 43, 45, 46 na 48, Kamati ilipendekeza kutotumia maneno ya "kiinua mgongo *(gratuity)*," kwa kuwa maneno hayo kwa muktadha wa sheria yanatumika kuwalipa watumishi wa Umma ambao ni Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Spika, Naibu wa Spika, Mawaziri, Manaibu Waziri, Wabunge, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Aidha, Kamati ilishauri Serikali kutumia maneno "malipo ya fadhila *(ex-gracia),"* kuakisi lengo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 51 inarekebishwa ili kuwaimarishia ulinzi Makamu wa Rais Mstaafu na Waziri Mkuu Mstaafu pamoja na familia zao za karibu. Hata hivyo, maneno ya "familia ya karibu" hayakupewa tafsiri rasmi kwenye sheria hii ili kutotolewa tafsiri ambazo hazikukusudiwa na kutokana na ufafanuzi wa Serikali kuwa wanakusudia kuimarisha ulinzi kwenye makazi ya viongozi hao. Kamati iliishauri Serikali kutumia neno 'makazi' kama mbadala kwa maneno ya "familia ya karibu."

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na umefanya mabadiliko kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati. Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya mabadiliko na kufuta maneno "kiinua mgongo" na kuandika maneno "malipo ya fadhila" na kufuta maneno 'familia ya karibu' na kuandika neno "makazi."

Mheshimiwa Spika, Marekebesho ya Sheria ya Vipimo, Ibara ya 97 inarekebisha kifungu cha 50 cha sheria hii kwa kuweka

taratibu za kutaifisha mali na kuziondoa, baada ya mmiliki kushindwa kutokea kujieleza kuhusu dosari zilizobainika kwenye mali zake. Kifungu hakijaweka wazi mmiliki atatokea kujitetea wapi, kwa kukiacha kama kilivyo kunaweza kuzua sintofahamu na kupelekea mali kutaifishwa. Kwa kuwa mahakama inajukumu la kikatiba la kusimamia utoaji wa haki nchini, kamati ilishauri Serikali kufafanua kuwa mmiliki huyu atafikishwa mahakamani kwenda kujibu tuhuma hizo.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali kwa kukubaliana na ushauri wa kamati na wamefanya mabadiliko kwa kuzingatia ushauri wa kamati. Hitimisho, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa wajumbe wa kamati kwa kujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia Muswada huu, naomba majina yao yaingizwe katika kumbukumbu rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Balozi, Dkt. Pindi Chana, Mbunge na Waziri wa Katiba na Sheria. Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge na Naibu Waziri Wizara ya Katiba na Sheria. Bi. Mary Makondo, Katibu Mkuu Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali, ndugu Onorius Njole, pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge, ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa upekee, sekretarieti ya kamati kwa uratibu wa shughuli za kamati, hadi kukamilisha kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja, baada ya kusema hayo, kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali, kuupitisha Muswada huu pamoja na jedwali la marekebisho kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI NA. 4 WA MWAKA 2023 *[THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.4) BILL, 2023]* – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali na Hadidu za Rejea

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2023)*.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa kumi na mbili, kikao cha tisa kwenye Bunge la 12, tarehe 8 Septemba, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136(14) na kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

### 1.2 Namna Kamati ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi wa Muswada

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 18 Oktoba, 2023 ili kupokea maelezo ya Mhe. Jaji

Eliezer Mbuki Feleshi (Mb) Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu maudhui ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali, na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya Mkutano wa Kusikiliza Maoni ya Wadau *(Public Hearing*) tarehe 19 Oktoba, 2023 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu na nichukue fursa hii kuwatambua kama ifuatavyo: -

1. Chama cha Wanasheria Tanganyika (*TLS*);
2. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*LHRC*); pamoja na
3. Wadau binafsi kutoka maeneo mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwa kuzingatia maoni ya wadau. Mnamo tarehe 23 Oktoba, 2023 Kamati ilikutana tena na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye alijibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA
### 2.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.4 wa Mwaka 2023 *[The*

*Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2023]* ukiwa umegawanyika katika sehemu kumi na moja (11) na unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria kumi (10) kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa Sheria hizo. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni zifuatazo: -

(a) Sheria ya Leseni za Biashara, Na. 25 ya Mwaka 1972; (*The Business Licensing Act, Act No. 25 of 1972*)

(b) Sheria ya Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam, Sura ya 144; (*The Dar es Salaam Institute of Technology Act* [*CAP.144*])

(c) Sheria ya Stahili na Mafao ya Majaji, Sura ya 424; (*The Judges (Remuneration and Terminal Benefits) Act,* [*CAP. 424*])

(d) Sheria ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Sura ya 93; (*The Mwalimu Nyerere Memorial Academy Act* [*CAP.* 93])

(e) Sheria ya Mafao ya Kustaafu katika Utumishi wa Kisiasa, Sura ya 225; (*The Political Service Retirement Benefits Act, [CAP. 255]*)

(f) Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298; (*The Public Service Act,* [*CAP. 298*])

(g) Sheria ya Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo, Sura ya 112; (*The Small Industries Development Organisation Act,* [*CAP. 112*])

(h) Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara, Sura ya 155; (*The Tanzania Trade Development Authority Act,* [*CAP. 155*])

(i) Sheria ya Usajili wa Wataalamu wa Mipango Miji, Sura ya 426; (*The Towns Planners (Registration) Act,* [*CAP.* 426]) na

(j) Sheria ya Vipimo, Sura ya 340. (*The Weights and Measures Act,* [*CAP. 340*])

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inayohusu masharti ya utangulizi, inajumuisha **Ibara ya 1** inyohusu jina fupi na **Ibara ya 2** inayoeleza marekebisho yanayofanyika katika sheria mbalimbali.

## 2.2 Sheria Zinazofanyiwa Marekebisho na Maudhui yake

**Mheshimiwa Spika**, Wakati tunafanya uchambuzi wa Muswada huu Pamoja na Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati ilibaini changamoto au mapungufu katika sheria Nne kati ya sheria kumi zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kama zilivyo wasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Leseni za Biashara, Na. 25 ya Mwaka 1972; (*The Business Licensing Act, N0. 25 of 1972*).** Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 3 hadi Ibara ya 11 ya Muswada. Marekebisho katika sehemu hii kwa ujumla yanalenga kuongeza tafsiri ya misamiati ambayo awali haikuwa imefafanuliwa, kuhariri masharti ya ukomo wa leseni na kuweka utaratibu wa kufuta au kusitisha leseni ya biashara. Pia, marekebisho haya yanahusisha kuongeza majukumu ya mamlaka ya utoaji leseni wakati wa ukaguzi na kuongeza adhabu kwa makosa yaliyoainishwa katika sheria hiyo. Marekebisho haya pia yanaweka masharti kwa mmiliki wa leseni ya biashara kuwasilisha taarifa kwa mamlaka husika ikiwa atapanga kusitisha au kuacha kufanya biashara, kubadili aina ya biashara au kubadili mahali pa biashara.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya **Sheria ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Sura ya 93; (*The Mwalimu Nyerere Memorial Academy Act* [*CAP. 93*])**.

Sehemu hii inahusu ibara ya 29 hadi 41 ambapo Marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria hii ni kuboresha na kurekebisha sheria ili kuendana na miongozo ya NACTVET (Baraza la Taifa la Mafunzo ya Ufundi na Ufundi Stadi), ambayo ni mamlaka ya usimamizi na udhibiti wa elimu na mafunzo ya ufundi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 32 ya Muswada inapendekeza kuweka jina la jumla la mamlaka ya usimamizi badala ya jina kamili la NACTVET, hii inalenga kuondoa ulazima wa kurekebisha Sheria kila yanapotokea mabadiliko ya jina la mamlaka hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Marekebisho mengine katika sehemu hii yanalenga kuboresha uongozi na utawala katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Baadhi ya marekebisho yanahusisha kubadili majina ya vyeo vya Mkuu wa Chuo na wasaidizi wake ili kuendana na miongozo ya NACTVET. Pia, marekebisho hayo yanahusu kuongeza na kuboresha tafsiri ya misamiati mbalimbali ili kutoa ufafanuzi wa misamiati iliyotumika kwenye Sheria lakini haijatafsiriwa.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Sita inapendekeza kufanya marekebisho ya **Sheria ya Mafao ya Kustaafu katika Utumishi wa Kisiasa, Sura ya 225; (*The Political Service Retirement Benefits Act, [CAP. 255]*)**. Kamati ilielezwa kuwa Marekebisho kwa ujumla yanalenga mambo yafuatayo: -

a) Kuongezwa kwa vifungu vipya vya 9A, 12A, na 14A ili kuwawezesha wenza wa Rais Mstaafu, Makamu wa Rais Mstaafu, na Waziri Mkuu Mstaafu kulipwa kiinua mgongo wakati wa kipindi cha uongozi wa wenza wao.

b) Kufanya marekebisho katika vifungu vya 11, 13, na 15 ili kuweka utaratibu wa malipo ya pensheni kwa wategemezi wa Rais Mstaafu, Makamu wa Rais Mstaafu, na Waziri Mkuu Mstaafu endapo watafariki wakiwa madarakani au baada ya kumaliza muda wao na kufariki kabla ya kulipwa mafao au stahiki zao.

c) Kurekebisha kifungu cha 14 ili kuwawezesha Mawaziri Wakuu wastaafu ambao walistaafu kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria ya Mafao ya Kustaafu katika Utumishi wa Kisiasa ya mwaka 1999 kuwa na wasaidizi (makatibu) kwa ajili ya kuwasaidia katika kazi zao.

d) Kurekebisha kifungu cha 18 ili kuweka utaratibu wa mwenza wa Spika Mstaafu aliyefariki kupokea mafao ya pensheni ya kila mwezi.

e) Kufanya marekebisho katika Jedwali la Sheria ili kuboresha stahiki za Viongozi Wakuu wa kisiasa pamoja na wenza wao ama familia ya karibu.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kumi na Moja ya Muswada inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Vipimo, Sura ya 340. (*The Weights and Measures Act,* [*CAP. 340*])**. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 77 hadi Ibara ya 98 ya Muswada. Kamati ilielezwa kuwa Marekebisho kwa ujumla yanalenga Kurekebisha makosa ya kiuandishi pamoja na kutoa tafsiri sahihi ya maneno yaliyotumika ili kuleta maana iliyokusudiwa na Kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wakala wa Vipimo kwa kuhamishia majukumu ya kiutendaji kwa Kamishna wa Vipimo badala ya Waziri. Marekebisho haya yanatarajiwa kuongeza ufanisi na kuboresha utekelezaji wa majukumu ya wakala.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu unapendekeza kuwaongezea uwezo Mamlaka ya Vipimo ya kukamata bidhaa ambazo hazijakidhi vigezo vya kisheria ikiwa ni pamoja na kufunga eneo ambalo mkaguzi / Afisa Vipimo anaamini limetumika kutenda kosa chini ya Sheria hii. Aidha, Ibara ya 97 inafuta kifungu cha 49 na kukiandika upya ili kutambua uthibitisho wa mkaguzi / Afisa Vipimo wa maandishi kuhusu uzito wa bidhaa au bidhaa yenyewe na kuwa utapokelewa Mahakamani kama ushahidi bila uthibitisho *(Judicial Notice)*. Vilevile, Ibara hiyo inafuta na kukiandika upya kifungu cha 50 ili kutoa nafasi kwa mmiliki wa vifaa vya kupimia au bidhaa zilizozuiliwa kujieleza na akishindwa kufanya hivyo ndipo vitataifishwa na hatimaye kuondoshwa kadiri ya amri ya Mahakama. Lengo ni kuondoa mapungufu yaliyobainika wakati wa utekelezaji na kuongeza ufanisi katika utendaji.

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI
### 3.1 Maelezo ya Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

### 3.2 Marekebisho ya Sheria ya Leseni za Biashara, Na. 25 ya Mwaka 1972; (The Business Licensing Act, N0. 25 of 1972).

**Mheshimiwa Spika**, Katika Ibara ya 8 Kamati ilipendekeza kuwaondoa Askari Polisi kwenye jukumu la moja kwa moja la kuingia kwenye biashara na kufanya ukaguzi wa leseni bila ya kutokuwa na sharti la kuambatana na Afisa Biashara. Aidha, Kamati ilishauri kuwa Sheria isiweke ulazima kwa Maafisa Biashara kuambatana na Polisi kwenye ukaguzi isipokuwa kama wataona kuna umuhimu wa kuambatana nao.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko Kwa kuzingatia ushauri wa Kamati. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufuata ushauri wa Kamati kwa kuwaondoa Askari Polisi kwenye jukumu la moja kwa moja la ukaguzi wa leseni za biashara na kuambatana na Maafisa Biashara pale watakapo hitajika.

### 3.3 Marekebisho ya Sheria ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Sura ya 93; (*The Mwalimu Nyerere Memorial Academy Act* [*CAP. 93*]).

**Mheshimiwa Spika**, Ibara 37 inaunda Kamati ya Taaluma inayoshughulikia udhibiti na uhakiki wa ubora wa taaluma kwenye Chuo hiki. Aidha, Ibara hiyo imeainisha wajumbe walioko kwenye Kamati hiyo, Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Serikali kuhusu umuhimu wa kuwepo na uwakilishi wa Mwamini wa Wanafunzi (*Dean of Students*) pamoja na Wakuu wote wa vitivo na idara ya Chuo kwenye Kamati hiyo. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali

ushauri na kuleta marekebisho kwa kuongeza wajumbe kama ilivyoshauriwa na Kamati.

**3.4 Marekebisho ya Sheria ya Mafao ya Kustaafu katika Utumishi wa Kisiasa, Sura ya *225*; (*The Political Service Retirement Benefits Act, [CAP. 255]*).**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Ibara ya 43, 45, 46 na 48 Kamati ilipendekeza kutokutumia maneno kiinua mgongo (*Gratuity*) kwa kuwa maneno hayo kwa muktadha wa sheria hii yanatumika kuwalipa Watumishi wa Umma ambao ni Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Spika, Naibu wa Spika, Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Wabunge, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Aidha, Kamati iliishauri Serikali kutumia maneno malipo ya fadhila (*ex-gratia*) kuakisi lengo linalokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 51 inarekebishwa ili kuwaimarishia ulinzi Makamu wa Rais Mstaafu na Waziri Mkuu Mstaafu pamoja na familia zao za karibu. Hata hivyo, maneno "familia ya Karibu" hayakupewa tafsiri rasmi kwenye sheria hii, na ili kutoleta tafsiri ambazo hazikukusudiwa na kutokana na ufafanuzi wa Serikali kuwa wanakusudia kuimarisha ulinzi kwenye makazi ya Viongozi hao wastaafu, Kamati iliishauri Serikali kutumia neno "makazi" kama mbadala wa maneno "familia ya Karibu".

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko Kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati. Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya mabadiliko ya kufuata maneno "kiinua mgongo" na kuandika maneno "malipo ya fadhila" na kufuta maneno "familia ya karibu" na kuandika neno "makazi".

**3.5 Marekebisho ya Sheria ya Vipimo, Sura ya 340. (*The Weights and Measures Act,* [*CAP. 340*]).**

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 97 inarekebisha kifungu cha 50 cha sheria hii kwa kuweka utaratibu wa kutaifisha mali na kuziondoa baada ya mmiliki kushindwa kutokea kujieleza kuhusu dosari zilizobainika kwenye mali zake. Kifungu hakijaweka wazi mmiliki

atatokea kujitetea wapi, kwa kukiacha kama kilivyo kunaweza kuzua sintofahamu na kupelekea mali kutaifishwa. Kwa kuwa Mahakama inajukumu la Kikatiba la kusimamia utoaji haki nchini, Kamati iliishauri Serikali kufafanua kuwa mmiliki huyo atafikishwa Mahakamani kwenda kujibu tuhuma hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Tunaipongeza Serikali kwa kukubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko Kwa kuzingatia ushauri wa Kamati.

## 4.0 HITIMISHO
### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb - Mjumbe
3. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana, (Mb) Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Pauline Philipo Gekul (Mb) Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria, Mhe. Eliezer Mbuki Feleshi Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndg. Onorius Njole, pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

### 4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Florent Laurent Kyombo (Mb)
**M/MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**
31 Oktoba, 2023

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana Makamu Mwenyekiti. Nimuite sasa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Balozi, Dkt. Pindi Chana, aje awasilishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa kama Waziri wa masuala ya katiba na sheria, nitakuwa mchoyo wa fadhila ikiwa sitatumia fursa hii leo kwa mara ya kwanza nikiwa kama Waziri wa Katiba na Sheria, nisipomshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Kwa

kuendelea kuniamini na kuniteua tena kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuridhia kutoa fedha za kuwezesha Mkutano wa 77 wa Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, unaoendelea jijini Arusha. Matokeo ya mkutano huu yamezidi kuing'arisha Tanzania kuwa kinara wa ulinzi na haki za binadamu duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nichukue fursa hii kukupongeza wewe kwa kupata ushindi wa kishindo, uliyokufanya kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU)*. Nampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unakusudia kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali za sekta ya sheria ili kuondoa mapungufu yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa sheria hizo. Muswada wa marekebisho ya sheria mbalimbali za sekta ya sheria wa mwaka 2023 kama ulivyowasilisha, unapendekeza marekebisho katika sheria zifuatazo. Zimeelezwa hapo kuanzia ukurasa wa pili hadi ukurasa wa nne, naomba ziingie kwenye *hansard* kama zinavyojieleza namba moja hadi 23.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu 24, ambapo sehemu ya kwanza inahusu masharti ya utangulizi, yanayojumuisha jina la Muswada na namna ambavyo sheria mbalimbali zinapendekezwa kurekebishwa na Muswada huu. Sehemu ya pili ya Muswada, inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mawakili sura ya 341, ambapo kifungu cha 4(a) kinapendekeza kurekebisha ili kuondoa cheo cha Wakili wa Serikali Mfawidhi, *State Attorney in charge*, na badala yake kuweka cheo cha Wakili wa Serikali wa Mkoa *(regional State Attorney)*.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya marekebisho haya ni kumfanya Wakili wa Serikali wa Mkoa, kuwa muwakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, katika kamati ya mawakili ya Mkoa. Pia kuendana na muundo wa sasa wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu

wa Serikali. Aidha Muswada unapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 8(1)(e) ili kuongeza wigo wa vyuo na kuweka sharti la lazima kupita katika shule ya sheria kwa vitendo. Lengo ni kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ubora wa Mawakili kwa kuwa na mafunzo yanayofanana kwa wote.

Mheshimiwa Spika, vifungu vya 41 na 42 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza adhabu kwa watu ambao siyo Mawakili wanaofanya kazi za Mawakili. Lengo la marekebisho haya yanayopendekezwa ni kuzuia utendaji wa makosa ambayo huathiri utaratibu wa upatikanaji wa haki hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ya Muswada inapendekeza kurekebisha sheria ya mamlaka ya rufaa sura ya 141 ambapo kifungu cha 4(e) kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka zuio kwa mahakama ya rufani kusikiliza maombi ya mapitio au uwamuzi wa muda isipokuwa kama maombi hayo yanaradhimu shauri la msingi.

Mheshimiwa Spika, vilevile kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha masharti ya kukata rufaa katika mashauri ya madai. Msingi wa marekebisho haya ni kuweka utaratibu utakaosaidia umalizaji wa mashauri ya madai kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya usuruhishi, sura ya 15 ambapo kifungu cha 82(3)(b) kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa mamlaka ya kusajili wasuruhishi kutoka kituo cha usuruhishi, kwa kuwa wasuruhishi husajiliwa na Msajili chini ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai, sura ya 33. Lengo la marekebisho haya ni kuowanisha masharti ya usajili wa wasuruhishi katika sheria hizo mbili.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, sura ya 391, ambapo kifungu cha 6 kinapendekezwa kurekebishwa ili kufuta maneno *Administrative Justice* na badala yake kuweka maneno *good Governance*.

Lengo la marekebisho haya ni kutumia maneno yanayoakisi majukumu ya Tume kama yalivyoainishwa katika Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, aya ya kwanza, inayopendekezwa kufutwa na kuandikwa upya. Lengo ni kuiacha tume na majukumu yake ya msingi ya uchaguzi na masuala ya kuendesha mashauri ya kisheria yabaki katika taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, aidha, kifungu cha 11 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kuanzisha eneo na cheo cha Naibu Makatibu wa Tume. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha utekelezaji wa majukumu ya tume. Vilevile kifungu cha 12 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka sharti kwa Naibu Makatibu wa Tume kuapa mbele ya Mheshimiwa Rais, kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya sita ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika sheria…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, subiri kidogo. Ni kitu gani hicho kinasikika huko? Waheshimiwa Wabunge, tafadhalini sana.

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, sehemu ya sita ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya mwenendo wa mashauri ya jinai, sura ya 20 kwa kuongeza kifungu cha 4(e) ili kuowanisha madhumuni ya msingi *(overriding objectives)* katika sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuzitaka mahakama kutenda haki kwa wakati na kuangalia haki msingi katika kusikiliza mashauri ya jinai bila kufungwa na kiasi kikubwa cha masharti ya kiufundi.

Mheshimiwa Spika, aidha vifungu vya 202, 204, 205(a) na 205(b) vinapendekeza kurekebishwa kwa kuahinisha namna ambavyo wataalam kama vile wataalam wa mripuko na wataalam wa uchunguzi wa makosa ya mtandao wanaweza kuteuliwa na Mkurugenzi wa mashitaka. Madhumuni ya marekebisho haya ni kubadilisha nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa

Serikali ili kuowanisha masharti ya sheria kuhusu taratibu za uteuzi na utangazaji wa wataalamu wanaoteuliwa chini ya sheria hii. Vilevile vifungu vya 361 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kubainisha mahakama ambayo *notice* ya kusudio la rufaa itawasilishwa kwa mashauri yaliyoamuliwa na mahakama za mahakimu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya saba ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya uhujumu uchumi ya makosa ya kupanga, sura ya 200, ambapo kifungu cha 29 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza kiwango cha thamani ya mali zinazohusika na kosa linaloweza kupewa dhamana kuwa shilingi milioni 300. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa mkanganyiko katika mashariti yanayotoa mamlaka kwa Mahakimu na Mahakama Kuu kusikiliza maombi ya dhamana kwa mashauri ya uhujumu uchumi ambapo kiwango cha fedha katika dhamana kwa mahakama na mahakimu kilipandishwa hadi kufika Shilingi milioni 300 kupitia marekebisho yaliyofanywa na sheria namba moja ya mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nane ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika sheria ya miamala ya kieletroniki, sura ya 442 ambapo kifungu cha 18(2) kinapendekezwa kurekebishwa ili kufuta masharti yanayohusu upokeaji wa ushahidi wa kieletroniki. Lengo la marekebisho haya ni kutenganisha masharti ya kupokea ushahidi wa kieletroniki chini ya kifungu kidogo cha kwanza na vigezo vya kufanya tathimini ya uzito wa ushahidi wa kieletroniki vilivyoainishwa katika vifungu vidogo cha pili.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tisa ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushahidi, sura ya sita, ambapo kifungu cha 127 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha ushahidi wa mtoto wa umri mdogo kupokelewa bila kujali vigezo vilivyotolewa na sheria au sheria nyingine yoyote kuhusu kupokelewa kwa ushahidi huo. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa changamoto ya tafsiri mahakamani, ambapo ushahidi wa mtoto umekuwa haupewi uzito, endapo mtoto hakutoa ahadi ya kuwa atasema kweli na kwamba hatasema uwongo.

Mheshimiwa Spika, hali hii imesababisha watuhumiwa katika kesi nyingi, hususani kesi za ukatili wa watoto kuachwa huru kutokana na kukosekana kwa uthibitisho wa ahadi ya mtoto kuwa atasema kweli na kwamba hatasema uwongo. Madhumuni ya marekebisho haya ni kupambana na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto kwa kuruhusu ushahidi wa watoto hao kupokelewa mahakamani bila kufungwa na masharti ya kiufundi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 10 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Chuo cha Usimamizi wa Mahakama Lushoto, sura ya 405 ambapo kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa ili kukipa chuo mamlaka ya kutoa mafunzo ya kimahakama na mafunzo endelevu ya sheria.

Mheshimiwa Spika, vilevile kifungu cha 6, cha 8 na cha 9 pamoja na jedwali vinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kumpa *Judge Mkuu* mamlaka ya kusimamia chuo. Aidha kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa ili kufanya Kamati ya Mipango ya Taaluma na Mitihani, kuwajibika kwa Baraza la Chuo badala ya kuwajibika kwa Mheshimiwa Waziri, *Judge Mkuu* na Mkuu wa chuo. Kifungu cha 23 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kulipa baraza mamlaka ya kutengeneza kanuni zinazohusu utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya chuo. Lengo la marekebisho haya ni kuianisha muundo wa uongozi na mifumo ya chuo na kanuni zinazotolewa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 11 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Mahakama, sura ya 237, ambapo kifungu cha 3, 33 na 34 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta cheo cha Msaidizi wa *Judge*. Msingi wa marekebisho haya ni kwenda sanjari na mabadiliko yaliyofanyika katika muundo wa mahakama ambao ulifuta kada ya wasaidizi wa ma-*Judge*. Vilevile kifungu cha 50 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumuwezesha Wakili wa Serikali wa Mkoa, kuwa mwakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, katika Kamati ya Maadili ya Mkoa na Maafisa wa Mahakama. Lengo la marekebisho haya ni kuweka masharti yanayoendana na muundo wa sasa wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 12 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, sura ya 216 ambapo kifungu cha 47 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuipa Mahakama ya Rufaa mamlaka ya kusikiliza rufaa kutoka Mahakama Kuu zinazotokana na mashauri ya ardhi yaliyosikilizwa na Mahakama Kuu katika kutekeleza mamlaka yake ya rufaa na mapitio. Lengo la marekebisho ni kuongeza wigo wa kutoa haki katika mashauri yanayohusu migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 13 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, sura ya 171, ambapo inapendekezwa kuongeza kifungu cha 4(a), ili kuiwezesha Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, kushirikishwa katika mchakato wa kutunga sheria. Hata hivyo tulipokea maoni ya kamati kuwa eneo hili linahitaji kufanyiwa kazi zaidi ili kubaini uwezo wa tume kukabiriana na wingi wa majukumu hayo. Serikali hii Sikivu inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, wetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kweli imekubaliana na maoni ya kamati na tumewasilisha jedwali la marekebisho kuondoa mapendekezo hayo ili kutoa nafasi yakufanya tathimini ya kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha kifungu cha 5 kinarekebishwa kwa kuongeza idadi ya Makamishina wa Tume wa muda kutokana na ongezeko la majukumu ya tume. Vile vile kifungu cha 22 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza idadi ya wajumbe wanaoweza kuunda akidi katika vikao vya tume. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya tume. Sehemu ya 14 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania, sura ya 425 ambapo vifungu vya 2, 9 na 15 vinapendekezwa kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo wakati Muswada huu umeshatangazwa nilipokea mapendekezo mengine ya ziada, mengi kuhusu sheria hii ambayo kimsingi yalikuwa hayajapita katika Kamati ya Waheshimiwa Mawaziri ya Katiba na Sheria *(KB)* na kuwa hayajapata nafasi ya kupata maoni ya wadau kwenye

*public hearing*, lakini pia yalikuwa hayajawasilishwa kwangu wakati kwa hati ya dharula.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu hizo na umuhimu wa sheria hii, tarehe 18 Oktoba, 2023 niliiomba kamati isijadili mapendekezo haya kwa kuwa kulikuwa na niya ya kuondoa kifungu hiki ili yalete katika sheria mahususi na kamati ilikubali, hivyo mapendekezo haya hayakujadiliwa na kamati, maana yake tume-*withdraw*.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 15 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Muswada wa Sheria, sura ya 21 ambapo jedwali la sheria linapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa maneno *Judge* anayehudumu *(serving Judge)* pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Bodi ya Taifa ya Ushauri wa Msaada wa Sheria, na badala yake kumuweka *Judge* Mstaafu au Wakili wa kujitegemea mwenye uzoefu usiyopungua miaka 10 na Afisa Sheria *(Law Officer)* ambaye atamuwakilisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, katika bodi hiyo. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuboresha utendaji kazi wa bodi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 16 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mahakama za Mahakimu, sura ya 11 ambapo kifungu cha 17 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti ya uanzishaji wa Mahakama maalumu. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha utowaji wa haki kwa kuharakisha umalizaji wa mashauri kutokana na uwepo wa mahakama mahususi kwa ajili ya shughuli na kushughulikia aina mahususi ya mashauri.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 17 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ofisi ya Taifa ya Mashitaka, sura ya 430, ambapo kifungu cha 23 kinapendekezwa kuboreshwa na kurekebishwa ili kuwajumuisha Maafisa Sheria na Mawakili we sheria na Mawakili wa Serikali, katika orodha ya watu wanaoweza kukasimiwa mamlaka na Mkurugenzi wa Mashitaka.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Mashitaka, hivyo kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 18 ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, sura ya 268, ambapo kifungu cha tatu kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza tafsiri ya misamiati inayopendekezwa kutumiwa katika sheria hii. Sehemu hii pia inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 7(a) na 7(b) ili kuweka masharti ya kuanzisha Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, katika muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, vile vile hii inapendekezwa kuongeza vifungu vipya vya 8(a) na 8(b) ili kuainisha majukumu ya Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, inayopendekezwa kuanzishwa pamoja na kumtambua Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama mamlaka ya uteuzi na nidhamu kwa watumishi katika Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria. Aidha marekebisho yanayopendekezwa pia yanaongeza kifungu kipya cha 10(a) kinachoainisha uhusiano kati ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wakili Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia kifungu cha 12(a) kinapendekezwa kuongezwa ili kumpa Mwanasheria Mkuu wa Serikali mamlaka ya kutoa maelekezo ya jumla au mahususi kwa Mwandishi Mkuu wa Sheria kuhusu Masuala ya uandishi wa sheria. Sambamba na marekebisho haya inapendekezwa kuongeza sehemu mpya inayoainisha vyanzo vya mapato ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pamoja na kuweka masharti mengine kuhusu masuala ya usimamizi wa sheria.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 19 ya Muswada inapendekezwa kufanya marekebisho katika Sheria ya Bodi ya Msamaha wa Wafungwa, Sura ya 400, ambapo Kifungu cha Tatu, kinapendekeza kurekebishwa ili kumuwezesha Mwendesha Mashitaka wa Mkoa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Msamaha wa Wafungwa wa Mkoa. Lengo la marekebisho haya ni kuiainisha

Sheria hii na Muundo wa sasa wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 20 ya Muswada, inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 ambapo kifungu cha 131, kinapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha umri wa mtoto kuwa ni chini ya miaka 18. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha umri wa mtoto katika Sheria hii na umri wa mtoto katika Sheria nyingine zinazohusu masuala ya mtoto.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 21 ya Muswada, inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Uthibitishaji Wosia na Usimamizi wa Mirathi, Sura ya 352, ambapo kifungu cha 49, kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti kwa wasimamizi wa mirathi kuwasilisha Mahakamani taarifa za mali za urithi pale wasimamizi wanapotenguliwa au kusimamishwa kuwa wasimamizi wa mirathi ili kulinda mali za urithi. Pia kuiwezesha Mahakama kujua kazi alizokuwa akitekeleza msimamizi wa mirathi kabla ya usimamizi wa aliyekuwa msimamizi kutenguliwa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 22 ya Muswada, inapendekezwa kufanya marekebisho katika Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256, ambapo kifungu cha 14, kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kuainisha utaratibu wa kulipia fidia kwa wahanga wa makosa ya uhalifu. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuwezesha wahanga wa uhalifu kulipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 23 ya Muswada, inapendekezwa kufanya marekebisho katika Sheria ya Chama cha Wanasheria Tanganyika, Sura ya 307, ambapo kifungu cha 15, kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza sifa za Wajumbe wa Baraza pamoja na kuongeza muda wa Wajumbe wa Baraza la Uongozi wa Chama kuwa madarakani. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha Uongozi na kuweka muda wa kutosha kwa viongozi kutekeleza vipaombele vya Baraza.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 24 ya Muswada, inapendekezwa kufanya marekebisho katika Sheria ya Usajili wa

Wadhamini Sura ya 318, ambapo kifungu cha 15, kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza tafsiri ya maneno Mkazi wa Kawaida, *Ordinary Resident*. Madhumuni ya marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa maneno hayo kama yalivyotumika katika kifungu hicho. Vile vile, kifungu cha 23, kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti bora yanayompa Kabidhi Wasii Mkuu mamlaka ya kushikiria mali zisizohamishika za mashirika ambayo yamefutwa nchini ya Sheria hiyo. Madhumuni ya marekebisho hayo ni kuzuia matumizi mabaya ya mali zilizo chini ya udhamini baada ya kufutwa kwa Mashirika ya Udhamini.

Mheshimiwa Spika, aidha, kifungu cha 28, kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kufanya ukiukwaji wa kifungu hicho kuwa kosa la kiutendaji badala ya kosa la jinai. Pia, kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza adhabu ya faini ili kuhakikisha kinatekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2023. Naomba kutoa hoja kwamba Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria wa Mwaka 2023 *(The Legal Sector Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023)*. Ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na ya tatu. Hatimaye, marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**MAELEZO YA MHESHIMIWA DKT. PINDI HAZARA CHANA, WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA, AKIWASILISHA MUSWADA WA MAREKEKEBISHO YA SHE-RIA MBALIMBALI ZA SEKTA YA SHE-RIA WA MWAKA 2023 (THE LEGAL SECTOR LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) BILL, 2023) KATIKA BUNGE IA JAMHURI YA MUUNGANO – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, naomba kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Kamati yako kuwasilisha Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria wa Mwaka 2023 (The Legal Sector Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023) unaopendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Ishirini na Tatu (23) zilizoainishwa katika Sehemu ya Pili hadi Ishirini na nne ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** nitakuwa.mchoyo wa fadhila jkiwa sitatumia fursa Wi leo kwa mara ya kwanza nikiwa kama Waziri wa Katiba na Sheria nisipomshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kuniteua tena kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Sisi katika lugha ya Sheria tunamsemo wa kilatini unasema "*quid por quo*" kwa Kiswahili chepesi ina maana "nipe nikupe" kwa imani aliyonyesha Mhe. Rais kwangu malipo nitakayomlipa ni kuchapa kazi kwa weledi,uaminifu,nidhamu na uadilifu.

**Mheshimiwa Spika,** namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuridhia na kutoa fedha za kuwezesha Mkutano wa 77 wa Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu unaoendelea katika Jiji la Arusha matokeo ya mkutano yamezidi kuing'arisha Tanzania kuwa kinara wa uiinzi wa haki za binadamu Duniani.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee nichukue fursa hii kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa kupata ushindi wa kishindo uliokufanya kuwa rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani(IPU) pamoja na kuwa wapo waliotamani ushindwe ila nataka niwaeleze Sisi wanasheria huwa tunamsemo unasema "res ipsa loquitur" (the thing speaks for itself) kwa lugha yetu adhimu ya Kiswahili tunasema

"chema chajiuza". Kwa namna unavyoliongoza Bunge letu hakuna ubishi Dunia inafahamu uwezo wako na ndio maana ukaibukuka na ushjndi wa kishjndo. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko(Mb) Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano kwa kuteuliwa na kuaminiwa kushika nafasi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu unakusudia kufanya marekebisho katika Sheria mbalimbali za Sekta ya Sheria ili kuondoa upungufu uliobainika wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria wa Mwaka 2023 kama ulivyowasilishwa, unapendekeza marekebisho katika Sheria zifuatazo:

1. Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 (The Advocates Act, Cap. 341);

2. Sheria ya Mamlaka ya Rufaa, Sura ya141 (The Appellate Jurisdiction Act, Cap. 141);

3. Sheria ya Usuluhishi, Sura ya 15 (The Arbitration Act, Cap. 15);

4. Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sura ya 391 (The Commission for Human Rights and Good Governance Act, cap. 391);

5. Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20 (The Criminal Procedure Act, Cap. 20);

6. Sheria ya Uhujumu Uchumi na Makosa ya Kupanga, Sura ya 200(The Economic and Organised Crime Control Act, Cap. 200);

7. Sheria ya Miamala ya Kielektroniki, Sura ya 442 (The Electronic Transactions Act, Cap. 442);

8. Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6 (The Evidence Act, Cap.6);

9. Sheria ya Chuo cha Usimamizi wa Mahakama Lushoto, Sura ya 405 (The Institute of Judicial Administration Lushoto Act, Cap. 405);

10. Sheria ya Usimamizi wa Mahakama, Sura ya 237 (The Judiciary Administration Act, Cap. 237);

11. Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216 (The Land Disputes Courts Act, Cap. 216

12. Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania Sura ya 171 (The Law Reform Commission of Tanzania Act, Cap. 171);

13. Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania, Sura ya 425 (The Law School of Tanzania Act, Cap. 425);

14. Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sura ya 21 (The Legal Aid Act, cap 21);

15. Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11 (The Magistrates' Courts Act, Cap. 11);

16. Sheria ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Sura ya 430 (The National Prosecutions Service Act, Cap. 430);

17. Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268 (The Office of the Attorney General (Discharge of Duties) Act, Cap. 268);

18. Sheria ya Bodi za Msamaha wa Wafungwa, Sura ya 400 (The Parole Boards Act, Cap. 400);

19. Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 (The Penal Code, Cap. 16);

20. Sheria ya Uthibitishaji Wosia na Usimamizi wa Mirathi, Sura ya 352 (The Probate and Administration of Estates Act, Cap. 352);

21. Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256 (The Proceeds of Crime Act, Cap. 256);

22. Sheria ya Chama cha Wanasheria Tanganyika, Sura ya 307 (The Tanganyika Law Society Act, Cap. 307); na

23. Sheria ya Usajili wa Wadhamini, Sura ya 318 (The Trustees' Incorporation Act, Cap. 318).

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Ishirini na Nne, ambapo Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi yenayojumuisha Jina la Muswada na namna ambavyo Sheria mbalimbali zinapendekezwa kurekebishwa na Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika** Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 ambapo kifungu cha 4A kinapendekezwa urekebishwa ili kuondoa cheo cha Mwanasheria wa Serikali (State Attorney Incharge) na badala yake kuweka cheo cha Wakili wa Serikali wa Mkoa *(Regional State Attorney)*. Madhumuni wa marekebisho haya ni kumfanya Wakili wa Serikali wa Mkoa mwakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serika katika Kamati ya Mawakili ya Mkoa na pia kuendana pa muundo wa sasa wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha Muswada unapendekeza kufanywa kwa marekebisho katika Kifungu cha 8 (1) (a) kwa kuongeza wigo wa vyuo na kuweka sharti la lazima ili kupitia katika shule ya sheria kwa vitendo. Lengo ni kuimarisha uwezo wa udhibiti wa ubora wa mawakili kwa kuwa na mafunzo yanayofanana kwawote.

Vifungu vya 41 na 42 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza adhabu kwa watu wasio mawakili wanaofanya kazi za mawakili. Lengo la marekebjsho yanayopendekezwa ni kuzuia utendaji wa makosa ambayo huathiri utaratibu wa upatikanaji wa haki hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kurekebish ya Sheria ya Mamlaka ya Rufaa Sura ya 141 ambapo kifungu cha 4A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka zuio kwa

Mahakama ya Rufani kusikiliza maombi ya mapitio au uamuzi wa muda isipokuwa kama maombi hayo yanamaliza shauri la msingi. Vilevile, kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha masharti ya kukata rufaa katika mashauri ya madai. Lengo la marekebisho haya ni kuweka utaratibu utakaosaidia umalizaji wa mashauri ya madai kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika** Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Usuluhjshi, Sura ya 15. ambapo Kifungu cha 82 (3) (b) kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa mamlaka ya usajiri wa usuluhishi kutoka Kituo cha Usuluhishi kwa kuwa wasuluhishi husajiriwa na Msajili kwa Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai, Sura ya 33. Lengo la marekebisho haya ni kuoanisha masharti ya wasuluhishi katika Sheria hizo mbili.

**Mheshimiwa Srika,** Sehemu ya Tano ya Muswada inapeadekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sura ya 39 ambapo kifungu cha 6 kinapendekezwa kurekebishwa ili kufuta manero "administrative justice" na badala yake kuweka meneno "good governance. Lengo la marekebisho haya ni kutumia maneno yunayoakisi majukumu ya Tume kama yalivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Aya ya (i) inapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya. Lengo ni kuiwezesha Tume kubaki na majukumu yake ya msingi ya uchunguzi na masuala ya kuendesha mashauri ya kisheri ya bakie katika taasisi husika. Aidha, kifungu cha 11 kinapendekezwa kufanyiwa maboresho ili kuanzisha cheo cha Naihu Katibu Mkuu wa Tume. Lengo la marekebisho haya ni kuboreshe utekelezaji wa majukumu ya Tume. Vilevile Kifungu cha 12 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwesha masharti ya Naibu Katibu Mkuu wa Tume kuapa mbele ya Rais kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika** Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mwenendo wa Masharti ya Jinai, Sura ya 22 kwa kuongeza kiungu cha 4A ili kuainisha madhumuni ya msingi (Overriding objectives) katika Sheria. Lengo

la marekebisho haya ni kuzitaka Mahakama kutenda haki kwa wakati na kuangalia haki msingi katika kusikiliza mashauri ya jinai bila kufungwa kwa kiasi kikubwa na masharti wa kifungu. Aidha, vifungu vya 202, 204, 205. 205A na 205B vinapendekeza kurekebishwa kwa kuainisha namna ambayo wataalamu kama vile wataalamu wa milipuko na watalaamu wa uchunguzi wa makosa ya mtandao kuweza kuteuliwa na wakurugenzi wa Mashtaka. Medhumuni ya marekebisho haya ni kubadilisha nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuoanisha masharti ya Sheria kuhusu taratibu za uteuzi na utangazaji watalaamu wanaoteuliwa chini ya Sheria hii. Vilevile, kifungu cha 361 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kubainisha Mahakama ambayo kusudio la rufaa itawasilishwa kwa mashauri yaliyoamuliwa na Mahakimu.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kalika Sheria ya Uhujumu Uchumi na nakosa ya Kupanga, Sura ya 200 anbapo kifungu cha 29 kinapedekeza Kurekebishwa kwa kuongeza Kiwango cha thamani ya mali zinazohusika na kosa linaloweza kupewa dhamana ku va shilingi milioni moja. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa mkanganyiko katika masharti yanayotoa mamlaka kwa mahakama za mahakimu na mahakama kuu kusikiliza maombi ya dhamana kwa mashauri ya uhujumu uchumi ambapo kiwango cha fedha katika dhamana kwa mahakama za mahakimu kilipandishwa hadi kufikia milioni mia tatu kupitia marekebisho yaliyofanywa na Sheria Na. 1 ya mwaka 2022.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Miamala ya Kielektroniki, Sura ya 442 ambapo kifungu cha 18(2) kinapendekezwa kurekebishwa ili kufuta masharti yanayohusu upokeaji wa ushahidi wa kielektroniki. Lengo la marekebisho haya ni kutenganisha masharti ya kupokea ushahidi wa Kielektroniki chini ya kifungu kidogo cha (1) na vigezo vya kufanya tathmini ya uzito wa ushahidi wa kielektroniki vilivyoanishwa katika kifungu kidogo cha (2).

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tisa ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6 ambapo kifungu cha 127 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha

ushahjdi wa mtoto wa umri mdogo kupokelewa bila kujali vigezo vilivyotolewa na Sheria au Sheria nyingine yoyote kuhusu kupokelewa kwa ushahidi huo. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa changamoto ya tafsiri mahakamani ambapo ushahidi wa mtoto umekuwa haupewi uzito endapo mtoto hakutoa ahadi ya kuwa atasema kweli na kwamba hatasema uongo, Hali hii imesababisha watuhumiwa katika kesi nyingi hususan kesi za ukatili kwa watoto kuachiwa huru kutokana na kukosekana kwa uthibjtisho wa ahadi ya mtoto kuwa atasema kweli na kwamba hatasema uongo. Madhumuni ya marekebjsho haya ni kupambana na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto kwa kuruhusu ushahidi wa watoto hao kupokelewa mahakamani bila kufungwa na masharti ya kiufundi.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Kumj ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Chuo cha Usimamizi wa Mahakama Lushotoı Sura ya 405, ambapo kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa ili kukipa Chuo mamlaka ya kutoa mafunzo ya kimahakama na mafunzo endelevu ya sheria. Vılevile, vifungu vya 6, 8 na 9 pamoja na Jedwali vinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kumpa Jaji Mkuu mamlaka ya kusimamia Chuo. Aidha, kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuifanya Kamati ya Mipango ya Taaluma na Mitihani kuwajibika kwa Baraza la Chuo badala ya kuwajibika kwa Wazjri, Jaji Mkuu na Mkuu wa Chuo. Kifungu cha 23 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kulipa Baraza mamlaka ya kutengeneza kanuni zinazohusu utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Chuo. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha muundo wa uongozi na mifumo ya chuo na kanuni zinazotolewa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Kumi na Moja ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Mahakama, Sura ya 237 ambapo vifungu vya 3, 33 na 34 vjnapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta cheo cha Msaidizi wa Jaji. Msingi wa marekebisho haya ni kwenda sanjari na mabadiliko yaliyofanyika katika muundo wa Mahakama ambao ulifuta kada ya Wasaidizi wa Majaji. Vilevile, kifungu cha 50 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumwezesha Wakili wa Serikali wa Mkoa kuwa

mwakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Kamati ya Maadili ya Mkoa ya Maafisa wa Mahakama. Lengo la marekebisho haya ni kuweka masharti yanayoendana na muundo wa sasa wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Kumi na Mbjli ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216 ambapo kifungu cha 47 kinapendekezwa kurekebishwa ilj kuipa Mahakama ya Rufaa mamlaka ya kusikiliza rufaa kutoka Mahakama Kuu zinazotokana na mashauri ya ardhi yaliyosikilizwa na Mahakama Kuu katika kutekeleza mamlaka yake ya rufaa na mapitio. Lengo la marekebisho ni kuongeza wigo wa utoaji haki katika mashauri yanayohusu migogoro ya ardhi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Sehemu ya Kumi na Tatu ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171 ambapo inapendekezwa kuongeza kifungu kipya cha 4A ili kuiwezesha Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania kushirikishwa katika mchakato wa kutunga sheria. Hata hivyo tulipokea maoni ya Kamati kuwa eneo hili linahitaji kufanyiwa kazi zaidi ili kubaini uwezo wa Tume kukabiliana na wingi wa majukumu hayo. Serikali hii Sikivu inayoongozwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassani Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekubaliana na maoni ya Kamati na tumewasilisha Jedwali la Marekebisho kuondoa mapendekezo hayo ili kutoa nafasi ya kufanya tathmini ya kina. Aidha, kifungu cha 5 kinarekebishwa kwa kuongeza idadi ya Makamishna wa Tume wa muda kutokana na ongezeko la majukumu ya Tume. Vilevi(e, kifungu cha 22 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza idadi ya wajumbe wanaoweza kuunda akidi katika vikao vya Tume. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Tume.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Kumi na Nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebjsho katika Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania, Sura ya 425 ambapo vifungu vya 2,9 na 15 vinapendekezwa kurebishwa. Hata hivyo wakati Muswada huu umeshatangazwa nilipokea mapendekezo mengine ya ziada

mengi kuhusu sheria hii ambayo kimsingi yalikuwa hayajapjtia katika Kamati ya Mawaziri ya Katiba na Sheria (KB) na kuwa hayapata nafasi ya kuapata maoni ya wadau kwenye (Public Hearing) lakini pia yalikuwa hayajawasilishwa kwangu kwa hati ya dharura. Kutokana na sababu hizo na umuhimu wa sheria hü tarehe 18 Oktoba, 2023 niliiomba kamati isijadili mapendekezo haya kwa kuwa kulikuwa na nja ya kuomba kuyaondoa ili yaletwe katika sheria mahusus na kamati ilitukubalia hivyo sheria mapendekezo haya hayakujadiliwa na kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Kumi na Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Msaada wa Sheria, Sura ya 21, ambapo Jedwali la Sheria linapendekezwa kurekebishwa ili kuwaondoa maneno "Jaji anayehudumu" (serving judge) pamoja na "Mwanasheria Mkuu wa Serikali" katika Bodi ya Taifa ya Ushauri wa Msaada wa Sheria na badala yake kumuweka "Jaji Mstaafu" au "Wakili wa Kujitegemea mwenye uzoefu usiopungua miaka kumi" na "Afisa Sheria (Law Officer)" ambaye atamwakilisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Bodi hiyo. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuboresha utendaji kazi wa Bodi.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Kumi na Sita ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Mahakama za Mahakimu Sura ya 11, ambapo kifungu cha 17 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti ya uanzishwaji wa Mahakama Maalumu. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha utoaji wa haki kwa kuharakisha umalizaji wa mashaurj kutokana na uwepo wa mahakama mahsusi kwa ajili ya kushughulikia aina mahsusi ya mashauri.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Kumi na Saba ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katjka Sheria ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Sura ya 430 ambapo kifungu cha 23 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwajumuisha Maafisa Sheria na Mawakili wa Serikali katika orodha ya watu wanaoweza kukasimiwa mamlaka na Mkurugenzi wa Mashtaka. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka hivyo kuongeza ufanisi.

**Mheshimiwa Spika** Sehemu ya Kumi na Nane ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268 ambapo kifungu cha 312 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza tafsiri ya misamiati inayopendekezwa kutumiwa katika Sheria hii. Sehemu hii pia inapendekeza kuongeza vifungu vipya vya 7A na 7 B ili kuweka masharti ya uanzishaji wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria katika muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vilevile, inapendekezwa kuongeza vifungu vipya vya 8A na 8B ili kuainisha majukumu ya Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria inayopendekezwa kuanzishwa pamoja na kumtambua Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama mamlaka ya uteuzi na nidhamu kwa watumishi wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria. Aidha: marekebisho yanapendekeza kuongeza kifungu kipya cha IOA kinachoainisha uhusiano kati ya Ofjsi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wakili Mkuu wa Serikali. Pia, kifungu cha 12A kinapendekezwa kuongezwa ili kumpa Mwanasheria Mkuu wa Serikali mamlaka ya kutoa maelekezo ya jumla au mahususi kwa Mwandishi Mkuu wa Sheria kuhusu masuala ya Uandishj wa Sheria. Sambamba na marekebisho haya, inapendekezwa kuongeza Sehemu mpya inayoainisha vyanzo vya mapato ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikati pamoja na kuweka masharti mengine kuhusu masuala ya usimamizi wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Kumi na Tisa ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Bodi za Msamaha kwa Wafungwa, Sura ya 400 ambapo kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumwezesha Mwendesha Mashtaka wa Mkoa kuwa mjumbe wa Bodi ya Msamaha wa Wafungwa ya Mkoa. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha Sheria hii na muundo wa sasa wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Kumi na Ishirini ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 ambapo kifungu cha 131 kinapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha umri wa mtoto kuwa ni Chini ya miaka kumi na nane. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha umri wa

mtoto katika Sheria hii na umri wa mtoto katika Sheria nyingine zinazohusu masuala ya watoto.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Ishirini na Moja ya Muswada Inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Uthibitishaji Wosia na Usimamizi wa Mirathi, Sura ya 352 ambapo kifungu cha 49 kinapendekezwa kurekebjshwa ili kuweka masharti kwa wasimamizi wa mirathi kuwasilisha mahakamani taarifa za mali za urithi pale wasimamizi wanapotenguliwa au kusimamishwa kuwa wasimamizi wa mirathi ili kulinda mali za urithi, Pia, kuiwezesha Mahakama kujua kazi alizotekeleza msimamjzi wa mirathi kabla ya usimamiz wa atiyekuwa msimamizi kutenguliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Ishirini na Mbili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256, ambapo kifungu cha 14 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kuainisha utaratibu wa kulipa fidia kwa wahanga wa makosa ya uhalifu. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuwezesha wahanga wa uhalifu ku!ipwa fidia.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Ishirini na Tatu ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sherja ya Chama cha Wanasheria Tanganyika, Sura ya 307 ambapo kifungu cha 15 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza sifa za wajumbe wa Baraza pamoja na kuongeza muda wa wajumbe wa Baraza Ia Uongozj wa Chama kuwa madarakani. Lengo Ia marekebisho haya ni kuimarisha uongozi na kuweka muda wa kutosha kwa viongozi kutekeleza vipaumbele vya Baraza.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Ishirini na Nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebjsho katika Sheria ya Usajili wa Wadhamini, Sura ya 318 ambapo kifungu cha 15 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza tafsiri ya maneno mkazi wa kawaida (ordinary resident). Madhumuni ya marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa maneno hayo kama yalivyotumika katika kifungu hicho. Vilevile, kifungu cha 23 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti bora yanayompa Kabidhi Wasii Mkuu mamlaka ya kushikilia mali zisizohamishika za mashirika ambayo yamefutwa

Chini ya Sheria hiyo. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuzuia matumizi mabaya ya mali zilizo Chini ya udhamini baada ya kufutwa kwa mashirika ya udhamini. Aidha, kifungu cha 28 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kufanya ukiukwaji wa kifungu hicho kuwa kosa la kiutendaji badala ya kosa la jinai. Pia, kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza adhabu ya faini ili kuhakikisha kinatekelezwa ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** wakati nahitimisha nichukue fursa hii kipekee kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa msaada mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Siku zote kamati imekuwa ikitupa ushauri na kutuunga mkono katika masuala mbalimbali yanahusu Wizara hawajawahi kutuacha. Aidha, shukrani hizi za kamati zikufikie na wewe Mheshimiwa Spika kwani mara zote tunapowasilisha maombi yetu kuhusu kamati umekuwa ukitukubalia.

Asante sana Mheshimiwa Spika.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

Dkt. Pindi Hazara Chana (Mb.,)
**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**
**31 Oktoba, 2023**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kwa niaba yake, Mheshimiwa Yahaya Massare. *(Makofi)*

**MHE. YAHAYA O. MASSARE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, naomba kusoma maoni ya Kamati kama nilivyopewa na Mwenyekiti wetu.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kuhusu Muswada wa

Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali katika Sekta ya Sheria wa Mwaka 2023 *(The Legal Sector Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023)*.

Mheshimiwa Spika, Utangulizi, maelezo ya awali na hadidu za rejea; kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria ya Mwaka 2023 *(The Legal Sector Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023)*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Kumi na Mbili, Kikao cha Tisa kwenye Bunge la Kumi na Mbili, tarehe 8 Septemba, 2023.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136(14) na kifungu cha 7(1)(b) cha nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, namna Kamati ilivyotekeleza jukumu la uchambuzi wa Muswada. Katika kutekeleza jukumu hilo Kamati ilikutana na Serikali tarehe 18 Oktoba, 2023 ili kupokea maelezo ya Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, (Mb) Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu maudhui ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali, na kupata maelezo ya ufafanuzi katika Ibara mbalimbali za Muswada.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilifanya Mkutano wa kusikiliza maoni ya wadau *(Public Hearing*) tarehe 19 Oktoba, 2023 ili kupokea

maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa wadau na makundi mbalimbali ya wadau ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu na nichukue fursa hii kuwatambua kama ifuatavyo: -

(i) Chama cha Wanasheria Tanganyika (*TLS*);

(ii) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*LHRC*); pamoja na

(iii) Wadau binafsi kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria na kwa kuzingatia maoni ya wadau. Mnamo Tarehe 23 Oktoba, 2023 Kamati ilikutana tena na Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria ambaye alijibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu Ibara mbalimbali za Muswada.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Muswada; Kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria wa Mwaka 2023 *(The Legal Sector Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023)* ukiwa umegawanyika katika sehemu ishirini na nne (24), na unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ishirini na tatu (23) kwa madhumuni ya kuondoa upungufu au dosari au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa sheria hizo. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni zifuatazo: -

(a) Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 (*The Advocates Act,Cap. 341*)

(b) Sheria ya Mamlaka ya Rufaa, Sura ya 141; (*The Appellate Jurisdiction Act, Cap.141*)

(c) Sheria ya Usuluhishi, Sura ya 15; (*The Arbitration Act, Cap. 15*)

(d) Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sura ya 391; (*The Commission for Human Rights and Good Governance Act, Cap. 391*)

(e) Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20; (*The Criminal Procedure Act, Cap. 20*)

(f) Sheria ya Uhujumu Uchumi na Makosa ya Kupanga, Sura ya 200; (*The Economic and Organised Crime Control Act, Cap. 200*)

(g) Sheria ya Miamala ya Kielektroniki, Sura ya 442; (*The Electronic Transcations Act,* Cap. 442)

(h) Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6; (*The Evidence Act, Cap. 6*)

(i) Sheria ya Chuo cha Usimamizi wa Mahakama Lushoto, Sura ya 405; (*The Institute Of Judicial Administration Lushoto Act, Cap. 405*)

(j) Sheria ya Usimamizi wa Mahakama, Sura ya 237. (*The Judiciary Administration Act,* Cap. 237)

(k) Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216 (*The Land Disputes Courts Act, Cap. 216)*

(l) Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura 171(*The Law Reform Commission of Tanzania Act, Cap. 171*)

(m) Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania, Sura ya 425 (*The Law School of Tanzania Act, Cap. 425*)

(n) Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sura ya 21 (*The Legal Aid Act, Cap. 21*)

(o) Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11 (*The Magistrates' Courts Act, Cap. 11*)

(p) Sheria ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Sura ya 430 (*The National Prosecutions Service Act, Cap. 430*)

(q) Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura 268 (*The Office of The Attorney General (Discharge of Duties) Act, Cap. 268*)

(r) Sheria ya Bodi ya Msamaha wa Wafungwa, Sura ya 400 (*The Parole Boards Act, Cap. 400*)

(s) Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 (*The Penal Code, Cap. 16*)

(t) Sheria ya Uthibitishaji Wosia ya Usimamizi wa Mirathi, Sura ya 352 (*The Probate and Administration of Estates Act, Cap. 352*)

(u) Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256 (*The Proceeds of Crime Act, Cap 256*)

(v) Sheria ya Chama cha Wanasheria Tanganyika, Sura 307 (*The Tanganyika Law Society Act, Cap 307*); Na

(w) Sheria ya Usajili wa Wadhamini, Sura ya 318 (*The Trustees' Incorporation Act, Cap. 318*)

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inayohusu masharti ya utangulizi, inajumuisha Ibara ya Kwanza inyohusu jina fupi na Ibara ya Pili inayoeleza marekebisho yanayofanyika katika Sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Sheria zinazofanyiwa marekebisho na maudhui yake. Wakati wa uchambuzi wa Muswada huu pamoja na maelezo ya Waziri wa Katiba na Sheria, Kamati ilibaini

changamoto au upungufu katika Sheria sita kati ya sheria ishirini na tatu zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kama zilivyo wasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 (*The Advocates Act, Cap. 341*). Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya Tatu hadi Ibara ya Saba ya Muswada. Marekebisho katika sehemu hii yanalenga kumfanya Wakili wa Serikali wa Mkoa kuwa Mwakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Kamati ya Mawakili wa Mkoa kwa kuondoa cheo cha Wakili wa Serikali Mfawidhi, ili kuendana na Muundo wa sasa wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, vilevile, marekebisho katika Sheria hii yanakusudia kuongeza adhabu kwa watu wanaofanya kazi za uwakili ambao hawana sifa au vigezo vya kufanya kazi hizo. Lengo la marekebisho haya ni kuzuia utendaji wa makosa ambayo huathiri upatikanaji wa haki.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sura ya 391; (*The Commission for Human Rights and Good Governance Act, Cap. 391*). Sehemu hii inahusu Ibara ya 13 hadi 16 ambapo marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria hii ni yanahusu kufuta maneno "*administrative justice*" na badala yake kuweka maneno "*good governance*" katika kifungu cha 6. Marekebisho haya yanalenga kuleta ulinganifu wa maneno ambayo yanalingana na Majukumu ya Tume kama yalivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 15 inapendekeza kufanya marekebisho kwa kuanzisha vyeo viwili vya Naibu Katibu Mkuu wa Tume, kwa lengo kuboresha utekelezaji wa Majukumu ya Tume kwa kuongeza nguvu kazi na uwiano wa majukumu ndani ya Taasisi hiyo. Aidha, marekebisho haya yanaweka sharti kwa Naibu Makatibu wa Tume kuapa mbele ya Mheshimiwa Rais, kabla ya kuanza utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nane inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura 171 (*The Law Reform Commission of Tanzania Act, Cap. 171*). Kamati Ilielezwa kuwa marekebisho katika Sheria hii yanajumuisha mambo mbalimbali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 48 inaongeza kifungu kipya cha 4(A) ambacho kimeweka sharti kwa Wizara, taasisi, idara ama wakala yeyote ya Serikali inayokusudia kurekebisha au kutunga Sheria kuwahusisha Tume kwanza kabla mapendekezo ya Sheria husika hayajapelekwa kwenye Baraza la Mawaziri. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha ubora wa Sheria na kuhakikisha kuwa maamuzi ya kurekebisha Sheria yoyote nchini yanafanywa baada ya kupata taarifa za kutosha kutoka Tume.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 49 inapendekeza kuongeza idadi ya Makamishna wa Tume kutoka wawili kama walivyo sasa hadi kufikia wanne. Lengo ni kuongeza nguvu kazi ili kuwezesha utekelezaji wa Majukumu ya Tume kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Nne ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania, Sura ya 425 *(The Law School of Tanzania Act, Cap. 425)*. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 51 hadi Ibara ya 55 ya Muswada. Ibara ya 52 inarekebisha kifungu cha 2 cha Sheria ili kuainisha sifa za watu wanaosimamiwa na Sheria hii. Ibara ya 53 inarekebisha kifungu cha 9 kwa kumuondoa Mkuu wa Shule ya Sheria katika Kamati ya Mitihani na badala yake kumuweka Naibu Mkuu wa Shule anayehusika na Masuala ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo na kuweka bayana muda wa uhai wa Kamati kuwa ni miaka mitatu na inaweza kuongezewa kipindi kingine kimoja. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi na uwajibikaji wa Kamati hiyo katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, aidha, Sheria inapendekeza kufanya mabadiliko ya Muundo wa Bodi ya Shule ya Sheria kwa vitendo ili kuwajumuisha Wajumbe ambao si Wanasheria. Madhumuni ya marekebisho hayo ni kuiwezesha Bodi kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Nne ya Muswada inapendekeza Marekebisho ya Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura 268 (*The Office of The Attorney General (Discharge of Duties) Act, Cap. 268*). Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 63 hadi Ibara ya 75 ya Muswada. Ibara ya 64 inapendekeza kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza tafsiri ya misamiati katika Sheria hiyo. Hii inalenga kuweka wazi maana ya maneno yaliyotumika katika sheria ili kuondoa utata wa tafsiri mbalimbali ambazo hazikukusudiwa katika Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 67 inapendekeza uanzishaji wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria katika Muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, Ibara ya 69 inaainisha majukumu ya Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria inayopendekezwa kuanzishwa. Hii inalenga kutoa mwongozo na utaratibu wa kazi kwa Ofisi hiyo ili kuleta uwiano na ushirikiano mzuri kati ya Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 72 inafafanua uhusiano kati ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wakili Mkuu wa Serikali. Hii inalenga kuweka wazi majukumu na mamlaka ya kila Ofisi na kuhakikisha ushirikiano mzuri na utaratibu katika masuala ya kisheria ndani ya Serikali. Aidha, marekebisho hayo pia yanaongeza sehemu mpya ambayo inaainisha vyanzo vya fedha vya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Hii inalenga kuweka mfumo wa kifedha thabiti na wenye uwazi kwa Ofisi hiyo ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Pia, masharti mengine kuhusu masuala ya fedha yanapendekezwa kuwekwa ili kusimamia matumizi sahihi ya rasilimali za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, marekebisho katika Sheria hii pia yanapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 12A. Kifungu hiki kinampa Mwanasheria Mkuu wa Serikali mamlaka ya kutoa maelekezo ya jumla au mahususi kwa Mwandishi Mkuu wa Sheria kuhusu Masuala ya Uandishi wa Sheria. Hii inalenga kuhakikisha utaratibu na ubora wa kisheria katika shughuli za Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, marekebisho ya Sheria hii yanalenga kuongeza uwazi na utaratibu wa majukumu ndani ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kujenga ushirikiano na taasisi zilizo chini ya au zinazofanya kazi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Mbili ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Chama cha Wanasheria Tanganyika, Sura 307 *(The Tanganyika Law Society Act, Cap 307)*. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 84 hadi Ibara ya 85 ya Muswada. Marekebisho katika sehemu hii yanalenga kuongeza sifa za Wajumbe wa Baraza. Hii inamaanisha kwamba, ili mtu aweze kuwa Mwanachama wa Baraza la Uongozi wa Chama, atahitajika kukidhi vigezo vilivyowekwa na marekebisho haya. Lengo la kuongeza sifa hizi ni kuimarisha uwezo na ujuzi wa Wajumbe wa Baraza katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Aidha, marekebisho haya yanapendekeza kuongeza muda wa kuwa madarakani kwa Wajumbe wa Baraza la Uongozi la chama cha Mawakili kutoka mwaka mmoja na kuwa miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, marekebisho haya yanalenga kuimarisha Uongozi wa Chama cha Wanasheria Tanganyika na kuweka mazingira bora na wezeshi zaidi kwa viongozi wa Baraza kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata. Marekebisho ya Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 *(The Advocates Act, Cap. 341)*.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 *(The Advocates Act, Cap. 341);* katika Ibara ya 7, Kamati ilipendekeza kuongeza kiwango cha faini kwa kosa la watu wanaofanya kazi za uwakili pasi na sifa au vigezo vya kisheria vya

kufanya kazi hizo. Katika pendekezo hili la Kamati limelenga kuhakikisha wale wanaojihusisha na kazi za uwakili wanakuwa na sifa, vigezo na uwezo unaohitajika katika kada hiyo. Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko haya na kuweka faini kwenye kosa hilo ya shilingi zisizopungua milioni tano na isiyozidi shilingi milioni 20. Kamati inaipongeza Serikali kwa kufuata ushauri.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sura ya 391. Kwa kuwa sheria hii inatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, Kamati ilishauri Ibara ya 15 iweke wazi kuwa, Naibu Katibu Mkuu wa Tume mmoja ateuliwe kutoka Bara na mwingine ateuliwe kutoka Zanzibar. Aidha, Kamati ilishauri, majukumu ya Naibu Makatibu wa Tume, yaainishwe kwenye sheria. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri iliyopewa na Kamati.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, kengele ya pili imeshagonga. Dakika tatu malizia.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Ibara ya 48 inapendekeza sharti la Wizara ya Serikali, Taasisi ya Mawakala kuhakikisha tume inarekebisha sheria katika mchakato wa utungaji sheria. Kamati ilibaini kuwa marekebisho haya yanaweza kusababisha ucheleweshaji wa mchakato wa kutunga sheria, migangano na kazi kati ya tume na mamlaka nyingine za Serikali zinazohusika na utungaji. Hivyo basi, Kamati ilishauri Serikali kufuta Ibara ya 48 na tunaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho; napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kujadili na kuchambua Muswada huu, kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho ya mapendekezo kwa mujibu wa mchango wao na kushughulikia Muswada. Naomba majina yao

yaingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge kwa maana ya *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Balozi Mheshimiwa Pindi Chana, Waziri wa Katiba na Sheria; Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria; Mheshimiwa Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndugu Onorius Njole pamoja na Watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kufanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc*. Kwa upekee niishukuru Sekretarieti ya Kamati yetu kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii ambayo ni msimamo wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kujadili, kuukubali, kuupitisha Muswada huu pamoja na jedwali la marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI ZA SEKTA YA SHERIA WA MWAKA 2023 *[THE LEGAL SECTOR LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) BILL, 2023]* KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali na Hadidu za Rejea

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria wa Mwaka 2023 (*The Legal Sector Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023*).

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa kumi na mbili, kikao cha tisa kwenye Bunge la 12, tarehe 8 Septemba, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

### 1.2 Namna Kamati ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi wa Muswada

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 18 Oktoba, 2023 ili kupokea maelezo ya Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana, (Mb) Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu maudhui ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali, na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya Mkutano wa kusikiliza maoni ya wadau *(Public Hearing*) tarehe 19 Oktoba, 2023 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao.

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuwashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu na nichukue fursa hii kuwatambua kama ifuatavyo: -

1. Chama cha Wanasheria Tanganyika (*TLS*);

2. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*LHRC*); pamoja na

3. Wadau binafsi kutoka maeneo mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria na kwa kuzingatia maoni ya wadau. Mnamo tarehe 23 Oktoba, 2023 Kamati ilikutana tena na Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria ambaye alijibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria wa Mwaka 2023 *[The Legal Sector Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023]* ukiwa umegawanyika katika sehemu Ishirini na Nne (24) na unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria Ishirini na tatu (23) kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au dosari au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa Sheria hizo. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni zifuatazo: -

(a) Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 (*The Advocates Act,Cap. 341*)

(b) Sheria ya Mamlaka ya Rufaa, Sura ya 141; (*The Appellate Jurisdiction Act, Cap.141*)

(c) Sheria ya Usuluhishi, Sura ya 15; (*The Arbitration Act, Cap. 15*)

(d) Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sura ya 391; (*The Commission for Human Rights and Good Governance Act, Cap. 391*)

(e) Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20; (*The Criminal Procedure Act, Cap. 20*)

(f) Sheria ya Uhujumu Uchumi na Makosa ya Kupanga, Sura ya 200; (*The Economic and Organised Crime Control Act, Cap. 200*)

(g) Sheria ya Miamala ya Kielektroniki, Sura ya 442; (*The Electronic Transcations Act,* Cap. 442)

(h) Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6; (*The Evidence Act, Cap. 6*)

(i) Sheria ya Chuo cha Usimamizi wa Mahakama Lushoto, Sura ya 405; (*The Institute of Judicial Administration Lushoto Act, Cap. 405*)

(j) Sheria ya Usimamizi wa Mahakama, Sura ya 237. (*The Judiciary Administration Act,* Cap. 237)

(k) Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216 (*The Land Disputes Courts Act, Cap. 216)*

(l) Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura 171(*The Law Reform Commission of Tanzania Act, Cap. 171*)

(m) Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania, Sura ya 425 (*The Law School of Tanzania Act, Cap. 425*)

(n) Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sura ya 21 (*The Legal Aid Act, Cap. 21*)

(o) Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11 (*The Magistrates' Courts Act, Cap. 11*)

(p) Sheria ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Sura ya 430 (*The National Prosecutions Service Act, Cap. 430*)

(q) Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura 268 (*The Office of the Attorney General (Discharge of Duties) Act, Cap. 268*)

(r) Sheria ya Bodi ya Msamaha wa Wafungwa, Sura ya 400 (*The Parole Boards Act, Cap. 400*)

(s) Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 *(The Penal Code, Cap. 16)*

(t) Sheria ya Uthibitishaji Wosia na Usimamizi wa Mirathi, Sura ya 352 *(The Probate and Administration of Estates Act, Cap. 352)*

(u) Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256 *(The Proceeds of Crime Act, Cap 256)*

(v) Sheria ya Chama cha Wanasheria Tanganyika, Sura 307 *(The Tanganyika Law Society Act, Cap 307);* na

(w) Sheria ya Usaji wa Wadhamini, Sura ya 318 *(The Trustees' Incorporation Act, Cap. 318)*

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inayohusu masharti ya utangulizi, inajumuisha **Ibara ya 1** inyohusu jina fupi na **Ibara ya 2** inayoeleza marekebisho yanayofanyika katika sheria mbalimbali.

## 2.2 Sheria Zinazofanyiwa Marekebisho na Maudhui yake

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa uchambuzi wa Muswada huu Pamoja na Maelezo ya Waziri wa Katiba na Sheria, Kamati ilibaini changamoto au mapungufu katika sheria Sita kati ya sheria Ishirini

na Tatu zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kama zilivyo wasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 (*The Advocates Act, Cap. 341*)**. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 3 hadi Ibara ya 7 ya Muswada. Marekebisho katika sehemu hii yanalenga kumfanya Wakili wa Serikali wa Mkoa kuwa mwakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kamati ya Mawakili wa Mkoa kwa kuondoa cheo cha Wakili wa Serikali Mfawidhi, ili kuendana na muundo wa sasa wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Vilevile, marekebisho katika sheria hii yanakusudia kuongeza adhabu kwa watu wanaofanya kazi za uwakili ambao hawana sifa au vigezo vya kufanya kazi hizo. Lengo la marekebisho haya ni kuzuia utendaji wa makosa ambayo huathiri upatikanaji wa haki.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya **Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sura ya 391; (*The Commission for Human Rights and Good Governance Act, Cap. 391*).** Sehemu hii inahusu ibara ya 13 hadi 16 ambapo Marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria hii ni yanahusu kufuta maneno "administrative justice" na badala yake kuweka maneno "good governance" katika kifungu cha 6. Marekebisho haya yanalenga kuleta ulinganifu wa maneno ambayo yanalingana na majukumu ya Tume kama yalivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 15 inapendekeza kufanya marekebisho kwa kuanzisha vyeo viwili vya Naibu Katibu Mkuu wa Tume, kwa Lengo kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Tume kwa kuongeza nguvu kazi na uwiano wa majukumu ndani ya Taasisi hiyo. Aidha, marekebisho haya yanaweka Sharti kwa Naibu Makatibu wa Tume kuapa mbele ya Rais kabla ya kuanza utekelezaji wa majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Nane inapendekeza kufanya marekebisho ya **Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura 171 (*The Law Reform Commission of Tanzania Act, Cap. 171*).** Kamati ilielezwa kuwa marekebisho katika Sheria hii yanajumuisha mambo mbalimbali kama ifuatavyo: -

a) Ibara ya 48 inaongeza kifungu kipya cha 4A ambacho kimeweka sharti kwa Wizara, Taasisi, Idara ama wakala yeyote ya Serikali inayokusudia kurekebisha au kutunga Sheria kuwahusisha Tume kwanza kabla mapendekezo ya Sheria husika hayajapelekwa kwenye Baraza la Mawaziri. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha ubora wa sheria na kuhakikisha kuwa maamuzi ya kurekebisha sheria yoyote nchini yanafanywa baada ya kupata taarifa za kutosha kutoka Tume.

b) Ibara ya 49 inapendekeza kuongeza idadi ya Makamishna wa Tume kutoka wawili kama walivyo sasa hadi kufikia wanne. Lengo ni kuongeza nguvu kazi ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Tume kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kumi na Nne ya Muswada inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania, Sura ya 425 (*The Law School of Tanzania Act, Cap. 425*)**. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 51 hadi Ibara ya 55 ya Muswada. Ibara ya 52 inarekebisha kifungu cha 2 cha Sheria ili kuainisha sifa za watu wanaosimamiwa na Sheria hii. Ibara ya 53 inarekebisha kifungu cha 9 kwa kumuondoa Mkuu wa Shule ya Sheria katika Kamati ya Mitihani na badala yake kumuweka Naibu Mkuu wa Shule anayehusika na masuala ya mafunzo ya sheria kwa vitendo na kuweka bayana muda wa uhai wa Kamati kuwa ni miaka mitatu na inaweza kuongezewa kipindi kingine kimoja. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi na uwajibikaji wa Kamati hiyo katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, Sheria inapendekeza kufanya mabadiliko ya Muundo wa Bodi ya Shule ya Sheria kwa Vitendo ili kuwajumuisha wajumbe ambao si Wanasheria. Madhumuni ya marekebisho hayo ni kuiwezesha Bodi kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kumi na Nne ya Muswada inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura 268 (*The Office of the Attorney General (Discharge of Duties) Act, Cap. 268*)** Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 63 hadi Ibara ya 75 ya Muswada, Ibara ya 64 inapendekeza kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza tafsiri ya misamiati katika sheria hiyo. Hii inalenga kuweka wazi maana ya maneno yaliyotumika katika sheria ili kuondoa utata wa tafsiri mbalimbali ambazo hazikukusudiwa katika sheria hii

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 67 inapendekeza uanzishaji wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria katika muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Aidha, Ibara ya 69 inaainisha majukumu ya Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria inayopendekezwa kuanzishwa. Hii inalenga kutoa mwongozo na utaratibu wa kazi kwa Ofisi hiyo ili kuleta uwiano na ushirikiano mzuri kati ya Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 72 inafafanua uhusiano kati ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wakili Mkuu wa Serikali. Hii inalenga kuweka wazi majukumu na mamlaka ya kila ofisi na kuhakikisha ushirikiano mzuri na uratibu katika masuala ya kisheria ndani ya Serikali.

Aidha, Marekebisho hayo pia yanaongeza sehemu mpya ambayo inaainisha vyanzo vya fedha vya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Hii inalenga kuweka mfumo wa kifedha thabiti na wenye uwazi kwa Ofisi hiyo ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Pia, masharti mengine kuhusu masuala ya fedha yanapendekezwa kuwekwa ili kusimamia matumizi sahihi ya rasilimali za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika** marekebisho katika sheria hii pia yanapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 12A, Kifungu hiki kinampa Mwanasheria Mkuu wa Serikali mamlaka ya kutoa maelekezo ya jumla au mahususi kwa Mwandishi Mkuu wa Sheria

kuhusu masuala ya uandishi wa sheria. Hii inalenga kuhakikisha uratibu na ubora wa kisheria katika shughuli za Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika** Kwa ujumla, marekebisho ya sheria hii yanalenga kuongeza uwazi na uratibu wa majukumu ndani ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Kujenga ushirikiano na Taasisi zilizo chini ya au zinazofanya kazi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Ishirini na mbili ya Muswada inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Chama cha Wanasheria Tanganyika, Sura 307 (*The Tanganyika Law Society Act, Cap 307*)** Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 84 hadi Ibara ya 85 ya Muswada. Marekebisho katika sehemu hii yanalenga kuongeza sifa za wajumbe wa Baraza. Hii inamaanisha kwamba, ili mtu aweze kuwa mwanachama wa Baraza la Uongozi wa Chama, atahitajika kukidhi vigezo vilivyowekwa na marekebisho haya. Lengo la kuongeza sifa hizi ni kuimarisha uwezo na ujuzi wa wajumbe wa Baraza katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Aidha, marekebisho haya yanapendekeza kuongeza muda wa kuwa madarakani kwa wajumbe wa Baraza la Uongozi la Chama cha Mawakili kutoka mwaka mmoja na kuwa miaka mitatu.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla, marekebisho haya yanalenga kuimarisha uongozi wa Chama cha Wanasheria Tanganyika na kuweka mazingira bora na wezeshi zaidi kwa viongozi wa Baraza kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi Zaidi.

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

**3.2 Marekebisho ya Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 (*The Advocates Act, Cap. 341*).**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Ibara ya 7 Kamati ilipendekeza kuongeza kiwango cha faini kwa kosa la watu wanaofanya kazi za uwakili pasina sifa au vigezo vya za kisheria vya kufanya kazi hizo, pendekezo hili la Kamati linalenga kuhakikisha wale wanaojihusisha na kazi za uwakili wanakua na sifa, vigezo na uwezo unaohitajika katika kada hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko Kwa kuweka faini kwenye kosa hilo la shilingi zisiozopungua milioni tano na isiyozidi milioni ishirini. Kamati inaipongeza Serikali kwa kufuata ushauri.

**3.3 Marekebisho ya Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sura ya 391; (*The Commission for Human Rights and Good Governance Act, Cap. 391*).**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Sheria hii inatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, Kamati ilishauri Ibara 15 iweke wazi kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Tume mmoja ateuliwe kutoka Tanzania Bara na mwingine ateuliwe kutoka Tanzania Zanzibar. Aidha, Kamati ilishauri majukumu ya Naibu Makatibu wa Tume yaainishwe kwenye Sheria. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

**3.4 Marekebisho ya Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura 171 (*The Law Reform Commission of Tanzania Act, Cap. 171*).**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Ibara ya 48 inayopendekeza kuweka sharti la Wizara, Idara za Serikali, Taasisi na Mawakala wa Serikali kushirikisha Tume ya Kurekebisha Sheria katika mchakato wa utungaji sheria Kamati ilibaini kuwa marekebisho hayo yanaweza kusababisha ucheleweshaji wa mchakato wa kutunga Sheria na migongano ya kazi kati ya tume na mamlaka nyingine za serikali zinazohusika na utungaji wa sheria.

**3.5 Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania, Sura ya 425 (*The Law School of Tanzania Act, Cap. 425*).**

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa uwasilishaji wa maudhui ya marekebisho ya Sheria hii, Mtoa hoja aliieleza kamati kuwa kuna mapendekezo mengine yaliotolewa na wadau mbalimbali wakiwemo Shule ya Sheria kwa Vitendo Tanzania kuhusu Sheria hii. Mapendekezo hayo yatahusisha kufanya marekebisho katika vifungu mbalimbali vya Muswada huo. Mtoa hoja aliiomba Kamati kutojadili sehemu ya Kumi na Nne kwa muktadha wa kuweka marekebisho yote kwenye Muswada mahususi ambao unatarajiwa kuwasilishwa kwa ajili ya kusomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa kumi na tatu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikubaliana na mapendekezo kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**3.6 Marekebisho ya Sheria ya Chama cha Wanasheria Tanganyika, Sura 307 (*The Tanganyika Law Society Act, Cap 307*).**

**Mheshimiwa Spika**, Marekebisho katika Sheria hii yameainisha sifa za mjumbe wa Baraza la uongozi wa Chama cha Wanasheria Tanganyika. Miongoni mwa sifa zilizoainishwa ni pamoja na Jaji aliyestaafu ambae ni mwanachama hai na Mtumishi wa umma aliyestaafu mwenye uzoefu wa miaka kumi au zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliishauri Serikali kuwa sifa za mjumbe wa Baraza la Chama hicho ibaki kuwa mwanachama mwenye sifa ya Uwakili pamoja na vigezo vingine vilivyoainishwa kwenye Sheria. Jaji aliyestaafu ambae ni mwanachama hai au mtumishi wa umma aliyestaafu watambuliwe kwa uwakili wao na sio utumishi wao kwa umma kama sifa ya kuwepo katika Baraza la Chama hicho.

**Mheshimiwa Spika**, Tunaipongeza Serikali kwa kukubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko Kwa kuzingatia ushauri wa Kamati. Aidha, Kamati ilishauri kuhusu marekebisho ya jumla ya kiuwandishi na maudhui katika Ibara ya 68, 69 na 73 ya

Muswada kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb | – | **Mwenyekiti** |
| 2. | Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb | - | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Omar Issa Kombo, Mb | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb | - | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb | - | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb | - | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb | - | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb | - | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb | - | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb | - | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb | - | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb | - | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb | - | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana, (Mb) Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Pauline Philipo Gekul (Mb) Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria, Mhe. Eliezer Mbuki Feleshi Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndg. Onorius Njole, pamoja

na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

### 4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Florent Laurent Kyombo (Mb)
**M/MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**

31 Oktoba, 2023

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana Mheshimiwa Yahaya Massare.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hoja hizo mbili kuwasilishwa kwetu na pia Kamati yetu kutoa maoni yake katika hoja zote mbili, tutazijadili zote kwa pamoja, halafu wakati wa kufanya maamuzi tutafanya moja baada ya nyingine.

Nimeletewa majina hapa ya Wabunge ambao wangependa kuchangia hoja hii. Tunaye Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahaya Massare na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki ajiandae.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada wa Sheria wa

Marekebisho ya Sheria katika sekta ya sheria. Naomba nianze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na Mawaziri wote wa sekta hii ya sheria, Mwanasheria Mkuu, pamoja na Watendaji wote wa sekta hii kwa jinsi ambavyo wanafanya kazi iliyotukuka.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kujielekeza kwenye Sehemu ya Tano ya sheria hii ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria ya mwaka 2020/2023. Naomba nijielekeze kwenye Sehemu ya Tano ya Muswada huu ambayo inarekebisha Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe Taasisi hii ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni taasisi muhimu sana kwenye nchi yetu na ni kati ya taasisi chache sana ambazo zimetokana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 katika ile Ibara ya 129.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 15 ya Muswada huu ulioletwa, inapendekezwa kuwekwa kwa nafasi ya Naibu Makatibu Wakuu wawili wa Tume. Pia, ukiangalia katika Sheria Mama katika kifungu cha 3 cha Sheria Mama ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, sheria hii imetamka kwamba itumike Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, Kamati tuliomba sheria hii itaje kwamba hawa Manaibu Makatibu wa Tume, mmoja atokane na Tanzania Zanzibar na mmoja Tanzania Bara, sheria itamke hivyo. Si hivyo tu, sheria hii katika Sheria Mama ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora katika kifungu cha 11(3), utaona sheria imebainisha wazi kabisa majukumu ya Kamishna Mkuu wa Tume.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo huo tumeshauri sheria hii itamke wazi majukumu ya hawa Naibu Makatibu Wakuu wawili, majukumu ya Naibu Mkuu wa Tume kutoka Tanzania Zanzibar na majukumu ya Naibu Katibu wa Tume kutoka Tanzania Bara yawe yametamkwa kabisa kwenye sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nijielekeze katika Sehemu ya Kumi na Tatu ya Muswada huu ambayo inafanya marekebisho katika Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura 171. Katika hii Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Muswada huu unapendekeza katika Ibara ya 48, kuwepo na takwa la lazima kwa Wizara zote, vitengo vyote, wakala wote pamoja na taasisi mbalimbali za Serikali inapoleta marekebisho madogo ya sheria au inapoleta sheria mpya lazima ipitie kwenye tume ili kupata utafiti ndipo ipite Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, ni jambo jema sana. Tukumbuke wakati tunapitisha bajeti ya taasisi hii muhimu ya mwaka 2023/2024, kama kuna changamoto kubwa tulikutana nayo ni changamoto kubwa ya ufinyu wa bajeti ya taasisi hii, lakini pia upungufu wa watumishi. Sasa tulipitishia bajeti ya shilingi bilioni 5.19, lakini pia taaasisi hii haina fungu la maendeleo. Kwa hiyo, tukiangalia mabadiliko haya yanayopendekezwa kwenye sheria hii ambayo anakusudia kuifanya sheria hii kuwe na takwa la kilazima kwamba Wizara zote, Taasisi zote za Kiserikali, Wakala na vitengo vyote kabla havijapeleka sheria kwenye Baraza la Mawaziri vipite kwenye tume hii ifanyiwe utafiti.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo jema, lakini kwa *concern* tuliyoona kwenye changamoto inayokumba taasisi hii, bajeti ndogo, upungufu wa wataalam, tunajua sheria zinakuja kutoka kwenye taasisi mbalimbali, watakuja Madaktari, Wanasheria wenyewe, watu wa kilimo hata watu wa *atomic*. Sasa hawa wote taasisi haina hao wataalam.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumeshauri ili kuepukana na ucheleweshaji wa utungwaji wa sheria maana zitaenda kurundikana kwenye tume kwa upungufu wa bajeti na watumishi, basi Serikali wakati inajiandaa kuipa majukumu hii taasisi iongezee bajeti na wataalam ili mwisho wa siku wanapokuja na sheria ili taasisi hii ishughulikie kila sheria na kila marekebisho ya sheria, basi iwe imeshawezeshwa vizuri ili iweze kuwa uwezo wa kufanya hayo maamuzi ili isije ikachelewesha sheria na hivyo kuchelewesha utaratibu mzima wa nchi kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo katika Sheria Mama ya Tume hii ya Kurekebisha Sheria, Kifungu cha 4(2)(e), jukumu hili limewekwa bayana katika Sheria Mama, lipo katika kifungu hiki, sema halikuwekwa takwa la ulazima. Kwa hiyo, sisi kama Kamati tulishauri kama inawezekana kifungu cha 4 kwenye Sheria Mama kiendelee kufanya kazi hiyo wakati wanaboresha uwezo wa taasisi hii nyeti.

Mheshimiwa Spika, pia Ibara ya 48 ya Muswada huu iondolewe. Kwa kweli niseme kwamba, Serikali kupitia Wizara ya Sheria wamekuwa ni watu ambao ni wasikivu sana, wanaonesha ushirikiano mkubwa na Kamati, wamepokea maoni yetu yote na wamekuja nayo kwenye jedwali la marekebisho. Nawapongeza sana na nawatakia kazi njema.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, watoa hoja wajiandae.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia sehemu chache sana kuhusu Miswada hii miwili. Kusema ukweli kama ambavyo amechangia mchangiaji wa kwanza, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuleta mabadiliko ya sheria za nchi yetu kwa ajili ya ustawi wa wananchi. Pia, niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mwanasheria Mkuu, kwa usikivu wao wanapokutana na Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, utagundua kwamba marekebisho ambayo Kamati tulishauri, mapendekezo tuliyoshauri kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Waziri wa Sheria, mengi yamekubaliwa na Serikali. Kwa hiyo, utaona hata uchangiaji wetu umefilisika sana kwa sababu mengi yamekubaliwa.

Mheshimiwa Spika, labda niseme mambo machache kwenye Sheria ile ya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali, kifungu cha 7,

kunaongeza kifungu cha 14B ambacho kwa kifupi niseme kuna mtu anaitwa *License Authority* anapewa mamlaka ya kufuta leseni ya biashara ya mtu na kwamba huyo Afisa, wasiwasi wa Kamati na wasiwasi wangu ni kwamba, huyu Afisa anaweza akafuta leseni bila sababu za msingi. Kwa hiyo, yalikuwa ni maoni yetu sisi kama Kamati kwamba, pengine sababu za kufuta hiyo leseni zinazopendekezwa na huyo Afisa, zingeweza kuwekwa kwenye sheria ili tusiwe na mchanganyiko na pengine labda upendeleo wa namna fulani kwenye kufuta leseni ya mtu. Maoni yetu ilikuwa ni kwamba, masharti au sababu za kufutwa zingeweza kuelezwa kwenye sheria.

Mheshimiwa Spika, kipengele kingine ni Kifungu cha 8 ambacho kinafuta Kifungu cha 17 cha sheria iliyokuwepo na kukiandika upya, hakuna matatizo hapo. Kulikuwa na shida ya uwepo wa Polisi uliokuwa unaashiria matumizi ya nguvu wakati tunafuatilia leseni hizi zinapoisha muda wake. Bahati nzuri nimesikia Serikali imekubali mapendekezo ya Kamati kwamba, uwepo wa Polisi hautokuwepo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na ushauri mmoja hapa kwamba, sasa hivi tunakwenda kwenye mifumo hii ya kidijitali. Sasa kama tukienda kwenye mifumo ya namna hii, kwa nini tusitengeneze mfumo ambao mtu anaweza akau-*manage* akiwa ofisini kwake. Hawa wote waliopewa leseni wakawa kwenye mfumo huo, inaonesha leseni yake inanza tarehe ngapi, inaisha tarehe ngapi na kwa hivyo wote ambao leseni zao zinakwisha, huyu mtu anaangalia kwenye mfumo, halafu anawasiliana nao na kuwaambia kuwa leseni yako imekwisha, kwa hiyo inabidi uhuishe upya kwa njia ya kimfumo, badala ya kuwa na watu wanaanza kufuatilia moja kwa moja kule, ili tukapunguza matumizi ya watu kwenye mifumo ya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala lingine kwenye sheria mbalimbali hasa zile za sekta ya sheria hasa kwenye sehemu ya13 Ibara ya 48. Kulikuwa kunaongeza kipengele cha 4A kifungu cha 1 na 2. Ilikuwa inamaanisha kabla sheria haijatungwa, utaratibu wa kutunga sheria unajulikana mpaka inapofika hapa Bungeni, lakini

kwenye utaratibu huo ilikuwa inaongeza masharti ya Tume ya Marekebisho ya Sheria nayo kuingia kwenye mchakato huo.

Mheshimiwa Spika, naona wakati wa maelezo, Mheshimiwa Waziri ameeleza kana kwamba alikubali ushauri wa Kamati na kama amekubali kwenye suala hili ni sawa, kwa sababu tulikuwa na wasiwasi kwamba, ikiwa itafanyika hivyo, kutakuwa na ucheleweshaji wa mchakato mzima wa utungaji wa sheria, kwa sababu inabidi tafiti kubwa zifanywe na Tume ya Kurekebisha Sheria, halafu utaratibu mwingine ndiyo uweze kufuatwa.

Mheshimiwa Spika, pia tuliona hii Tume ya Kurekebisha Sheria haina rasilimali watu wa kutosha, vifaa vya kutosha na rasilimali fedha za kutosha kuweza kufanya kazi hiyo iliyokuwa inaongezwa kwenye Tume hiyo. Kwa hiyo, tukaona pengine majukumu hayo yangeweza yasitekelezwe kabisa au yakatekelezwa lakini kwa kuchelewa sana na hivyo tukawa na sheria zinazoendelea kuumiza watu na hatua hazichukuliwi. Hata hivyo, kwa sababu Serikali imekubali nadhani sio suala tena la kujadili.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ya kwangu yalikuwa ni hayo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, aje ahitimishe hoja yake.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii. Pia nashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na wadau wote ambao walishiriki kwa namna moja au nyingine kwenye mchakato wa marekebisho ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, tunaenzi na kuheshimu sana kauli iliyotolewa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo kwa jinsi ambavyo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika hatua za kuandaa Muswada huu tulikaa muda wa kutosha na Kamati na kupokea maeneo yote. Haikuwa rahisi kama ambavyo inaweza kufikiriwa. Kwa hiyo, tunaheshimu michango ya Wanakamati wote, lakini na wadau wote.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mashimba Ndaki katika mchango wake amaeongelea lile suala la matumizi ya Polisi. Suala matumizi ya Polisi lilikuwepo kwenye Kifungu Mama, lakini baada yya kukutana na Kamati na kupata hoja na kuangalia matumizi ya teknolojia tulipofikia, bado tuliona kuna mazingira ya kipekee yanaweza yakalazimu hao maofisa wenye mamlaka na utoaji leseni, mara moja moja kulazimika kufika kwenye maeneo ya biashara inapofanyika hasa kwa kuwa kwenye sheria hii kumekuwa na matakwa mamlaka inayohusika kupata taarifa zilizo sahihi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya kuzingatia hoja za Wajumbe na maendeleo tuliyoyafikia kwenye Jedwali letu la Marekebisho tukaona tuweke kwamba, pale ambapo Afisa mwenye mamlaka atakapoona kuna ulazima ndipo ambapo atahitaji kuambatana na Polisi lakini siyo lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ningependa kueleza kwamba, kwa maendeleo ya uchumi yanayofanyika nchini kwa sasa kupitia Wizara za Kisekta na taasisi zingine, wafanyabiashara kuanzia hawa wa ngazi ya chini wanaanza kutambuliwa na kupewa usaidizi unaostahili. Kwa hiyo, hata matumizi ya teknolojia tunachukulia tahadhari kwamba siyo kila mmoja atafikia kiwango cha kuweza kuwa na matumizi yaliyo bora zaidi lakini wataendelea kusaidiwa kuwa na matumizi bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ambalo niendelee tu kuahidi kwenye Bunge lako Tukufu ni kwamba, kwa yote ambayo tumeyaleta kwenye hizi sheria zote ambazo zimeletwa kupitia Muswada huu, yote ililenga kufanya maboresho ambayo yanaleta ustawi wa jamii katika nyanja zote kisiasa, kiuchumi, lakini na kwa kuangalia mazingira halisi na changamoto zilizojiri. Kwa hiyo, wajibu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Serikali sasa kama Muswada huu kwa Baraka za Bunge lako utatamatika kwa kupitishwa, itakuwa ni kuhakikisha kwamba unaleta mabadiliko yaliyo chanya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuahidi hili, naomba sasa Bunge lako lilidhie hoja zilizotolewa lakini vilevile na ahadi hii ambayo naitoa.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, sasa nimuite Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Dkt. Pindi Chana aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa fursa ya kuhitimisha hoja hii. Tumepata wachangiaji takribani watatu pamoja na maoni ya Kamati, ambayo ni maoni muhimu sana. Kamati imekuwa ikitupa ushirikiano wa hali ya juu chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Mhagama na Makamu Mheshimiwa Florent Kyombo, tunawashukuru sana na maoni mengi ambayo kimsingi Kamati imetupa na nikuhakikishie tumeshirikiana kwa pamoja na kuyazingatia.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na maoni kwamba tunayo Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Hii Tume ni chombo cha Muungano, sasa tunakuja na suala kwamba, Katibu Mtendaji wa Tume lazima awe na Wasaidizi wawili, ambapo mmoja atatoka Bara, mmoja atatoka Visiwani. Tumekuwa na utaratibu wa Vyombo vya Muungano kuwa na ushirikishwaji wa Bara na Visiwani. Kwa hiyo, pale tumesema kutakuwa na *Deputy* wawili, *Executive Secretary* wa Bara na Visiwani.

Mheshimiwa Spika, Kamati ikashauri, pamoja na kuwa na *Executive Secretary Deputy* wawili, Bara na Visiwani, ipo haja ya kusema majukumu yao. Hawa *Deputy* wawili watafanya nini, nasi kama Serikali tumeona hilo ni jambo la msingi sana. Unaposema Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Chombo cha Muungano kitakuwa na *Deputy Secretary* mmoja wa Bara, mmoja Visiwani, hawa watu watafanya nini. Kwa hiyo, tumekuja na marekebisho, *Schedule of Amendments* ambapo tumeeleza wazi kabisa *functions of the Deputy Executive Secretary* zitakuwa ni nini. Pale tumeeleza katika marekebisho C, Kifungu cha 16 kwenye *Schedule of Amendment.* Kwa hiyo, tumeeleza kabisa majukumu

yao yatakuwa ni nini, watakuwa na jukumu la kuhakikisha kwamba wanam-*assist Executive Secretary* na kufanya shughuli zingine kama tulivyoeleza kwenye *Schedule of Amendments*, tunashukuru sana kwa maoni haya muhimu ya Kamati, tusichukue tu *for granted*, uhakika kwamba wakishakuwepo majukumu yao yatajulikana, Hapana! lazima tueleze kwenye sheria, hao Naibu Makatibu, mmoja Bara, mmoja Visiwani, watafanya nini.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na Tume nyingi kama hizi, Tume ya Uchaguzi, ina mmoja Bara, mmoja Visiwani na Tume hizi za Kimuungano ambazo ziko kwenye Katiba, hilo nalo tumelizingatia.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka hapa mara nyingi sana wakati tunarekebisha sheria, Kamati ya Katiba na Sheria na Kamati Ndogo wamekuwa wanasema mara kwa mara kwamba fanyeni tafiti ya sheria hizi, kwa hiyo, Serikali ilikuja na kifungu kwamba, Tume ya Kurekebisha Sheria kuhusishwa katika kutunga sheria, tulikuja nayo na tulipokuja na hili, tulipokwenda kwenye Kamati wakasema, pamoja na hili wazo zuri kabisa la Tume ya Kurekebisha Sheria kufanya tafiti, kuhusishwa katika masuala ya kutunga sheria ni lazima tuangalie uwezo wa Tume, tuangalie bajeti ya Tume, hayo yote baada ya kuyafanyia kazi tumekubaliana na Kamati kwamba eneo hili linahitaji kufanyiwa kazi zaidi.

Mheshimiwa Spika, hivyo, tumekuja na maamuzi ya *Schedule of Amendment*, ambayo tumesema kwamba kifungu hiki tunaki-*delete* na kukubaliana na Kamati. Kwa hiyo, nitoe shukurani nyingi za dhati kwa maoni ya Kamati na niwashukuru wote ambao wamechangia. Mheshimiwa Yahya Massare, Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, Mheshimiwa Ndaki Mashimba lakini pia nikushukuru wewe mwenyewe na Kamati nzima na Wataalam wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano mkubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, tutaendelea kutoa ushirikiano kwa Bunge na sasa ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Tutaanza na hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments) Bill, 2023)***

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 8

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11

Kifungu cha 12
Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35
Kifungu cha 36

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 37

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 38
Kifungu cha 39
Kifungu cha 40

Kifungu cha 41
Kifungu cha 42

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 43

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 44

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 45
Kifungu cha 46

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 47

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 48

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 49
Kifungu cha 50

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 51

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 52
Kifungu cha 53
Kifungu cha 54
Kifungu cha 55
Kifungu cha 56
Kifungu cha 57
Kifungu cha 58
Kifungu cha 59
Kifungu cha 60
Kifungu cha 61
Kifungu cha 62
Kifungu cha 63
Kifungu cha 64
Kifungu cha 65
Kifungu cha 66
Kifungu cha 67
Kifungu cha 68
Kifungu cha 69
Kifungu cha 70
Kifungu cha 71
Kifungu cha 72
Kifungu cha 73
Kifungu cha 74
Kifungu cha 75
Kifungu cha 76
Kifungu cha 77
Kifungu cha 78
Kifungu cha 79
Kifungu cha 80
Kifungu cha 81
Kifungu cha 82
Kifungu cha 83
Kifungu cha 84
Kifungu cha 85

Kifungu cha 86
Kifungu cha 87
Kifungu cha 88
Kifungu cha 89
Kifungu cha 90
Kifungu cha 91
Kifungu cha 92
Kifungu cha 93
Kifungu cha 94
Kifungu cha 95
Kifungu cha 96

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 97

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 98

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. PAMELA PALLANGYO- KATIBU KAMATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Sasa kabla Bunge halijarejea, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenye ile Sheria Mama uko nayo hapo? Ile Sheria Mama unayo? Hebu kwenye ile *schedule part two* ule ukurasa wa 21 umeshafika hapo? Ukienda hapa B siyo sehemu ya haya marekebisho ndiyo maana nimesubiri tumalize kwanza lakini ni jambo ambalo wewe na *CPD* ni jambo la kulitazama. Hapa kwenye B halafu *two*, inazungunzia *description of benefit to be granted to the widow or widower of the Former Vice President,* lakini inasema hapo kwenye *two, a monthly maintenance allowance through his life of the same equal to 40 percent of the*

*salary of the incumbent President*, hapa anazungumziwa *Vice President* kwa nini mafao ya huyu *widow or widower* wa *former Vice President* awe *pegged* kwenye *salary* ya *President*?

Lingine ni hapa kwenye 'C', umeshafika hapo? Kwenye 'C' inazungumzia *description of benefit to be granted to the widow or widower of the Former Prime Minister*. Ukienda kwenye *two* inasema; *a monthly maintenance allowance through his life of the same equal to 40 percent of the salary of the incumbent President*. Kwa nini mafao ya *widow* ama *widower* wa *Former Prime Minister* yawe *pegged* kwa *salary* ya *incumbent President* badala ya *incumbent Prime Minister* ama ile niliyosema mwanzo, *incumbent Vice President* kwa sababu ndiyo *level* yake? *(Makofi)*

Kwa hiyo, hii inaleta huo mkanganyiko na ikiwa hivi maana yake ndivyo tutaendelea, kwa hiyo, hili ni eneo ambalo inabidi mkatayarishe mabadiliko ili sheria zetu ziwe zinasomana vizuri. *(Makofi)*

Eneo lingine ambalo inabidi kulitazama kwa ujumla wake, nalisemea hapa badala ya kwenye Bunge kwa sababu ndiyo tunatungia sheria hapa kwenye Kamati ya Bunge Zima. Eneo lingine la kulitazama ni kwamba hawa *widower or widow* yale mafao wanayopewa na wale viongozi ambao ni *former*, yaani hawa ni *widow* ama *widower* wa huyo aliyekuwa kiongozi halafu kuna hawa ambao ni *former* viongozi, mnapoyatazama yale mafao yao myatazame kwa sura ambayo hamuwaweki mazingira magumu watu ambao walishika madaraka wawe na maisha magumu kuliko aliyekuwa mke wa mtu ambaye alikuwa madarakani, nadhani nimeeleweka.

Kwa hiyo, hilo nalo mlitazame kwa sababu hamuwezi kumpa mengi zaidi huyo aliyekuwa mke wa aliyekuwako madarakani kuliko aliyekuwa kiongozi, ninyi nadhani hoja imeeleweka. Kwa hiyo, nadhani mtakapokuwa mnafanya marekebisho ya hizi *pegging* mlitazame na hili ili liwe linaenda *across* na sheria zetu zikae vizuri. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo sasa, Katibu sema yale maneno yako ili yakae baada ya kusema haya ili Taarifa zetu Rasmi za Bunge zikae vizuri.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

*(Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi. Mtoa hoja, taarifa, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**T A A R I F A**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Toleo la Mwaka 2023, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) ya mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No.4) Bill, 2023)* ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) ya Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No.4) Bill, 2023)* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana. Sasa nitahoji kwa utaratibu wetu wa kibunge kuhusu hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, inayohusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka

2023 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No.4) Bill, 2023]*.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali zipatazo kumi kwa lengo la kuondoa upungufu ambao umejitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika sheria hizo *(A Bill for Enact Amend Certain Written Laws, in order to Keep the Laws Updated With some Challenges Observed in its Implementation)*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya Kusomwa Mara ya Tatu, Bunge limeshamaliza kazi yake ya kupitisha Muswada huu ambao ulileta na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Kamati yetu ya Katiba na Sheria kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kupitia Muswada huu na wakatoa mapendekezo yao ambayo Serikali imeyachukuwa kwa asilimia kubwa sana na ninyi mmesikia hapa Kamati ikisoma taarifa yake kuonesha kwamba hii baada kusomwa huu Muswada, katika utungaji wa Sheria Serikali imewasikiliza Wabunge. Vile vile Wabunge wamekuwa wakitoa maoni hayo wakiwa wamewasikiliza wadau mbalimbali ambao wamewataja kwenye taarifa yao.

Kwa hiyo, tunaipongeza pia Serikali kwa kusikiliza maoni ya Waheshimiwa Wabunge katika utungaji wa sheria. Hivyo kwa upande wa Bunge tumemaliza taratibu zetu za kutunga Sheria hii na hivyo tutapeleka kwa Mheshimiwa Rais ili aweze naye kuitazama halafu atakapotoa kibali chake sheria iweze kuanza kazi, tutawatangazia Waheshimiwa Wabunge.

Kwa hiyo, katika yale ambayo mmeyaweka humu tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wake.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea na utaratibu wetu. Ah, sijawasomea sheria tuliyopitisha. *(Kicheko)*

Haya, Bunge limepitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa mwaka 2023 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No.4) Bill, 2023]* kwa hiyo, Bunge limepitisha rasmi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na hoja nyingine ambayo nayo iliwasilishwa kwetu.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tuketi.

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea na Muswada wa *The Legal Sector Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2023*

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 7

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 15

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:** Baada ya Kifungu cha 15 kuna kifungu kipya kilichoongezwa na Serikali.

Kifungu Kipya cha 16

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Sasa hiki kifungu kipya kitapewa namba 16, kwa hiyo hizi namba tutazibadilisha baadaye kwa kifungu kimoja. Kwa hiyo, tutakapokuwa tunahoji kifungu 16 ni kile ambacho kinasomeka kwenye Muswada tulionao sasa. Kwa hiyo, ongezeko la kile kifungu kipya tutalifanya baadaye.

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35
Kifungu cha 36
Kifungu cha 37
Kifungu cha 38
Kifungu cha 39
Kifungu cha 40
Kifungu cha 41
Kifungu cha 42
Kifungu cha 43
Kifungu cha 44
Kifungu cha 45
Kifungu cha 46
Kifungu cha 47

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 48

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilifutwa na Serikali)*

Kifungu cha 49
Kifungu cha 50

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya 14 ambayo inaanzia kifungu cha 51 mpaka cha 55 imefutwa na Serikali.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hii sehemu Mheshimiwa Waziri, tukiwa kwenye Bunge ameshatoa maelezo ya kwa nini amefuta sehemu hii.

Kifungu cha 51
Kifungu cha 52
Kifungu cha 53
Kifungu cha 54
Kifungu cha 55

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilifutwa na Serikali)*

Kifungu cha 56
Kifungu cha 57
Kifungu cha 58
Kifungu cha 59
Kifungu cha 60
Kifungu cha 61
Kifungu cha 62
Kifungu cha 63
Kifungu cha 64
Kifungu cha 65
Kifungu cha 66
Kifungu cha 67

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 68
Kifungu cha 69

*(Vifungu vilivvyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 70
Kifungu cha 71
Kifungu cha 72

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 73

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 74

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 75

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 76
Kifungu cha 77
Kifungu cha 78
Kifungu cha 79
Kifungu cha 80
Kifungu cha 81
Kifungu cha 82
Kifungu cha 83
Kifungu cha 84

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 85

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 86
Kifungu cha 87
Kifungu cha 88

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 89

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

**NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na marekebisho hayo sasa kile kifungu cha 16 hadi cha 89 vitapangwa upya, na sasa vitasomeka kuanzia kuwa kifungu cha 17 hadi 84.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mabadiliko hayo ya namba kwenye vile vifungu yanaafikiwa.

*(Mabadiliko ya namba kutokana na marekebisho yaliyofanywa kwenye baadhi ya Ibara zilizotajwa katika Muswada huu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)*

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima, imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge, linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tuketi. Mtoa hoja, taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102, ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la mwaka 2023. Napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta za Sheria ya Mwaka 2023 *[The Legal Sector Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023],* ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria ya Mwaka 2023 *[The Legal Sector Laws (Miscellaneus Amendments) Bill, 2023*], kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria ya Mwaka 2023 *[The Legal Sector Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023.*

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wote mmeafiki, ahsante sana. Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria zipatazo 23, kwa lengo la kuondoa upungufu

ambao umejitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya Masharti katika Sheria hizo *[A Bill for Enact to Amend Legal Sector Laws In order to Keep the Laws Updated with some challenges observed on its Implementation]*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa kwa mara ya tatu na kwa hiyo, sehemu yetu kama Bunge tumemaliza kazi yetu. Nitumie tena fursa hii kuwashukuru sana Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Kamati nzima ya Utawala Katiba na Sheria kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kupitia sheria mbalimbali ambazo zimeletwa kwenye marekebisho ya sheria hii, na kwa namna Serikali ilivyokiri hapa, ushirikiano umekuwa mzuri. Kwa hiyo, mazingira ya kufanya kazi yamekuwa mazuri. Kwa hiyo, tunawashukuru sana Kamati yetu kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Pia, tunaishukuru Serikali kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote cha kufanya kazi hii. Naamini kwa sababu Mheshimiwa Waziri umesema hapa kwamba ushirikiano huo utaendelea kati yako na Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, Bunge limeshamaliza kazi yake kwa hatua hii. Kwa hiyo, tutampelekea Mheshimiwa Rais kama ilivyo ada na Katiba yetu inavyotutaka ili naye aweze kutazama Muswada huu na kuona kama atauridhia, basi utakuwa sheria.

Sasa Bunge limepitisha rasmi Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria wa Mwaka 2023 *[The Legal Sector Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023]*.

Waheshimiwa Wabunge wote, mlioshiriki kwenye zoezi hili la Utungaji wa Sheria, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwashukuru kwa kazi hiyo nzuri mnayoifanya, mambo mawili; moja, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hili moja tunalifahamu Wanasheria lakini pengine ni wakati muafaka wa kuanza kuliweka kwenye

sheria zinazohusika hasa kwa sababu wakati mwingine ujumbe unapoenda huko, yaani Muswada unapochapishwa na Bunge kwamba utaanza kutazamwa watu walete maoni wanaleta maoni na Serikali tunashukuru huwa mnayasikiliza, lakini wakati mwingine kunakuwa na upotoshaji hapa na pale kwa sababu watu wanakuwa hawaelewi wengine hii michakato namna inavyokwenda.

Sasa kwa sababu hiyo, iko haja ya kutazama ile *principle,* kuwa mtu hawezi kupokea malipo mara mbili kwa wakati mmoja kutoka Serikalini. Kwa hiyo, ni muhimu pia hata hawa Wenzi wa Viongozi, pawepo mahali kwamba ikiwa hafanyi kazi ama ameacha kazi; kama anafanya kazi, hawezi kulipwa mara mbili. Sasa mwananchi anakuwa hafahamu kwamba, kama anafanya kazi na bado ni mwenza wa kiongozi, hawezi kulipwa mara mbili, atalipwa mojawapo kwa sababu bado anatumikia kazi yake, kwa hiyo analipwa huku. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hilo nalo ni vizuri kuonesha kwamba pengine mahali itaonekana haya atapewa yule ambaye hafanyi kazi, yule ambaye hana mshahara mwingine kutoka upande wa Serikali ama hana malipo mengine, maana huko tunapokwenda tutajikuta kwamba wapo watu ambao ni wenza lakini wote ni viongozi. Kwa hiyo, kila mtu ana mafao yake. Sasa mwananchi anaweza akafikiri analipwa yote mawili wakati yeye analipwa mafao ya aina moja kwa sababu kuna huo utaratibu wa kawaida kabisa wa kisheria kwamba huwezi kupokea mafao au malipo mara mbili. Unalipwa mojawapo ambalo lina mafao zaidi.

Kwa hiyo, hilo nalo utalitazama na Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Mwandishi Mkuu wa Sheria ili sheria zetu ziwe zinakaa katika hali ya usafi, ili mtu anaposoma basi awe anapata picha yote hapo hapo.

Jambo lingine, ambalo ni la kulitizama kwa ujumla wake, kwa sababu tumeshaona na tunaendelea kujifunza, pengine ni muda muafaka wa kuanza kutafakari muda ambao huyu kiongozi amefanya kazi na yale malipo anayotakiwa kulipwa. Kwa nini? Kwa sababu, anaweza kuwa amefanya kazi mwezi mmoja, lazima

kuwe na muda kwa sababu hata yale mafao ya kawaida wanayolipwa wafanyakazi huwa kuna muda ambao lazima awe amefanya kazi kwa muda fulani.

Kwa hiyo, pengine ni muda muafaka wa viongozi pia kuanza kutazama haya mafao yanayolipwa awe amefanya kwa muda gani? Kwa mwezi mmoja, miezi miwili, miezi mitatu, na je, mafao yatafanana au yatakuwa tofauti? Au amefanya kazi mwaka mmoja, amefanya kazi miaka mitatu, pengine kuwe na muda ule ambao ni wa chini kabisa, yaani kwamba akifikisha kipindi hiki anastahili hivi, lakini kama tukiweka tu wazi namna hii, maana yake hata aliyefanya mwezi mmoja naye anastahili, ni sawa tu na yule aliyefanya miaka mitano, miaka kumi.

Pengine ni muda wa kufanya utafiti na kwa sababu leo hapa tumeizungumzia kwa sehemu Tume ya Kurekebisha Sheria, ni jambo la kulitazama tuanze kuangalia. Kwa sababu, katika mazingira yetu mambo mengi yamebadilika kwa wema. Mheshimiwa Rais ameboresha sana mazingira ya afya kwa maana sasa hivi watu tunaishi muda mrefu. Sasa katika mazingira hayo, mzigo unaweza ukawa mzito sana kwa Serikali tusipolitazama hili jambo. Kama mtu akifanya kazi mwezi mmoja akitoka anafanana na yule aliyefanya kazi miaka mitano, inaweza kidogo ikaleta mzigo mkubwa sana kwa Serikali. Hilo ni la kulifanyia utafiti, halafu mkishamaliza huo utafiti, basi mtaona namna bora ya kuliweka kwenye sheria zetu ili kuwe na huo muda wa chini kabisa kwa maana ya *minimum serving time au service time*, kitu kama hicho.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.20 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 1 Novemba, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*